## *TANZANIA OSAKA ALUMNI*

# Kitabu cha

# Mbinu Bora 6

**Ofisi ya Rais**
**Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa**
**P.O. Box 1923,**
**Dodoma.**

**DISEMBA, 2018**

# KITABU CHA MBINU BORA 6 (2018)

**Kimeandaliwa kwa ajili ya Tanzania Osaka Alumni (TOA) na:**

| | | |
|---|---|---|
| **Paulo Faty** | - | **Mhadhiri, Chuo Kikuu Mzumbe** |
| **Ahmed Nassoro** | - | **Mhadhiri Msaidizi, Chuo cha Serikali za Mitaa** |
| **Michiyuki Shimoda** | - | **Mshauri Mwandamizi, TAMISEMI** |

**Na kuhaririwa na:**

| | | |
|---|---|---|
| **Liana Hassan** | - | **Mshauri** |
| **Honorina Ng'omba** | - | **Mtaalam wa Kitaifa, TAMISEMI** |

# Yaliyomo


| Mada | Kurasa |
|---|---|
| ***Vifupisho*** | ***i*** |
| ***Dibaji*** | *iii* |
| ***Utangulizi (TOA)*** | ***iv*** |
| ***Utangulizi (JICA)*** | *v* |
| ***SURA YA KWANZA: UTANGULIZI; MASUALA YALIYOIGWA KUTOKANA NA UZOEFU WA JAPANI*** | ***1*** |
| ***SURA YA PILI: JITIHADA ZA JAMII KATIKA KUBORESHA UTOAJI WA HUDUMA*** | *20* |
| ***Kibaha DC: Self Help Efforts in Improving Service Delivery*** | *23* |
| ***Halmashauri ya Wilaya ya Mpimbwe: Jitihada Za Jamii Katika Kuboresha Mazingira Ya Kufundisha Na Kujifunza*** | *30* |
| ***Halmashauri ya Wilaya ya Tabora: Jitihada za Jamii Katika Kuanzisha Shule ya Sekondari*** | *38* |
| ***Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu: Jitihada Za Kikundi Cha Vijana Katika Kuleta Mabadiliko Ya Kijamii Na Kiuchumi*** | *45* |
| ***Halmashauri ya Wilaya ya Urambo:Jitihada za Jamii Katika Uboreshaji Wa Huduma ya Afya*** | *53* |
| ***SURA YA TATU: USHIRIKISHWAJI WA JAMII KATIKA UTOAJI WA HUDUMA*** | *63* |
| ***Halmashauri ya Manispaa ya Mpanda: Jitihada Shirikishi za Kuboresha Ufaulu wa Wanafunzi Katika Elimu ya Msingi*** | *67* |
| ***Halmashauri ya Manispaa ya Sumbawanga: Uboreshaji na Urasimishaji Shirikishi wa Ardhi na Majengo*** | *75* |
| ***Halmashauri Ya Manispa Ya Kigoma Ujiji: Urasimishaji wa Umiliki Wa Ardhi ili Kutokomeza Makazi Holela na Migogoro*** | *82* |
| ***Halmashauri ya Mji Kibaha: Ujenzi Shirikishi wa Soko Kwa Ajili ya Kuboresha Hali Ya Maisha*** | *88* |
| ***Halmashauri ya Wilaya ya Kibondo: Ujenzi Shirikishi wa Soko kwa Ajili ya Kuboresha Hali ya Maisha*** | *97* |
| ***Halmashauri ya Wilaya ya Mafia: Ushiriki wa Jamii Katika Ujenzi Na Usimamizi wa Skimu ya Maji*** | *105* |
| ***Halmashauri Ya Wilaya Ya Kaliua: Uhifadhi wa Mazingira kwa Maendeleo Endelevu*** | *112* |
| ***Halmashauri Ya Wilaya Ya Uvinza: Uanzishaji wa Karakana ya Useremala ya Halmashauri Katika Kuboresha Utoaji wa Elimu*** | *120* |
| ***SURA YA NNE: MAENDELEO YA JAMII KIUCHUMI*** | *127* |
| ***Halmashauri Za Wilaya Za Kibondo na Kakonko: Ufugaji Nyuki Wa Kisasa Na Uongezaji Thamani Mazao Ya Nyuki*** | *129* |
| ***Halmashauri Ya Wilaya ya Sumbawanga: Usimamizi Shirikishi wa Skimu ya Umwagiliaji*** | *139* |
| ***Halmashauri Ya Wilaya Ya Nkasi: Uanzishaji Wa Jumuiya ya Wafugaji Kuhimiza Ufugaji Wa Koo Bora za Ng'ombe*** | *147* |
| ***REJEA*** | *154* |

# Vifupisho

| | |
|---|---|
| ADF | Agency Delegated Functions |
| ALAT | Association of Local Authorities In Tanzania |
| AMCOs | Agricultural Marketing Cooperatives |
| ANCO | Amenity Non-Profit Charity Organization |
| BOQ | Bill of Quantitates |
| BTC | Belgium Technical Cooperation |
| CBOs | Community Based Organizations |
| CCM | Chama Cha Mapinduzi |
| CHAWASA | Chama cha Wakulima wa Umwagiliaji Sakalilo |
| CHF | Community Health Fund |
| CMT | Council Management Team |
| COSTECH | Commission for Science and Technology |
| COWSO | Community Owned Water and Sanitation Organization |
| CUGs | Cooperative Union Groups |
| D by D | Decentralization by Devolution |
| DADPs | District Agriculture Development Programme |
| DAWASCO | Dar es Salaam Water Supply Company |
| DIDF | District Irrigation Development Fund |
| DIDFT | District Irrigation Development Facilitation Team |
| DPs | Distribution Points |
| FCS | Foundation for Civil Society |
| GePG | Government e-Payment Gateway |
| GIS | Geographical Information System |
| GPS | Global Positioning System |
| H/W | Halmashauri ya Wilaya |
| INSET | Internal Service Training Programme |
| IRDP | Institute of Rural Development Planning |
| JICA | Japan International Cooperation Agency |
| JKT | Jeshi la Kujenga Taifa |
| KASODEFO | Kawie Social Development Foundation |
| KIKUMUMI | Kikundi cha Kutunza Mazingira na Utafiti wa Miti |
| LANES | Literacy and Numeracy Education Support |
| LAT | Local Allocation Tax Grant |
| LE1 | Local Electricity One |
| LED | Local Economic Development |
| LG | Local Government |
| LGA | Local Government Authority |
| LGRP | Local Government Reform Programme |
| LGTI | Local Government Training Institute |
| MITI | Ministry of International Trade and Industries |
| MVG | Mboni ya Vijana Group |
| NGOs | Non - Governmental Organizations |
| NHIF | National Health Insurance Fund |
| NMB | National Microfinance Bank |

| | |
|---|---|
| **O&OD** | **Opportunities and Obstacles to Development** |
| **OJT** | **On the Job Training** |
| **OR - TAMISEMI** | **Ofisi ya Rais – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa** |
| **OSM** | **Open Street Map** |
| **OVOP** | **One Village One Product Movement** |
| **OWM - TAMISEMI** | **Ofisi ya Waziri Mkuu - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa** |
| **PACF** | **Pan African Competitiveness Forum** |
| **RAS** | **Regional Administrative Secretary** |
| **RBF** | **Result Based Financing** |
| **SACCOs** | **Savings and Credit Cooperative Societies** |
| **SAGCOT** | **Southern Agricultural Growth Corridor of Tanzania** |
| **SAP** | **Structural Adjustment Programme** |
| **SIDO** | **Small Industry Development Organization** |
| **SK** | **Serikali Kuu** |
| **SM** | **Serikali za Mitaa** |
| **SRI** | **System of Rice Intensification** |
| **SUMATRA** | **Surface and Marine Transportation Agency** |
| **TANAPA** | **Tanzania National Parks** |
| **TANESCO** | **Tanzania Electric Supply Company** |
| **TANROADs** | **Tanzania National Roads Agency** |
| **TBS** | **Tanzania Bureau of Standards** |
| **TFDA** | **Tanzania Food and Drugs regulatory Agency** |
| **TFS** | **Tanzania Forest Services** |
| **TOA** | **Tanzania Osaka Local Government Reform Alumni** |
| **TPB** | **Tanzania Postal Bank** |
| **UKI** | **Ushirika wa Wafuganyuki Kibondo** |
| **UKIMWI** | **Ukosefu wa Kinga Mwilini** |
| **UWAMTUSA** | **Umoja wa Umwagiliaji Maji Tujikomboe Sakalilo** |
| **VETA** | **Vocational Educational Training Athority** |
| **VVU** | **Virusi Vya Ukimwi** |
| **WSDP** | **Water Sector Development Programme** |

# Dibaji

Maboresho ya Serikali za Mitaa Tanzania yamelenga katika utoaji bora wa huduma wa Serikali za Mitaa kwa kuzingatia sera za kitaifa za Serikali Kuu. Maboresho yamekaribisha ushirikiano kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, washirika wa maendeleo na wadau wengine tangu awamu ya kwanza hadi sasa. Sera ya Ugatuaji wa Madaraka (D by D) iliwekwa dhahiri mwaka 1998 na utekelezaji wake wa maboresho ya Serikali za Mitaa ulianza mwaka 2000. Kupitia ushirikiano huu maboresho ya Serikali za Mitaa hapa Tanzania yamefanikiwa kuleta Serikali za Mitaa za kidemokrasia, matumizi bora ya raslimali watu, kuongozeka kwa ruzuku toka hazina, kuimarika kwa utawala bora katika Serikali za Mitaa, kuongezeka kwa ushiriki wa wananchi na kwa ujumla kuongezeka kwa uhuru wa Serikali za Mitaa katika utoaji wa huduma.

Maboresho ya Serikali za Mitaa Tanzania yametekelezwa kwa mkakati wa jumla ambao umejumuisha kujifunza jitihada za maboresho na utekelezaji wake katika nchi nyingine, Afrika na kwingineko na kuunda mkakati sahihi wa utekelezaji wake na mbinu mbadala kwa Tanzania. Tangu mwaka 2002 Serikali ya Tanzania kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OWM – TAMISEMI – Wakati huo) na Serikali ya Japani kupitia Shirika la Kimataifa la Maendeleo la Japani (JICA) kwa pamoja wameendesha mafunzo kuhusu Ugatuaji nchini Japani kupitia mafunzo ya Osaka. Mafunzo haya yamehudhuriwa na Wakurugenzi na Watumishi wengine toka OR – TAMISEMI, Makatibu Tawala wa Mikoa, Wakurugenzi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa (MSM) na wadau wengine wa maboresho ya Serikali za Mitaa. Mafunzo haya pia yalitolewa kwa Makatibu Tawala Wasaidizi, Wakuu wa Wilaya, Makatibu Tawala wa Wilaya na wakuu wa idara kupita mafunzo ya mikoa baada ya mafunzo ya Osaka (Reginal Post Osaka Training).

Mafunzo ya Osaka na yale ya Mikoa yametoa fursa kwa watumishi wa Serikali Kuu na Serikali za Mitaa kujifunza uzoefu wa ugatuaji madaraka wa Kijapani, kuchagua mbinu bora za ugatuaji wa Kijapani na kutekeleza mbinu hizo katika Sekretarieti za Mikoa na Serikali za Mitaa. Hili limeibua umuhimu wa kutoa taarifa za utekelezaji wa mbinu hizi bora kupitia kitabu, ili kuzifanya Sekretarieti za Mikoa na MSM kuona na kujifunza utekelezaji na siri zake humuhumu nchini.

Kitabu hiki cha Sita ni mwendelezo wa juhudi za pamoja kati ya OR – TAMISEMI na JICA kuimarisha sera ya ugatuaji wa madaraka Tanzania. Kitabu hiki kinaanza kwa kuonesha historia ya mafunzo ya Osaka na mbinu bora kama ifuatavyo; Sura ya Kwanza inaonyesha kwa ufupi Masuala mazuri yaliyoigwa toka Japani; Sura ya pili inahusu Jitihada za Jamii katika Kuboresha Utoaji wa Huduma ikiwasilisha Mbinu Bora kutoka Halmashauri za Wlaya za Kibaha, Mpimbwe, Tabora, Kasulu na Urambo. Sura ya Tatu inahusu Ushirikishwaji wa Jamii katika Utoaji wa Huduma ikiwasilisha Mbinu Bora kutoka Halmashauri za Manispaa za Mpanda, Sumbawanga na Kigoma Ujiji, Halmashauri ya Mji wa Kibaha na Halmashauri za Wilaya za Kibondo, Mafia, Kaliua na Uvinza. Sura ya Nne inahusu Maendeleo ya Jamii Kiuchumi na inawasilisha Mbinu Bora kutoka Halmashauri za Wilaya za Kibondo na Kakonko, Sumbawanga na Nkasi.

OR – TAMISEMI inashauri watumishi wa Sekretarieti za Mikoa na wa MSM na wadau wote wa maboresho ya Serikali za Mitaa Tanzania kusoma kitabu hiki, kufahamu jitihada za ndani, kujifunza siri za mafanikio na kutumia fursa zilizopo kwenye maeneo yao kuonesha utendaji mzuri katika mazingira ya ugatuaji wa madaraka.

-------------------------------------------------

**Mhandisi Mussa Iyombe**
**KATIBU MKUU**
**OR-TAMISEMI**

# Utangulizi (TOA)

Kitabu cha Mbinu Bora cha Sita ni matokeo ya jitihada za pamoja za Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia OR – TAMISEMI na Serikali ya Japani kupitia JICA tangu mwaka 2002 kwa kuendesha mafunzo huko Osaka na mafunzo baada ya Osaka katika kila Mkoa juu ya uzoefu wa Ugatuaji Madaraka huko Japani. Mafunzo haya yalitoa fursa kwa watumishi wa Sekretarieti za Mikoa, MSM na wadau mbalimbali wa maboresho hapa Tanzania kujifunza uzoefu wa Kijapani kuhusu Ugatuaji katika maeneo ya Utawala katika Serikali za Mitaa na Usimamizi wa Raslimali Watu, Ugatuaji wa Masuala ya Fedha na Uboreshaji wa Mapato, Upangaji na Utoaji Huduma Shirikishi na Maendeleo ya Kiuchumi katika MSM hasa kupitia wimbi la OVOP. Masuala mazuri yaliyoigwa yametekelezwa katika Sekretariati za Mikoa na MSM nyingi kwa lengo la kuboresha utoaji huduma kwa jamii ndani ya sera ya ugatuaji, yaani "D by D". Mbinu Bora nyingi za utekelezaji zimeonyesha mafanikio na matokeo chanya kwa jamii. Kamati ya Utendaji ya TOA imeamua kutoa Mbinu Bora ambazo zimewasilishwa kwenye toleo hili la tano. TOA itaendelea kutoa matoleo mengine ya kitabu hiki siku za mbele sambamba na utekelezaji unaondelea wa Masuala mazuri yaliyoigwa kwenye mafunzo ya Osaka na yale ya Mikoa.

Kukamilika kwa kitabu hiki cha Sita cha Mbinu Bora kumetokana na misaada kutoka taasisi na watu binafsi mbalimbali. TOA inapenda kutambua na kutoa shukrani kwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Ofisi ya Rais- Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwa kufikia makubaliano na Serikali ya Japani, kufadhili na kuruhusu watumishi wa Tanzania kuhudhuria mafunzo ya Ugatuaji nchini Japani toka mwaka 2002 hadi sasa. Pili, TOA inaelekeza shukrani za dhati kwa Serikali ya Japani na JICA kwa kuandaa, kusaidia na kufadhili mafunzo ya Osaka na Mafunzo ya Mikoa na uzalishaji wa kitabu hiki. TOA pia inapenda kutambua na kushukuru juhudi za utekelezaji wa yale yaliyojifunzwa za Makatibu Tawala wa Mikoa na Wakurugenzi wa MSM na utayari wao wa kuandika Mbinu Bora kamilifu kama zinavyoonekana kwenye kitabu hiki.

Uchambuzi na uunganishi wa Mbinu Bora zilizopo kwenye kitabu hiki ulifanywa na Bwana Paulo F. Faty (Mhadhiri - Chuo Kikuu Mzumbe) na Bwana Ahmed Nassoro (Mhadhiri Msaidizi - Chuo cha Serikali za Mitaa – Hombolo), pia Masuala yaliyoigwa Japani yamechambuliwa na Bwana Michiyuki Shimoda (Mshauri Mwandamizi, OR – TAMISEMI). TOA inapongeza kwa dhati mchango wao na inawashukuru sana.

Mwisho TOA inapenda kuwashukuru watumishi wote wa OR – TAMISEMI, JICA na TOA kwa kushiriki katika mikutano mbalimbali iliyoboresha na kuunda kitabu hiki. Siyo rahisi kutaja wote waliochangia katika kazi hii, hata hivyo TOA inaheshimu michango yote iliyotolewa na Taasisi na Watu mbalimabali.

Mwisho kabisa, ingawa Watu na Taasisi nyingi zimechangia katika kitabu hiki, TOA na timu ya uchambuaji wanawajibika kwa makosa na mapungufu yanayoweza kuhisiwa na wasomaji wa kitabu hiki.

-------------------------------------------------------

**MUSSA NATTY**
**MWENYEKITI WA TOA**

# Utangulizi (JICA)

Wasomaji Wapendwa!

Utekelezaji wa sera ya Ugatuaji wa Madaraka (D by D) umechukua zaidi ya miaka 10 sasa ukiwa na lengo la kuboresha huduma kwa kugatua shughuli, majukumu na raslimali toka Serikali Kuu kwenda Serikali za Mitaa.

Kutokana na ukweli huu hapo juu Shirika la Kimataifa la Maendeleo la Japani (JICA) limejikita katika kusaidia utekelezaji wa sera hii hasa katika kuimarisha utoaji huduma katika ngazi za msingi kwa kujenga uwezo wa Mamlaka za Serikali za Mitaa ikiwa ni pamoja na maendeleo ya sekta za afya, kilimo, maji na barabara.

Toka mwaka 2002, JICA kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR – TAMISEMI) imekuwa ikiendesha mafunzo kuhusu maboresho katika Serikali za Mitaa yanayoitwa "Osaka Training". Mafunzo haya yalilenga Maofisa wa juu wa Menejimenti katika maboresho ya Serikali za Mitaa, yaani Makatibu Tawala wa Mikoa, Wakurugenzi wa MSM, Maofisa wa OR – TAMISEMI na Vyuo vya Elimu ya Juu kwa malengo ya kujifunza uzoefu wa Kijapani katika maboresho ya Serikali za Mitaa. Katika kurudi kwao, waliwasilisha na kujadiliana uelewa na uzoefu walioupata kwenye warsha za mafunzo za mikoa (2003 – 2007). Matokeo yake Umoja wa Makatibu Tawala na Wakurugenzi wa MSM (TOA) ulianzishwa ili kuwa na jukwaa ambalo wajumbe wa TOA wanapata fursa ya kubadilishana uzoefu, mbinu bora na changamoto zilizopo. JICA imekuwa ikisaidia uimarishaji wa taasisi ya TOA.

Kutokana na utekelezaji wa Masuala yaliyoigwa kwenye mafunzo ya Osaka, mbinu bora nyingi ziliwasilishwa na Mamlaka za Serikali za Mitaa katika warsha za Mikoa zilizofanyika katika kanda sita mwaka 2011/12. Baada ya uhakiki na uchambuzi wa mbinu hizi bora, toleo la kwanza, la pili, la tatu, la nne na hili la tano la "kitabu cha mbinu bora" hatimaye limetoka. Kitabu hiki kinathibitisha kuwa ***"tunatakiwa kujifunza siyo tu kutoka nchi nyingine bali katika jitihada nyingi zilizopo ndani ya nchi".***

Nitafurahi kama mtajifunza vipengele muhimu kutoka kitabu hiki na kuchukua hatua ndogo lakini za uhakika ili kuboresha utendaji katika eneo husika.

JICA ina mpango wa kuisaidia TOA kuendesha mafunzo ya Watumishi wa Sekretarieti za Mikoa na Wakuu wa Idara katika Mikoa yote kwa kutumia vitabu hivi. Tungependa kufuatilia na kujua mbinu bora zitakazofuata zilizotokana na kitabu hiki na mafunzo yake. Tunatarajia kuanzisha jukwaa la kujifunza wenyewe kwa wenyewe (Horizontal Learning) katika ngazi za Msingi.

**------------------------------------------------------------**

**Toshio Nagase**

***Mwakilishi Mkuu – Ofisi ya JICA Tanzania***

# Sura ya Kwanza

# Utangulizi; Masuala Yaliyoigwa Kutokana na Uzoefu wa Japani

### 1.0 MAFUNZO YA OSAKA

Kitabu hiki kimeandaliwa na Umoja wa Washiriki wa Mafunzo ya Osaka kuhusu Serikali za Mitaa wanatoka Tanzania (TOA). TOA ni Umoja wa washiriki wa kozi inayotolewa na Shirika la Kimataifa la Maendeleo la Japan (JICA). Mafunzo yenyewe yanaitwa "Mafunzo yenye Mrengo wa Nchi – Programu ya Maboresho ya Serikali za Mitaa Tanzania", lakini yajulikanayo sana kama "Mafunzo ya Osaka". Umoja una wanachama ambao ni Makatibu Tawala wote wa Sekretarieti za Mikoa na Wakurugenzi wote wa Halmashauri nchini.

Mafunzo ya Osaka yalianza mwaka 2002. Kipindi cha miaka mitano ya mwanzo, Makatibu Tawala wote kutoka Mikoa 21 (kipindi hicho) pamoja na Wakurugenzi wa Halmahauri wawili kutoka kila Mkoa walihudhuria. Pia maofisa wa juu toka OWM – TAMISEMI (wakurugenzi na wakurugenzi wasaidizi)[1], Katibu Mkuu wa ALAT na baadhi ya wanataaluma mashuhuri walihudhuria kozi hii.

Kutokana na mafanikio na matokeo dhahiri, JICA iliamua kuendelea na mpango huu, kwa kupanua wigo wake kwa kuongeza nchi nyingine tatu za kiafrika ambazo zilikuwa zikipanga maboresho ya ugatuaji, yaani Kenya, Uganda na Zambia, pamoja na Tanzania. Mpaka leo zaidi ya viongozi 100 wa maboresho wanaojumuisha Makatibu Tawala wa Mikoa na Wakurugenzi wa Halmashauri wamefaidika moja kwa moja na mafunzo ya Osaka. Pia washiriki hawa waliporudi katika mikoa yao waliendesha warsha za ndani zijulikanazo kama "mafunzo ya Post Osaka" ili kubadilishana uzoefu na uelewa walioupata Osaka kwa kuwaalika Wakurugenzi waliobaki pamoja na wakuu wa idara. Hivyo wafaidika wa mafunzo haya waliongezeka mpaka kufikia zaidi ya 1,500, ingawa uanachama wa TOA ulibakia kuwa wa Makatibu Tawala wa Mikoa na Wakurugenzi wa Halmashauri.

Kutoka katika Masuala mbalimbali yaliyoigwa Osaka na mafunzo ya Post Osaka, Halmashauri zilizohudhuria ziliandaa mipango kazi ya kuboresha utendaji wao. Kukiwa na zaidi ya miaka 10 ya utendaji, imethibitishwa kuwa kuna idadi kubwa ya mbinu bora zinajitokeza katika Halmashauri nyingi kwa kutekeleza ile mipango kazi ambayo ni vyema kuwashirikisha wengine.

[1] Pamoja na Makatibu wakuu wawili wa Zamani wa OWM-TAMISEMI, yaani, MS. Tarishi M.K. na Bwana H.A. Katanga

Kwa hiyo TOA iliamua kuhakiki na kuchambua kesi hizo za mbinu bora na kutengeneza kitabu hiki, ili viongozi wa Halmashauri waweze kuzirejea kesi hizi na kuzitumia pale wanapoona zinafaa na zina tija, katika kuboresha kazi zao.

Kabla ya kuingia kwenye kesi zenyewe za mbinu bora, ni vyema katika sura hii tukaangalia kwa nini JICA iliamua kutoa mafunzo haya kwa viongozi wa maboresho wa kitanzania, nini ilikuwa maana ya mafunzo ya Osaka kwa Tanzania na Masuala gani yalijadiliwa kwenye mafunzo haya.

## 2.0 HISTORIA YA MAFUNZO YA OSAKA

Kwa nini JICA iliamua kutoa mafunzo haya? Na yalikuwa na maana gani kwa Tanzania?

### 2.1 Maoni ya JICA Kuhusu Msaada kwenye Ugatuaji

JICA ina maoni ya kipekee kuhusu misaada kwenye utawala ambayo yanaweza kutofautiana na maoni ya washirika wengine wa maendeleo. JICA imeshuhudia programu kubwa kubwa za maboresho zikifanywa katika nchi zinazoendelea na washirika wa maendeleo kama Programu wa kurekibisha Miundo ya Uchumi (SAPs) na maboresho ya utawala ikiwa ni pamoja na Ugatuaji wa madaraka. Inaweza kusemwa kuwa programu hizi na maboresho haya yaliyofanywa katika nchi zinazoendelea ni sawa kabisa na yale yanayojaribiwa sasa katika nchi zilizoendelea bila kujali tofauti iliyopo ya kihistoria na mazingira kati ya nchi hizi. Pia mara kwa mara inajidhihirisha kuwa maboresho haya yanatekelezwa kwa msukumo mkubwa toka kwa wafadhili, bila kuzingatia asili ya mchakato wa maendeleo na umiliki wa nchi husika.

Kutokana na machungu ya kushindwa kufikia malengo katika ushirikiano wa kimataifa wa aina hii, JICA imekuwa na msimamo ufuatazo katika kusaidia ugatuaji.

(i) Hakuna mfumo wowote unaoweza kutumika katika nchi zote.
(ii) Ugatuaji wenyewe siyo lengo bali ni njia ya kufikia lengo fulani.
(iii) Kuasilisha na kukuza mfumo ndani ya nchi kupitia majadiliano ya kitaifa ni muhimu.
(iv) Jinsi gani ya kuhakikisha viwango vya chini vya kitaifa vya huduma[2] vinafikiwa ni muhimu katika kuandaa maboresho ya Ugatuaji.
(v) Maboresho ya Ugatuaji ni mchakato mrefu, ambao hautakiwi kuchukuliwa kama Mradi au Programu tu.
(vi) Maboresho ya Ugatuaji ya haraka haraka yanaweza kuleta fujo. Katika kila maboresho ya Ugatuaji (d by d), ni lazima kuhakikisha kuna mazingira sahihi kwa upande wa Halmashauri na wanajamii kupokea majukumu makubwa yanayogatuliwa.

## 2.0 Changamoto Kubwa Iliyogunduliwa katika Programu ya Tanzania ya Maboresho ya Serikali za Mitaa na Ujumbe wa Maandalizi ya Mafunzo wa Mwaka 2002

[2] Viwango vya chini vya kitaifa vya huduma ni nadharia kuwa kiwango fulani cha huduma lazima kifikiwe hata kama ni katika jamii maskini vijijini sawa na kwenye miji mikubwa.

Baada ya maombi ya Serikali ya Tanzania kuhusu kuwepo kwa Mpango wa mafunzo wa maboresho katika serikali za mitaa mwaka 2001, JICA iliamua kutuma ujumbe kwenda kuchambua hali ilivyo ili kuunda kozi ya mafunzo yenye maudhui ya kumaliza Masuala muhimu. Ujumbe ule ulipofika Tanzania, Novemba mwaka 2002, uligundua kuwa Programu ya maboresho ya Serikali za Mitaa Tanzania ilikuwa na changamoto zifuatazo;

(i) Jedwali kubwa na lenye hatua nyingi za utekelezaji (zaidi ya kurasa 80)
(ii) Programu ya maboresho ilikuwa ukitekelezwa kwa jedwali zuri sana lakini halikuruhusu maboresho/mabadiliko zaidi. Ujumbe uliona kulikuwa na nafasi ndogo sana iliyoachwa ya kuweza kubadili lolote ili kuruhusu majaribio ya suala ambalo ni muhimu. Ujumbe uliona kuwa kila kitu kimeshadhamiriwa, na Serikali ya Tanzania ililazimika kufuata reli hiyo bila kwenda pembeni au kurudi vyuma.
(iii) Programu iliandaliwa kwa msaada mkubwa kutoka kundi la wafadhili.
(iv) Wafadhili wa kawaida waliopo kwenye mfuko "Basket funding" waliunda kamati ya msukumo pamoja na serikali. Kuandikwa kwa Programu yenyewe kulifanywa na wataalamu washauri wa nje na hata utekelezaji wenyewe. Ujumbe ulihofia kuwa Programu ya maboresho iliandaliwa bila kupitia mchakato stahiki wa kujenga uelewa ndani ya nchi na kupata makubaliano yanayohusu mahitaji ya mabadiliko.
(v) Hatari ya kukimbilia kwa haraka Ugatuaji wa Madaraka (D by D).

Sera ya ugatuaji (D by D) iliyokuwa ikihamasishwa na Serikali ilidhihirika kwenye ujumbe huo kuwa ni kama vile Tanzania ilikuwa inatekeleza ugatuaji wa madaraka sawa na ule wa nchi zilizoendelea. Swali likawa; Je ni kweli uwezo na mtazamo wa Halmashauri na Wizara zote ulikuwa tayari kwa mabadiliko haya ya haraka? Ujumbe huu uliaona changamoto zifuatazo katika hili;

- Upinzani kutoka Wizara za kisekta
- Ukosefu wa majadiliano ya kina kuhusu ugatuaji katika jamii
- Hakukuwa na uwezo kamilifu kwa upande wa Halmashauri kuchukua majukumu yote yaliyogatuliwa

### 2.3 Uwezekano wa Umuhimu wa Uzoefu toka Japani katika Ujenzi wa Taifa na Maboresho ya Ugatuaji - Ujumbe kutoka Japan kwenda Tanzania kupitia Mafunzo ya Osaka.

Baada ya kuona hali halisi ya Tanzania iliyoelezewa hapo juu, JICA iliamua kuwa uzoefu wa Japani kwenye ujenzi wa Taifa na Maboresho yaliyokuwa na mchakato wa muda mrefu ya Ugatuaji ungeweza kuwa unastahili na muhimu kwa viongozi wa maboresho wa Tanzania kujifunza na kupitia upya maboresho yao.

Japani ni nchi ndogo huko Bara la Asia isiyo na ustaarabu wa Magharibi, ambayo ilianza ujenzi wa taifa kama nchi iliyo nyuma kabisa lakini ikafikia maendeleo ya ajabu. Japani ina uzoefu mwingi wa aina yake wa kutumia mifano (models) ya nje (mfano wa Magharibi) ambayo wafadhili wengine hawana. (Mataifa ya Ulaya yamekuwa mara zote mstari wa mbele na katikati ya dunia na hujiona hayana sababu ya kujifunza toka nje). Kwa kweli, Japani ilianza

Ujenzi wa taifa na maendeleo, kwa kujaribu kuiga mifano ya Magharibi lakini ikashindikana mwanzoni kabisa. Tokea hapo ikawa ni mchakato mrefu wa kujaribu na kushindwa mpaka hatimaye ilipofikia Japani ikaunda mfumo wake wa kipekee unaoitwa "Nusu kijapani nusu Magharibi". Japani inaamini kuwa aina hii ya uanzishaji wa mfumo, pamoja na umiliki wake thabiti kupitia kujaribu na kushindwa mara nyingi ni muhimu sana kwa maendeleo endelevu ya nchi.

Mchakato huu ambao Japan ilitumia ili kuanzisha mfumo wake wa serikali za mitaa na maboresho ya Ugatuaji ni tofauti kabisa na mifano ya Ulaya ambayo nchi zinazoendelea zinajaribu kuanzisha kwa sasa. JICA ilifikiri kuwa kuwasilisha "mfumo huu tofauti" unaweza kuwa muhimu, kwani kuwa na mfano mmoja tu, inaonekana kama vile "ndio njia pekee" hakuna nyingine. Lakini kukiwa na mifano zaidi ya miwili, wanaweza wakaanza kulinganisha na kuona ni mfano upi unafaa zaidi katika mazingira yao, na ni hatua ipi iwe ya kwanza katika kuandaa mfumo wao wenyewe.

Ifuatayo ni mifano tu ya kuvutia ya vigezo vinavyoweza kuigwa toka mfumo wa kijapani kati ya mengi yaliyopo;

**(1) Mchakato wa Maboresho wa Polepole Sana Lakini wa Uhakika**

Japani ilitumia miaka 110 toka ilipoanza kuunda mfumo wa Serikali za Mitaa na Ugatuaji; ingawa tunahesabu miaka 55 ya Maboresho Makuu baada ya Vita Kuu ya Pili ya Dunia hadi kufika ugatuaji halisi (D by D) mwaka 2000. Serikali ilijaribu kuhakikisha kuwa Halmashauri zimeshajengewa uwezo wa kutosha kabla ya kugatua majukumu, na siyo kukimbilia kurekebisha taasisi za Ugatuaji (D by D). Uzoefu huu wa Japani unaipa Tanzania fursa ya kufikiria mara mbili kama mwendo wa maboresho siyo kasi sana, na kama nchi inataka kuendelea na mwendo kasi uliopo, basi haina budi kuhakikisha kuna ujenzi wa uwezo stahiki kwa upande wa Serikali za Mitaa.

**(2) Ukasimishaji wa Shughuli/Majukumu kwa Wakala (Agency Delegated Functions)**

Katika kipindi tajwa cha miaka 55, serikali ilichagua mfumo wa "kukasimu" unaoitwa ADF kama hatua ya mpito, badala ya kurukia Ugatuaji moja kwa moja. Kwa sababu ya mfumo huu Japani ilipingwa sana na nchi za Magharibi kwa kipindi kirefu kuwa haijafanya Ugatuaji sahihi, na mwishoni kabisa Serikali ikaamua kuingia katika Ugatuaji halisi mwaka 2000 na kuondokana na mfumo wa kukasimu (ADF). Hata hivyo sasa hivi imethibitika kuwa ADF ilichangia kwa kiasi kikubwa kukua kwa mfumo mzuri wa Serikali za Mitaa na kupelekea kufikiwa kwa ugatuaji halisi (D by D) nchini Japani; hasa katika vipengele vifuatavyo;

- Shukrani kwa ADF, Halmashauri zilifanya kazi kwa ushirikiano wa karibu na Wizara husika, na zikaweza kujenga uwezo wao kupitia mafunzo kazini (on the job training) kukiwa na usaidizi wa kitaalamu wa karibu toka wizarani. Kila walipopata changamoto, maofisa wa Serikali za Mitaa waliweza kuwasiliana na maofisa wa wizara husika kwa simu na maofisa wa wizara waliweza kusaidia kwa wema na kumaliza changamoto hizo pamoja. Haya yote yaliwezekana kwa sababu kimsingi shughuli zote zilikuwa ni wajibu wa Wizara na zilikasimishwa tu kwa Halmashauri. Hivyo hakukuwa na upinzani wowote

toka wizarani, zaidi ya ushirikiano ilipofikia Ugatuaji wa shughuli; kinyume kabisa na yanayotokea katika nchi zinzoendelea zinapotekeleza ugatuaji.

- Hoja ya msingi ilikuwa ni kuhakikisha kuwa raslimali ambazo ni chache zilizopo ndani ya nchi zinaweza kutumika vizuri zaidi kuelekea upande mmoja yaani maendeleo ya nchi, badala ya kuzigawa na kutengeneza tofauti kati ya Serikali Kuu na Serikali za Mitaa.
- Ilikuwa ni muhimu sana katika hatua za mwanzo ambapo Mamlaka za Serikali za Mitaa zilikuwa na uwezo dhaifu. Bila mfumo wa kukasimu (ADF) kipindi hicho Halmashauri zisingeweza kufanya vizuri shughuli zao za kuhudumia watu wala uwezo wao usingejengeka.
- Sababu nyingine muhimu ilikuwa mafunzo kazini (OJT). Shukrani kwa mchakato wa mafunzo kazini (OJT), kwa miaka 55, watumishi wote wa Serikali za Mitaa pamoja na muundo wao kwa ujumla walijenga uwezo thabiti, kwa kupokea ufahamu na utaalamu kutoka wizarani, na kuwa tayari Serikali Kuu ilipoamua kugatua madaraka (D by D).

Uzoefu huu wa Japan unaleta swali moja la msingi kwa Tanzania juu ya namna gani nchi inaweza kujithibitishia uhakika na ubora wa mchakato wa kuzijengea uwezo Halmashauri ilihali Ugatuaji (D by D) ukiendelea; kuhakikisha matumizi mazuri ya raslimali chache zilizopo nchini na kukwepa kabisa upinzani toka Wizara za kisekta.

**(3) Mfumo wa Kubadilishana Watumishi kati ya Serikali Kuu na Serikali za Mitaa**

Nchini Japani, kipindi cha hatua za mwanzo za maboresho, mtindo wa kubadilishana watumishi kati ya Serikali Kuu na Serikali za Mitaa ulitumika sana kama mbinu bora kabisa ya (a) kujaza upungufu wa watumishi hasa wenye sifa katika Halmashauri za pembezoni na (b) kuhakikisha uhamishaji wa ujuzi na utaalamu kutoka kwa wasomi wa Wizara kwenda kwa watumishi wa Halmashauri waliokuwa na ujuzi na uzoefu mdogo ili kujenga uwezo wa Halmshauri hizo.

Serikali iliunda jopo kubwa la maofisa wataalamu katika wizara ya Serikali za Mitaa na kuwapeleka kwenda kwenye Halmashauri zilizokuwa na uwezo mdogo huko pembezoni ili kuzisaidia. Hatua hii ya uhamisho wa muda ilidumu kwa muda wa miaka 4 - 5 na baadaya watumishi hawa walirudishwa kwenye nafasi zao za kawaida kwenye wizara zao. Kadri walivyokuwa na uwezo wa kitaalamu kuwezesha wengine ndivyo walivyopelekwa kwenye Halmashauri za mbali na zenye udhaifu mkubwa. Pale walipofaulu na kutenda vizuri katika vituo hivi vipya, waliahidiwa kupanda vyeo zaidi wanaporudi, ambayo iliwapa motisha wataalamu hawa waliobobea kwenda kwenye sehemu zisizovutia kwa hamasa ya juu kabisa. Pia Halmashauri nyingi zilipeleka watumishi wao kwenye wizara mbalimbali kufanya kazi, katika misingi ya mafunzo kazini kwenye maeneo ambayo Halmashauri husika ilihitaji.

Baada ya kurudia mizunguko kadhaa ya kubadilishana watumishi, ujuzi na utaalamu wa kutosha ulihamishwa kikamilifu toka Wizara kwenda Halmashauri, kitu ambacho kilisaidia sana kujenga uwezo wa Halmshauri nchini Japanni. Sasa Halmashauri zinajitegemea katika raslimali watu bila kuitegemea Serikali Kuu tena.

Nidhahiri kuwa ugatuaji wa raslimali watu ukifanyika kwa ukamilifu wake bila kuwa na mbinu za kutatua matatizo, hupelekea upungufu mkubwa wa watumishi kwenye Halmashauri ambazo zipo katika maeneo maskini na pembezoni. Ni kwa sababu hii Tanzania iliamua kurudisha Masuala ya raslimali watu kwa sehemu kubwa Serikali Kuu. Hata hivyo haina mantiki kuendeleza Ugatuaji wa madaraka (D by D) bila Ugatuaji halisi wa raslimali watu. Badala ya "0 au 100", serikali inatakiwa kutafuta mkakati wa namna ya kugatua raslimali watu na wakati huohuo kukwepa kutengeneza upungufu katika maeneo ya vijijini, na kujiridhisha kuwa kuna mchakato wa kujenga uwezo wa baadaye wa Halmashauri.

## 3.0 MASUALA YALIYOJITOKEZA NA KUJADILIWA WAKATI WA MAFUNZO YA OSAKA

Kutokana na upungufu wa nafasi Masuala machache tu ya msingi yameweza kuwasilishwa kwenye sehemu hiyo hapo juu, kati ya mambo mengi yanayotokana na uzoefu wa Japani ambayo Tanzania imepewa. Hapa vipengele vingine vitatajwa na kuelezewa kwa kifupi.

### 3.1 Masuala ya Jumla

Masuala na Maswali yafuatayo yalijitokeza na kujadiliwa wakati wa mafunzo ya Osaka:

**(1) Umuhimu wa kukuza uwezo wa Mamlaka za Serikali za Mitaa kama kigezo cha mafanikio ya Ugatuaji wenyewe**

- Je hakuna hatari ya kudidimiza utoaji huduma, kugatua wajibu mkubwa kiasi hiki ndani ya muda mfupi?
- Ni namna gani ya kukabiliana na hali halisi kuwa Halmashauri zinahitaji uwezo zaidi ili kutekeleza shughuli zilizogatuliwa?
    - Vipi kuhusu ajira? Namna gani itawezekana kupata watumishi wenye sifa katika Halmashauri zilizopo kwenye maeneo maskini na pembezoni?
    - Ni jinsi gani ya kuziba pengo kati ya ujuzi na utaalamu katika Serikali za Mitaa na kuziendeleza? Je siyo muhimu kwanza kuweka mbinu za kuhamisha ujuzi na utaalamu, pamoja na usaidizi wa kitaalamu kutoka serikali kuu kwenda Halmshauri? Siyo muhimu kwanza kuimarisha mahusiano ya ushirikiano kati ya Serikali Kuu na Halmashauri badala ya kutegemea misaada toka nje?

**(2) Ugatuaji na Maendeleo**

- Ili kuweza kuleta maendeleo ya kijamii na kiuchumi ya nchi na kwa raslimali chache zilizopo, ni muhimu kutafuta mbinu mkakati ya kuzitumia raslimali hizi (hivi ndivyo ambavyo Japani imekuwa ikifanya kujiletea maendeleo yake)
- Namna gani unaweza kusimamia maendeleo ya nchi na ugatuaji kwa pamoja wakati mara kadhaa hupingana? Unawezaje kujiridhisha kuwa hakutakuwa na utengano wa raslimali na tofauti (kutokuelewana) kati ya Serikali Kuu na Halmashauri au kati ya Halmashauri zenyewe?

**(3) Ugatuaji na Viwango vya chini vya kitaifa**

- Jinsi gani ya kusimamia ugatuaji na kuzingatia viwango vya chini vya kitaifa? Ni jinsi gani itahakikishwa kuwa Halmshauri zilizopo vijijini zitakuwa na uwezo wa kutosha

kama zilivyo zile tajiri katika kigezo cha utoaji huduma kwa watu? (uwezo wa watumishi na fedha).

**(4) Ukweli Kuhusu Uwezo wa Halmashauri kuweza Kutoa Huduma**

- Swali liliulizwa; Ni Maofisa Ugani wangapi waliopo katika Halmashauri ukijumuisha na wale ambao wanatumikia katika kata na vijiji? Swali hili liliulizwa kwa washiriki ili kuwafanya waelewe hali ilivyo mbaya ambayo Halmashauri za Tanzania zinatakiwa kukabiliana nayo. Ukichukua Mkoa mmoja kama mfano, Mkoa wa Nagano nchini Japani, ni mkoa mdogo kabisa ulioko maeneo ya vijijini lakini una maofisa ugani wa kilimo wapatao 1500. Pia kuna Halmshauri 77 za ngazi za chini katika Mkoa huu ambazo kila moja inaajiri maofisa ugani kati ya 20 – 30. Maana yake kuwa wakulima katika Mkoa (prefecture)[3] wa Nagano wanafurahia huduma zinazotolewa na zaidi ya maofisa ugani 3,000 wa Halmshauri ikilinganishwa na wakulima wa Tanzania ambao wana maofisa ugani wasiozidi 100[4]. Pia nchini Japani kuna mashirika mengi ya binafsi yanayouza mashine za kilimo, mbolea, madawa, mbegu n.k pamoja na taasisi za ushirika zilizo imara; zote hizi hutoa huduma mbalimbali za ugani na ushauri wa kitaalamu.
- Ni vyema kutambua hali ngumu iliyoelezewa hapo juu na kuanzisha mkakati mpya. Hatutakiwi kuota ndoto kwamba Tanzania inaweza kufikia kutoa huduma nzuri kama za nchi zilizoendelea kwa idadi ndogo hivi ya watumishi kwenye eneo lote hata kama Serikali Kuu itaamuwa kufanya kila kitu peke yake.

**(5) Umuhimu wa Juhudi za Wananchi na Ushirikiano kati ya Halmashauri na Jamii**

- Kutokana na Ukweli ulioongelewa hapo juu, haikwepeki kutumia kwa kiasi kikubwa Uwezo wa watu na Juhudi za kujitegemea ili kutoa huduma zilizo bora.
- Ni imani ya JICA kuwa kama watu wataongozwa na kuwezeshwa vizuri, wana uwezo wa kufanya mambo mengi wenyewe, kama kujenga shule za msingi, zahanati, barabara zao na kuzitunza.
- Kwa Japani pia, kipindi cha hatua za mwanzo za Maendeleo, Serikali haikuwa na uwezo wa kujenga shule za msingi. Kwa mfano, ilikuwa ni watu katika jamii zao waliochangia kutoka mifukoni mwao na wakafanya kazi pamoja kujenga na zaidi wakatafuta watu wanaoweza kufundisha na wakawalipa mishahara yao. Ndiyo maana shule nyingi za kipindi hicho hazikuwa za “umma” bali “binafsi”, kwa maana ya “shule zinazomilikiwa na jamii; ilikuwa ni baada ya miongo kadhaa, serikali ilipotajirika na ikaanza kuzimiliki na hatimaye kuwa shule za umma.
- Inahitaji mabadiliko ya mtazamo wa Serikali na Watu, kutoka fikra kuwa ni jukumu la Serikali kutoa huduma zote kwa watu kuelekea mtazamo kuwa watu wanaweza kufanya

---

[3] Mkoa (prefecture) huko Japani ni karibu sawa na wilaya za Tanzania kwa ukubwa wa eneo. (Ingawa Wilaya nyingine za Tanzania ni kubwa sana kuliko Mikoa ya Kijapani).

[4] Pia si kwamba Japani ina hali nzuri katika maana hii. Kinyume chake, Japani ni nchi ambayo ina idadi ndogo kabisa ya watumishi kwa idadi ya watu waliopo ikilinganishwa na nchi zilizoendelea. Maana yake ni kuwa Uingereza, Ufaransa, Ujerumani, Italia n.k wana watumishi wengi zaidi wa serikali.

mengi sana kwa juhudi zao wenyewe na serikali ikawezesha tu mchakato huo badala ya Serikali kutekeleza peke yake.

**(6) Umuhimu wa Kuainisha Ukubwa Sahihi wa Sehemu za Serikali za Mitaa; na Kuunda Mbinu Mpya za Kuzifikia Jamii kutoka makao makuu ya Halmashauri**

- Kutokana na vigezo hivyo hapo juu ni lazima kuunda mbinu imara sana za Halmashauri kuzifikia jamii. Hapa Tanzania, Halmashauri za Wilaya ni kubwa mno, hivyo ni muhimu kufikiria jinsi ya kujenga daraja kati ya Halmashauri na jamii.
- Kutoka kwenye wazo la kukuza mtazamo wa watu kuwa na uhuru wao, eneo la Halmashauri linatakiwa kuwa dogo sana ili watu waweze kuona kuwa sehemu hiyo kweli ni yao. Kwa upande mwingine sehemu hii ndogo ya Serikali za Mitaa inatakiwa iwe na uimara wa kutosha kutoa huduma za kutosha ambayo inahitaji kiasi cha raslimali fedha na watu. Haya ni mahitaji muhimu mawili yanayopingana.
- Kuweza kutoa majibu kwa swali hili hapa juu linalojipanga lenyewe, sahihisho lililopo ni kuwa na mfumo wenye ngazi nyingi kutoka Halmashauri hadi jamii. Kwa Japani mfumo huu wa ngazi nyingi unafanya kazi vizuri. Lakini Tanzania pia ina mfumo mzuri wenye wilaya – kata – kijiji – kitongoji. Hii inasaidia sana kukuza uhuru wa jamii na jitihada shirikishi za maendeleo kati ya Halmashauri na jamii. Zaidi ya hayo, Mfumo wa Upangaji Mipango Shirikishi Jamii (O&OD) unaweza kuwa jukwaa zuri zaidi la kuboresha mfumo huu na kuuwezesha kufanya kazi vizuri zaidi.

### 3.2 Usimamizi na Ugatuaji wa Raslimali Watu

Kama ilivyo kwenye sehemu iliyotangulia, mafunzo ya Osaka yalitoa tahadhari kwa Viongozi wa Tanzania katika miaka michache ya mwanzo kuwa waangalifu kuhusu kutoharakisha kugatua na kupeleka madaraka maarufu kama *D-by-D*. Hata hivyo, kuhusu ugatuaji wa masuala ya rasilimali watu, ujumbe ulikuwa tofauti kidogo kwa vile ilionekana kwamba madaraka haya yalikwisha anza kurudishwa Serikal Kuu; kwani uteuzi wa Wakurugenzi wa Halmasahuri na Wakuu wa Idara unafanywa na Wizara pamoja na kuanzishwa kwa Sekretarieti ya Ajira ili kuendesha mchakato wa ajira kwa kada nyingine za watumishi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Nchi ya Japani haikugatua madaraka na kuyapeleka Halamashauri kwa haraka, bali Serikali Kuu ilendelea kuhodhi baadhi ya shughuli. Kwa mantiki hii, ugatuaji nchini Japani haukuwa umekamilika kwa miaka mingi mpaka ilipofika mwaka 2000. Hata hivyo, kuhusiana na kugatua masuala ya usimamizi wa rasilimali watu, Japan ilihakikisha kwamba madaraka haya yamegatuliwa na kupelekwa Halmashauri kikamilifu tangu mwanzo kabisa wa maboresho.

Hii ni kwa sababu kugatua masuala ya usimamizi wa rasilimali watu ndiyo jambo la muhimu sana na msingi wa ugatuaji. Kulingana na mfumo wa Serikali za Mitaa Japani, masuala yote huamuliwa na kutekelezwa ndani ya Mamlaka za Serikali Mitaa husika bila kuingiliwa na Serikali Kuu, yaani kuajiri na kufukuza, kuendesha mafunzo, kupanga ngazi za mishahara, kufanya uhamisho, kupandisha vyeo, mpaka kustaafu. Mamlaka za Serikali za Mitaa Japani huajiri wahitimu wapya kutoka vyuo vikuu kila inapofika mwezi Aprili kulingana na mahitaji yao. Wahitimu walioajiriwa na Mamlaka fulani ya Serikali za Mitaa, wataitumikia Mamlaka husika

kwa maisha yao yote mpaka watakapostaafu. Hakuna kanuni ya uhamisho kutoka Mamlaka moja ya Serikali za Mitaa kwenda mamlaka nyingine.

Zaidi ya hayo, Wenyeviti au Mameya ni wanasiasa na huchaguliwa na wananchi kwa njia ya kura, na ndio wakuu wa Tawi la Utawala/Utendaji sambamba na Tawi la Baraza la Madiwani la Halmashauri husika. Watendaji wanawajibika kwa Meya/Mwenyekiti na siyo kwa Madiwani, kwa hiyo masuala ya watendaji hulindwa na huwakilishwa na Meya/Mwenyekiti katika Baraza la Madiwani.

Kwenye mafunzo ya Osaka, mambo matatu yafuatayo yalitiliwa mkazo kwamba ndivyo vitu muhimu katika kufikia uwezo wa juu wa rasilimali watu katika Halmashauri:

1) Kuajiri
   Kuajiri watumishi wenye sifa kuliko wote na wanaofaa katika kufikia dhima/malengo ya mamlaka husika; na
2) Mafunzo
   Baada ya kuajiri, kuwapa mafunzo yanayolenga na kuwezesha kufikiwa kwa dhima/malengo ya mamlaka husika (siyo malengo ya mtu binafsi); na
3) Kujipanga
   Kuhakikisha kuwa uwezo wote wa Raslimali watu katika Halmashauri unatumika kikamilifu ili kutimiza malengo ya mamlaka husika

Kwa minajili hiyo, Japani iliona kuwa ni jambo lisilokwepeka kutangulia kugatua madaraka yahusuyo usimamizi wa rasilimali watu ili kila Halmashauri iweze kuchambua hali halisi, kupanga mipango, kuajiri, kutoa mafunzo, kupanga majukumu na kudhibiti watumishi. Mtumishi wa Halmashauri lazima awe mtu anayelipenda eneo husika na watu waliopo, anayefanya kazi kwa bidii kwa ajili ya watu, anayeelewa vizuri kuhusu hali ya eneo husika, anayewafahamu watu vizuri na kuwa na uwezo wa kufanya kazi kwa karibu na wakazi wa eneo husika; hii ndiyo mantiki ya ugatuaji. Ni uzoefu wa nchi ya Japani kwamba, kwenye Halmashauri zenye mafanikio ya kuridhisha, kuna maofisa na watendaji wanaofanya kazi kwa kujituma hasa katika kuwahudumia watu, na kushirikiana na wakazi; na walio wengi wao ni wale watendaji waliozaliwa na kukulia katika maeneo hayo na wanayapenda makazi hayo, pamoja na uongozi thabiti wa Meya/Mwenyekiti ambaye naye ni mzawa.

Jambo jingine muhimu linalozifanya Halmashauri za Japani ziwe na nguvu ni juhudi waliyonayo katika kuwapa watumishi wao mafunzo. Halmashauri za Japani zinawekeza sana kwa watumishi kwa kuwapeleka kwenye mafunzo pamoja na mpango wa mafunzo kazini ambao uko kimkakati kulingana na mahitaji ya kitaasisi (siyo mahitaji binafsi) na kwa mtazamo wa mbali.

Hili linawezekana kule Japani kwa sababu hakuna uhamisho wa watumishi toka Halmashauri moja kwenda nyingine ya na kiwango cha kubakiza/kushikilia watumishi kazini ni kikubwa sana, hivyo Halmashauri huwekeza bila hofu kwamba baada ya kuwasomesha watakimbia.

Kinyume chake, Tanzania kuna uhamisho wa mara kwa mara wa watumishi muhimu kutoka Halmashauri moja kwenda nyingine na hivyo ni vigumu sana kuwabakiza/kuwashikilia watumishi kwenye Halmashauri moja. Katika hali kama hii, changamoto kubwa ni jinsi ya kuhakikisha kwamba matokeo yatokanayo na mafunzo ya watumishi yanabaki ili yalete maboresho katika utendaji kazi wa mamlaka husika, na kuzifanya Halmashauri ziwe na bidii katika kujenga uwezo wa watumishi licha ya uwezekano mkubwa wa kuwapoteza baada ya kuwasomesha. Swali moja liliulizwa kwenye mafunzo ya Osaka kama Tanzania inaweza kuandaa na kutekeleza mpango mkakati na thabiti wa muda mrefu wa mafunzo ya kuwajengea watumishi wake uwezo katika hali hii.

Kwa upande mwingine, mafunzo ya Osaka yaliibua suala la “kufanya kazi kama timu” ili kuweza kutumia asilimia 120 ya uwezo wa nguvu kazi iliyopo na kuyafikia malengo ya kitaasisi. Kule Japani, kuna mambo kadhaa kuhusu mfumo wa usimamizi wa rasilimali watu ambayo yamefafanuliwa kwa uangalifu mkubwa kwa ajili hiyo, kama vile:

1) Ngazi za mishahara zimewekwa makusudi kwa lengo la kuondokana na rushwa na kuchochea watumishi wafanye kazi kwa bidii hadi watakapostaafu;
2) Mfumo wa kipekee wa Japani “kuchelewesha upandishaji vyeo” ili kumfanya kila mtu afanye kazi kwa bidii kwa miaka mingi kabla ya kupandishwa cheo (kukamua asilimia 120 ya uwezo wa kila mmoja);
3) Watumishi kufanya kazi kwa kuzunguka kila idara ya Halmashauri husika na mtindo wa kuweka kumbukumbu za kila mwaka za utendaji wa kila mtumishi ili kufanya za tathimini kwa haki na kwa malengo na kuchagua wale wenye uwezo mkubwa na wanaostahili kupandishwa vyeo kuwa Wakurugenzi;
4) Shughuli zote zinazohusu rasilimali watu ziko chini ya Idara ya Uendelezaji Rasilimali Watu ili iwezeshe namba 3) hapo juu;
5) Mazingira ya kipekee ya Japani yanawezesha “utendaji kazi kama timu”, usimamizi unaofanywa na wakuu/viongozi, na mafunzo kazini yanayoendeshwa na wasimamizi, mtindo unaojulikana kama mtindo wa “chumba kikubwa” yaani ofisi ya wazi mithili ya ofisi za benki.


Yote yaliyoelezwa kwenye sehemu hiyo hapo juu yamewekwa na kanuni zinazotawala Mamlaka za SM za Japani ili kuhakikisha mambo matatu yahusuyo usimamizi wa rasilimali watu yanazingatiwa mfano 1) Kuajiri; 2) Mafunzo; na 3) Kushughulika kwa bidii. Swali liliulizwa, katika mazingira ya sasa ya Halmashauri za Tanzania, ni kwa jinsi gani zinaweza kutekeleza mambo haya matatu.

**3.3 Fedha za Serikali za Mitaa na Ugatuaji wa Masuala ya Fedha**

**a) <u>Misingi ya kifedha katika Halmashauri</u>**

Michoro (1) na (2) inaonyesha japo kwa ufupi hali ya Halmashauri za Japani kuhusu masuala ya fedha.

Mchoro (1) unaonyesha ukubwa wa majukumu ya Halmashauri katika matumizi ya kutoa huduma ndani ya kila sekta. Ukiangalia sekta ya afya, Halmashauri hutumia 94% ya fedha iliyotengwa kwenye bajeti ya afya ya taifa na Serikali Kuu hutumia 6% tu. Kwenye elimu uwiano kati ya Halmashauri na Serikali Kuu ni 85% kwa 15%. Ukizingatia uhusiano wa karibu uliopo kati ya uzito wa majukumu na matumizi,





**Mchoro (1) Uwiano wa Matumizi ya SK na SM kwa kila sekta**
Chanzo: White Paper on Local Public Finance, 2010
(Ministry of Home affairs of Government of Japan)

Halmashauri za Japani zinafanya sehemu kubwa zaidi ya majukumu ya Serikali ya kutoa Huduma. Kwa upande mwingine, ni muhimu kutambua kwamba kiasi kikubwa cha bajeti <u>hutengwa</u> kwa ajili ya kuziwezesha Halmashauri kutekeleza majukumu mazito yaliyogatuliwa na kupelekwa kwao.


Je hali ikoje Tanzania? Ukweli ni huu, ukiangalia majukumu yote yaliyogatuliwa na kupelekwa kwenye ngazi za msingi katika Halmashauri Tanzania, ukubwa wa majukumu ni sawa tu yale ya Halmashauri za Japani. Lakini, bajeti iliyotengwa kwa ajili ya Halmashauri Tanzania, ilikuwa pungufu ya TZS trilioni 3 ya bajeti ya taifa ya zaidi ya TZS trilioni 11 ya mwaka 2011/12.

Ulinganisho unaofanywa, ni ule unaohusu bajeti za Halmashauri zenye kuwa na masharti au uhuru wa matumizi. Mchoro (2) unaonyesha viwango na vyanzo mbalimbali vya mapato ya Halmashauri za Japani. Kama ilivyothibitishwa na takwimu hizi, 51% ya mapato hutokana na vyanzo vya ndani (kodi ushuru na malipo mbalimbali). Pia kuna <u>ruzuku ambazo hazina masharti yoyote ya matumizi</u> zinazoitwa "ruzuku toka SK kwenda SM" (ruzuku za LAT). Ruzuku ya LAT ni <u>fedha nyingi inayotoka SK kwa mara moja</u> kwenda SM na serikali za mikoa. Fedha hii inahamishwa toka Wizara ya Fedha kwenda kwenye akaunti kuu ya kila Halmashauri <u>siku ya kwanza ya kila robo mwaka</u>. Ukijumlisha mapato ya ndani na ruzuku za LAT toka SK, Halmashauri za Japani zina aslimia 75% ya bajeti yao isiyo na masharti na wanaweza kutumia kama wanavyoamua wenyewe.

Mchanganuo huu ni wa muhimu sana kwa Halmashauri SM za Japani katika kufikia malengo ya mipango yao ya maendeleo, kwani wana bajeti ya kutosha na ya uhakika kila mwaka. Washiriki toka Tanzania walipochunguza hali za Halmashauri za kwao, walithibitisha kwamba zina hali mbaya ya kifedha pia fedha nyingi wanayopokea ina masharti ya matumizi kama ilivyo kwenye Mchoro, (3).




**Mchoro (3): Muundo wa vyanzo mapato ya SM za Tanzania**
**Chanzo: Ni hesabu zilizofanywa na mwandishi toka tovuti ya serikali ya Tanzania**





**Mchoro(2): Vyanzo na viwango vya mapato ya SM za Japani**
**Chanzo: White Paper on Local Public Finance, 2010 (Ministry of Home Affairs of Government of Japan)**

Ama kwa hakika, hata kwa hali hii ingelikuwa jambo la maana kama 94% ya ruzuku wanayopokea isingelikuwa na masharti ili Halmashauri ziwe na uhuru wa kuzitumia. Bahati mbaya, kuna ruzuku mbalimbali zinazokuja zikiambatana na masharti katika matumizi. Hivyo basi, hata kama Halmashauri itaanda mipango mizuri ya maendeleo, ni vigumu sana kutekeleza miradi yao ya vipaumbele kwa sababu ya ruzuku zenye masharti, ambazo husababisha mipango ya maendeleo isitekelezeke kirahisi.

Ikumbukwe kwamba kiasi cha fedha inayotengwa kwenye bajeti za Halmashauri ni kidogo mno cha Shilingi trilioni 3 kati ya trilioni 11 za bajeti ya taifa (2011/12). Hizi Shilingi trillioni 3 ni sawa na 94% ya bajeti nzima ya Halmashauri, na hii inathibitisha jinsi ambavyo hawana vyanzo vya ndani vya kutosha.

Mafunzo ya Osaka yaliwataka viongozi wa Serikali ya Tanzania kutenga kiasi cha kutosha cha bajeti kutekeleza wingi wa majukumu ya Halmashauri yaliyogatuliwa na kupelekwa kwao kama




**Mchoro (4): Aina za Kodi kwenye Majiji/Miji**
**Chanzo: White Paper on Local Public Finance, 2010**
**(Ministry of Home Affairs of Government of Japan)**

kweli wameazimia kufikia ugatuaji wa madaraka. Fedha hii inaweza kuwa zile kutoka vyanzo vya ndani au katika ruzuku isiyo na masharti[5]. Kama hakuna bajeti ya kutosha inayotengwa, basi hakuna sababu ya kugatua majukumu kwenda ngazi za Halmashauri. Vinginevyo, shughuli hizo hazitatekelezwa na mwishowe jamii itateseka kwa kukosa huduma. Kama tulivyoona kwa Halmashauri za Japani, ikitokea kwamba 85% ya majukumu ya kutoa huduma za elimu yamegatuliwa na kupelekwa ngazi za Halmashauri, basi kiasi cha kutosha cha bajeti ya kutekeleza majukumu hayo hugatuliwa na kupelekwa Halmashauri ili kufikia malengo. Vinginevyo si haki hata kidogo kwa Halmashauri na hasa kwa watu wanaotegemea huduma.

**b) <u>Kodi za Ndani kwa ajili ya Uendelevu na ushamiri wa Serikali za Mitaa</u>**

Kule Japani, kuna sababu zilizo wazi kabisa kuhusu aina zote za kodi zinazotengwa kwenye ngazi zote mbili za SM. Prefectures(SM za Wilaya ndiyo ngazi ya juu za SM) na Municipalities (Miji na Majiji) ndiyo ngazi za chini za SM[6]). Japokuwa Wilaya (Prefecture) ndiyo ngazi ya juu ya SM ya Japani, zinaweza kulinganishwa na Halmashauri za Tanzania kwa ukubwa wa eneo. Kuhusu majukumu, ngazi za chini za SM Japani (Municipalities) ndizo zinalinganishwa na ngazi za Halmashauri za Wilaya/Miji/Manispaa/Jiji kwa Tanzania. Hata hivyo kule Japani, huduma zote za muhimu kwa jamii hutolewa na Majiji/Miji (Municipalities) kwa sababu ndizo ngazi za msingi zilizo karibu na watu, huku Prefecture/Wilaya wanahusika hasahasa na maendeleo ya kiuchumi kwa vile majukumu haya yanahitaji eneo kubwa kwa ajili ya mipango na kuyatekeleza kimkakati.

Kulingana na majukumu yalivyo na wajibu wa Majiji/Miji, zifuatazo ni kodi ambazo zinaweza kutozwa na Majiji: Kama inavyoonekana katika mchoro (4), kodi za nyumba na mali zisizo hamishika ni sawa na 45.3% ya mapato yatokayo na kodi, ambayo ni karibu na nusu ya mapato yote yatokanayo na kodi. Ukijumlisha na "Kodi ya mkazi"(kodi ya Kichwa) pamoja na "kodi ya mipango miji", inakuwa ni zaidi ya 80% ya mapato yatokanayo na kodi. Kodi za nyumba na kodi ya mipango miji hutozwa kwenye ardhi na majengo na hizi ni kodi ambazo hakuna awezaye kuzikwepa. Kama ardhi yote na majengo yote yamesajiliwa na kuthaminiwa vizuri, basi hivi ni vyanzo vya uhakika kwa serikali za Mitaa.

[5] Kwa hatua zilipofikia kwa sasa, bado haishauriwi kugatua madaraka ya kifedha na kuwapa SM mamlaka makubwa ya kutoza kodi. Hii ni kwa sababu hali hii itaziumiza zile SM zilizo kwenye maeneo yenye ufukara ya vijijini, kwa vile hazina vyanzo vya uhakika vya kodi, huku zile SM tajiri za mijini zitakuwa na mapato mengi kutoka vyanzo vyao vya ndani . Kwa hiyo ni busara zaidi kuendelea kutoa ruzuku kutoka chanzo kimoja, lakini SM ziwe na uhuru na maamuzi wa kuzitumia kulingana na vipaumbele vyao kwa sasa.

[6] Kuna Prefecture/Wilaya 47 na (Munispaa) 1,742 hadi kufikia Octoba 2012. Manispaa za Japani zinajumuisha Majiji**<u>, Miji na Vijiji</u>**, na tofauti na mgawanyiko wa ngazi za SM za Tanzania.

"Kodi ya kila mkazi wa Halmashauri za Japani" ni "kodi ya kichwa" iliyofutwa hapa Tanzania ambayo ni "kodi ya maendeleo"[7]. Chanzo hiki cha kodi pia huwa ni chanzo cha kuaminika kwa sababu wakazi wote wameandikishwa na Halmashauri inajua wanapoishi. Tukiangalia hali ya Tanzania, vyanzo vingi vya mapato ni vile vinavyohusiana na shughuli za kiuchumi, mfano ushuru wa mazao (23%), ushuru wa huduma (18%), ushuru wa nyumba za kulala wageni (3%), leseni (10%), karo na malipo mbalimbali (17%), ambazo hubadilika kulingana na mabadiliko ya hali ya uchumi wa eneo husika, na cha kushangaza ni kwamba kodi ya majengo ni 8% tu ya mapato yatokanayo na kodi.

Mafunzo ya Osaka yaliwapa viongozi wa Tanzania changamoto kwamba ili Halmashauri ziweze kutoa huduma endelevu zinazohitajika kwa wakati na viwango vinavyotegemewa, ni lazima kujenga wigo mpana na mfumo wa uhakika wa kukusanya kodi ndani ya Halmasahuri zenyewe. Uzoefu wa Japani unaonyesha kwamba bila kuweka msisitizo kwenye vyanzo vyenye uhakika vya kodi/ushuru kama vile kodi za majengo, kodi ya kichwa/kodi ya maendeleo, siyo rahisi hata kidogo kwa Halmashauri kutekeleza majukumu yake. Kwa mazingira haya, ni muhimu kuwa na mfumo wa daftari la kuandikisha ardhi na mali zisizo hamishika pamoja na daftari la wakazi wote kwa kila Halmashauri, hii itasaidia nchi nzima siyo tu kwenye masuala ya kukusanya mapato, bali kwa matumizi mengine mengi.

Kuhusu utaratibu huu, inafaa kusema kwamba tayari Tanzania kuna mifano ya kufurahisha na inayotia moyo ya Halmashauri zinazotekeleza kile kinachopendekezwa hapa, rejea kisa mkasa cha Manispaa ya Mtwara Mikindani kwenye Sura ya Tatu.

### 3.4 Maendeleo ya Kiuchumi ya Serikali za Mitaa – Uzoefu wa kufurahisha wa dhana ya ki-Japani ya "Kijiji kimoja zao moja" au (OVOP)"

Hitaji la maendeleo ya kiuchumi ya Halmashauri limekuwa likisumbua vichwa vya Wakurugenzi wengi wa Tanzania. Kuhusiana na hili, kuna uzoefu maarufu nchini Japani wa dhana ijulikanayo kama "zao moja kwa kijiji kimoja" maarufu kama OVOP, iliyoanzia kwenye wilaya/ Prefecture ya Oita ambayo hapo awali ilikuwa moja ya wilaya fukara kuliko zote nchini humo. Uzoefu unaotokana na dhana hii unaweza kuwa muafaka kwa Tanzania kama utatafsiriwa na kutumika inavyostahili kulingana na mazingira ya Tanzania.

#### (a) Zao moja kwa kijiji kimoja (OVOP) ni nini?

Vuguvugu la "zao moja kwa kijiji kimoja" au OVOP ni mkusanyiko wa ubunifu wa shughuli za maendeleo ya jamii zilizobuniwa na kupata msukumo wa viongozi kutoka jamii husika katika Wilaya (Prefecture) ya Oita, ambao waliipenda jamii yao na wakahuzunishwa kutokana na hali ya ufukara uliokuwa umekithiri huko miaka ya nyuma. Japokuwa juhudi kama hizo za mtu

[7] Tofauti pekee ni kwamba kodi ya kichwaTanzania hutozwa kwa kiwango sawa kwa kila mtu, kwa Japani kodi ya mkazi hutozwa kulingana na viwango vya kipato cha kaya. Kama hakuna kipato cha kiasi fulani kinachokubalika, basi wanakaya wa kaya hiyo hawana sababu ya kulipa kodi ya mkazi.

mmoja mmoja zilikuwepo hapa na pale kwenye Wilaya (Prefecture) ya Oita tangu miaka ya 1960, dhana yenyewe ya "zao moja kwa kijiji kimoja" au OVOP ilianzishwa rasmi mwaka 1979 na Dr. Morihiko HIRAMATSU, akiwa Gavana[8] wa Wilaya hiyo kwa kuanza kuzitambua baadhi ya juhudi za jamii zilizokwisha anza na kuziendeleza.

Dr. HIRAMATSU, alikuwa ni msomi mwenye mafanikio makubwa akiwa mtumishi wa cheo cha juu kwenye Wizara ya Biashara za kimataifa na Viwanda yaani "Ministry of International Trade and Industry (MITI)". Hii ilikuwa Wizara yenye nguvu sana, lakini aliamua kuacha kazi hiyo na kurudi kwenye Wilaya ya Oita yaani nyumbani kwao. Kilichomsukuma ni kwa sababu alihofia sana kuwa Wilaya ya nyumbani kwake iliendelea kubaki nyuma kimaendeleo na kuwa miongoni mwa Wilaya fukara kuliko zote nchini Japani kwa wakati huo.

Baada ya kurudi kwao, aligombea na kushinda cheo cha Ugavana wa Wilaya ya Oita. Alipoanza kazi hii jambo la kwanza alilolifanya ni kutembelea vijiji vyote kwenye Wilaya hiyo. Wakati akifanya matembezi haya, alikuta kuna miradi ya maendeleo na jitihada mbalimbali za watu wenyewe kujaribu kujinasua huko vijijini. Aliguswa sana na jitihada hizo za wananchi wakiongozwa na viongozi wao wenye mapenzi mema na juhudi hizi zilikuwa hazijulikani kwa serikali. Alithamini sana juhudi za jamii, na akawatia moyo waendelee na jitihada za kujikwamua. Kwa wanavijiji, wengi wao walikuwa hawajawahi kutoka nje ya vijiji vyao, kwa hiyo kwao ilikuwa ni faraja kubwa kutembelewa na mtu mkubwa kama Gavana na kusifiwa kwa kile walichokuwa wanakifanya! Hawakuwahi kuwaza kwamba kile walichokuwa wanakifanya kilikuwa ni kitu cha kipekee na cha thamani machoni pa wengine. Tangu Gavana wao Dr. HIRAMATSU alipofanya matembezi haya, juhudi hizo za jamii zilipewa msukumo mkubwa na watu wakahamasika zaidi na kujisikia fahari wenyewe.

Kwa upande wake, Dr. HIRAMATSU alifikiri ni jukumu muhimu kwa Serikali ngazi ya Wilaya kuunga mkono na kuendeleza juhudi za thamani kubwa zilizoanzishwa na wananchi kutaka kuboresha maisha yao wenyewe, kuzieneza zaidi na kubadilisha uzoefu huu mzuri na viongozi wa vijiji vingine ndani ya Wilaya yao.

Vuguvugu la "zao moja kwa kijiji kimoja" yaani OVOP ina mambo muhimu yanayolitofautisha na dhana nyingine kwani Vuguvugu hili hupelekea kuzalisha bidhaa za kipekee (ikijumuisha utalii), ili kupata maendeleo kwa kutumia rasilimali zilizopo ndani ya jamii husika. Hata hivyo, jambo jingine la tofauti kwenye vuguvugu la "zao moja kwa kijiji kimoja" ni kwamba: kuna uzoefu dhabiti wa jamii unaopatikana kutokana na utekelezaji wa miradi midogo ya maendeleo ya shughuli za kiuchumi ngazi za msingi. Wananchi husika huunganisha uwezo wao wa kujipanga na kutekeleza mustakabali wa maisha yao; jamii zimejijengea uwezo, zimeamka na zina ujasiri; Jamii zimeimarika na zimefikia uwezo wa kujitawala na kujiendesha wenyewe kama kijiji. Ukweli uliopo hapa ni kwamba wananchi wana uzoefu wa kufanikiwa na wakati mwingine kushindwa (lakini wamejijengea uwezo na tabia ya kujikwamua katika kushindwa huko), siyo tu kwamba jamii inategemea kupata mafanikio ya kiuchumi pekee, bali pia jamii inatarajia

[8] Cheo cha Gavana wa Prefecture ni cheo cha juu zaidi kwenye SM za juu Japani ikilinganishwa na Meya wa kwenye SM za Tanzania (Ona "3.2. Usimamizi wa Rasilimali Watu na Ugatuzi wa madaraka" kwa Meya.)

kujijengea uwezo, uzoefu na ujasiri na kupata nguvu zaidi katika mchakato huo. Ukweli huu ni muhimu ufahamike ili kulielewa vizuri vuguvugu la "zao moja kwa kijiji kimoja". Ikumbukwe kwamba ni rahisi sana kupata mafanikio au faida ya mara moja katika biashara au mradi fulani kutokana na msaada wa mara moja kutoka nje ya jamii, lakini kama jamii hiyo itakumbana na vikwazo fulani fulani baadaye, hawataweza kuvishinda kama watakuwa hawajajijengea uwezo kupitia michakato iliyotangulia ya kutatua matatizo yao kwa nguvu na jitihada zao wenyewe.

Kwa mantiki hii, ni vyema kutambua kwamba nyingi kati ya juhudi zilizojitokeza kwenye Vuguvugu la "zao moja kwa kijiji kimoja" kule Oita, zilipitia mchakato ufuatao:

- Kabla ya vuguvugu la "zao moja kwa kijiji kimoja"au OVOP, wanavijiji wa Oita walikuwa fukara sana, walikuwa wamekata tamaa kuhusu mabadiliko, wenye kijicho na kuoneana wivu wao kwa wao, kutokana na hali hii haikuwezekana kushirikiana baina yao ili kuboresha maisha kwa pamoja. Hata hivyo, kupitia Vuguvugu la "zao moja kwa kijiji kimoja" walianza kujitambua kwamba "Ndiyo, tunaweza kama tunataka!" Haya ni mafanikio makubwa katika mchakato wa kubadili fikra.
- Katika badiliko la fikra hapo juu, wanavijiji walianza kujijengea uzoefu wa kushirikiana kwenye shughuli mbalimbali ndani ya jamii, wakizikabili changamoto wanazokutana nazo na kuzishinda kwa pamoja. Mchakato huu uliwafanya waweze kujipanga vizuri na vizuri zaidi.
- Kupitia mchakato huo huo, waliimarisha mahusiano na taasisi za nje zenye usaidizi ikijumuisha Halmashauri na Asasi za kiraia na mashirika yasiyo ya kiserikali.
- Pamoja na ujenzi wa uwezo wa jamii ulioelezwa hapo juu, jamii husika zilifanikiwa kupata matokeo dhahiri ya maendeleo ya kiuchumi.

**(b) Dr. HIRAMATSU alifanya nini akiwa Gavana wa Wilaya?**

Kwanza kabisa, ieleweke vizuri kwamba vuguvugu la "zao moja kwa kijiji kimoja" halikuwa ni programu ya lazima ("maamrisho ya kutoka juu kwenda ngazi za msingi") iliyoandaliwa na Dr. HIRAMATSU na kwamba watu hawakuambiwa cha kufanya. Kwa bahati mbaya, baadhi ya nchi zinazoendelea ambazo zilivutiwa na Vuguvugu la "zao moja kwa kijiji kimoja", waliuelewa vibaya ukweli huu. Walizingatia tuu zile faida za kiuchumi zinazotokana na OVOP na kujaribu kuendeleza vuguvugu la "zao moja kwa kijiji kimoja" kama sera ya taifa na kutoa maamrisho kutoka juu kwamba kila kijiji kizalishe kitu ambacho kinaweza kuuzwa hapa nchini au nje ya nchi. Kinyume chake sasa, alichokifanya Dr. HIRAMATSU kwenye Wilaya ya Oita ilikuwa ni, kwanza, kutembelea vijiji vyote, kuzitambua juhudi za wananchi za thamani ambazo zilikwishaanza, akawasifia na kuwatia moyo.

Pili, alivishirikisha vijiji vingine na viongozi wao kuhusu mambo mema yanayofaa kuigwa ili habari hii iwe kichocheo, waanze na wao kufikiri kuhusu maendeleo yao wenyewe kwa kutumia rasilimali zilizopo kwenye maeneo husika, badala ya kulalamika eti hawana chochote kwenye vijiji vyao na kukata tamaa.

Tatu, alipotambua bidhaa fulani za kipekee kwenye baadhi ya vijiji, alisaidia kutafuta soko la ndani na nje ya Wilaya ya Oita. Alitumia maarifa yake, uzoefu na mitandao ambayo alikwisha jijengea alipokuwa afisa wa ngazi za juu Wizara ya Biashara ya Kimataifa na Viwanda. Alizitangaza bidhaa hizi nchi nzima.

Nne, aliwezesha suala zima la kubadilishana uzoefu baina ya viongozi wa vijiji mbalimbali ili wajifunze na kuhamasika kutokana na kujifunza kwa watu walio kwenye ngazi moja na siyo kujifunza kwa ngazi tofauti ya maendeleo. Alianzisha shule ya kuendeleza rasilimali watu[9]" iliyoitwa "*Toyonokuni*[10]. Juhudi hizi za Gavana, zilisaidia kuchochea ari ya viongozi na hii ikapelekea kuibuka kwa miradi mingi yenye sura ya "zao moja kwa kijiji kimoja" yaani OVOP.

Kama inavyoonekana hapo juu, dhamira ya vuguvugu la "zao moja kwa kijiji kimoja" au OVOP ilikuwa ni Halmashauri kuzitambua, kuzisifia, kutia moyo juhudi za kimaendeleo zinazojitokeza kwa jamii. Jukumu la Halmashauri ni "uwezeshaji" na siyo "utekelezaji" au "uelekezaji". Dr. HIRAMATSU hakuwaambia wanavijiji jambo la kufanya katika kuendeleza vuguvugu hili, bali aliheshimu juhudi zao na umiliki wao, pamoja na nguvu zao. Mafunzo ya Osaka yanasisitiza vuguvugu la"zao moja kwa kijiji kimoja", kwani ni dhana muafaka kwa mazingira ya Tanzania, na inaaminika kwamba tayari zipo juhudi za namna hiyo kwenye Vijiji na wapo viongozi wazuri wanaojali maendelo ya nyumbani kwao. Ingelikuwa ni jambo la manufaa makubwa kwa Tanzania kuunga mkono vuguvugu hili na kutoa fursa ya wazalishaji kujifunza kwa wenzao walio ngazi moja. Mafunzo ya Osaka yaliwataka viongozi wa Tanzania kudhani kwamba eti hakuna chochote kwenye vijiji vyao. Kuna mambo mengi mazuri yanayostahili kuigwa lakini pengine wao ndio hawajayatambua. Ni wajibu wa viongozi wa Halmashauri kuanza kuzitambua juhudi za jamii zilizopo, kuzitia moyo, na kubadilishana uzoefu na wengine. Ingekuwa ni njia yenye tija zaidi ya wazalishaji kujifunza kutoka kwa wenzao walio kwenye ngazi moja kuliko kujifunza watu wa ngazi tofauti au kutoka kwenye vitabu. Ni kutokana na mtizamo huu ndipo kitabu hiki kikaandaliwa.

### 3.5 Masuala Mengine

Kuna mengi ambayo hatukugusia hapo juu kutokana na kukosa nafasi. Lakini, yapo ambayo ni ya muhimu kugusia ambayo yanafaa kwa Tanzania kama vile kisamkasa cha Minamata na uzoefu unaotokana na "Ugonjwa wa Minamata"(Minamata Disease) na jinsi walivyoweza kuhuisha jamii kutokana na mkasa huo; Upangaji mipango shirikishi jamii; mipango miji; mipango ya matumizi bora ya ardhi na marekebisho ya ardhi, uzoefu wa Japani kuhusu maendeleo ya kiuchumi na mchango wa Halmashauri katika mkasa huo, n.k.

Kuhusu kisamkasa cha Minamata, mafunzo ya Osaka yanaweka msistizo kwenye umuhimu wake, na inaaminika kwamba nchi zinazoendelea ikiwemo Tanzania zina mengi ya kujifunza kutokana na kisa mkasa hiki.

---

[9] Inaitwa "shule" lakini hakuna majengo. Huwa ni aina fulani ya mafunzo kwanjia ya warsha kwa ajili ya viongozi ili kuwakutanisha pamoja.
[10] "Toyonokuni" jina la kienyeji la eneo hili la Wilaya ya Oita

## 4.0 MAENDELEO BAADA YA MAFUNZO YA OSAKA YALIYOSABABISHA KUCHAPWA KWA KITABU HIKI

Kama ilivyoelezwa kwenye sehemu ya 1 hapo juu, mafunzo ya Osaka yalikuwa yameandaliwa mahsusi kwa nchi ya Tanzania kwenye miaka mitano ya mwanzo (2002 – 2007), yaliendelea kwa miaka mingine sita lakini wigo wake ukapanuliwa na kuingiza nchi nyingine tatu (2008 – 2012). Mafanikio makubwa katika miaka hii 11 hapa Tanzania ni kule kuanzishwa kwa Umoja wa Makatibu Tawala wa Mikoa na Wakurugenzi waliosoma Osaka, kwa kifupi TOA. Huu ni mfano wa pekee Duniani kuwa na Umoja wa Wahitimu wa kozi ya aina moja ukijumuisha Wadau Maarufu ambao ni viongozi wa maboresho kama vile Makatibu Tawala wa Mikoa (RAS) na Wakurugenzi wa Halmashauri pamoja na wakuu wengine kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OWM-TAMISEMI). Japokuwa haikutegemewa, lakini ni jambo la kupendeza hata kwa JICA ambao wanaendesha maelfu ya kozi za mafunzo duniani kote.

Kwa nyongeza, TOA wameshaanza kuendesha semina mbalimbali na warsha za mafunzo kama vile Mafunzo baada ya Osaka na Warsha za Mafunzo za Kanda kwa ajili ya kubadilishana uzoefu baina ya Halmaushauri wanachama. Fursa hizi, siyo tu kwamba zina saidia kubadilishana maoni baina ya Halmashauri wanachama, bali yametoa uwanja ambao ni nadra kuupata wa majadiliano na kuhusu uhalisia wa Ugatuaji wa Madaraka, hususan changamoto wanazokutana nazo katika kutekeleza maboresho ya Serikali za Mitaa.

Mpaka sasa, hakuna asasi ya namna hii hapa Tanzania, inayowahusisha Watendaji wa Serikali za Mitaa na wale wa Sekretarieti za Mkoa. Jumuia ya Serikali za Mitaa (ALAT) ipo, lakini wahusika wake wakuu ni Wenyeviti wa Halmashauri, Mameya na Wabunge. Vikao vya Jumuiya hii haviwapi fursa Wakurugenzi wa Halmashauri kushiriki kikamilifu na kutoa ushauri wa kitaalamu ingawa wao pia ni wajumbe. Kwa mantiki hii, TOA ina uwezekano mkubwa wa kukua hadi kuwa Umoja wa Watendaji Wakuu wa Serikali za Mitaa na Tawala za Mikoa yaani Wakurugenzi wa Halmashauri na Makatibu Tawala wa Sekretarieti za Mikoa ambao ni wataalamu na watekelezaji wa ugatuaji wa madaraka na maboresho nchini. Hawa ndio wanaoshughulika kila siku kwenye mstari wa mbele wa maboresho. Maoni na mapendekezo yao ya pamoja yanaweza kuwa ni ya maana sana na ya kuongeza ufanisi kwenye kutekeleza maboresho.

Kuhusu mambo mema yanayofaa kuigwa, tayari Tanzania imekwishajijengea uzoefu kwa zaidi ya muongo mmoja wa utekelezaji Ugatuaji wa Madaraka kwenda ngazi za msingi katika kila Mamlaka ya Serikali za Mtaa. Lazima kutakuwepo na idadi kubwa ya mambo ya kufurahisha na uzoefu mzuri kwenye Halmashauri nyingi kote nchini ambao unafaa kushirikisha Halmashauri nyingine. Japani inaamini kwamba aina hii ya kujifunza kwa taasisi zilizo kwenye ngazi zinazofanana inaweza kuwa muafaka zaidi kuliko kujifunza kutoka nje ya nchi yaani kutoka kwenye ngazi tofauti au ya juu sana. Tanzania inaweza kujifunza vizuri kutokana na uzoefu ulioko ndani mfano shughuli za OVOP kama zilivyoelezwa kwenye 3.4. hapo juu. Kitabu hiki cha rejea kiliandaliwa kwa kuzingatia maelezo na msingi huo ulioelezwa hapo juu. Ni matumaini ya TOA na mafunzo ya Osaka kwamba yatachangia kuboresha utendaji ndani ya Mamlaka nyingi za Serikali za Mitaa, kila moja ikimchochea mwenzie, na kuendeleza mambo mema

yanayojitokeza, ambayo yatapelekea kwenye ufanisi na mafanikio ya ugatuaji wa madaraka katika nchi hii.

Mwishowe, inastahili kusema kwamba kutokana na matokeo ya kufurahisha yaliyotokana na mafunzo ya Osaka kwa nchi ya Tanzania, ambayo yameelezwa kwenye sura hii, Shirika la Ushirikiano wa Kimataifa la Japani (JICA) limeaamua kuendelea kutoa mafunzo ya Osaka kwa miaka mingine mitano, yakilenga Tanzania kwa mara nyingine tena na litatoa msisitizo maalumu katika kuwezesha shughuli za wanaumoja wa TOA na juhudi zake za ujenzi wa kitaasisi. Hii ina maana kwamba, viongozi wengine wengi wa maboresho Tanzania watafaidika kutokana na mafunzo ya Osaka ili waweze kuchangia utekelezaji mzuri zaidi wa maboresho ya ugatuaji wa madaraka kwenda ngazi za msingi nchini.

# Sura ya Pili

# Jitihada za Jamii kwa Ajili ya Huduma Bora

Mtazamo wa Jitihada za Jamii ni mfumo mpya katika eneo la maendeleo vijijini, ambao lengo kuu ni maendeleo vijijini. Malengo Mahsusi ya mfumo huu ni kuongeza ubora wa maisha ya watu maskini, na kuboresha miuondombinu. Ni mfumo wa hiari wa kundi la watu wanojiendesha wenyewe wakiwa na tabia zinazofanana za kijamii na kiuchumi, ambao wanaungana ili kuanzisha fikra zitakazochochea maendeleo endelevu. Mtazamo wa Jitihada za Jamii kwa ajili ya Maendeleo Vijijini katika hali ya kendesha mipango ya kiuchumi huleta ajira, miondombinu ambayo jamii inaweza kujitengenezea, stadi za kazi pamoja na shughuli mchanganyiko. Pia mtazamo huu huleta mipango ya ustawi wa jamii ili kuboresha afya, lishe na maslahi ya jamii kwa ujumla.

Jitihada za jamii huwa na maana ya majaribio ya jamii kupambana na changamoto zinazoikabili kijamii na kiuchumi bila kusubiri miradi mikubwa kutoka serikalini. Jitihada za jamii hujumuisha maazimio ya kutatua matatizo ya jamii kupitia jamii kujipanga, kushiriki na kutekeleza. Katika haya yote jamii yenyewe huona hitaji, hupanga namna ya kufikia hitaji, hutafuta raslimali zilizopo zinazohitajika kufikia hitaji, hujipanga katika makundi ya utekelezaji na kutekeleza mradi.

Mara nyingi jitihada za jamii huwa na maana ya uundaji wa vyama vya hiari katika jamii, ambapo wanchama huwa na malengo yanayofanana, hujipanga na kuratibu mipango wakiwa na lengo mahsusi la kuboresha hali ya kijamii na kiuchumi katika jamii yote. Tafiti zinaonesha kuwa vikundi katika jamii kwa miaka mingi vimefanikiwa kujiendesha katika kujenga barabara, vituo vya afya, madaraja na nyumba, kulima mashamba, kufadhili masomo, na kuanzisha taasisi za viwanda; kutaja machache. Ushahidi wa haya umeleta ongezeko na kupanuka kwa uanachama na jitihada za jamii katika vijiji.

Hapa Tanzania, Jitihahada za Jamii na Ushiriki wa Jamii vimekuwa dhahiri kutokana na historia ya itikadi ya kijamii na kiuchumi ya kujitegemea. Tangu Uhuru, jamii katika vijiji vyao zilishauriwa kuishi katika jamii na kutumia mbinu za ushirika katika kutatua matatizo yao. Kileleni kabisa mwa itikadi hii, kati ya miaka ya 1960 na 1970 na hasa baada ya Azimio la Arusha, jamii zilianzisha miradi mbalimbali na kuitekeleza ikiwa ni pamoja na ujenzi wa shule na zahanati, kuchimba visima na mabwawa madogo, kulima barabara na kuendesha kilimo cha ushirika.

Pamoja na kuwa mbinu hizi zilipungua katika miaka ya 1990 kuelekea milenia mpya kutokana na madai ya serikali kuwa inaweza kutoa huduma zote, kuna jamii ambazo siku za karibuni zimetumia jitihada za jamii kwa kina katika ujenzi wa shule, zahanati, madarasa na majengo ya serikali; vyote vikilenga kuboresha utoaji wa huduma.

Katika Sura hii Mbinu Bora mbalimbali zimewasilishwa kutoka Halmashauri za Wilaya za Kibaha, Mpimbwe Tabora, Kasulu na Urambo.

Mbinu bora ya Halmashauri ya Wilaya ya Kibaha inatumia uzoefu wa Kitongoji cha Disunyara kueleza Jitihada za Jamii katika Kuboresha Utoaji wa Huduma. Kabla ya mwaka 2016 Kitongoji cha Disunyara i hakikuwa na jengo la ofisi suala ambalo lilileta mifarakano na ushiriki duni katika shughuli za maendeleo, mahudhurio duni katika mikutano ya kisheria na matukio mengi ya ushindani usio na tija. Mikakati iliyotumika kuondoa changamoto hizi ni kutambua fursa zilizokuwepo kama ardhi, wanajamii, wadau na utayari wa jamii kushiriki katika shughuli za maendeleo. Mikakati mingine ni utafutaji wa fedha na ushirikishaji wa wadau mbalimbali, maandalizi na kupitishwa kwa andiko la gharama za ujenzi, manunuzi ya vifaa vya ujenzi, kuunda Kamati ya Maendeleo ya Kitongoji na ujenzi wa mindombinu ya shule. Matokeo ya jitihada hii ni uwepo wa ofisi ya Kitongoji ambayo ina nafasi ya Diwani, Mwenyekiti, Ukumbi wa mikutano, chumba cha Maafisa Ugani, chumba cha kuhifadhi nyaraka na chumba cha mahabusu, maboresho katika sekta ya elimu, kuongezeka kwa ushiriki wa jamii na kubadilika kwa mtazamo wa jamii. Matokeo haya yanatokana na umoja, utashi wa kisiasa juu ya maendeleo na uongozi wenye vipaji na ari ya kujitoa.

Halmashauri ya Wilaya ya Mpimbwe ina mbinu bora inayohusu Jitihada za Jamii Katika Kuboresha Mazingira ya Kufundisha na Kujifunza. Katika shule ya Msingi Majimoto, kulikuwa na msongamano wa wanafunzi uliokithiri ambao uliathiri mchakato wa kufundisha na kujifunza kwa walimu na wanafunzi. Hali hii ilisababisha mahudhurio duni, kuongezeka kwa utoro na matukio ya milipuko ya magonjwa. Kuboresha mazingiza ya kufundisha na kujifunza, Halmashauri iliendesha uhamasishaji wa jamii, utafutaji wa raslimali na ukusanyaji wa michango ya fedha taslimu na vifaa vya ujenzi kwa kutumia vikosi vya sungusungu vya Kijiji na Kata na viongozi maarufu wa jamii. Jitihada hii imeleta maboresho katika miundombinu ya shule, kuimarika kwa mahusiano kati jamii na Halmashauri, kupungua kwa utoro na ukwepaji vipindi, ujanishaji na usafi wa mazingira ya shule na elimu ya uhifadhi wa mazingira. Jamii ina mpango wa kuongeza miundombinu ya shule. Mafanikio ya jitihada hii yanatokana na kujitoa kikamilifu kwa jamii katika mchakato wote wa utekelezaji wa mradi.

Mbinu ya Halmashauri ya Wilaya ya Tabora inahusu Jitihada za Jamii Katika Kuanzisha Shule ya Sekondari katika Kata ya Kizengi. Kabla ya kuanzishwa kwa shule hii wanafunzi walitembea kwenda shule ya Sekondari ya Tura iliyo jirani katika Kata ya Tura (65km). Baadhi ya wanafunzi wa kiume walijiingiza katika makundi mabaya ya wahuni na watumia madawa ya kulevya wakati wanafunzi wa kike walikuwa katika hatari ya kuvamiwa na kubakwa. Jamii ya Kizengi ilikubaliana kwa kauli moja kuanzisha Shule ya Sekondari ya Kata kwa lengo kuu la kuboresha utoaji wa elimu ya sekondari. Jitihada hii ilitekelezwa kupitia mikutano mbali mbali ya vijiji na ukusanyaji wa michango. Matokeo yanajumuisha; Shule ya Sekondari imekamilika, inatoa huduma za elimu na wanafunzi wanapata chakula cha mchana. Shule ya Sekondari lilikuwa hitaji la jamii suala ambalo lilileta utayari wa wanajamii kuchangia.

Jitihada ya H/W ya Kasulu inahusu Jitihada za Kikundi cha Vijana katika Kuleta Mabadiliko ya Kijamii na Kiuchumi ikitumia uzoefu wa kikundi cha Mboni ya Vijana katika Kijiji cha Zeze. Kijiji cha Zeze kilikuwa na changamoto nyingi kama ukosefu wa ajira, mbinu duni za kilimo, upatikanaji duni wa maji, ukosefu wa elimu na stadi za biashara, uwezo duni wa kupata mitaji, kukosekana kwa kituo cha ufundi cha kufundisha stadi za teknolojia na kutokuwepo kwa uongozi wa vijana wa kuanzisha na kusimamia programu za maendeleo. Lengo kuu la jitihada hii lilikuwa kuleta mazingira sahihi yenye fursa za ajira na uhakika wa kipato na chakula kwa vijana na jamii. Malengo haya yalifikiwa kwa kujenga uelewa, kusajili kikundi, kujenga miundombinu ya ofisi, kuanzisha vitalu vya miche ya miti ili kuhifadhi mazingira na kuanzisha shughuli za kukukuza uchumi. Matokeo ya jitihada hii ni pamoja na kuwepo kwa fursa ya elimu kwa wanafunzi na vijana, kupatikana kwa elimu ya biashara na mitaji kwa wanawake na vijana,

kuongezeka kwa upatikanaji wa maji safi na salama, kupatikana kwa ajira na uhifadhi wa mazingira. Jitihada hii ilifanikiwa kutokana na uongozi bora, kujituma kwa wanachama wa kikundi na usaidizi thabiti kutoka washirika wa maendeleo na Halmashauri.

Mbinu bora ya H/W ya Urambo inatumia uzoefu wa Kijiji cha Motomoto kuhusu Jitihada za Jamii Katika Uboreshaji wa Huduma za Afya. Siku za nyuma kijiji hiki hakikuwa na zahanati; wanakijiji walilazimika kutembea 8km kwenda Zahanati ya Vumilia ili kupata huduma za afya. Hali hii ilisababisha changamoto mbalimbali kama vifo vingi vya akina mama na utegemezi kwa wakunga wa jadi. Jitihada hii ililenga kujenga zahanati ili kuboresha huduma za afya. Kufikia malengo haya Halmashauri ya Kijiji iliendesha mikutano ya uhamasishaji kwa wanajamii wote ambapo uamuzi ulifanyika kutumia mbinu ya jitihada ya jamii kwa kuchangia ujenzi na kushirikisha wadau. Huduma za afya katika Kijiji cha Motomoto na vijiji vya jirani vya Chekeleni, Ukondamoyo and Magere (H/W ya Kaliua) zimeimarika. Kijiji cha Motomoto kilifanikiwa katika jitihada hii kutokana na kutumia mbinu ya jitihada ya jamii, mawasiliano bora na ushirikiano thabiti na wadau.
zaji na kutekeleza mradi.

# HALMASHAURI YA WILAYA YA KIBAHA


**JITIHADA ZA JAMII KATIKA KUBORESHA UTOAJI WA HUDUMA**




*Uzoefu wa Kitongoji cha Disunyara*

**1.0 UTANGULIZI**

Halmashauri ya Wilaya ya Kibaha ilianzishwa Januari 1, Mwaka 1984, kwa Sheria ya Serikali za Mitaa Na. 7 ya 1982. Halmashauri hii ni mojawapo ya Halmashauri 9 za Mkoa wa Pwani na hupakana na H/W ya Bagamoyo upande wa Kaskazini, Mji wa Kibaha upande wa Mashariki, H/W ya Kisarawe Upande wa Kusini na H/W ya Morogoro (Mkoa wa Morogoro) upande wa Magharibi. Halmashauri inapatikana kati ya Latitudo $6^0$ and $8^0$ Kusini na Longitudo $38^0$.9' na $39^0$.05' Mashariki ikiwa umbali wa 40km kutoka Jiji la Dar es salaam. Kiutawala, Halmashauri ina Tarafa 2, Kata 14, Vijiji 25 na Vitongoji 100. Kwa mujibu wa Sensa ya mwaka 2012, Halmashauri in watu 70,209 ambao 35,694 (50.8%) ni wanawake na 34,515 (49.2%) ni wanaume. Halmashauri in makabila makuu matatu; Wakwere, Wazaramo na Waluguru.




***Ramani ya H/W ya Kibaha***

H/W ya Kibaha ina eneo la 1,251.7$km^2$ ambazo ni 3.9% ya eneo lote la Mkoa wa Pwani; sehemu kubwa ikiwa tambarare, milima midogo na mabonde. Hali ya hewa huwa ya joto na jua kwa mwaka mzima, kukiwa na joto kali zaidi mwezi Disemba na joto la chini mwezi Julai na misimu tofauti mitatu; msimu wa ukame katika mwezi Mei/Juni hadi Oktoba na vipindi viwili vya mvua. Mvua za vuli hunyesha mwezi Oktoba/November na Disemba na mvua za masika hunyesha kati ya mwezi Machi na Mei/Juni. Kiwango cha mvua kwa mwaka ni kati ya 800mm - 1,000mm.

**2.0 TATIZO**

Ofisi ya Kitongoji ndio kituo cha kwanza cha mahusiano kati ya serikali, wakazi na biashara zao; shughuli yake kuu ikiwa kuendesha shughuli za kiutawala za sera, miradi, sheria ndogo na masuala ya fedha katika Kitongoji. Kitongoji ndicho chombo cha msingi katika mfumo wa Serikali za Mitaa za vijijini na

maeneo ya pembezoni mwa miji na huwa sehemu ya kijiji au mji mdogo ulioandikishwa. Kila Kitongoji kina Mwenyeketi aliyechaguliwa na wakazi wote wenye umri wa kupiga kura kulingana na taratibu za uchaguzi zilizotolewa na Waziri anayehusika na masuala ya Serikali za Mitaa.

Kitongoji ni taasisi ambayo huwakutanisha wakazi kila mwezi kujadili na kutatua masuala yahusuyo amani, ulinzi na maendeleo, kutatua mifarakano midogo na kuandikisha wakazi wote wa Kitongoji ikiwa ni pamoja na kumbukumbu za vizazi na vifo.

Kitongoji kama taasisi ya kisheria hutarajiwa kuhamasisha wakazi kulipa kodi na tozo zinazotakiwa kama ilivyoainishwa na Halmashauri ya Wilaya, kushughulika na masuala ya mazingira na afya, kufuatilia na kuhakikisha kuwa watoto wote wenye umri wa kwenda shule wanapata shule na kuhudhuria inavyotakiwa, kuhamasisha wakazi kushiriki elimu ya watu wazima na kuhimiza wakazi kushiriki katika shughuli za maendeleo. Kwa kuzingatia umuhimu wa Kitongoji, shughuli za kiutawala zilizokasimiwa kwa ngazi hii zinahitaji majengo bora ya ofisi.

Kabla ya mwaka 2016, Kitongoji cha Disunyara kilikuwa hakina Jengo la Ofisi. Shughuli za kiofisi ziliendeshwa katika ofisi za Chama Cha Mapinduzi (CCM). Hali hii ilileta ugumu kwa baadhi ya wanajamii ambao wana mitazamo tofauti ya kisiasa, kufuata huduma na kupata haki. Kwa miaka mingi kulikuwa na kutokuelewana kati ya Wenyeviti wa Vitongoji na Wenyeviti wa vyama vingine kutokana na tofauti za itikadi. Kutokuelewana huku kulichochea ushiriki duni wa jamii katika shughuli za maendeleo, mahudhurio duni katika mikutano ya kisheria na matukio mengi ya ushindani gombanishi usio wa lazima. Licha ya kukosekana kwa jengo la ofisi Jamii ya Disunyara ilikuwa na changamoto nyingine kama ukosefu wa kituo cha kulelea watoto na upungufu wa madarasa katika shule ya msingi. Changamoto hizi ziliihamasisha jamii ya Disunyara kuanzisha miradi mbalimbali ya jamii ili kupunguza matatizo katika utoaji wa huduma.

**3.0 MALENGO**

Lengo kuu la jitihada hii lilikuwa kuboresha utoaji wa huduma. Mahsusi kabisa, jitihada ililenga kujenga ofisi ya Kitongoji ili kuleta usawa katika utoaji wa huduma za kiserikali, kuboresha upatikanaji wa huduma na kuimarisha ushiriki thabiti wa wakazi katika shughuli za maendeleo. Kitongoji pia kililenga kuboresha mazingira ya kufundisha na kusoma na kuimarisha utoaji wa huduma za afya.

**4.0 MIKAKATI YA UTEKELEZAJI**

Mwaka 2009 jamii ya Disunyara iliamua kujikita katika ujenzi wa ofisi ambayo ingeboresha utoaji wa huduma za serikali na utawala. Swali muhimu la kwanza ambalo jamii ilijiuliza lilikuwa “tuna rasilimali asili na fursa zipi zinazoweza kusaidia mchakato wa ujenzi wa jengo la kudumu na ofisi ya kisasa ya Kitongoji?” Swali hili liliwezesha Kitongoji kuainisha fursa zilizopo ambazo zilijumuisha ardhi, wanajamii, wadau na utayari wa jamii kushiriki katika shughuli za maendeleo. Baada ya kuainisha fursa, jamii ilikubaliana kujenga ofisi katika ardhi iliyomilikiwa na Kitongoji. Eneo limekaa kimkakati kwani lipo katikati ya Kitongoji, rahisi kufikiwa na kila mkazi na lipo pembezoni mwa barabara iendayo Kijiji cha Mzenga na Mjimdogo wa Mlandizi.

Ukusanyaji wa fedha na ushiriki wa wadau mbalimbali; fedha za kujenga ofisi zilipatikana kutokana na michango ya wanajamii. Kila kaya ilichangia TZS 30,000/= katika kipindi kisichozidi miaka 2. Aidha, fedha zilikusanywa toka kwa wadau na Serikali. Baadhi ya kaya na wadau maarufu ni Kanali Mbele, Wakili Rwehongeza, Shule ya Sekondari ya Getrude na Kanisa Katoliki - Kazaroho; hawa walitembelewa kiofisi na uongozi wa Kitongoji, kujadili umuhimu wa ofisi na kuazimia kuchangia kama wakazi wa Kitongoji.

Wadau wote walioainishwa walichangia kiasi kikubwa cha fedha kwa awamu mbalimbali kati ya mwaka 2009 na 2014.

Uundaji kamati ya ujenzi; wakazi wa Disunyara walitambua kuwa uongozi wa Kitongozi unakabiliwa na majukumu mengi ya kila siku. Kukabidhi shughuli za ujenzi kwa uongozi kungesababisha ucheleweshaji na urasimu. Mkutano mkuu wa Kitongoji uliamua kuunda kamati ya wajumbe 10 walioteuliwa kati ya wakazi ikiwa ni pamoja na wanawake. Kamati ilipewa jukumu la kukusanya fedha na rasilimali nyingine, kuandaa na kufuatilia ratiba za kazi, usimamizi wa fedha na usimamizi wa shughuli za ujenzi. Kamati ilitakiwa kutoa taarifa ya ujenzi kila robo mwaka katika Mikutano ya wakazi wote wa Kitongoji.

Maandalizi na kupitishwa kwa andiko la ramani na gharama za ujenzi (BOQ); Halmashauri, kupitia idara ya ujenzi, iliandaa na kukipatia Kitongoji andiko la gharama za ujenzi ili kuwezesha ukadiriaji wa gharama halisi za vifaa, nguvukazi na usimamizi. Andiko hili lilipitishwa na Mkutano wa Kitongoji na kukubaliwa kuwa mwongozo rasmi wa kufanya manunuzi, kununua vifaa vya viwandani na kugawa nguvukazi katika shughuli za ujenzi. Kwa kutumia andiko hili, wakazi wa Disunyara walilinganisha gharama za utekelezaji wa mradi kati ya kuajiri mkandarasi na kutumia mafundi waliopo Kitongojini ambapo pendekezo la pili lilidhihirika kuwa la gharama nafuu. Hivyo, ujenzi wa ofisi ya Kitongoji cha Disunyara ulitekelezwa na mafundi wenyeji wakisaidiwa na makundi ya wakazi kulingana na ratiba ya ujenzi.

Manunuzi ya vifaa vya ujenzi vya viwandani na ujenzi; fedha zilizochangwa na wakazi na wadau zilitumika kununua vifaa na mitambo ya viwandani. Wakazi wa Disunyara walishiriki katika kusafisha eneo, kufyatua matofali, kuchimba msingi, kukusanya mawe na mchanga na ujenzi wa kuta chini ya usimamizi wa mafundi wenyeji. Hii ilisaidia kupunguza gharama katika ukusanyaji wa rasilimali zilizopo Kitongojini, usafishaji wa eneo la ujenzi na ujenzi wa kuta. Shughuli zote zilisimamiwa na kamati ya ujenzi.



***Ofisi ya Kitongoji cha Disunyara***

Kuundwa kwa Kamati ya Maendeleo ya Kitongoji; kutokana na ukweli kuwa Kitongoji kilikuwa na shughuli nyingine za maendeleo, kulikuwa na haja ya kuanzisha taasisi ya kudumu ya kusimamia masuala ya maendeleo. Hivyo Kamati ya Kitongoji ya Maendeleo ilianzishwa na kupewa jukumu la kusimamia utekelezaji wa miradi na kuratibu jitihada zote za maendeleo. Kamati hii ilitokea kuwa na ubunifu wa hali ya juu na iliiga mikakati iliyotumika katika ujenzi wa ofisi ili kuboresha huduma katika elimu na afya, ngazi ya Kitongoji.

Ujenzi wa miundombinu ya shule; kamati ya maendeleo iliwezesha ujenzi wa kituo cha kulelea watoto na madarasa mawili, maktaba na ofisi ya walimu katika shule ya msingi Disunyara. Kituo cha kulelea watoto wadogo kilijengwa ili kusaidia wazazi kulea watoto wao katika kituo kimoja wakijifunza na kucheza; suala ambalo lingeruhusu wazazi kuendelea na kazi zao pamoja na shughuli nyingine za kiuchumi. Baada ya mikutano mbalimbali kati ya viongozi, wazazi na walimu, ilikubalika kwa pamoja ufanyike ujenzi wa vyumba vya madarasa kwa kutumia jitihada za jamii. Licha ya miundombinu ya shule, jamii pia ilianza ujenzi wa zahanati.



*Kituo cha watoto -Disunyara*



*Madarasa mapya*

Katika shughuli zote hizi H/W ya Kibaha ilitoa msaada wa kitaalamu katika kuandaa michoro, andiko la gharama za ujenzi, ufungaji wa umeme katika shule ya msingi Disunyara, upelekaji wa watumishi katika shule na zahanati na usimamizi na ufuatiliaji katika utoaji huduma.

**5.0 RASILIMALI**

Rasilimali zilizotumika katika jitihada hii zinajumuisha nguvukazi, fedha na vifaa mbalimbali. Rasilimali watu zilijumuisha wakazi, wataalamu kutoka Halmashauri, uongozi wa Kitongoji na Diwani. Mtiririko wa rasilimali fedha na michango ya wadau imeoneshwa kwenye Jedwali 1 hapa chini. Michango ya jamii kwa ujumla ni 82% ya jitihada ikiwa ni nguvukazi na fedha. Halmashauri ilichangia 18%.

**Jedwali 1: Rasilimali fedha za ujenzi wa ofisi ya Kitongoji**

| MICHANGO YA WADAU | KIASI TZS | ASILIMIA (100%) |
|---|---|---|
| Jamii | 49,000,000/= | 82% |
| H/W ya Kibaha | 11,000,000/= | 18% |
| Jumla | 60,000,000/= | 100% |

Rasilimali nyingine zilizotumika ni pamoja na ardhi. Rasilimali fedha zilizotumika kwenye ujenzi wa madarasa, maktaba, ofisi ya walimu na zahanati hazikupatikana wakati wa uhakiki wa jitihada hii.

**6.0 MATOKEO**

H/W ya Kibaha na jamii zilifanikiwa kupata matokeo mbalimbali kupitia jitihada za jamii; jengo la ofisi limekamilika na lina ofisi ya Diwani, ofisi ya Mwenyekiti wa Kitongoji, ukumbi wa mikutano, ofisi za maofisa ugani, stoo ya nyaraka na chumba cha mahabusu. Huduma za serikali zinatolewa katika ofisi ambayo haina mrengo na ushindani wa kisiasa. Wakazi wanafurahia ubora wa huduma zinazotolewa.



***Ofisi ya Kitongoji yenye matumizi mbalimbali ya kiofisi***

Jamii imeshuhudia maboresho makubwa katika sekta ya elimu; kituo cha kulelea watoto wadogo kinatoa huduma kwa watoto wa Disunyara na Vitongoji vya jirani. Kituo kina watumishi wote na kipo karibu na shule ya msingi Disunyara. Wazazi wanafurahia uwepo wa kituo. Kituo hiki kimewapa wazazi hasa wanawake nafasi ya kushiriki kikamilifu katika shughuli za kiuchumi na kijamii. Kituo hiki pia kimepunguza mzigo wa walimu wa shule ya msingi kuanza kufundisha watoto wa chekechea. Mazingira ya kufundisha na kujifunzia yaliyoboreshwa yameongeza ari ya walimu na wanafunzi katika shule ya msingi.




***Kituo cha Watoto cha Disunyara***



***Madarasa mapya***

Ushiriki wa jamii umeongezeka; kumekuwa na ongezeko dhahiri katika ushiriki wa jamii katika shughuli za serikali na za maendeleo ikiwa ni pamoja na kuongezeka kwa mahudhurio katika mikutano na hafla za Kitongoji. Kabla ya ujenzi wa ofisi wakazi waliamini kutokuwepo kwa umuhimu wa kushiriki mikutano, lakini baada ya uhamasishaji na uboreshaji wa mahusiano Kitongoji sasa kinashuhudia mahudhurio ya kutosha katika mikutano na hafla mbalimbali za umma. Kutokana na umoja na mshikamano huu katika jamii, Kitongoji kinatekeleza miradi ya maendeleo katika ujenzi wa zahanati na maabara.



***Zahanati ya Dusinyara***

Kubadilika kwa mtazamo; jamii imebadilika na kujikita katika maendeleo badala ya ushidani potofu na migogoro iliyokuwepo kabla. Jamii imejikusanyia uzoefu katika ushirikiano, kutambua changamoto na kupambana nazo kupitia mijadala bora. Kumekuwepo na kuaminiana na mahusiano chanya na wadau ambao nao wapo tayari kushiriki katika miradi ya jamii.

**7.0 MIKAKATI YA UENDELEVU**

Jamii na Halmashauri zimeweka mikakati mbalimbali ili kuhakikisha uendelevu wa jitihada hizi. Mikakati hii ni pamoja na ukarabati wa mara kwa mara wa ofisi ya Kitongoji, uimarishaji wa kamati ya usimamizi wa miradi na kuendelea kuhamasisha na kutia motisha jamii. Kitongoji kimedhamiria kuboresha huduma zote kwa kuendelea kutoa michango na kushirikisha wadau.

**8.0 SIRI YA MAFANIKIO**

Mafanikio yaliyoelezwa katika jitihada hii ni matokeo ya kufanya kazi kama timu, utashi wa kisiasa kuhusu maendeleo, na uongozi wenye vipaji na moyo wa kujitoa. Mwenyekiti wa Kitongoji cha Disunyara na Mkurugenzi Mtendaji wa H/W ya Kibaha ni viongozi ambao wana mrengo wa maendeleo. Walitumia jitihada nyingi kujenga daraja kati ya wakazi wa Kitongoji na wadau. Kwa maelezo ya wakazi waliohojiwa na kwa mujibu wa Afisa Mtendaji wa Kata ya Kilangalanga, Mwenyekiti wa Kitongoji cha Disunyara (ni Mwanamke) ana nguvu, ni kiongozi mbunifu; na anayefuata sheria na kanuni. Mwenyekiti ana uwezo mkubwa wa kuhamasisha jamii, yupo wazi na ni mkweli. Muungano huu imara kati ya Mwenyekiti na wakazi ndio siri ya kweli ya mafanikio.

# HALMASHAURI YA WILAYA YA MPIMBWE


**JITIHADA ZA JAMII KATIKA KUBORESHA MAZINGIRA YA KUFUNDISHA NA KUJIFUNZA**



*Uzoefu wa Shule ya Msingi Mkuyuni*

## 1.0 UTANGULIZI

Halmashauri ya Wilaya ya Mpimbwe ni majawapo ya Halmashauri 5 katika Mkoa wa Katavi iliyoanzishwa mwaka 2016 baada ya kugawanywa kwa H/W ya Mlele ya awali. Halmashauri nyingine ni Manispaa ya Mpanda na H/W za Mpanda, Nsimbo na Mlele. H/W ya Mpimbwe inapatikana 120km kutoka makao makuu ya Mkoa wa Katavi Manispaa ya Mpanda. Halmashauri ipo kati ya Longitudo $33^0$ 31' Mashariki na Latitudo $5^0$7' to $15^0$ 30' Kusini. Mwinuko wa ardhi ni kati ya 1000m – 1250m juu ya usawa wa bahari na hali ya hewa ya wastani; joto likiwa kati ya $18^0$C - $30^0$C.  Kuna misimu miwili ambayo ni msimu wa kiangazi kati ya mwezi Mei na Novemba na miezi iliyobaki ni msimu wa masika. Halmashauri ina Tarafa 2, Kata9, Vijiji 31 na Vitongoji 137. Shughuli kuu za kiuchumi ni kilimo na ufugaji wa wanyama na nyuki. Mazao makuu ya biashara ni ufuta, alizeti na karanga na mazao ya chakula ni mahindi, mpunga, maharage, mihogo na viazi vitamu. Kwa mujibu wa sense ya mwaka 2012, H/W ya Mpimbwe ina watu 117,543; 57,588 wanaume na 59,955 wanawake na ongezeko la watu la 3.2% kwa mwaka.




**Ramani ya H/W ya Mpimbwe**

Halmashauri ina shule za msingi 29 zenye jumla ya wanafunzi 23,380; wavulana 11,815 na wasichana 11,565.  Mwaka 2017 uandikishaji wa darasa la kwanza ulikuwa 98%. Halmashauri ina shule 4 za sekondari zenye jumla ya wanafunzi 1,956; wavulana 1,215 na wasichana 741. Hali ya miundombinu na samani imeoneshwa kwenye jedwali 1 na 2 hapa chini.

**Jedwali 1: Miundombinu katika shule za msingi**

| Na | AINA | MAHITAJI | YALIYOPO | PUNGUFU |
|---|---|---|---|---|
| 1. | MADARASA | 497 | 172 | 325 |
| 2. | MATUNDU YA VYOO | 635 | 246 | 389 |
| 3. | NYUMBA ZA WALIMU | 507 | 97 | 410 |

**Jedwali 2: Miundombinu katika shule za sekondari**

| Na | AINA | MAHITAJI | YALIYOPO | PUNGUFU |
|---|---|---|---|---|
| 1. | MADARASA | 65 | 49 | 16 |
| 2. | MATUNDU YA VYOO | 51(m) | 40 | 11 |
| | | 38 (f) | 28 | 10 |
| 3. | NYUMBA ZA WALIMU | 90 | 28 | 62 |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 4. | MAABARA | 12 | 11 | 1 |

**2.0 TATIZO**

Shule ya Msingi Mkuyuni ni mojawapo ya shule za msingi 29 katika Halmashauri hii. Shule hii ilianzishwa kutokana na msongamano uliokithiri katika shule ya msingi Majimoto. Utekelezaji wa mpango wa serikali wa elimu bure kwa wote unaaminika kuongeza uandikishaji wa wanafunzi wa darasa la kwanza. Kutokana na ongezeko hili mazingira ya kufundisha na kujifunza yameathiriwa na idadi kubwa ya wanafunzi kwa chumba cha darasa na upungufu wa walimu. Katika shule ya msingi Majimoto kulikuwa na msongamano mkubwa ulioathiri mchakato wa kufundisha na kujifunza kwa walimu na wanafunzi. Darasa moja lilikuwa na wanafunzi kati ya 70 hadi 100. Miundombinu (ofisi) na vifaa (meza) kwa ajili ya walimu havikuwepo vya kukidhi mahitaji.



***Msongamano wa wanafunzi katika Shule ya Msingi Mkuyuni***

Changamoto hizi zilihitaji hatua za haraka kutoka kwa uongozi wa Kata au Kijiji. Maazimio yalifikiwa kupitia kikao cha Kamati ya Maendeleo ya Kata cha tarehe 20/01/2016; kujenga madarasa mawili na ofisi ya walimu katika shule ya msingi Mkuyuni. Jamii ilikubali na kuanza kujenga madarasa mawili hadi kwenye lenta. Halmashauri ilisaidia ukamilishaji wa ujenzi kwa kuezeka, kupiga plasta, kuweka sakafu na kufunga madirisha na milango.

Pamoja na jitihada za jamii za kujenga madarasa mawili na matundu mawili ya vyoo kwa ajili ya wanafunzi, msongamano wa wanafunzi ulikithri; zaidi ya wanafunzi 200 katika darasa moja, hasa baada ya utekelezaji wa mpango wa elimu bure mwaka 2016. Aidha, wanafunzi wengine walitumia Mkuyu uliopo katika eneo la shule kama darasa. Changamoto hizi zilisababisha yafuatayo;

(i) Mahudhurio duni; kati ya wanafunzi 420 ni wanafunzi 370 waliohudhuria masomo mara kwa mara.

(ii) Kuongezeka kwa utoro; wanafunzi wa darasa la kwanza walipungua kutoa 242 hadi 202 na darasa la pili kutoka 178 hadi 168 kutokana na mazingira hasi yaliyosababishwa na msongamano na uwiano wa juu kati ya mwalimu na wanafunzi.

(iii) Mlipuko wa magonjwa kutokana na upungufu wa matundu ya vyoo; wagonjwa wa homa ya matumbo waliongezeka kutoka 50 hadi 90, Kipindupindu kutoka 0 hadi 5 na minyoo 50 hadi 200.

(iv) Wanafunzi wachafu kutokana na kuketi chini ya mti kwenye vumbi kutwa nzima wakihudhuria vipindi vya kusoma, kuandika na kuhesabu.



***Mkuyu uliotumika kama darasa***



***Wanafunzi waliosongamana kwenye Mkuyu***

**3.0 LENGO**

Lengo kuu la jitihada hii lilikuwa kuboresha mazingira ya kufundisha na kujifunza. Mahsusi, jitihada hii ililenga;

(i) Kujenga madarasa matano, ofisi ya walimu, matundu 14 ya vyoo na kununua madawati 170.

(ii) Kupunguza utoro kutokana na maboresho ya mazingira ya kufundisha na kujifunza ambayo yatawatia motisha walimu na wanafunzi kujikita kikamilifu katika shughuli za elimu.

(iii) Kupunguza milipuko ya magonjwa iliyosababishwa na miundombinu duni (upungufu wa madarasa na matundu ya vyoo)

**4.0 MIKAKATI YA UTEKELEZAJI**

Jitihada za jamii za awali hazikuweza kumaliza tatizo la msongamano, upungufu wa matundu ya vyoo, utoro na afya duni. Kupambana na hali hii, jamii, Timu ya Menejimenti ya Halmashauri na Baraza, kwa pamoja walikubaliana kujenga madarasa 5, matundu ya vyoo 14 (12 ya wanafunzi na 2 ya walimu) na kununua madawati 170 katika mwaka 2015. Wadau wakuu katika mchakato huu walijumuisha jamii yote, wafanyabiashara wadogo, vyombo vya habari, sungusungu, viongozi wa jadi, watu maarufu na H/W ya Mpimbwe.

Uhamasishaji wa jamii na ukusanyaji wa rasilimali; utekelezaji ulianza kwa kuhamasisha jamii kupitia vyombo vya habari vya kijijini, sungusungu, watu maarufu na mikutano ya umma. Viongozi wa Kijiji na Vitongoji walikuwa muhimu katika mchakato huu; walihamasisha wadau kuchangia rasilimali mbalimbali. Wadau wakuu walipewa majukumu mbalimbali; watumishi wa vyombo vya habari walipewa

jukumu la kuiunganisha jamii na kujenga uelewa kuhusu namna ambavyo kila raia katika kijiji na kata atachangia ujenzi wa miundombinu ya shule. Sungusungu wa ngazi ya Kijiji na Kata walikabidhiwa jukumu la kusimamia utekelezaji wa sheria ndogo zilizokubaliwa na jamii michango ya fedha na nguvukazi; wakwepaji wengi walishughulikiwa na kuhakikisha malengo yanafikiwa. Viongozi wa jadi na watu maarufu walipewa jukumu la kuhamasisha jamii, kujenga uelewa na kuwatia moyo wanakijiji kushiriki kikamilifu katika kuchangia fedha taslimu, kusafisha eneo la mradi na kutekeleza mradi.



***Kikao cha Halmashauri ya Kijiji kipindi cha Uhamasishaji***

Ukusanyaji wa fedha na vifaa vya ujenzi; wanakijiji na wafanyabiashara walichangia fedha au nguvukazi katika ujenzi wa madarasa. Wafanyabiashara maarufu (wenye nyumba za wageni, migahawa, maduka ya jumla na vituo vya mafuta) walichangia vifaa vya ujenzi (saruji, mchanga, kokoto) na fedha taslimu za kulipa vibarua. Wanawake na vikundi vya vijana walishiriki katika kufyatua matofali, kuteka maji na kushiriki katika shughuli za ujenzi kama vibarua. Wasafirishaji walisaidia usafirishaji wa vifaa vya ujenzi. Muundo huu wa timu ulisaidia ujenzi wa haraka na bora wa kuta hadi kwenye lenta. Baadaye, Halmashauri iliwezesha ukamilishaji wa miundombinu ya shule kwa kuezeka, kupiga plasta, kufunga milango na madirisha, kuleta madawati 170 na kujenga matundu 14 ya vyoo (12 kwa ajili ya wanafunzi na 2 ya walimu).



***Miundombinu ya shule iliyoboreshwa***

**5.0 RASILIMALI**

Jamii na Halamshauri zilitoa rasilimali mbalimbali kuhakikisha jitihada inakamilika kwa mafanikio. Michango ya jamii ilijumuisha vifaa vya ujenzi kama matofali, kokoto, nondo, saruji na mbao vyenye thamani ya TZS 26,478,000/=. Kujiridhisha kuwa gharama zinafikiwa, kila kaya ililazimika kuchangia TZS 15,000/=. Wale ambao walikwepa kulipa, walilipishwa faini ya TZS 10,000/= pamoja na kuchangia TZS 15,000/=. Hivyo kaya zilizokiuka makubaliano na kutaka kukwepa kulipa zililipa TZS 25,000/= kwa kaya.

Mchango wa Halmashauri ulijumuisha vifaa vya ujenzi vya viwandani ikiwa ni pamoja na mabati (geji 28), misumari, mbao za kenchi, saruji, rangi, ufungaji wa milango na madirisha, ununuzi wa madawati

ambavyo kwa jumla ni TZS. 46,942,000. Aidha, Halmashauri ilitoa utaalamu katika kusimamia na kufuatilia utekelezaji wa mradi kipindi chote. Gharama ya kukamilisha mradi kwa mbinu ya ushiriki wa jamii ilikuwa TZS 73, 420,000 ikilinganishwa na TZS 118,000,000 kama angepewa mkandarasi. Kipindi cha utekelezaji wa mradi kilikuwa miezi 12.

**6.0 MATOKEO**

Utekelezaji wa jitihada hii ulileta mafanikio mbalimbali yaliyochambuliwa hapa chini.

Miundombinu ya shule iliyoboreshwa; jamii na Halmashauri kwa ujumla zimefanikiwa kukamilisha ujenzi wa madarasa 5, ofisi 1 ya walimu, matundu 14 ya vyoo (12 ya wanafunzi na 2 ya walimu) na kununua madawati 170 katika Shule ya Msingi Mkuyuni. Kwa kuhakikisha uwepo wa miundombinu na samani hizi, mazingira ya kufundisha na kujifunza yameboreshwa na hivyo kuwepo kwa huduma bora ya elimu.

Kuimarika kwa mahusiano mazuri kati ya jamii, wadau na Halmashauri; kutokana na kukamilika kwa ujenzi wa miundombinu ya shule, Halmashauri, jamii na wadau wamefanikiwa kuwa na muungano imara. Muungano huu ambao umeanzia katika shule ya Mkuyuni umesambaa kwenye vijiji vingine na kuwezesha kukamilika kwa miradi ya aina hii katika shule tano za msingi za Kata ya Majimoto. Shule hizi za msingi ni pamoja na Kitupa iliyojenga madarasa 4, Migunga iliyojenga madarasa 3 na nyumba 1 ya mwalimu na Luchima iliyojenga madarasa 2 na ofisi 1 ya walimu. Aidha ushirikishaji wa jamii, wazee maarufu, kaya, walimu, kamati za shule na viongozi wa vijiji kumechangia maboresho makuu katika mazingira ya kufundisha na kujifunza.

Kupungua kwa utoro na kuimarika kwa mahudhurio; jitihada hii imefanikiwa kupunguza utoro kwa kiasi kikubwa na kuimarisha mahudhurio ya wanafunzi wa shule za msingi kwa 100% kwani wanafunzi wanavutiwa na kuachagizwa na mazingira bora ya kujifunza. Aidha, miundombinu iliyoboreshwa imeongeza mahudhurio ya darasani kutoka 86% mwaka 2015 hadi 100% mwaka 2017 na uandikishaji umeongezeka zaidi kama inavyooneshwa kwenye jedwali 3 hapa chini.

**Jedwali 3: Idadi ya Wanafunzi Shule ya Msingi Mkuyuni mwaka 2017**

| Na | DARASA | WAVULANA | WASICHANA | JUMLA |
|---|---|---|---|---|
| 1 | CHEKECHEA | 100 | 98 | 198 |
| 2 | DARASA I | 322 | 304 | 626 |
| 3 | DARASA II | 208 | 232 | 440 |
| 4 | DARASA III | 100 | 102 | 202 |
| 5 | DARASA IV | 84 | 84 | 168 |
| 6 | JUMLA | 814 | 820 | 1634 |

Jamii imenunua meza 5 za walimu na zinatumika, imejenga jiko la muda na kila mzazi/mlezi anachangia TZS 300/=; kwa sasa shule ina jumla ya TZS 130,000/= kwa ajili ya kutoa uji kwa wanafunzi wote wakiwa shuleni. Michango ya wazazi/walezi ni endelevu.

Maboresho katika miundombinu yameongeza mahudhurio ya wanafunzi; walimu wameweza kuwasimimamia kikamilifu wanafunzi kuwepo darasani muda wote, kuwafikia katika madawati yao na kuwasaidia kusoma, kuandika, kuhesabu na kukokotoa. Wanafunzi kwa upande wao wanafurahia kukaa kwenye madawati, kuwepo kwenye mazingira yaliyopangwa ya shule na kutumia maeneo ya shule kwa michezo na riadha. Haya yote yameboresha uwezekano wa kufaulu mitihani ya kitaifa.



***Madarasa na vyoo vipya katika shule ya msingi Mkuyuni***

Ujanishaji na upendezeshaji wa mazingira ya shule; jamii, walimu na wanafunzi wameungana katika kupendezesha mazingira ya shule. Kuandaa bustani na kupanda miti kumefanya shule hii mpya kuwa ya kuvutia na safi. Kutokana na kupungua kwa msongamano wa wanafunzi, uwezekano wa magonjwa ya mlipiko umepunguzwa sana. Mazingira ya shule yana hewa ya kutosha yakiambatana na upepo mwororo unaotawanya hewa ya oksijeni kutoka kwenye miti kuelekea madarasani na maofisini. Picha zilizopo hapa chini zinaonesha mazingira mazuri ya Shule ya Msingi Mkuyuni.



***Mazingira mazuri ya shule***

Elimu ya uhifadhi; ushiriki wa wanafunzi katika kuandaa bustani, kupanda miti, kumwagilia maji na kutunza miti umejenga stadi mpya na mtazamo chanya kuhusu miti na utunzaji wa miti. Mabadiliko haya yalioanzia shuleni yamesambaa kwenye jamii na kupunguza kasi ya uharibifu wa misitu. Walimu wamejikita katika kuandaa wanafunzi kuwa mabalozi wa upandaji miti katika kaya zao.

## 7.0 MIKAKATI YA UENDELEVU

Katika kuhakikisha jitihada hii ni endelevu, jamii imepanga kujenga miundombinu zaidi ya shule kukidhi mahitaji yote. Jamii imemiliki 4ha za ardhi kwa ajili ya upanuzi wa shule. Halmashauri inaendelea kuisaidia jamii kikamilifu kwa kutumia fedha za elimu bure zinazotolewa na serikali, mapato ya ndani na michango ya jamii.

Kuimarisha Kamati za Ujenzi za Kata na Kijiji; hili litatekelezwa kwa kuendesha mafunzo kuhusu ufuatiliaji na usimamizi wa miradi na shughuli za maendeleo. Mkakati mwingine muhimu ni kuwaelekeza maafisa watendaji wa Kata na Vijiji kutoa taarifa za mapato na matumizi za mwezi au robo mwaka kwa uwazi katika mikutano ya hadhara ya vijiji na katika Kamati ya Maendeleo ya Kata. Mkakati huu utaongeza uaminifu na kufanya jamii kuendelea kushiriki katika harakati za maendeleo.

Ushirikishwaji wa jamii kutoa maoni katika uandaaji wa miradi, utekelezaji, ufuatiliaji na tathmini umeimarisha uwezo wa jamii katika shughuli za maendeleo na kujenga hali ya umiliki vyote vikisababisha uendelevu wa jitihada za maendeleo.

**8.0 SIRI YA MAFANIKIO**

Siri ya mafanikio ya jitihada hii ni;

(i) Kujitoa kwa jamii katika michakato yote ya utekelezaji wa mradi.
(ii) Wanajamii wanaopenda kufanya kazi na wenye malengo thabiti.
(iii) Timu ya Menejimenti ya Halmashauri iliyojikita kikamilifu katika kusimamia na kutoa utaalamu na ushauri kwa watekelezaji wa mradi.
(iv) Uwepo wa utashi wa kisiasa kusaidia jitihada hii.
(v) Uwazi katika mapato na matumizi kwenye utekelezaji wa mradi.

# HALMASHAURI YA WILAYA YA TABORA

**JITIHADA ZA JAMII KATIKA KUANZISHA SHULE YA SEKONDARI**



***Uzoefu wa Kata ya Kizengi***

**1.0 UTANGULIZI**

Halmashauri ya Wilaya ya Tabora ni mojawapo ya Halmashauri 8 za Mkoa wa Tabora na inapakana na H/W za Igunga na Nzega upande wa Kaskazini, Sikonge upande wa Kusini, Urambo na Kaliua upande wa Magharibi, Manyoni (Mkoa wa Singida) upande wa Mashariki na Kahama (Mkoa wa Shinyanga) upande wa Kaskazini Magharibi. Halmashauri inapatikana katika Latitudo $05^{0}04'$ na $06^{0}15'$ Kusini na Longitudo $32^{0}15'$ na $32^{0}00'$ Mashariki ikiwa na eneo la 13,453km$^2$. Kwa mujibu wa sensa ya 2002 jamii ya Kizengi ina wakazi 21,356; wanaume 10,498 na wanawake 10,858, ongezeko la watu la 2.8% kwa mwaka na kaya 3,558. Makabila makuu katika Kata ya Kizengi ni wasukuma, wanyamwezi na wanyiramba; wasukuma wakiwa wengi zaidi.

H/W ya Tabora ina shule 18 za sekondari ikiwemo 1 ya kidato cha 5na6 (Shule ya Sekondari ya Ndono). Aidha, kuna sekondari 7 ambazo hazijasajiliwa zinazojumuisha shule ya sekondari ya Kizengi ambayo inachambuliwa hapa. Kata ya Kizengi ni mojawapo ya kata 30 za H/W ya Tabora yenye shule za msingi katika vijiji vya Kizengi, Malongwe, Kabisile, Isuli na Mwamdaki.

Kata hii ina vijiji 6 vya Mpumbuli, Malongwe, Mwamdaki, Kabisile, Isuli na Kizengi na Vitongoji 32. Huduma za usafirishaji zinapatikana kwani Kata ipo pembezoni mwa reli ya kati na barabara kuu ya Tabora - Dar es Salaam. Shughuli kuu ya kiuchumi in ufugaji, ikifuatiwa na kilimo na ufugaji nyuki. Mazao makuu yanayozalishwa ni mahindi, muhogo, viazi vitamu, karanga na mtama. Kuna wafanyabiashara wadogo hasa wachuuzi wa asali na wenye maduka madogo ya mahitaji ya nyumbani.

**2.0 TATIZO**

Kata ya Kizengi ipo pembezoni mwa Halmashauri na ina changamoto mbalimbali katika sekta za elimu, maji na afya. Hitaji kuu la Kata hii lilikuwa shule ya sekondari kwani wanafunzi walilazimika kwenda shule ya jirani ya sekondari ya Tura katika Kata ya Tura umbali wa 65km. Umbali huu ukiambatana na mapori na uwepo wa wahuni njiani ulisababisha matatizo kama ubakaji, mimba za utototni na matumizi ya madawa ya kulevya. Hali hii iliongeza utoro hadi kufikia 52%. Jedwali 1 linaonesha umbali kutoka vijiji 6 vya kata ya Kizengi kwenda Sekondari ya Kata ya Tura.

**Jedwali 1: Umbali kutoka Kata ya Kizengi Kwenda Sekondari ya Tura**

| KIJIJI | UMBALI KWA KM |
|---|---|
| Kizengi | 45 km |
| Kabisile | 50 km |
| Malongwe | 35 km |
| Mdaki | 65 km |
| Isuli | 32 km |
| Mpumbuli | 55 km |

Utoro ulichangiwa na wanafunzi kuwepo mbali na familia zao, kukosa walezi bora, kuishi katika makazi duni na kutokuwepo kwa chakula cha kutosha. Wanafunzi wa kike walilazimika kuishi katika upweke bila mahitaji ya msingi hali iliyosababisha vishawishi na mimba (Jamii ya Kizengi ilishuhudia mimba za wanafunzi 3-5 kila muhula). Jedwali 2 inaonesha taarifa za utoro. Kwa mfano kati ya wavulana waliochaguliwa kujiunga na Sekondari ya Tura mwaka 2007 ni 16 tu walioandikishwa na 9 tu ndio waliomaliza kidato cha nne. Ikumbukwe kabla ya mwaka 2015 Tura na Kizengi zilikuwa katika Kata moja ya Tura.

**Jedwali 2: Hali ya Utoro**

| KATA | JINA LA SHULE | MWA KA | WALIOCHAGULIWA | | | WALIOANDIKISHWA | | | WALIOMALIZA KIDATO IV | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | BOYS | GIRLS | TOTAL | BOYS | GIRLS | TOTAL | BOYS | GIRLS | TOTAL |
| Tura | Tura | 2007 | 48 | 32 | 80 | 16 | 11 | 27 | 9 | 6 | 15 |
| | Tura | 2008 | 23 | 17 | 40 | 21 | 15 | 36 | 7 | 4 | 11 |
| | Tura | 2009 | 55 | 38 | 93 | 52 | 27 | 77 | 14 | 8 | 22 |
| | Tura | 2010 | 37 | 24 | 61 | 30 | 14 | 44 | 10 | 3 | 13 |
| Tura and Kizengi | Tura and Kizengi | 2015 | 66 | 49 | 115 | 63 | 42 | 105 | 39 | 23 | 62 |
| | Tura and Kizengi | 2016 | 46 | 44 | 90 | 46 | 44 | 90 | 37 | 36 | 73 |
| | Tura and Kizengi | 2017 | 74 | 74 | 148 | 72 | 70 | 142 | 63 | 62 | 125 |

Baadhi ya wanafunzi waliathirika na kujunga na vikundi vya wahuni na watumia madawa ya kulevya, wakijikita katika kutumia, kuuza bangi na kuvuta sigara. Kijiji cha Tura ni kituo ambapo madereva na wahudumu wa magari makubwa ya safari ndefu hupumzika. Uwepo wao ulichangia sana wanafunzi wa kike na kiume kuwa katika mazingira hatarishi. Baadhi ya wanafunzi walioacha masomo katika sekondari ya Tura walisema. *"jina langu ni Lucia Edward….nina miaka 24, nilianza masomo katika sekondari ya Tura mwaka 2008 na nikaacha mwaka 2010 nikiwa kidato cha pili kwa sababu ya mimba……hakuna ambalo ningeweza kufanya…….kwani kulikuwa hakuna chakula, wala ada….pote palijaa wanaume"*.

Mwathirika mwingine, Susana Daniel Masile mwenye umri wa miaka 25, alianza kidato cha kwanza katika sekondari ya Tura mwaka 2008 na akaacha shule mwaka 2010 kwa sababu ya mimba. Susana alisema *"mazingira ya shule hayakuwa rafiki kwetu….tulipanga vyumba kijijini, tukiwalipa wamiliki wa nyumba kwa mwezi….hakuna fedha kutoka nyumbani……nilijikuta nikiwa mjamzito…..ikanibidi niache shule nikiwa kidato cha tatu……"*



***Lucia and Suzan wakiwa kijijini Kizengi***

Bwana Mtembezi Boniface alisema, *"nina miaka 25, nilianza kidato cha kwanza mwaka 2008 na kumaliza kidato cha nne mwaka 2011……nilifeli mtihani wa Taifa kutokana na changamoto mbalimbali…….umbali……nikaamua kupanga chumba……wazazi wangu walishindwa kunisaidia chakula na kodi ya chumba……..tukaamua kuishi kwenye makundi……..wavulana wanne kwenye chumba kimoja ili kuchangia kodi…….hali hii haikuwa rafiki……tuliamua kuanzisha biashara ndogondogo badala ya kusoma……wengine walianza kuchoma mkaa……nilijiunga na makundi mabaya kijijini na kuanza kutumia*

*na kuuza madawa, pamoja na kuvuta bangi".* Picha iliyopo hapa chini inaonesha vijana watatu ambao walikumbana na changamoto hizi kipindi cha shule katika sekondari ya Tura; wawili waliacha shule na mmoja alimaliza lakini hakufaulu.




***Kutoka kushoto ni Halfan Salum, Mtembezi Boniface na Makenzi Holela***

**3.0 LENGO**

Elimu ya sekondari nchini Tanzania imeandaliwa kipekee ili kuunganisha na kupanua wigo wa fikra, elimu, stadi na kanuni zinazotolewa na kuendelezwa katika elimu ya msingi. Elimu ya sekondari inapendekezwa na serikali ili kuendeleza na kuuenzi umoja wa kitaifa, kutambulika na maadili, kujiheshimu, kuheshimu na kuwa tayari kufanya kazi, haki za binadamu, sifa za kiutamaduni na maadili, mila, desturi, majukumu na wajibu wa kijamii.

Kwa kuzingatia umuhimu wa elimu ya sekondari kitaifa serikali imezitaka Kata zote kuanzisha shule ya sekondari. Kutokana na historia hii na kwa kushirikiana na H/W ya Tabora, jamii ya Kizengi ilikubali kwa ujumla kuanzisha shule ya sekondari ya kata kwa lengo kuu la kuboresha utoaji wa elimu ya sekondari kwa wanafunzi wanaomaliza darasa la saba katika shule saba za msingi. Malengo mahsusi ya jamii yalikuwa kujenga miundombinu ili kuanzisha shule ya sekondari, kupunguza umbali ambao wanafunzi walitembea kwenda sekondari ya Tura, kutokomeza utoro na mimba za utotoni na kuongeza ufaulu kwenye mitihani ya kitaifa.

**4.0 MIKAKATI YA UTEKELEZAJI**

Wazo la kujenga shule ya Sekonbdari ya Kizengi lilianza Mei, 2011. Wanajamii waliukabili uongozi wa Kata na kuwasilisha pendekezo la kuanzisha shule. Pendekezo hili lilikubaliwa na viongozi walianzisha kampeni katika vijiji vyote. Mikutano ya vijiji iliendeshwa kulitangaza pendekezo la kuanzisha shule ya sekondari ya Kata ya Kizengi. Maazimio yaliyofikiwa katika mikutano hiyo yalijumuisha utafutaji wa ardhi kwa ajili ya kujenga shule na kuanzisha michango. Kijiji cha Kizengi kilitoa ardhi ya ekari 50 bure. Aidha ilikubalika kuwa kila kaya ichangie; wafugaji TZS 20,000/=, wafanya biashara wadogo TZS 15,000/= na wakulima TZS 10,000/=. Wakazi wote walitarajiwa kuchangia nguvukazi kipindi chote cha utekelezaji wa mradi.

Ukusanyaji wa michango; ukusanyaji ulianza Mei 2011, na ilipofika Julai 2011 jumla ya TZS milioni 11 zilikusanywa. Fedha hizi zilitumika kununua saruji na usafirishaji wa vifaa vya ujenzi. Jamii ilifyatua matofali ya zege 3,000 na ilipofika Januari 2012, jamii ilikamilisha ujenzi wa msingi wa jengo la madarasa manne. Aidha, ilikubalika kuwa michango iwe endelevu. Hadi Januari 2018, jamii ilikuwa imekusanya TZS 96.4 million kwa ajili ya mradi wa sekondari. Octoba 2017, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

alitembelea Mkoa wa Tabora na kupewa taarifa ya Mradi wa Kata ya Kizengi na kuamua kuchangia TZS 5 million kusaidia jitihada za jamii.

Usaidizi wa kitaalam; Halmashauri ilitoa ushauri wa kitaalamu kwa kuandaa michoro, andiko la makadirio ya gharama za ujenzi, usimamizi na ufuatiliaji wa shughuli za ujenzi. Baadaye Halmashauri iliwapanga walimu, ikatoa vifaa vya elimu na kufungua shule hata kabla ya usajili kukamilika kuwapunguzia wanafunzi adha ya umbali kwenda shule ya Sekondari ya Tura.

## 5.0 RASILIMALI

Halmashauri na jamii zilitumia aina mbalimbali za rasilimali kukamilisha jitihada hii. Jedwali 3 hapa chini linaonesha rasilimali fedha.

**Jedwali 3: Rasilimali Fedha**

| | | | |
|---|---|---|---|
| **Awamu 1** | | | |
| **Mwaka** | **Shughuli** | **Fedha** | **Chanzo** |
| **2011/12-2013/14** | Ujenzi wa madarasa 4, nyumba ya mwalimu, maabara 3 na vyoo 3 | 54,464,400 | Jamii |
| | | 40,000,000 | H/W Tabora |
| **Sub-total** | | **94,464,400** | |
| **Awamu 2** | | | |
| **2015/2016** | Ujenzi wa jengo la utawala, madarasa 2 | 43,302,000 | Jamii |
| | Vifaa vya maabara | 5,000,000 | Rais |
| | Ujenzi wa zahanati | 5,000,000 | Rais |
| | Jengo la utawala | 21,000,000 | H/W Tabora |
| **Jumla ndogo** | | **74,302,000** | |
| **JUMLA** | | **168,766,400** | |

## 6.0 MATOKEO

H/W ya Tabora na Jamii ya Kata ya Kizengi zimefanikiwa kuwa na makubalino na muungano katika vijiji ambao umewezesha utekelezaji bora wa jitihada hii. Matokeo makuu ya jitihada hii yametajwa kwa muhtasari katika kisanduku 1 hapa chini.

**Kisanduku 1: Muhtasari wa Matokeo**

- *Shule ya Kata imefunguliwa na inafanya kazi*
- *Wanafunzi wanahudhuria masomo katika Kata yao kutoka vijiji 6 na vitongoji 32*
- *Umbali umepunguzwa toka 50km hadi kati ya 0km na 10km*
- *Utoro umepunguzwa kutoka 52% hadi 13.6% na lengo 5% mwaka 2018*
- *Mimba za ututoni zimetokomezwa*
- *Matumizi ya madawa yametokomezwa na wanafunzi wanaendelea na masomo kwa utulivu karibu na vijiji vyao, wengi wakiishi katika familia zao*
- *Wanafunzi wanapata chakula cha mchana shuleni*
- *Uandikishaji na usajili katika shule ya sekondari umeongezeka kutoka wanfunzi 28 hadi 99. Mwaka 2015 shule ilianza na wanafunzi 28; idadi inaongezeka kwani wanafunzi wanahama kutoka shule nyingine kuja shule ya sekondari ya Kizengi kwani ina mazingira rafiki. Kwa sasa shule ina wanafunzi 99 kuanzia kidato cha I hadi III na inatarajiwa kuwa mwaka 2018 wanafunzi watazidi 150*
- *Hatari zilizowakabili wanafunzi zimetokomezwa*
- *Mwaka 2016, wanafunzi wote walifaulu mtihani wa kidato cha II, ishara kuwa elimu bora ya sekondari inatolewa*
- *Wazazi na jamii kwa ujumla wanafurahia mafanikio ya jitihada hii.*

Kukamilika kwa miundombinu ya msingi kumeruhusu jamii kuongeza miradi na kujikita katika ujenzi wa nyumba za walimu na maabara.



***Nyumba ya mwalimu***



***Maabara ya Biolojia***



***Maabara zikijengwa***



***Ujenzi wa madarasa 2 na jengo la utawala***

Utoaji wa chakula cha mchana kwa wanafunzi; kila familia yenye mwanafunzi inachangia TZS 4,000/= kwa mwaka kwa kutoa fedha taslimu, mifugo ua mazao. Shule ina shamba ambalo huzalisha mahindi kwa ajili ya chakula cha wanafunzi. Wanafunzi ambao vijiji vyao vipo mbali kuanzia 10km na zaidi huhifadhiwa katika nyumba za kupanga katika kijiji cha Kizengi; hata hivyo jamii yote huwapatia ulinzi na malezi stahiki kuhusu tabia na heshima.



***Wanafunzi wakila chakula cha mchana shuleni***

**7.0 MIKAKATI YA UENDELEVU**

H/W ya Tabora na jamii ya Kizengi zina mipango mbalimbali ya kuhakikisha jitihada hii ni endelevu na shule inaendeshwa kwa ubora unaotakiwa. Jamii imewapa jukumu viongozi wa kuchaguliwa kama diwani, wenyeviti wa vijiji sita na wenyeviti 32 wa vitongoji kuhakikisha kuwa shule inaendelea bila vikwazo. Aidha, Kamati ya Maendeleo ya Kata ina agenda ya kudumu katika mikutano yake kuhusu maendeleo ya shule hii na afua zinazotakiwa kwa ajili ya uendelevu.

Kuhusu uendelevu wa rasilimali fedha, jamii imeazimia kuendelea kutoa michango ya aina yoyote iwezekanayo kuhakikisha shule yao ya sekondari inafanya vizuri katika Nyanja zote na ni endelevu.

Halmashauri inaendelea kutenga bajeti ya maendeleo kila mwaka na kuongeza walimu na wafanyakazi ikiwa ni pamoja na vifaa vya elimu katika shule hii. Mikakati hii itajenga uwezo wa shule na kuipandisha kuwa shule ya sekondari kamili kwani kwa sasa inaendeshwa kama shule shikizi ya shule ya sekondari ya kata ya Tura. Mchakato wa kusajili shule utakamilisha jitihada ya kuanzisha shule ya Sekondari ya Kata ya Kizengi.

**8.0 SIRI YA MAFANIKIO**

Shule ya sekondari ya kata lilikuwa hitaji halisi la pamoja la jamii lilizalisha utayari na uhiari wa wanajamii kuchangia kwa uwezo wote uanzishaji, uendeshaji na maendeleo ya shule. Haya yote yaliwezeshwa na uongozi bora na utashi wa kisiasa.

# HALMASHAURI YA WILAYA YA KASULU


**JITIHADA ZA KIKUNDI CHA VIJANA KATIKA KULETA MABADILIKO YA KIJAMII NA KIUCHUMI**



*Uzoefu wa Kikundi cha Vijana cha Mboni katika Kijiji cha Zeze*

**1.0 UTANGULIZI**

Halmashauri ya Wilaya ya Kasulu ni mojawapo ya Halmashauri 8 za Mkoa wa Kigoma ambayo inapatikana Magharibi mwa Tanzania upande wa Kaskazini – Magharibi mwa Mkoa wa Kigoma. Halmashauri hii ilianzishwa mwaka 1983, ikiwa na eneo la 5,324km² ambalo ni sawa na 10.62% ya eneo lote la mkoa wa Kigoma. Kwa mujibu wa sensa ya mwaka 2012 Halmashauri ina wakazi 425,794 (wanawake 218,373 na wanaume 208,244) kwa ongezeko la watu la 2.4% kwa mwaka. Idadi ya kaya ni 63,695 zenye wastani wa watu 7.6.




***Ramani ya H/W Kasulu***

Uchumi wa Halmashauri hutegemea kilimo kinachoajiri 85% ya wakazi. Kilimo kinajumuisha uzalishaji wa mazao na ufugaji. Mazao makuu ya chakula ni pamoja na mahindi, maharage, muhogo, viazi vitamu, ndizi, mpunga na mbogamboga na mazao ya biashara hujum uisha kahawa, tumbaku, tangawizi na miwa. 15% ya wakazi hufanya shughuli za ufugaji wa nyuki na bishara ndogondogo.

Kikundi cha Vijana cha Mboni ni kikundi cha kijamii kinachoendeshwa na vijana wenyewe kilichoanzishwa mwaka 2014 na kusajiliwa na H/W ya Kasulu kwa namba 0057 na kuweka makao makuu yake katika kijiji cha Zeze. Kikundi cha Mboni kinashughulika na kubadili maisha ya watu kwa uendelezaji wa ujasiriamali, utunzaji wa mazingira na utoaji wa elimu kwa makundi mbalimbali. Historia ya kikundi cha Mboni ilianza na Bwana Benedicto Hosea ambaye aliwahamasisha vijana kuanzisha asasi hii. Jina "Mboni ya Vijana" linaashiria hamu ya kuwafanya vijana kuwa wenye akili, maono na uwezo katika jamii kwa kuanzisha vita dhidi ya umaskini; na kuleta maendeleo na ustawi katika maisha.

Kikundi kilianza na vijana 7 na hadi mwaka 2018 kilikuwa na wanachama hai 13. Kikundi cha Mboni ya Vijana huendesha shughuli zake kwa kutumia vibarua na vijana wa kujitolea ambao wana upendo wa kufanya kazi katika asasi za msingi za kunyanyua watu maskini na kuwaletea maendeleo na ustawi.

**2.0 TATIZO**

Jamii za maeneo ya vijijini za Kigoma zina umaskini uliokithiri, kutokujua kusoma na miundombinu duni kijamii na kiuchumi. Kijiji cha Zeze kipo pembezoni mwa Halmashauri na kina wakazi wapatao 8,400 wa

kabila asili la Waha, kikiwa 45km Kusini – Magharibi mwa Mji wa Kasulu na 69km Kaskazini – Mashariki mwa mji wa Kigoma. Kijiji cha zeze hukumbana na changamoto nyingi kama ukosefu wa ajira, mbinu duni za kilimo (hasa kilimo cha kuhamahama), upungufu wa huduma za maji, ukosefu wa elimu na stadi za biashara, ukosefu wa mitaji, kutokuwepo kwa kituo cha elimu ya ufundi ili kutoa mafunzo ya stadi teknolojia na ukosefu wa uongozi kwa vijana ili kuwasaidia kuanzisha na kuendesha programu za maendeleo. Changamoto hizi huchochea umaskini wa kipato, kutokuwepo kwa maendeleo na huduma duni za kijamii na kiuchumi. Kikundi cha Mboni ya Vijana kilianzishwa ili kupambana na changamoto hizi zinazoonesha umaskini katika kijiji cha Zeze. Picha iliyopo hapa chini inaonesha mbinu duni za kilimo zinazosababisha kupotea kwa misitu.



***Uharibifu wa misitu utokanao na mbinu duni za kilimo***

---

**3.0 LENGO**

Lengo kuu la jitihada hii lilikuwa kuunda mazingira wezeshi ambayo yanaweza kutengeneza ajira na kuleta uhakika wa kipato na chakula kwa vijana na jamii. Aidha, jitihada hii ililenga;

(i) Kuanzisha na kusimamia kilimo bora na endelevu kwa kutoa mafunzo, kuwezesha na kufuatilia mashamba yanayomilikiwa na vijana na kaya mojamoja.
(ii) Kuhakikisha uwepo wa uhakika wa kipato na chakula kwa vijana, familia na jamii na kutokomeza kilimo duni kinachotishia mazingira.
(iii) Kuanzisha na kusimamia viwanda na biashara ndogondogo kwa ajili ya vijana na wanawake.
(iv) Kutoa mafunzo na kuhimiza ubunifu, ugunduzi na mabadiliko ya kidunia kiuchumi na hali ya hewa kwa vijana na jamii.

**4.0 MIKAKATI YA UTEKELEZAJI**

Kikundi cha Mboni ya Vijana kilianzishwa ili kuinua hali ya maisha ya watu walioishi katika umaskini uliokithiri. Katika kutekeleza jitihada hii mikakati ifuatayo ilitumika.

Ujenzi wa uelewa; uelewa ulihusu kuwafumbua macho watu kuhusu hali halisi ya umaskini kijijini na kubadilishana fikra kuhusu mbinu za kutatua tatizo la umaskini. Ujenzi wa uelewa ulianza mwaka 2012 kwa kuwakusanya vijana na kuwahamasisha wajiunge kwenye vikundi ili kujadili changamoto za umaskini na kuainisha afua zake. Uhamasishaji ulifanyika kupitia mikutano isiyo-rasmi ambayo iliwezesha kuundwa kwa kikundi cha Mboni ya Vijana mwaka 2013.

Kusajili Kikundi; mwaka 2014 Halmashauri ilipendezwa na jitihada za kikundi na kukisajili kama asasi ya kijamii kwa namba ya usajili 0057. Jukumu kubwa la kikundi kuhusu utunzaji wa mazingira ulisababisha

Halmashauri kukiunganisha na asasi nyingine zenye jitihada kama hii.

Kuandaa picha za Satellite za Kijiji cha Zeze; kikundi cha mboni ya vijana kikishirikiana na taasisi ya Janet Chapman ya Uingereza kiliunda ramani ya kimtandao ya Kijiji cha Zeze kwa kutumia teknolojia ya Ramani Wazi ya Mtaa (Open Street Map - OSM) na mfumo wa simu za Android wa *Maps.Me* na kufanya kijiji cha Zeze kuweza kupatikana katika ramani ya kidigitali kupitia gumisha (satellite).




***Sura ya satellite ya kijiji cha Zeze kutoka juu***

Kuanzisha kituo cha Kikundi; ili kuratibu kwa ufanisi shughuli za kikundi, kikundi kilitafuta na kumiliki ekari 20 za ardhi ambayo ilitolewa na Halmashauri ya Kijiji na kuanzisha kituo chenye ofisi na karakana kwa ajili ya kufundisha na kuratibu shughuli za kiuchumi kama mashamba darasa, mabwawa ya samaki na visima vya maji. Picha zilizopo hapa chini zinaonesha wanachama wa kikundi wakishiriki shughuli za kiuchumi katika shamba la mfano.



***Shughuli za kiuchumi za kikundi***

Ujenzi wa miundombinu ya ofisi; kabla ya ujenzi huu kikundi hiki kilifanya shughuli zake katika jengo la walilopewa na wazazi wa mwanzilishi wa kikundi. Baadaye kikundi kiliamua na kuanza ujenzi wa jengo la ofisi na karakana. Picha zilizopo hapa chini zinaonesha ujenzi wa jengo la ofisi na karakana ukiendelea.



***Jengo la ofisi, mashine katika karakana na kisima cha maji***

Kuanzisha vitalu vya miti kwa lengo la kutunza mazingira; ili kukabili tatizo la kutoweka kwa miti na misitu kikundi kikishirikiana na Halmashauri kilianzisha vitalu vya miti katika maeneo mbalimbali. Miche iliyopatikana ilipandikizwa katika eneo linalozunguka kituo cha kikundi na mingine iligawanywa kwa jamii na kupandikizwa katika maeneo ya kaya. Halmashauri ilisaidia kikundi kwa kutoa ushauri wa kitaalamu na kugawa mifuko maalumu ya kupanda mbegu za miti. Picha iliyopo hapa chini inaonesha uanzishaji wa kitalu cha miche ya miti.



***Kitalu cha miti kikiandaliwa***

Kuanzisha shughuli za kiuchumi na uzalishaji; kikundi kilianzisha shughuli hizi kwa lengo la kuinua vipato, kutunza mazingira na kituo cha kujifunzia. Shughuli za kiuchumi na uzalishaji zinajumuisha kilimo ambapo kikundi kimejikita katika uzalishaji wa mahindi, maharage na mbogamboga. Shughuli nyingine ni ufugaji wa nyuki, ufugaji wa samaki, uungaji wa vyuma, useremala na uchimbaji wa visima vya maji. Halmashauri ilitoa ushauri wa kitaalamu katika kuanzisha shughuli hizi za kiuchumi. Picha zilizopo hapa chini zinaonesha baadhi ya shughuli za kiuchumi za kikundi.



***Ufugaji nyuki,***



***Ufugaji samaki,***



***Utengenezaji wa sabuni***



***Uchimbaji wa visima***

Kutoa elimu kwa wanafunzi na vijana waliokosa elimu ya msingi na sekondari; ili kupambambana na ujinga na kutokujua kusoma kama ilivyo kwenye sera ya taifa, kikundi kiliamua kuanzisha madarasa kwa

wote ambao hawakupata elimu ya msingi. Kikundi kiliingia katika shughuli hii ili kuwezesha vijana wengi kujua kusoma na kuandika ili kuwafanya wazalishaji bora katika jamii na kuimarisha shughuli zao za vipato. Picha zilizopo hapa chini zinaonesha wanafunzi wakijifunza.



***Wanafunzi darasani***

Kutafuta ufadhili wa nje; Kikundi cha Mboni ya Vijana kilipanua mtandao wake hadi nje ya Halmashauri na kupata ufadhili wa kitaalamu na rasilimali. Kikundi kiliandaa andiko la mradi na kutuma kwa taasisi mbalimbali ndani ya nchi na kimataifa. Shughuli zinazofanywa na kikundi ziliwavutia wafadhili kadhaa ambao walichukua hatua za kutoa ufadhili wa rasilimali na utaalamu kuendeleza shughuli za kikundi. Wafadhili hao ni Amenity Non-Profit Charity Organization (ANCO) iliyoko Kigoma, Kawie Social Development Foundation (KASODEFO) iliyopo Maswa, Women Chamber of Commerce (TWCC) iliyopo Dar es Salaam, Institute of Rural Development Planning (IRDP) iliyopo Dodoma, Kisangani Blacksmith, Southern Highlands Organization (SHIPO) ya Njombe, SeedChange Tanzania ya Kigoma na the Foundation for Civil Society (FCS) iliyopo Dar es Salaam. Mashirika ya kimataifa ni pamoja na King's College, Imperial College na GlobalGiving (GG) za Uingereza na Marekani, Local Electricity One (LE1) ya Uingereza na Australia na The Pollination Project ya Marekani.

Kuendesha mafunzo ya kuzalisha umeme kwa mitambo ya upepo; Julai 2017, kikundi cha mboni ya vijana kiliandaa warsha ya mafunzo kwa vijana yaliyohusu uzalishaji wa umeme kwa kutumia mitambo ya upepo. Warsha hii iliwezeshwa na Kampuni ya Local Electricity One ya Australia na Uingereza. Warsha ilihusisha washiriki kutoka Kijiji cha Zeze na Chuo cha Mipango ya Maendeleo Vijijini (IRDP). Lengo la warsha lilikuwa kujenga uwezo wa vijana kuunda mitambo ya upepo ya kuzalisha umeme kwa kutumia rasilimali asilia na takataka/masalio ya vifaa vya umeme. Lengo la kuiga teknolojia ya mitambo ya upepo ni kutengeneza nishati endelevu ambayo ni rafiki kwa mazingira.



***Uundaji wa mitambo ya umeme wa upepo***

**5.0 RASILIMALI**

Uanzishaji wa Kikundi cha Mboni ya Vijana na utekelezaji wa jitihada hii ulitumia rasilimali watu, fedha na vitu mbalimbali; kuna wanachama hai 13 ambao wanashughulika kwa pamoja na kusaidiana na

kamati ya menejimenti ya wajumbe watano wa kujitolea. Kikundi kina miundombinu mbalimbali ya kufanyia kazi ikiwa ni pamoja na karakana, jengo la ofisi, bwawa la samaki, ardhi na stoo kama inavyoelezwa kwenye jedwali namba moja hapa chini.

**Jedwali 1: Rasilimali mbalimbali**

| Na | Rasilimali | kiasi | Thamani (TZS) | Chanzo |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Ardhi | Ekari 20 | haijulikani | **Serikali ya Kijiji** |
| 2 | Stoo | 1 | 13,295,000 | **Kikundi na wafadhili** |
| 3 | Choo | 1 | 3,845,000 | **Kikundi na Misaada** |
| 4 | Jengo la Utawala | 1 | 11,789,300 | **Kikundi** |
| 5 | Kisima cha Maji | 1 | 4,760,000 | **Kikundi na Misaada** |
| 6 | Jengo la karakana na useremala | 2 | 7,500,000 | **Kikundi na Misaada** |
| 7 | Bwawa la samaki | 2 | 6,850,000 | **Kikundi na Misaada** |
| 8 | Shamba la minazi | 1362 | 6,810,000 | **Kikundi na Misaada** |
| 9 | Miti ya Asili | 40,000 | 800,000,000 | **Miti iliyohifadhiwa** |
| 1 0 | Shamba la Migomba | 300 | 1,500,000 | **Kikundi** |
| 11 | Mizinga ya Nyuki | 65 | 3,900,000 | **Kikundi na Misaada** |
| 12 | Jenereta | 1 | 3,800,000 | **Kikundi na Misaada** |
| 13 | Oltoneta | 1 | 2,600,000 | **Kikundi na Misaada** |
| 14 | Mfumo wa kusambaza umeme | 1 | 2,268,000 | **Kikundi na Misaada** |
| 15 | Vifaa vya karakana na useremala | 57 | 3,986,500 | **Kikundi na Misaada** |
| 16 | Vifaa vya kuzalisha sabuni | 52 | 2,640,700 | **Kikundi/Mkopo** |
| 17 | Samani za ofisi | 24 | 840,000 | **Kikundi** |
| 18 | Vifaa vya jikoni | 70 | 1,400,000 | **Kikundi** |
| 19 | Mitambo ya kuchimba visima vya maji | 8 | 24,689,000 | **Kikundi na Misaada** |
| 20 | Kompyuta mpakato | 6 | 4,440,000 | **Msaada** |
| 21 | Simu pana (tablets) | 11 | 1,320,000 | **Msaada** |
| 22 | Vitabu | 96 | 1,152,000 | **Msaada** |
| 23 | Mashine za kurudufu | 1 | 460,000 | **Kikundi** |
| 24 | Pampu za maji | 2 | 1,118,000 | **Kikundi na Misaada** |
| 25 | Zana za kilimo | 30 | 450,000 | **Kikundi na Misaada** |
| 26 | Zana za umwagiliaji | 0 | 1,688,900 | **Msaada** |
| 27 | Makabati ya kutunza kumbukumbu | | | **kikundi** |
| 28 | Mavazi ya Kazi | 13 | 650,000 | **Kikundi na Misaada** |
| | **JUMLA** | | **913,752,400** | |

## 6.0 MATOKEO

Kikundi cha Mboni ya Vijana kinasaidia vijana na wanawake katika; kupata elimu ya biashara ndogondogo na mitaji kupitia skimu ya mikopo midogo na kuanzisha kilimo endelevu (mfuko wa kilimo chenye tija) kwa kuwapatia mikopo wakulima wadogo ili kuhakikisha uzalishaji wa juu kwa ekari na uhakika wa chakula. Hadi Machi 2015 kikundi kilikuwa kimehudumia wateja 378 ikijumuisha vijana na wanawake ambao walipata mafunzo na kupata mikopo chini ya skimu ya mikopo midogo. Kila mfaidika alipata mkopo-anzia wa biashara wa TZS 360,000 na kusaidiwa kuanzisha na kuendesha biashara ambazo kwa hakika ziliongeza vipato vyao.



***Wanawake wakiwa katika mafunzo na biashara***

Kikundi cha mboni ya vijana kinajihusisha na uchimbaji wa visima vifupi na virefu vya maji, uundaji na ufungaji wa pampu za Kamba za mikono kutatua tatizo la maji na kuendesha karakana ya uungaji vyuma na useremala. Shughuli nyingine ni pamoja na uzalishaji wa sabuni, ufugaji wa samaki, ufugaji wa nyuki na utunzaji wa mazingira.

Uwepo wa kamati ya kujitolea inayosaidia jamii; kikundi kinafanya kazi kupitia kamati ya menejimenti yenye wajumbe 5 wa kujitolea ambao wamejitoa kikamilifu na wapo makini katika kusukuma maendeleo na kuleta ustawi wa kijamii na kiuchumi kwa wakazi wa Zeze.

Kuongezeka kwa usalama wa chakula; kikundi kimeanzisha skimu ya kilimo endelevu ambayo inasaidia wakulima wadogo kujifunza mbinu za kilimo bora, kupata pembejeo za kilimo, kufanya ufuatiliaji na usimamizi wa mashamba na kuanzisha masoko yanayofaa. Katika msimu wa kilimo wa 2016/17 skimu ya majaribio ilifanyika ambapo ekari 35 za wakulima 28 na kikundi zilifikiwa; na uzalishaji ulikuwa kati ya gunia 18 – 24 za mahindi kwa ekari ikilinganishwa na uzalishaji wa gunia 0 –3 kabla ya skimu hii. Picha zilizopo hapa chini zinaonesha kuongezeka kwa uzalishaji.



***Kuongezeka kwa uzalishaji***

Kuongezeka kwa upatikanaji wa maji; Kikundi cha Mboni ya Vijana kilianzisha uchimbaji wa visima vya maji kwa kutumia teknolojia rahisi ya mikono na kufunga pampu zenye kamba za maji za mikono kwa lengo la kutatua changamoto ya upatikanaji wa maji. Mwaka 2016 kikundi kilichimba na kufunga pambu zenye Kamba katika kisima ambacho huzalisha lita 10,286 za maji kwa siku na kuhudumia watu 500 katika masaa 12. Aidha kikundi kimefunga pampu za mikono zenye Kamba katika visima vilivyokuwa vinatumia pampu za mikono aina ya India Mark II na Afridev ambazo ziliharibika; ili kuleta uhakika wa maji safi na salama kwa jamii.



***Pampu ya mkono kwa ajili ya maji safi na salama***

Uzalishaji wa ajira; kikundi hiki kina miundombiinu mbalimbali ambayo inatoa fursa za ajira kwa wanachama na vijana wengine wenye ari ya maendeleo. Miundombinu hii inajumuisha mizinga 65 ya nyuki, karakana ya uungaji wa vyuma na useremala, mabwawa 2 ya samaki, minazi 120, shamba 1 la migomba na kitalu 1 cha miche ya miti.

Utoaji wa elimu na mafunzo kwa vijana na watoto; kikundi cha Mboni ya Vijana kina mradi wa elimu ambao hutoa mafunzo kuhusu stadi za kusoma na kuandika kwa wale ambao walikosa elimu ya msingi katika umri wa kwenda shule. Aidha, mradi huu hujenga stadi za kutumia Kompyuta kwa vijana wote waliohitimu elimu ya msingi na sekondari. Chini ya Skimu hii ya elimu, kikundi kinafanya kazi kwa kushirikiana na shule zilizopo kijijini Zeze kwa kutoa vifaa vya kufundishia na kujifunzia na kuendesha vipindi vya masomo kwa vitendo. Vifaa vya kufundishia na kujifunzia ni pamoja na vitabu, simu kubwa za mikononi (tablets), visomeo vya ki-eletroniki (e-readers), Kompyuta, nishati ya umeme, mtandao na wi-fi.



***Watoto wakisoma vitabu katika Kituo cha Kikundi***

Utunzaji wa Mazingira; kikundi kimeshiriki kikamilifu katika usimamizi wa mazingira kupitia ufugaji wa nyuki, ufugaji wa samaki, upandaji wa minazi na uanzishaji wa kitalu cha miche ya miti. Kikundi

kimeweka alama na mabango yanayoonya watu kukata miti na kuchoma misitu. Matokeo ya jitihada hizi yamesaidia eneo la Zeze kutoathiriwa na moto kwa miaka miwili mfululizo na jamii imejifunza na kuiga utunzaji wa mazingira stahiki.



***Ufugaji wa Nyuki***

**7.0 MIKAKATI YA UENDELEVU**

Utayari wa jamii kushiriki katika jitihada hii ndio mwanzo wa uendelevu wa yote yanayofanyika katika Kijiji cha Zeze. Kikundi cha Mboni ya Vijana pamoja na H/W ya Kasulu wamedhamiria kuhakikisha jitihada hii ni endelevu kwa;

(i) Kuanzisha miundombinu ya kudumu ili kufanya huduma za jitihada hii kuwa endelevu.

(ii) Kuendelea kutoa elimu na stadi kwa wanachma na jamii ili kuimarisha ushiriki na uchangiaji katika jitihada hii.

(iii) Kuendeleza, kupanua na kuimarisha ushirikiano na wadau, marafiki na jamii yote ili kuendeleza jitihada hii ya kuleta maendeleo na ustawi kiuchumi na kijamii.

**8.0 SIRI YA MAFANIKIO**

Mafanikio ya jitihada hii ya kuleta maendeleo na ustawi kiuchumi na kijamii yalitokana na uongozi wa kipekee na kujitoa kikamilifu kwa wanachama wa kikundi cha Mboni ya Vijana. Aidha uwezeshi thabiti kutoka kwa washirika wa maendeleo na Halmashauri ulichangia kufikia matokeo haya makuu.

# HALMASHAURI YA WILAYA YA URAMBO

**JITIHADA ZA JAMII KATIKA UBORESHAJI WA HUDUMA ZA AFYA**





***Uzoefu wa Kijiji cha Motomoto***

## 1.0 UTANGULIZI

Halmashauri ya Wilaya ya Urambo ni mojawapo ya Halmashauri 8 za Mkoa wa Tabora iliyopo katika Latitudo $4^0$.420' na $5^0$.460' Kusini na Longitudo $31^0$.45' na $32^0$.300' Mashariki. Halmashauri inapakana na H/W za Sikonge na Tabora upande wa Mashariki, Mpanda (Mkoa wa Katavi) upande wa Kaskazini na Kaliua upande wa Magharibi. Halmashauri ina eneo la 6,110$km^2$ sawa na 8.2% ya eneo lote la Mkoa wa Tabora. Eneo linalofaa kwa kilimo ni 8.4%, eneo lenye maji ni 0.9%, hifadhi za misitu ni 52.3% na maeneo ya wazi na misitu ni 12.9%. Kiutawala, Halmashauri in Tarafa 2, Kata 18, Vijiji 58 na Vitongoji 254. Kwa mujibu wa sensa ya mwaka 2012 Halmashauri ina wakazi 192,781, kati yao 95,997 ni wanaume na 96,618 ni wanawake na ukuaji wa wastani wa 4.8%.

Shughuli kuu za kiuchumi ni kilimo na ufugaji. Shughuli nyingine za kiuchumi ni pamoja na biashara, ajira katika sekta ya umma, uzalishaji katika viwanda vidogo vya kilimo, utengenezaji wa samani, uendeshaji wa karakana ndogondogo, ufugaji wa nyuki, uvunaji wa miti na biashara ya mbao na biashara nyingine ndogondogo. Kilimo ndio shughuli kuu ya kiuchumi inayoajiri 90% ya wakazi na kuzalisha mazao ya chakula na biashara. Mazao makuu ya chakula ni mahindi, mpunga, mtama, muhogo na viazi vitamu. Mazao ya biashara hujumuisha tumbaku, karanga, pamba na alizeti. Ufugaji hufanyika kwa kiasi kidogo ukihusisha ng'ombe wa kienyeji, mbuzi, kondoo, kuku na nguruwe. Aidha, kuna shughuli za utalii katika hifadhi ya Ugalla.

Halmashauri ina vituo 25 vya kutolea huduma za afya ikiwa ni pamoja na Hospitali ya Wilaya, Kituo cha Afya na Zahanati 24 ambapo zahanati 2 zinamilikiwa na taasisi za dini. Pamoja na ukweli kuwa Halmashauri ina wakazi 225,664, Hospitali ya Wilaya ya Urambo inahudumia jumla ya watu 586,139 kwani H/W ya Kaliua ambayo ni jirani haina Hospitali ya Wilaya.




***Ramani ya H/W ya Urambo ikionesha mgawanyo wa vituo vya huduma za afya***

## 2.0 TATIZO

Kwa mujibu wa ilani ya uchaguzi na sera ya afya, kila Kata inatakiwa kuwa na Kituo cha Afya na Kila Kijiji kuwa na zahanati. H/W ya Urambo ina Kata 18 na Vijiji 59 lakini kuna Kituo 1 cha Afya ikimaanisha kuna upungufu wa vituo vya afya 17 sawa na 94%. Kati ya vijiji 59 ni vijiji 23 tu ambavyo vina zahanati ikionesha upungufu wa zahanati 36 sawa na 61%.

Upungufu huu wa vituo vya kutolea huduma za afya ulisababisha watu kutembea umbali wa zaidi ya 30km kufuata zahanati za jirani. Kituo cha Afya kilichopo huhudumia jamii zinazoishi ukanda wa Mashariki mwa Halmashauri na kuziacha kanda nyingine tatu bila huduma za afya za ngazi hii.

Kijiji cha Motomoto kina wakazi 2,732 ambao 1,372 ni wanaume na 1, 194 ni wanawake. Kwa kipindi kirefu Kijiji hakikuwa na Zahanati; wanakijiji walilazimika kutembea zaidi ya 8km kwenda Zahanati ya Vumilia kujipatia huduma za afya. Hii ni kinyume na sera ya afya inayoelekeza umbali mrefu wa vituo vya kutolea huduma za afya katika jamii kuwa 2km tu. Kutokana na ukosefu wa huduma za afya katika kijiji, jamii iliathirika sana na kukumbana na changamoto za; viwango vya juu vya vifo vya wajawazito na utegemezi kwa wakunga wa jadi katika kaya hivyo kuongezeka kwa uwezekano wa vifo. Baadhi ya akina mama wajawazito walijifungua njiani kuelekea zahanati ya Vumilia. Idadi ya wanawake wajawazito waliojifungua kwa msaada wa wakunga wa jadi ilikuwa kati ya 40% hadi 60% kwa mwaka.

Wazee na walemavu walizifikia huduma za afya kwa tabu sana. Msongamano katika Zahanati ya Vumilia ulisababisha wagonjwa kusubiri huduma kwa muda mrefu. Zahanati ya Vumilia ilihudumia watu 8,418 (wanaume 4,283 na wanawake 4,135) kutoka vijiji vya Usimba, Chekeleni na Imalamihayo vya H/W ya Kaliua na Vijiji vya Uhuru and Motomoto vya H/W ya Urambo. Umbali wa kwenda Zahanati ya Vumilia ulisababisha chanjo ya watoto kutolewa kwa kiwango cha chini sana.

**3.0 LENGO**

Wakazi wa Kijiji cha Motomoto walilenga kutekeleza takwa la sera ya afya ya Taifa; hivyo lengo kuu la jitihada hii lilikuwa kuboresha huduma za afya kwa wakazi. Aidha wanakijiji waliazimia kujenga jengo la zahanati ili kupunguza vifo vya akina mama hasa wajawazito kutoka 168 hadi 112 kwa vizazi 100,000, kuwezesha wakazi kujikita katika shughuli za uzalishaji, kusaidia wazee na walemavu kupata huduma za afya kwa ufanisi na kuongeza upatikanaji wa chanjo, ifikapo 2020.

**4.0 MIKAKATI YA UTEKELEZAJI**

Nia ya kuanzisha zahanati ya kijiji ilianza tangu mwaka 2009 katika Mkutano wa Kijiji na baadaye kuenezwa katika ngazi ya vitongoji kwa ajili ya majadiliano na utekelezaji. Halmashauri ya Kijiji ilichukua jukumu la kuhamasisha wanajamii; wajumbe wa Halmashuri ya Kijiji walipewa jukumu la kuhudhuria mikutano ya vitongoji, kutangaza na kuelezea pendekezo la kujenga na kuanzisha zahanati ya Kijiji cha Motomoto. Timu hii iliwaeleza wanakijiji kinaga-ubaga faida za kuwa na zahanati katika kijiji. Wanakijiji walielezwa kuwa uanzishaji wa zahanati ulikuwa unaenda sambamba na sera ya afya na ilani ya uchanguzi ambazo kwa pamoja zinaelekeza kila kijiji kuwa na zahanati. Pendekezo la kuanzishwa kwa zahanati lilikubalika katika ngazi zote.

Halmashauri ya Kijiji ilifanya uamuzi wa kutumia mbinu ya jitihada ya jamii kuboresha huduma za afya katika Kijiji cha Motomoto. Baada ya ushawishi na uhamasishaji, mkutano wa kijiji uliitishwa ili kufanya maamuzi kuhusu mfumo wa utekelezaji wa shughuli ya ujenzi. Katika mkutano huu iliamuliwa kuwa zao la tumbaku liwe chanzo cha kukusanya michango ya jamii kwa ajili ya ujenzi. Pendekezo hili lilipitishwa na kuelekezwa kuwa kila mkulima wa tumbaku achangie TZS. 20,000/= kwa kukatwa moja kwa moja kwenye mauzo yake katika chama cha msingi cha wakulima cha Kasela (AMCOS). Wazalishaji wa mazao mengine walielekezwa kuchangia TZS. 10,000/= kwa kaya. Ili kufanya utekelezaji kuwa fanisi, kamati ya ujenzi iliundwa na kupewa madaraka ya kusimamia fedha zote zilizopatikana na kufuatilia shughuli za ujenzi.

Kwa sababu za usalama na uwazi katika usimamizi wa fedha, kamati ya ujenzi ilifungua akaunti ya benki katika Benki ya NMB; akaunti namba 51310001511. Michango yote kwa ajili ya ujenzi wa zahanati ya Motomoto iliwekwa katika akaunti hii na wachangiaji walipatiwa risiti. Jumla ya TZS. 9,800,000/= zilipatikana kutoka kwa wakulima wa tumbaku na TZS. 500,000/= kutoka kwa wazalishaji wa mazao mengine. Mfuko wa Mendeleo wa Kijiji ambao husimamiwa na Halmashauri ya Kijiji ulitoa TZS. 28,483,404.00/=.

Kuandaa na kutangaza zabuni ya ujenzi; mwaka 2011 kijiji kilikuwa kimekusanya fedha za kutosha kuanza ujenzi, hivyo kamati ya ujenzi ilielekezwa kuandaa na kutangaza zabuni ili kuleta ushindani na kupata bei nafuu ya ujenzi. Taratibu za tathmini ya zabuni na kumpata mkandarasi zilifanywa na kamati ya ujenzi kwa kusaidiwa kitaalamu na Mhandisi wa Halmashauri. Uchaguzi wa mzabuni ulifanyika kwa ushindani na Kampuni ya Ms. MESHACK TITO NSELO ilichaguliwa. Mwaka huohuo kamati ya ujenzi iliingia mkataba na kampuni ya Ms. MESHACK TITO NSELO wenye gharama ya TZS 10,300,000/= na ujenzi ukaanza mara moja kwa kundaa michoro na eneo la kujenga msingi.

Michango kwa ajili ya ujenzi awamu ya pili; mwaka 2012 Halmashauri ya Kijiji iliagiza kila kaya kuchangia TZS.10,000/=. Michango kutoka mfuko wa maendeleo wa kijiji na kaya ilisaidia kukamilisha awamu ya pili ya ujenzi. Awamu hii ilitekelezwa na mkandarasi mwingine, ambaye naye alipatikana kwa zabuni shindani. Ni kampuni ya MS KOTIRIA ROAD WORKS E.A TZ LTD ambayo ilishinda zabuni na kupewa mkataba wenye thamani ya TZS 16,650,000/= (kwa ajili ya ubomoaji na uondoaji wa majengo ya zamani TZS 4,116,000/=, uandaaji wa michoro TZS 3,910,000/= na ujenzi wa ukuta TZS 8,625,000).

Ukamilishaji wa awamu ya tatu ulishirikisha wadau mbalimbali. Jengo la zahanati liliezekwa na mafundi wa karakana ya useremala iliyopo katika Kata ya Vumilia. H/W ya Urambo ilitoa TZS 5,000,000/= zilizotumika kununua fremu za milango na madirisha kutoka kwa karakana ya useremala iliyopo kijijini Motomoto. Halmashauri ya Kijiji kwa kupitia chama cha msingi cha wakulima ( KASELA Agricultural Market Cooperative Society, KASELA - AMCOS), iliomba msaada wa kukamilisha uanzishaji wa zahanati kutoka kwa kampuni ya Japan Tobacco International (JTI). Kampuni ya JTI ilikubali kukamilisha shughuli zote za umaliziaji wa jengo na kufunga umeme na viyoyozi kwa gharama za jumla ya TZS 76,271,186/=.

Halmashauri ya Kijiji na Kamati ya Ujenzi wa Zahanati ya Motomoto kwa kuwezeshwa na Mganga Mkuu wa Wilaya, walipeleka ombi la pili kwa JTI la kupatiwa msaada wa vifaa tiba. JTI iliridhia ombi hilo na kufanya ugavi wa vifaa tiba kwa zahanati ya Motomoto vyenye thamani ya TZS. 25,795,200/=. Zahanati ikawa imekamilika kwa maana ya majengo na vifaa tiba.

Maombi ya watumishi wa afya; mwaka 2013 Halmashauri ya Kijiji iliomba watumishi wa zahanati na Mganga Mkuu wa Wilaya alipanga wauguzi wawili kwenye Zahanati ya Motomoto. Kwa mujibu wa muundo wa Zahanati ya Motomoto, idadi ya chini ya watumishi inatakiwa kuwa 5 na ya juu kuwa 8; yaani Daktari 1, Wauguzi 2, Mhudumu wa afya 1 na mtaalamu wa maabara 1. Zahanati hii ina vifaa na mitambo ya afya ambayo haijafungwa ili kutumiwa kutokana na ukosefu wa watumishi wenye sifa za kutumia vifaa hivi.

**5.0 RASILIMALI**

Utekelezaji wa jitihada ya kuanzisha Zahanati ya Motomoto uliwezekana kutokana na ukusanyaji madhubuti wa rasilimali na ushiriki kamilifu wa jamii, Halmashauri na wadau. Rasilimali fedha zilizotumika hadi kukamilika kwa mradi ni jumla ya TZS. 160,549,790/= kutokana na vyanzo vifuatavyo;

(i) Michango ya fedha taslimu kutoka kwa jamii, TZS. 10,300,000/=

(ii) Msaada kutoka JTI, TZS 102,066,386/=
(iii) H/W ya Urambo, TZS. 5,000,000/=
(iv) Mfuko wa Mendeleo wa Jimbo (Serikali Kuu), TZS 3,000,000/=
(v) Mfuko wa Maendeleo wa Kijiji (unatokana na ushuru wa mazao), TZS. 28,483,404/=

Rasilimali nyingine zilijumuisha; rasilimali watu zilitumika katika usimamizi na usafishaji wa eneo la ujenzi na thamani yake inakadiriwa kuwa TZS. 500,000/=, ardhi ya ekari 4 kwa ajili ya ujenzi wa zahanati iliyotolewa na jamii bila fidia (yenye thamani ya TZS. 1,200,000/=) na vifaa vya ujenzi kama mawe na mchanga vilivyoletwa na jamii vyenye thamani ya TZS. 10,000,000/=.

**6.0 MATOKEO**

H/W ya Urambo na wanakijiji wa Motomoto wamekamilisha kwa mafanikio ujenzi wa zahanati ambayo ina vifaa tiba vya kutosha, watumishi wa afya na madawa yanayotakiwa katika zahanati. Jedwali 1 linaonesha vifaa tiba vilivyopo katika zahanati hii.

**Jedwali 1: Vifaa Tiba katika Zahanati ya Motomoto**


| Na | Aina | Maelezo | Idadi |
|---|---|---|---|
| 1 | MASHINE YA KUPIMA BP | AINA YA MERCURY - KUBWA | 2 |
| 2 | SPHYGMOMANOMETER | ANEROID | 2 |
| 3 | STETHOSCOPE | BINAURAL | 4 |
| 4 | STETHOSCOPE FOETAL PINARD | MONAURAL | 2 |
| 5 | HAEMOCUE BLOOD HEMOGLOBIN | (HEMOCUE HB 201+) PHOTOMETER | 1 |
| 6 | DELIVERY KIT | SUPERIOR QUALITY WITH SELF STERILIZATION TRAY | 2 |
| 7 | BED LABOUR AND DELIVERY | TWO-PIECE MATTRESS | 1 |
| 8 | HOSPITAL BED | | 4 |
| 9 | DRESSING TROLLEY | | 2 |
| 10 | DRIP STAND | DOUBLE-HOOK ADJ TO 2.5 M HEIGHT | 4 |
| 11 | EXAMINATION LAMP LIGHT | | 2 |
| 12 | DRUM DRESSING | MEDIUM 24CM X 24CM | 2 |
| 13 | PORTABLE PRESSURE AUTOCLAVE | 20 LITRES WITH STAND AND KEROSENE STOVE | 1 |
| 14 | SUCTION PUMP | ELECTRIC 1000 CAP. | 2 |
| 15 | SCALE ADULT | METRIC 140 KG X 100 G; STANDING TYPE | 2 |
| 16 | SCALE INFANT | CLINIC METRIC 15.5 KG X 5 G | 1 |
| 17 | SCREEN FAULDING | WITH CURTAINS | 2 |
| 18 | EXAMINATION BED | TWO SECTION WITH PAD | 2 |
| 19 | HOSPITAL BLANKET | GREY IN COLOR 153X203CM | 8 |
| 20 | DRESSING KIT | | 3 |
| 21 | BEDSHEET | COTTON 270 X 150 CM | 8 |
| 22 | MATTRESS FOAM | 200 X 95 X 12 CM (WITH PVC WATER PROOF COVER | 2 |
| 23 | OXYGEN CONCENTRATOR | DUAL MODEL 2FLOW METERS 6LPM | 1 |
| 24 | THERMOMETER | CLINICAL | 5 |
| 25 | MANUAL VACUUM ASPIRATION KIT | | 1 |
| 26 | WHEEL CHAIR | INVALID FOLDING ADULT | 2 |
| 27 | STRETCHER | EMERGENCY/RECOVERY | 1 |
| 28 | CABINETS FOR MEDICINE/MATERIALS | WOODEN | 2 |
| 29 | OFFICE CHAIRS | WOODEN | 10 |
| 30 | BENCHES FOR PATIENTS | WOODEN | 5 |
| 31 | OFFICE TABLES | WOODEN | 6 |
| 32 | BEDSIDE LOCKERS | WOODEN | 4 |
| 33 | MICROSCOPE BINOCULAR | ADVANCED | 1 |

Huduma za afya katika Kijiji cha Motomoto na vijiji vya jirani vya Chekereni, Ukondamoyo na Magere (H/W ya Kaliua) zimeimarika, zinapatikana kwa urahisi na zimeboreshwa. Zahanati inatoa huduma za wagonjwa wa nje, huduma za uzazi na kujifungua, chanjo, mpango wa uzazi, kliniki ya wajawazito, kliniki ya watoto wachanga, kliniki ya watoto, huduma za dawa, huduma za maabara na kliniki ya watu waishio na virusi vya UKIMWI.




***Vifaa tiba vya kisasa***

Hudma za afya zimeboreshwa; wanawake wajawazito wanapata huduma za kujifungua katika zahanati na hivyo kupunguza utegemezi kwa wakunga wa jadi pekee. Wazee na walemavu wanapata huduma bora za afya bila malipo kwani Halmashauri imewapatia kadi za matibabu bure au misamaha kwa huduma za kumwona daktari, upimaji na tiba. Msongamano katika Zahani ya Vumilia umepungua sana kwani wagonjwa kutoka vijiji vinavyozunguka kijjiji cha Motomoto wanapendelea Zahanati ya Motomoto. Muda ambao wagonjwa wanatumia katika zahanati hizi mbili kupata huduma umepungua kutoka wastani wa saa 10 hadi wastani wa juu wa saa 2 tu.



***Kiti chenye magurudumu na benchi la wagonjwa***

Uwepo wa uhakika wa madawa na vifaa tiba; uwepo wa zahanati inayofanya kazi kwa ufanisi umeleta hali ya utlivu katika upatikanaji wa dawa na vifaa tiba; hapo awali wanakijiji walinunua katika maduka binafsi ya dawa. Zahanati hii imerahisisha matumizi ya kadi za mfuko wa afya ya jamii (CHF) na Mfuko wa Bima ya Afya ya Taifa (NHIF). Idadi ya kaya ambazo zimeandikishwa kwenye mfuko wa afya ya jamii ni 151 sawa na 27.86% ya kaya 542 katika kijiji. Skimu hizi za bima ya afya ni muhimu sana kwa zahanati kupata madawa na vifaa tiba.




***Mifumo ya malipo (pamoja na CHF)***

Wanafunzi wa shule za msingi wamefaidika na zahanati hii kwani umbali waliolazimika kutembea kwenda kupata huduma Zahanati ya Vumilia umepungua hadi chini ya 1km na kuwapa fursa zaidi ya kuhudhuria vipindi kwa uhakika. Zahanati ina wateja wengi kwani tangu Julai 2017 hadi Januari 2018 Zahanati ya Motomoto ilikuwa imehudumia wagonjwa 2,522 kama inavyooneshwa kwenye Jedwali 2 hapa chini.

**Jedwali 2: Wagonjwa Waliopata huduma (Jul 2017 hadi Jan 2018)**

| Na | MWEZI | MWAKA | IDADI |
|---|---|---|---|
| 1 | JULAI | 2017 | 192 |
| 2 | AGOSTI | 2017 | 280 |
| 3 | SEPTEMBA | 2017 | 336 |
| 4 | OKTOBA | 2017 | 346 |
| 5 | NOVEMBA | 2017 | 421 |
| 6 | DISEMBA | 2017 | 395 |
| 7 | JANUARI | 2018 | 552 |
| **JUMLA** | | | **2,522** |

Kati ya Julai na Novemba 2017, Zahanati ya Motomoto ilitoa huduma kwa magonjwa makuu kumi kama ifuatavyo; maambukizi ya mfumo wa hewa (370), malaria (255), maambukizi ya njia ya mkojo (200), pumu (40), maradhi ya ngozi (36), minyoo (24), magonjwa ya macho (23), kuhara (17) na ajali za barabarani (07). Zahanati inatoa elimu ya afya kuhusu malaria, mpango wa uzazi, magonjwa ya tumbo na kuhara, chanjo, UKIMWI/VVU na usafi wa mazingira.

Kupitia tathmini ya Programu ya Matokeo Makubwa Sasa (BRN) iliyofanyika mwaka 2017 na 2018, Zahanati ya Motomoto ilipewa hadhi ya nyota tatu. Hadhi hii iliwafurahisha wanakijiji na kuhamasika kuanza ujenzi wa nyumba za makazi ya watumishi wa zahanati.

## 7.0 MIKAKATI YA UENDELEVU

Zahanati ya Motomoto kwa sasa inamilikiwa na Halmashauri ya Kijiji na inaendeshwa na kusimamiwa na Kamati ya Huduma za Jamii. Kupitia mipango na bajeti za mwaka, kijiji hutenga 60% ya mapato yake kila mwaka kwa ajili ya ukarabati na maboresho ya zahanati. Aidha, Serikali ya Kijiji kupitia kwa mkutano wa kijiji imeazimia kuendelea na michango ya jamii ya TZS. 4,500/= kwa kaya kila mwaka kwa ajili ya upanuzi wa zahanati kuelekea kuanzisha Kituo cha Afya. Kutokana na zahanati kupata nyota tatu kwenye tathmini ya BRN, mwaka 2018, zahanati itapokea TZS. 10,000,000/= za malipo yatokanayo na utaratibu

wa Malipo kutokana na Matokeo (Result Based Financing -RBF). Fedha hizi zitatumika kwa ukarabati na shughuli nyingine za matengenezo. Halmashauri itaendelea kupeleka watumishi madawa na vifaa tiba.

**8.0 SIRI YA MAFANIKIO**

Kijiji cha Motomoto kilifanikiwa jitihada hii kwa sababu ya siri kadhaa ambazo zimejikita katika mbinu ya jitihada ya jamii, mawasiliano thabiti na ushirikiano na wadau. Siri ya kwanza ni hitaji la jamii la kuwa na huduma bora za afya na zinazopatikana karibu na wakazi. Hitaji hili liliitia hamasa jamii kuchangia kwa utayari, kuwepo kwa umiliki na hivyo utekelezaji usiokuwa na vikwazo. Jamii ilishiriki kikamilifu katika kila hatua ya ujenzi na viongozi walikuwa na uwazi na usikivu wa hali ya juu.

Siri nyingine zilizochangia mafanikio haya ni uwepo wa zao la tumbaku, utayari wa JTI kuchangia utekelezaji na kaulimbiu ya kijiji cha Motomoto *"mvumilivu hula mbivu"* viliamsha ari ya kujituma. Aidha, Mh. Diwani aliiomba H/W ya Urambo kuzindua zahanati kipindi cha mbio za mwenge; kitendo ambacho kilichochea kasi ya ukamilishaji wa ujenzi tarehe 22.07.2017. Kama ilivyopangwa, zahanati ilizinduliwa rasmi na Bwana Amour Hamad Amour; Kiongozi wa Kitaifa wa Mbio za Mwenge mwaka 2017.

# Sura ya Tatu

## Ushirikishwaji wa Jamii katika Utoaji wa Huduma

Utoaji huduma ni jukumu muhimu katika mahusiano ya taasisi za Serikali na wananchi. Huduma ni mfumo au mpangilio unaokidhi mahitaji ya jamii. Helmsing (1995) anaeleza kuwa utoaji wa huduma ni uamuzi wa lazima unaofanywa na maafisa wa kuchaguliwa au kuajiriwa kutumikia au kutoa bidhaa na huduma kwa wapokeaji. Utoaji wa huduma ni wa namna ya mtazamo na mwelekeo, ukihusisha sifa na desturi za kimataifa..

Utoaji huduma ni mchakato endelevu na unaojirudia wa kupanga na kutoa huduma zinazozingatia mpokea huduma. Huhusu ushiriki wa mpokea huduma katika kuainisha wapokea huduma na kutambua mahitaji yao. Utoaji wa huduma pia unahitaji mchakato wa kubuni na kupanga huduma kati watumiaji, watoaji, wasambazaji na washirika katika kuanzisha, kubuni na kupanga huduma na kuhakikisha mahitaji ya watumiaji wa huduma yanafikiwa. Hatimaye utoaji wa huduma unahusu uzalishaji, usambazaji na uwasilishaji wa huduma ambazo zinakidhi lengo na zinafaa kwa mahitaji ya watumiaji. Katika utoaji wa huduma muda wote panahitajika mfumo wa ufuatiliaji na uboreshaji wa kukusanya maoni ya watumiaji na vipimo vya utendaji ili kuwezesha ufuatiliaji na uboreshaji wa bidhaa na huduma wa mara kwa mara.

Utoaji wa huduma ni shughuli ya msingi ya Serikali. Serikali huwepo, pamoja na sababu nyingine, kwa sababu ndio chombo pekee kinachoweza kutoa kwa usahihi maelekezo kuhusu huduma muhimu kama usalama wa raia, ulinzi, miundombinu, usimamizi na ukarabati wa barabara na kadhalika. Ulazima na umuhimu wa masuala haya huleta uhalali katika shughuli za Serikali. Imewekwa katika katiba na mikataba ya kimataifa kwamba Serikali inawajibika na huduma za msingi katika maeneo mengi ya kijamii ambayo ni pamoja na elimu, hifadhi ya jamii, mahitaji ya msingi, ulinzi wa kisheria na makazi. Serikali lazima iwapatie wananchi uhakika wa kuendeleza utoaji huduma; kupatikana huduma kwa wote bila kujali tofauti za kijamii na kiutamaduni na kwa bei zinazofaa. Hili lina matokeo kwa taasisi za Serikali. Uwazi, ufanisi, upatikanaji na mambo mengine, huleta ubora katika bidhaa zitolewazo na Serikali kama huduma kwa wananchi wake.

Kwa wananchi wengi, Serikali yao ya Mtaa ndio Serikali yenye mashiko zaidi, pia ndiyo ngazi ya Serikali ambayo huwasiliana nayo zaidi katika maisha yao ya kila siku. Mfumo wa Tanzania wa Serikali za Mitaa unaonesha kuwa MSM hutoa huduma ambazo zina asili ya kijamii, yaani, afya, maji, elimu, ustawi, usimamizi wa taka, na zile zenye asili ya kiuchumi, yaani, ardhi na makazi, muindombinu, kilimo, mazingira na maendeleo ya jamii.

Nadharia ya utoaji huduma shirikishi iliyotumika katika sura hii, ina maana ya utoaji huduma ambao huhusisha wadau wote. Kiini cha ushiriki ni jamii ambayo hufaidika na huduma zitolewazo na jamii yenyewe, MSM, Serikali Kuu, mashirika yasiyo ya kiserikali na hata mashirika ya kimataifa. Utoaji

huduma shirikishi huweka jamii faidika kama msingi wakati wa kupanga, utoaji wa huduma na upimaji wa ubora wa huduma. Utoaji huduma shirikishi huleta uendelevu wa huduma inayotolewa.

Katika sura hii, mbinu bora Nane kuhusu utoaji huduma shirikishi zimewasilishwa kutoka Halmashauri za Manispaa za Mpanda, Sumbawanga na Kigoma Ujiji, Halmashauri ya Mji wa Kibaha na Halmashauri za Wilaya za Kibondo, Mafia, Kaliua na Uvinza.

Halmashauri ya Manispaa ya Mpanda inawasilisha mbinu bora ya Jitihada Shirikishi za Kuboresha Ufaulu wa Wanafunzi Katika Elimu Ya Msingi ikitumia uzoefu wa Shule za Msingi za Msakila na Uhuru. Halmashauri illipata changamoto nyingi za kitaaluma zilizoambatana na ufaulu duni katika mitihani ya kumaliza elimu ya msingi. Kukabiliana na changamoto hizi, Halmashauri ililenga kuboresha ufaulu katika mitihani ya kumaliza elimu ya msingi kutoka 31% (2011) hadi 99% (2020) kwa kuwapa motisha watumishi, kutoa huduma bora kwa mteja na kuanzisha huduma za ufuatiliaji na tathmini. Halmashauri ilijikita katika kuandaa na kutumia mpango mkakati wa elimu, kuteua walezi wa Kata, kuendesha maboresho katika elimu, kuhamasisha ushiriki wa jamii, marejeo ya mara kwa mara ya mitihani ya zamani ya ndani, nje na taifa, kutoa zawadi kwa shule, Kata, walimu na wanafunzi waofanya vizuri na kutambua jitihada za walimu na wanafunzi. Matokeo ya jitihada hii yanajumuisha kuongezeka kwa uandikishaji na ufaulu. Utekelezaji wa Mpango Mkakati wa Elimu wa Halmashauri umeifanya Manispaa ya Mpanda kuongoza katika ufaulu wa Mitihani ya darasa la saba, ikishika nafasi ya kwanza kati ya Halmashauri zote Tanzania kwa miaka mitatu mfululizo; 2014, 2015 and 2016. Siri kuu ya mafanikio ni motisha kwa watumishi na uongozi imara katika ngazi ya Halmashauri.

Mbinu Bora ya Halmashauri ya Manispaa ya Sumbawanga inahusu Uboreshaji na Urasimishaji Shirikishi wa Ardhi na Majengo katika Kijiji cha Kasisiwe ambacho kilikuwa na changamoto za umiliki wa ardhi, kuongezeka kwa makazi yasiyo rasmi na kukosekana kwa barabara katika maeneo ya makazi. Lengo kuu la kurasimisha makazi katika Kijiji cha Kasisiwe lilikuwa kupunguza migogoro ya ardhi katika jamii ili kuboresha vipato na utoaji huduma. Lengo hili lilifikiwa kwa kuandaa mikutano/warsha za uelemishaji jamii, kuanzisha kamati ya uboreshaji matumizi ya ardhi, kutoa mafunzo kuhusu uboreshaji na urasimishaji wa ardhi na ushiriki wa jamii kwa kutoa nguvu kazi na fedha taslimu. Matokeo ya jitihada hii ni maboresho katika ukusanyaji wa taka ngumu, mazingira ya kuvutia na kuongezeka kwa thamani ya ardhi na majengo. Kijiji cha Kasisiwe kimekuwa kituo cha kujifunzia urasimishaji wa ardhi. Jitihada hii ilikuwa hitaji la jamii hivyo ushiriki ulikuwa kamilifu.

Mbinu bora ya Manispaa ya Kigoma Ujiji inahusu Urasimishaji wa Umiliki wa Ardhi Ili Kutokomeza Makazi Holela na Migogoro. Manispaa hii ilishuhudia migogoro mingi ya ardhi katika maeneo ya Bangwe, Kamala, Mwasenga, Vamia na Kagera. Mwaka 2016, jumla ya migogoro 419 iliandikishwa. Aina za migogoro iliyokuwepo ilitokana na kukosekana kwa mipango ya upimaji ardhi, matumizi ya ardhi yaliyoratibiwa na miundombinu. Lengo kuu la jitihada hii lilikuwa kupunguza migogoro ya ardhi na kutokomeza makazi yasiyo rasmi katika Halmashauri. Lengo hili lilifikiwa kwa kuanzisha programu ya urasimishaji wa ardhi, uhamasishaji wa jamii, kuundwa kwa kamati ya ardhi ya wanajamii, ukusanyaji wa taarifa na uandaaji wa michoro ya mipango miji, upimaji wa ardhi na utoaji wa vyeti vya umiliki wa ardhi. Manispaa ilipima viwanja 4,864 na hivyo kuongeza mapato ya Halmashauri, kuboresha ufanisi wa kazi wa watumishi wa Halmashauri na kuongezeka kwa thamani ya ardhi. Kufanikiwa kwa jitihada hii kunatokana na vigezo kama kuchangia gharama za machakato wa urasimishaji, utayari wa jamii kushiriki kikamilifu, ushirikiano bora na sekta binafsi na mahusiano bora kati ya wadau.

Mbinu bora ya Halmashauri ya Mji wa Kibaha inahusu Ujenzi Shirikishi wa Soko ili Kuboresha Kipato. Awali, Halmashauri ilikuwa na soko katika eneo la Mailimoja. Baadaye soko lilibomolewa kutokana na upanuzi wa barabara ya Dar es Salam – Kibaha. Matokeo ya kubomolewa kwa soko ni pamoja na kukosekana kwa huduma za soko na Halmashauri kupoteza kiasi kikubwa cha mapato. Kutokana na changamoto hii Halmashauri iliamua kuweka mipango, kuandaa michoro na kujenga soko kubwa la kukidhi mahitaji ya jamii kwa kushirikisha wadau. Uhamasishaji na kujenga uelewa kwa wafanyabiashara ulifanyika ili washiriki kikamilifu katika utekelezaji wa jitihada hii kwa kuchangia rasilimali. Halmashauri ililazimika kusitisha baadhi ya miradi mingine na kuelekeza rasilimali zote katika kutekeleza jitihada hii. Kukamilika kwa ujenzi wa soko kuliongeza upatikanaji wa huduma za soko, kuongezeka kwa idadi ya wafanyabiashara na mapato ya Halmashauri.

Jitihada ya H/W ya Kibondo inahusu Ushiriki wa Jamii katika Usimamizi wa Skimu ya Maji ambao umetekelezwa katika Kijiji cha Kumuhasha. Kabla ya utekelezaji wa jitihada hii, kijiji kilishuhudia upungufu wa maji, wananchi walilazimika kutembea umbali wa kati ya 2- 4km na kutumia muda mwingi wa kati ya saa 4 hadi 5 kutafuta maji. Migogoro ndani ya familia ilikithiri kutokana na wanawake kutumia muda mwingi wakati wa kutafuta maji. Vilevile, wananchi waliathiriwa na magonjwa yatokanayo na matumizi ya maji yasio safi na salama. Mwaka 2016, wananchi waliamua kushirikiana kutatua matatizo haya kwa kufanya ukarabati na kupanua miundombinu ya maji, kuhifadhi mazingira ya kuzunguka vyanzo vya maji na kuanzisha Jumuiya ya Watumia Maji (COWSO) kwa ajili ya usimamizi wa skimu ya maji. Utekelezaji wa jitihada hii uliongeza kiwango cha maji safi na salama ndani ya 400m na kupungua kwa magonjwa yatokanayo na maji. Upatikanaji wa maji umeboresha usafi katika maeneo ya shule kutokana na kuanzishwa kwa bustani za maua. Aidha, shughuli mbalimbali za kiuchumi kama kufyatua tofali, kilimo cha mboga mboga na vitalu vya miti zinaendelea.

Mbinu bora ya H/W ya Mafia inahusu Ushiriki wa Jamii katika Ujenzi na Usimamizi wa Skimu ya Maji. Jitihada hii litekelezwa katika Vijiji vya Juani na Chole. Vijiji hivi ni visiwa ambavyo vimetengana na kisiwa kikuu cha Utende. Kabla ya utekelezaji wa jitihada hii Vijiji vya Juani na Chole vilishuhudia uhaba wa maji. Wanakijiji walilazimika kusafiri 3km - 7km kuvuka bahari hadi Kijiji cha Utende ili kupata maji. Wananchi ambao walishindwa kufuata maji katika umbali huo walilazimika kununua kwa gharama kubwa kati ya TZS 500 - TZS 1000 kwa ndoo ya lita 20. Magonjwa yatokanayo na maji machafu yalikithiri. Baada ya kubaini matatizo haya, wananchi kutoka vijiji vya Juani na Chole waliainisha uhitaji mkubwa wa maji wakati wa mchakato wa bajeti ya mwaka 2014/2015. Mikutano ya kujenga uelewa wa pamoja kwa wanakijiji ilifanyika na kuhamasisha uchangiaji wa rasilimali na ushiriki katika kutekeleza jitihada hii. Halmashauri ilitoa uzaidizi wa kutafuta fedha kutoka Serikali Kuu pamoja na kutoa msaada wa kitaalamu wakati wa utekelezaji. Matokeo ya jitihada hii ni upatikanaji wa maji safi na salama ndani ya Vitongoji, kupungua kwa magonjwa yatokanayo na matumizi ya maji yasiyo safi na salama, na kupungua kwa gharama za kununua maji.

Mbinu bora ya H/W ya Kaliua inaelezea Uhifadhi wa Mazingira kwa Maendeleo Endelevu. Halmashauri ilishuhudia tatizo la uharibifu wa misitu uliosababishwa na shughuli za kibinadamu kama utengenezaji wa mkaa, uchomaji wa misitu, kilimo cha kuhamahama na ukataji wa magogo na miti kwa shughuli za ukaushaji wa tumbaku. Athari za ukataji holela wa miti zilisababisha uharibifu wa rasilimali za mazingira, mabadiliko ya tabia nchi na kuharibu mfumo wa maisha ya viumbe. Halmashauri ilibaini athari hizi na kuamua kuchukua hatua kwa kujenga uelewa kuhusu uhifadhi wa mazingira, kuunda vikundi vya uhifadhi wa mazingira, kuanzisha vitalu vya miti, kugawa miche ya miti na kuanzisha teknolojia ya utengenezaji wa mkaa mbadala. Utekelezaji wa jitihada hii ulibadilisha mtazamo wa watu na kuacha shughuli zinazoharibu mazingira na kuanza kutekeleza shughuli ambazo ni rafiki kwa mazingira. Uelewa

kuhusu umuhimu wa miti kwa mazingira na maisha ya watu umeongezeka na vitalu vya miti vya watu binafsi vimeanzishwa.

Jitihada ya H/W ya Uvinza inahusu Uanzishaji wa Karakana ya Useremala ya Halmashauri katika Kuboresha Utoaji wa Elimu. Kabla ya utekelezaji wa jitihada hii, Halmashauri ilishuhudia tatizo la uhaba wa madawati kwa shule za msingi. Uwiano wa wanafunzi kwa dawati ulikuwa 6:1 kinyume na mahitaji ya kitaifa ya 3:1. Hali hii ilisababisha mazingra magumu ya kujifunza na ufaulu wa chini katika mitihani. Timu ya Menejimenti ya Halmashauri (CMT), Wazazi na Wanafunzi hawakufurahishwa na mazingira ya kusomea hivyo kuamua kutatua changamoto hizo. Wazo la kuanzisha karakana ya Useremala ya Halmashauri lilitokana na CMT na kuliwasilisha katika mkutano wa Baraza kupata baraka. Halmashauri ilianzisha kikosi kazi kuratibu zoezi la uanzishaji wa karakana na wazazi walishiriki katika kutayarisha mbao na kuchangia nguvu kazi. Matokeo ya jitihada hii ni pamoja na uwepo kwa Karakana ya Halmashauri yenye vifaa vya kutosha, kutengenezwa kwa madawati ya kutosha na samani nyingine za ofisi, ajira kwa vijana mafundi kutoka kwenye jamii na kupungua kwa gharama za kutengeneza madawati.

# HALMASHAURI YA MANISPAA YA MPANDA

**JITIHADA SHIRIKISHI ZA KUBORESHA UFAULU WA WANAFUNZI KATIKA ELIMU YA MSINGI**




*Uzoefu wa Shule za Msingi za Msakila na Uhuru*

**1.0 INTRODUCTION**

Halmashauri ya Minispaa ya Mpanda ni mojawapo ya Halmashauri 5 za Mkoa wa Katavi iliyoanzishwa mwaka 2015 ikiwa na eneo la 527km$^2$, Tarafa 2, Kata 15, Vijiji 14,Mitaa 43, Vitongoji 78 na kaya 28,971 households. Kwa mujibu wa sensa yam waka 2012, Halmashauri ina wakazi 141,004; wanaume ni 69,357 na wanawake ni 71,647 na wastani wa ongezeko la watu la 3.6% kwa mwaka. Shughuli kuu za kiuchumi ni kilimo, ufugaji, uchimbaji madini, viwanda vidogovidogo na biashara ndogondogo. Mazao makuu ya chalula ni mahindi, mpunga, mtama, viazi vitamu na muhogo.

Halmashauri ina shule za msingi 34 ambazo zina wanafunzi 35,968 pupils; 17,789 wavulana na 18,179 wasichana. Kwa wastani, 95% ya watoto wote huandikishwa elimu ya msingi na 100% ya wanfunzi wanaohitimu darasa la saba hujiunga na elimu ya sekondari. Manispaa in shule za sekondari 14; shule za sekondari 10 zinamilikiwa na serikali na 4 ni za binafsi. Aidha kuna Chuo Kikuu Huria cha Tanzania na Taasisi ya Mafunzo ya Ufundi (VETA).

**2.0 TATIZO**

Manispaa ya Mpanda imewahi kuwa na vikwazo vingi katika kufikia maendeleo ya kijamii na kiuchumi katika sekta nyingi hasa elimu. Tangu mwaka 2012 Manispaa ilishuhudia changamoto za kitaaluma zilizojidhihirisha katika matokeo duni ya mitihani ya kumaliza darasa la saba. Mwaka 2011 ufaulu katika halmashauri hii ulikuwa 31% tu. Sababu za ufaulu duni zilikuwa;

(i) Kukosekana kwa mkakati wa elimu; kabla ya 2013 Halmashauri haikuwa na mkakati rasmi wa elimu unaotoa mwelekeo na mwongozo wa ushiriki wa wadau kwenye program za maboresho ya elimu ya msingi.

(ii) Hakukuwa na jukwaa thabiti la kushirikishana na kujadili taarifa za masuala ya elimu na maendeeleo ya jamii. Aidha, hapakuwa mifumo ya mrejesho kwa jamii kuhusu mipango na bajeti za shule msingi.

(iii) Kulikuwa na ushirikiano duni kati ya madiwani, watumishi wa makao makuu ya manispaa na jamii.

(iv) Ushiriki duni wa jamii katika masuala ya elimu; jamii iliamini kuwa utoaji wa huduma wa elimu ni jukumu la maafisa elimu na serikali tu.

**3.0 LENGO**

Katika jitihada hii Halmashauri ililenga kuboresha ufaulu katika mitihani ya shule ya msingi kutoka 31% (2011) hadi 99% 2020 kwa kuwapa motisha watumishi, kutoa huduma bora kwa mteja na kuanzisha huduma za ufuatiliaji na tathmini. Aidha, Halmashauri ilikuwa na malengo mahsusi ambayo ni;

(i) Kuongeza kiwango cha ufaulu kutoka 31% mwaka 2011 hadi 97% mwaka 2016.

(ii) Kuongeza mahudhurio ya wanafunzi na walimu kutoka 75% to 100% (wanafunzi) na kutoka 84% hadi 100% (walimu).

(iii) Kuongeza ushiriki wa jamii katika kuinua elimu ya msingi.

(iv) Kuimarisha mifumo ya ufuatiliaji na tathmini katika mbinu na jitihada za kufundisha.

(v) Kufikia matokeo ya haraka katika uelewa wa jamii kwa kushirikisha jamii kuchangia vifaa na fedha taslimu kwa maendeleo ya elimu.

**4.0 MIKAKATI YA UTEKELEZAJI**

Manispaa ya Mpanda kwa kutumia mpango jumuishi na mkakati ililenga katika kuboresha utoaji wa huduma na uboreshaji wa utendaji katika sekta ya elimu. Kufikia lengo hili, Halmashauri iliweka mikakati mbalimbali. Mwaka 2013, Halmashauri iliandaa mpango mkakati wa miaka mitano unahusu namna za kuongeza ufaulu katika mitihani ya kuhitimu elimu ya msingi kutoka 31% to 99%. Mpango mkakati huu

uliainisha mkakati wa elimu ambao ungetumiwa katika shule zote za Halmashauri. Baadhi ya shule ziliutumia mkakati huu kikamilifu na shule zilizofanya vizuri katika utekelezaji wa mkakati ndizo zimetumiwa kueleza uzoefu wa Manispaa ya Mapanda kama ilivyo hapa chini.

Kuundwa kwa mipango mkakati ya elimu; Halmashauri iliziwezesha shule za msingi kuunda mipango mkakati. Mpango mkakati wa Milala (2013), Kashato (2014) na Magamba (2015) hueleza mbinu za kuboresha elimu ya msingi katika maeneo yao. Wazo hili lilianza katika idara ya elimu ya manispaa kuhusu kuwa na mikakati ya kufikia ndoto ya ufaulu wa juu kwa kujenga uelewa, kuwa na dira na dhima. Maadalizi ya mipango mikakati yalianza kwa kutumia taarifa za msingi zilizopatikana kwa kuchambua taasisi husika kutumia ufaulu wa 31% kama mwanzo wa uchambuzi. Hatua ya pili ilikuwa kutafuta michango ya mawazo kutoka kwa wadau wa ndani na nje ili kufikia malengo. Mkakati ulihitaji wahusika wote kuanzia ngazi za juu hadi chini kutambua na kutimiza majukumu yao kikamilifu. Ujenzi wa uelewa na uhamasishaji ulifanyika kwa madiwani, maafisa watendaji wa kata, waratibu wa elimu kata, viongozi wa kimila, viongozi wa kidini na viongozi wa kijamii kuhusu utayari wa kuchangia na kutoa misaada ya vifaa, fedha na ubinadamu.

Kuanzishwa kwa walezi wa Kata; kila kata ilipatia mlezi mmoja kutoka kati ya maafisa elimu wa manispaa. Mlezi siyo mbadala wa afisa elimu kata, bali ni nyongeza katika utekelezaji wa nafasi na majukumu ya afisa elimu. Mlezi ni kiungo kati ya jamii na makao makuu ya manispaa. Mlezi anatarajiwa kujihusisha kwa kina na masuala ya maendeleo ya elimu katika kata husika na anatakiwa kuwa na taarifa za masuala haya mapema na inapolazimu kuchukua hatua za haraka kabla hali haijawa mbaya. Mlezi anatarajiwa mbele mar azote na kila mwezi, kuiita jamii ili kufanya kampeni za kuboresha uendeshaji wa shughuli za elimu.

Maboresho ya usimamizi wa huduma ya elimu; maboresho haya yaliaznzisha mipango, usimamizi, ufuatiliaji, na tathmini ya kila siku. Kutekeleza mpango huu Halmashauri iliteua walimu wakuu na maafisa elimu kata kwa kutumia kigezo cha sifa; sifa ya chini ilikuwa diploma ya kawaida. Hii ilifuatiwa na zoezi la ukaguzi wa ndani wa watumishi wa shule za msingi na kutoa taarifa kwa mkuu wa idara ya elimu kila wiki. Mkakati huu ulijumuisha uitishaji wa mikutano wa mara kwa mara wa kamati za shule ambao hufanyika kila robo mwaka ili kupima maendeleo ya shule katika utendaji kitaaluma, nidhamu shuleni na maboresho ya miundombinu ya shule.

Kuhamasisha ushiriki wa jamii; mkakati uliunda mfumo wa ufuatiliaji wa pamoja na ushiriki thabiti katika program zote za elimu, kushirikisha wadau kama asasi zisizo za kiraia (NGOs), wanasiasa na viongozi wa jamii. Mkakati wa elimu ulioanzishwa unagawa majukumu kwa wadau wote; kwa mfano "fomu ya taarifa za mwanafunzi" inayoonesha taarifa za maendeleo ya mwanafunzi; fomu hii lazima itiwe saini na mzazi/mlezi na atoe maoni kuhusu maendeleo ya mwanafunzi. Wadau wa maendeleo wamepewa jukumu la kushiriki kwa kutoa vifaa na misaada ya kifedha ili kuwezesha utoaji bora wa huduma za elimu katika maeneo ya manunuzi ya madawati, ujenzi wa vyoo na madarasa na kusaidia upatikanaji wa vifaa kwa ajili wa wanfunzi wenye mahitaji maalumu. Haya yote yalifanyika baada ya mapitio ya miundombinu ya shule kutambua uwepo na upungufu wa madarasa, samani, nyumba za walimu na vifaa vya kufundishia na kujifunzia.



***Miundombinu ya Shule ya Msingi Msakila***

Kuimarisha ushiriki wa jamii; Halmashauri ilianzisha mbinu sahihi za kufundishia na kujifunza kama vifaa vya uwezeshi na mbinu shirikishi ambazo zinajumuisha vifaa halisi, maigizo, maswali na majibu, mijadala na safari za mafunzo. Kwa mfano; Halmashauri ilianzisha timu ya uwezeshi ya walimu 5 wenye sifa waliopitia maeneo yote magumu ya mitaala na kuandaa vitini vya kufundishia vilivyotumika vifaa vya kufundishia walimu wengine wakati wa kutekeleza mpango wa mafunzo ya ndani (INSET). Aidha, ziliendeshwa warsha za ndani za amfunzo kwa maafisa elimu wa kata, walimu wakuu na walimu wakuu wasaidizi ili kubadilishana uzoefu kususu usimamizi wa taasisi na stadi za kimeneja za kuendesha shule. Halmashauri iliandaa na kutekeleza safari ya mafunzo katika mbuga ya wanyama ya taifa ya Katavi kama sehemu ya mkakati wa ujenzi wa uwezo kwenye eneo la maliasili na uhifadhi wa mazingira.

Marudio ya mara kwa mara na ya kina ya mitihani ya zamani ya ndani, nje nay a taifa; mkakati huu ulielezwa kwenye mpango mkakati wa elimu wa Milala unaoenda sambamba na skimu ya Wizara Elimu, sayansi na Teknolojia. Skimu hii ya wizara inaelekeza kuwa mitihani ndio kiashiria kikuu cha kupima maendeleo ya kitaaluma ya wanafunzi. Shabaha ilikuwa kujiridhisha kuwa kabla mwanafunzi hajafanya mtihani wa taifa (iwe darasa la 4 au la 7), awe na uzoefu wa miundo ya mitihani ya darasa husika. Mitihani iliyopendekezwa ilikuwa mitihani ya majaribio katika ngazi za Kata, Vikundi vya shule, Halmashauri na Mkoa. Utaratibu huu ulisaidia kukadiria alama za ufaulu wa mitihani ya mwisho kwa maana ya alama A, B na C na kuweka mkazo wa kusaidia wanafunzi wanaopata alama za D na E kwa kuwapatia majaribio zaidi na mara kwa mara.

Kutoa zawadi kwa Shule, Kata, Walimu na Wanafunzi waliofanya vizuri; katika mkakati wa elimu ulioanzishwa aliyefanya vizuri kuliko wote anapewa cheti na fedha taslimu. Shule ya Msingi Msakila ilishikika nafasi ya kwanza kwa miaka 4 mfululizo tangu 2014 hadi 2017. Shule pia ilizawadiwa na Wizara ya Elimu na Mfunzo ya Ufundi kama shule bora katika mitihani ya kumaliza elimu ya msingi tangu 2013 hadi 2016. Hali kadhalika; serikali kupitia sekretarieti ya mkoa ilianzisha skimu ya kuwapa zawadi wakuu wa Wilaya kulingana na matokeo; kwa Wilaya zilizofanya vibaya, Mkuu wa Wilaya hiyo anapewa zawadi hasi ya ubao ulioandikwa “amefanya vibaya”, na kupewa masharti ya kurudisha kibao hicho mwaka unaofuata ili apewe Mkuu wa Wilaya mwingine ambaye Wilaya yake itakuwa imefanya vibaya.

**Jedwali 1: Zawadi kwa Shule zilizofanya vizuri**

| NA | MWAKA | SHULE | NAFASI | ZAWADI |
|---|---|---|---|---|
| 1. | 2014 | KAWANZIGE | 1 | 500,000.00 |
| | | MAJENGO | 2 | 400,000.00 |
| | | MKAPA | 3 | 300,000.00 |
| 2. | 2015 | MSAKILA | 1 | 400,000.00 |
| | | MKAPA | 2 | 300,000.00 |
| | | UHURU | 3 | 200,000.00 |
| 3. | 2016 | MSAKILA | 1 | 400,000.00 |
| | | KASHAULILI | 2 | 300,000.00 |
| | | MBUGANI | 3 | 200,000.00 |

**Jedwali 2: Zawadi kwa Kata zilizofanya vizuri**

| NA | MWAKA | KATA | NAFASI | ZAWADI |
|---|---|---|---|---|
| 1 | 2014 | KAKESE | 1 | 300,000.00 |
| | | KASHAULILI | 2 | 200,000.00 |
| | | KAZIMA | 3 | 100,000.00 |
| 2 | 2015 | MAKANYAGIO | 1 | 250,000.00 |
| | | KAWAJENSE | 2 | 200,000.00 |
| | | KAZIMA | 3 | 100,000.00 |
| 3 | 2016 | KASHAULILI | 1 | 200,000.00 |
| | | KAWAJENSE | 2 | 150,000.00 |
| | | KAZIMA | 3 | 100,000.00 |

Kuanzishwa kwa utungaji wa mitihani ya ndani ulioboreshwa; timu ya menejimenti ya shule ya msingi Msakila ilitumia mkakati wa elimu wa Halmashauri na kuanzisha mikakati ya utekelezaji ambayo ilichangia kwenye ufaulu wa juu. Shule iliamua kuingia mkataba na kampuni iliyopo Dar es salaam na kuipatia jukumu la kutunga na kusimamia mitihani ya ndani ya shule. Utaratibu huu ulilenga kuboresha na kuthibiti ufundishaji wa ndani na kujihakikishia ubora wa mitihani, kufuata kanuni za mitihani ya Taifa, kuwalazimu walimu kumaliza mitaala kabla ya kufanya marudio ya maeneo magumu na kuwazuia walimu kutunga mwaswali katika mada walizofundisha tu.

Kuboresha utungaji wa maswali ya Hesabu; ili kujenga uwezo wa wanafunzi katika somo la hesabu, shule iliwafundisha wanafunzi kutunga maswali binafsi ya hesabu na kubadilishana na wengine kama sehemu ya mazoezi. Zoezi hili hufanyika chini y aungalizi wa mwalimu. Mkakati huu umeleta matokeo chanya kwa wanafunzi wa darasa la saba kwani wanaweza kutabiri maswali yatakayotoka kwenye mitihani ya mwisho. Aidha mkakati huu unaimarisha uwezo wa kujenga hoja, kufikiri kwa kina, kujiamini na kuwa huru.

Utambuzi wa walimu na wanafunzi; Mei mwaka 2017 Halamashauri ilifanya sherehe ya kuwapongeza walimu na wanafunzi kwa kufanya vizuri katika mitihani ya taifa yam waka 2016. Zawadi mbalimbali zilitolewa kwa walimu 15 wa masomo zikiwa na jumla ya TZS 1,150,000.00. Halmashauri pia iliwapa zawadi wanafuzi 6 waliofanya vizuri zaidi (wasichana 3 na wavulana 3).

Vipindi vya pamoja kati ya walimu na wanajamii; mkutano huitishwa kila robo mwaka ili kuainisha mazuri, changamoto na afua za changamoto zilizoainishwa. Uhamasishaji wa jamii hufanyika mara kwa mara kupitia siku ya wadau ambayo hutanguliwa na wiki ya elimu kila mwaka. Lengo kuu la utaratibu

huu ni kukusanya maoni ya washirika wa ndani nan je kama viongozi wa jamii, asasi zisizo za kiserikali, mashirika ya umma, taasisi za fedha na asasi za kijamii; lengo likiwa kuunda umiliki na ushiriki bora.

Mikakati mingine katika jitihada hii ni pamoja na utungaji wa mitihani kwa kutumia walimu wa shule nyingine, vipindi vya ziada hasa kwa darasa la saba msimu wa likizo ndefu, kuhamasisha wanafunzi kutunga maswali na kuhakikisha maeneo yote ya mitaala yamekamilika mapema.

**5.0 RASLIMALI**

Manispaa ya Mpanda iliamua kutumia raslimali mbalimbali kuweza kufikia lengo la jitihada lilikusudiwa. Kuhusu raslimali fedha; Halmashauri iliandaa bajeti ya kutosha kuendesha programu ya uboreshaji elimu ya msingi. Bajeti ilijumuisha ruzuku ya (Capital Block Grant) TSZ 420,000,000.00, fedha za wafadhili, TZS 39,000,000.00 na fedha za malipo ya matokeo (Pay For Result) naTZS 19,000,000.00 fedha za mpango wa Kusoma na Kuhesabu (LANES).

Raslimali watu; waru wengi walishiriki katika utekelezaji wa jitihada hii, ikiwa ni pamoja na madiwani, wakuu wa irada/vitengo, maafisa elimu waliopo makao makuu ya manispaa, maafisa watendaji wa kata, maafisa elimu wa kata, maafisa watendaji wa mitaa, maafisa watendaji wa vijiji, walimu wakuu, walimu, wazazi na wajumbe wa kamati za shule.

**6.0 MATOKEO**

Mkakati wa Elimu wa Manispaa ya Mpanda umeleta matokeo mengi ambayo yana faida kubwa ka jamii na ni mfano kwa Halmashauri nyingine. Matokeo haya yanatokana na uandaaji na matumizi ya Mpango Mkakati wa Elimu ya Msingi. Mkakati wenyewe upo, ukifanya kazi ya kuongoza uendeshaji wa elimu ya msingi katika shule zote za manispaa. Mpango Mkakati huu unaelekeza maboresho katika utendaji wa Halmashauri na watumishi katika kupanga, kusimamia, kuratibu, kuongoza, kufuatilia na kutathmini elimu ya msingi. Utaratibu huu umeipatia Halmashauri watumishi ambao wamejitoa kikamilifu na kufanya kazi kwa nguvu zote kuhakikisha wanafunzi katika Manispaa ya Mpanda wajifunza kwa kina na kupata elimu stahiki.



*Mwalimu mwenye ari ya kazi*


Kuongezeka kwa uandikishaji na ufaulu; jitihada ya Manispaa ya Mpanda imeongeza idadi ya wanafunzi wanaoandikishwa darasa la 1 hadi la 7 kutoka 19,367 mwak 2014 hadi 27,786 in 2016; kuongezeka kwa mahudhurio na kumaliza elimu ya msingi ikiwa ni pamoja na kuongezeka kwa viwango vya ufaulu kama

ilivyooneshwa hapo juu. Mkakati wa elimu ya msingi umeboresha kiwango cha ufaulu katika mitihani ya kumaliza elimu ya msingi kutoka 31% mwaka 2011 hadi 96.5% in 2016.



***Vyeti vya ushindi vya shule za msingi za Uhuru na Msakila***

Utekelezaji wa Mapano Mkakati wa Halmashauri wa Elimu ya Msingi umefanya Manispaa ta Mpanda kuwa mshindi wa kwanza katika ngazi ya kitaifa, ikishika nafasi ya kwanza kati Halmashauri zote Tanzania kwa miaka mitatu mfululizo, yaani 2014, 2015 na 2016.




***Cheti cha Ushindi cha Manispaa ya Mpanda***

Jitihada hii imeimarisha ushiriki wa jamii katika utoaji wa elimu ya msingi kama inavyojidhihirisha katika michango ya wazazi kwa ajili ya chakula cha wanafunzi na motisha kwa walimu; na kuleta mahusiano fanisi kati ya wazazi, walimu na maafisa elimu. Zaidi ya yote, jitihada hii imeanzisha mtandao na ushirikiano imara kati ya wadau mbalimbali wa elimu ambao wameongeza thamani katika utoaji wa elimu ya msingi bora na iliyoboreshwa katika manispaa.

**7.0 MIKAKATI YA UENDELEVU**

Ili kufanya matokeo ya jitihada hii kuwa endelevu, Halmashauri imeazimia kuimarisha ushiriki wa madiwani, kuongeza utendaji na uwajibikaji katika masuala ya elimu na kukazia hali ya kuaminiana kati watumishi, madiwani na jamii ili kupeana habari kifanisi na kusisitiza uelewa wa jamii kupitia maandalizi sahii ya jamii ili kuongeza ushiriki wa jamii katika kuanzisha na kutekeleza miradi.

Kuendeleza motisha kwa watumishi; Halmashauri itaendelea kuandaa na kutafuta fursa za mafunzo ya ndani ya watumishi hasa kwa walimu, wajumbe wa kamati za shule na maafisa elimu wa kata na kuendesha mafunzo ya ndani na nje kwa makundi haya yanayosimamia na kuendesha shughuli za elimu katika Manispaa ya Mpanda.

**8.0 SIRI YA MAFANIKIO**

Mafanikio ya jitihada ya Manispaa ya Mpanda yanatokana na sababu zilizoelezwa hapa chini;

(i) Motisha kwa watumishi; Mkurugenzi wa Manispaa ana utaratibu wa kukutana na maafisa elimu wa kata na walimu wakuu. Kitendo hiki huwatia motisha watumishi wa elimu ngazi za msingi kutokana na kujisikia kutambuliwa na uongozi wa juu.

(ii) Uongozi thabiti katika ngazi ya Halmashauri; uongozi thabiti na fanisi ndio ulileta mazingiza wezeshi kwa utekelezaji wa mikakati. Aidha uwezeshi wa kisiasa ulisukuma kwa kasi utekelezaji wa jitihada hii.

(iii) Utoaji wa zawadi; utoaji wa zawadi chanya na hasi, unaofanywa ha Halmashauri, Walimu wakuu na Kamati za Shule kwa waliofanya vizuri na ambao hawakufanya vizuri kuliongeza motisha kwa walimu na wanafunzi.

(iv) Ushiriki kamili wa jamii na wadau; ushiriki huu katika mikutano na kutoa michango ulichochea motisha, kujituma katika kufanya kazi na utendaji kwa makundi yote.

# HALMASHAURI YA MANISPAA YA SUMBAWANGA

## UBORESHAJI NA URASIMISHAJI SHIRIKISHI WA ARDHI NA MAJENGO





***Uzoefu wa Kijiji cha Kasisiswe***

## 1.0 UTANGULIZI

Halmashauri ya Manispaa ya Sumbawanga ni mojawapo ya Halmashauri 4 zinazounda Mkoa wa Rukwa. Halmashauri nyingine ni Sumbawanga, Kalambo na Nkasi. Halmashauri inapatikana kati ya Latitudo $07^0$48' na $08^0$31' Kusini na Longitudo $30^0$29' na $31^0$49' mashariki. Kiutawala Manispaa ya Sumbawanga ina Tarafa 2 za Lwiche na Itwelele, Kata 19, Vijiji 24, Mitaa 167 na Vitongoji 173. Manispaa ina ina eneo 1329$km^2$ ambapo 39.6$km^2$ ni sehemu ya mjini na 1292.44$km^2$ eneo la vijijini. Kwa mujibu wa Sensa ya mwaka 2012 Manispaa ina wakazi 209,793; 100,734 wanaume na 109,059 wanawake.

Manispaa hii inapatikana Kusini Magharibi mwa Tanzania kwenye milima ya uwanda wa Ufipa, ikiwa na hali ya hewa yenye ukavu na unyevu kiasi kwa sehemu kubwa yam waka. Kuna joto la wastani la $27^0$C likiambatana na baridi, ukavu na pepo za mara kwa mara hasa kati ya miezi ya Mei na Oktoba. Miezi yenye baridi sana ni Juni na Julai ambapo joto huwa kati ya 16°C - 5°C. Manipaa hii hupata mvua za wastani wa kati ya 900mm - 1000mm kwa mwaka na kuwa na wasatani wa 646.8mm wa mvua.




***Ramani ya Kiutawala ya Manispaa ya Sumbawanga***

Manispaa ya Sumbawanga hutegemea kilimo ambacho huajiri 80% ya wakazi na ndio huchangia kwa kiasi kikubwa uchumi wa Halmashauri na Mkoa kwa ujumla. Wakazi wengine huendesha maisha yao kwa ufugaji. Aidha, Manispaa hii ina eneo lipatalo 89,000ha ambazo 64,516ha zinafaa kwa kilimo na 63,476ha zinatumika kwa uzalishaji, hasa wa mazao ya chakula. Mazao ya ziada kama mahindi, maharagwe, ngano, viazi, karanga, matunda, alizeti na mbogamboga huuzwa ili kujipatia kipato.

## 2.0 TATIZO

Upangaji wa makazi ni shughuli muhimu katika maeneo ya mijini. Hata hivyo kutokana na sababu mbalimbali maeneo ya mijini katika nchi zilizopo kusini mwa sahara hayajapangwa na hivyo kuwepo kwa makazi holela. Makazi holela katika miji ni maeneo yenye wakazi wengi kupita kiasi na huambatana na majengo duni na machafu. Tafsiri halisi ya makazi holela ianyotumiwa na Umoja wa Mataifa; ni eneo ambalo hujumuisha kwa kiasi kikubwa ukosefu wa maji salama, upatikanaji duni wa huduma za usafi na miundombinu, nyumba zenye ubora duni, msongamano wa watu uliokithiri na ukosefu wa usalama katika makazi (UN-Habitat, 2003).

Migogoro kuhusu mazingira na maisha katika jamii yamekuwa yakiongezeka katika Manispaa ya Sumbawanga. Sababu za migogoro hii ni nyingi, lakini masuala ya ardhi yamekuwa yakiongoza. Daftari la malalamiko linaonesha wastani wa migogoro 10 husajiliwa kila siku katika dawati la manispaa la malalamiko. Halmashauri ilizidiwa na migogoro ya kijamii itokanayo na umiliki wa ardhi na kuongezeka kwa makazi yasiyopangwa.

Kabla ya mwaka 2016, Kijiji cha Kasisiwe kilikuwa na changamoto za umiliki wa ardhi, kuongezeka kwa makazi yasiyo rasmi na ukosefu wa barabara katika makazi ya watu. Hali hii ilichochewa na kukamilika kwa barabara kuu ya Tunduma – Sumbawanga ambayo iliongeza shughuli za kiuchumi na biashara na kuongeza wahamiaji wanaofuata fursa mbalimbali na kuzidisha mahitaji ya ardhi katika eneo la Kasisiwe. Changamoto nyingine zilizowakabili wakazi wa Kasisiwe zilijumuisha kuporomoka kwa thamani ya majengo kutokana na kutokuwepo kwa mipango miji kukiambatana na ukosefu wa barabara na nafasi za kuweka nguzo za umeme na mabomba ya maji. Jamii ilikosa huduma muhimu kama maji na umeme kutokana na kukosekana kwa barabara na njia za kupitisha miundombinu hii. Kutokana na kukosekana kwa barabara, huduma kama za magari ya wakonjwa na zimamoto hazikuwepo. Usafirishaji wa bidha na huduma haukuwezekana.



***Eneo la Kasisiwe kabla ya Urasimishaji***

**3.0 LENGO**

Lengo kuu la urasimishaji wa makazi katika kijiji cha kasisiwe lilikuwa kupunguza migogoro ya kijamii kuhusu ardhi ili kuboresha vipato na utoaji wa huduma. Kuwepo kwa viwanja ambavyo vimepimwa husaidia utoaji wa huduma za kiuchumi na kijamii kama maji, umeme na mtandao wa barabara. Aidha jitihada hii ilikuwa na malengo mahsusi ambayo ni; kupima eneo lote na kijiji na kutenga maeneo ya barabara, kuboresha usafi wa mazingira kwa kujenga miundombinu ya kudhibiti taka ngumu na majitaka, kuongeza thamani ya ardhi na majengo yaliyopo, kuwezesha umiliki rasmi wa ardhi ili wananchi waweze kupata hati na kuimarisha muungano katika jamii kwa kutokomeza migogoro yote ya ardhi. Manispaa ililenga katika kuongeza uwekezaji kwa kuunda mazingira wezeshi, kutenga maeneo ya umma kwa ajili ya shughuli za kijamii na kuwepo kwa nafasi za kuendeleza miundombinu ya huduma za maji, umeme na barabara.

**4.0 MIKAKATI YA UTEKELEZAJI**

Uboreshaji wa matumizi ya ardhi na urasimishaji hutumia mbinu mbalimbali kama utengaji wa maeneo, mipango kazi ya jamii na mipango ya mabadiliko jumuishi ya matumizi ya ardhi. Utengaji wa maeneo huwa na lengo kuu la kuboresha mazingira ya utumiaji wa ardhi. Mifano inaweza kuwa uwekaji wa minudombinu ya maji safi na maji taka, maeneo ya makazi na aina nyingine za miundombinu. Mipango kazi ya jamii (mipango midogo) ni mbinu shirikishi ambayo huwa na mfumo wa ushiriki wa jamii katika kuanzisha, kuunda, kupanga, kutekeleza na kuendeleza mradi wa matumizi ya ardhi. Mbinu hii huanza na warsha inayoshirikisha wadau mbalimbali ambapo wanajamii hushiriki sawa na wataalamu wa masuala ya ardhi. Matokeo ya warsha hii huwa ni mango kazi uliopewa kipaombele cha utekelezaji katika kuboresha matumizi ya ardhi. Mwisho, mbinu ya tatu ya mipango ya mabadiliko jumuishi ya matumizi ya ardhi hutumia teknolojia kama king'amuzi cha mbali (remote sensing), picha za angani (aerial photography) na mfumo wa taarifa za kijiografia (GIS) kuunganisha sura ya ardhi na takwimu za

matumizi ya ardhi kijamii na kiuchumi. Takwimu hizi hutumika kuandaa afua za matumizi ya ardhi. Mbinu zote hizi zilitumiwa na Manispaa ya Sumbawanga kuandaa mikakati ya utekelezaji kama inavyoelezwa hapa chini.
Mwaka 2016, utekelezaji wa jitihada hii uliazimiwa na wanajamii baada ya kutambua changamoto zolizoambatana na makazi yasiyo rasmi. Jamii ilijipanga kupitia mikutano ya kijiji na kuwa na majadiliano na maamuzi kuhusu mbinu za kufikia malengo. Kutambulika kwa mahitaji ya jamii kulitokana na mchakato ulioendeshwa kwa mbinu ya fursa na vikwazo kwa maendeleo (O&OD). Jamii ikishirikiana na viongozi wa kijiji iliweka vipaombele vya uboreshaji wa matumizi ya ardhi na urasimishaji wa makazi.

Maandalizi ya mikutano na warsha za uhamasishaji; mkutano wa kijiji ulifanyika 24/07/2016 kwa lengo la kuelimisha jamii kuhusu umuhimu wa kurasimisha makazi na majengo. Pendekezo hili lilipowasilishwa kwa mara ya kwanza tu, wakazi wote wa Kasisiwe walivutiwa na kukubaliana nalo. Makubaliano haya yalifikiwa baada ya maelezo ya kina kuhusu faida za kurasimisha makazi ikiwa ni pamoja na kupungua kwa migogoro ya ardhi katika jamii, kuongezeka kwa thamani ya ardhi na majengo, kupata hati miliki za ardhi na kuongeza fursa ya kupata mikopo kutoka taasisi za fedha.



***Kamati ya Maboresho ya Matumizi ya Ardhi ya Kijiji cha Kasisiswe***

Kuanzishwa kwa kamati ya uboreshaji wa matumizi ya ardhi; katika hatua za mwanzo za mradi huu, mkutano wa kijiji uliunda kamati yenye uwakilishi wa kutosha wa wanawake na vijana waliochaguliwa na mkutano wa kijiji. Kamati hii ilipewa jukumu la kukusanya raslimali ikiwa ni pamoja na raslimali watu kwa ajili ya ushauri wa kitaalamu, kukusanya fedha kutoka kwa wanajamii na kuandaa taarifa za mapato na matumizi.

Kendesha mafunzo kuhusu uboreshaji wa matumizi ya ardhi na urasimishaji; kama sehemu ya kujenga uwezo, maafisa wa manispaa wa mipango miji na maendeleo ya jamii waliendesha mafunzo ya kina kwa viongozi wa kijiji na wanajamii kuhusu umuhimu wa uboreshaji wa matumizi ya ardhi na urasimishaji. Mafunzo haya yaliamsha ushiriki kamilifu wa wakazi. Imani kwa viongozi wa kijiji ilitokana na uzoefu uliotokana na jitihada ya awali ya kuwaunganisha wananchi na kukamilisha ujenzi wa madarasa matatu katika shule ya Msingi Kasisiwe. Umoja thabiti kati ya wananchi, wajumbe wa kamati na viongozi wa Kijiji ulisababishamafanikio makuu katika kukamilisha jitihada hizi mbili.



***Upanuzi wa Sule ya Msingi Kasisiwe***

Ushiriki wa jamii kwa michango ya nguvukazi na fedha taslimu; zoezi la kupima ardhi ni la gharama sana. Ili kufikia lengo la uboreshaji wa matumizi ya ardhi na urasimishaji, jamii iliamua kuchangia fedha taslimu ili kukamilisha zoezi hili. Kamati iliweza kuzifikia kaya 555 ambazo kwa hiari zilichangia TZS 50,000/- kwa kila kiwanja kilichopimwa kama ilivyokubalika kwenye mkutano wa kijiji. Julma ya michango iliyokunywa hadi 15 Disemba 2017 ilikuwa TZS 32,014,000. Matumizi ya fedha hizi yalikuwa jumla ya TZS 16,649,080. Kamati ilibaki na salio la TZS 15,364,920 ambazo zilitumika kukodi teknolojia bora ya kupima na kuboresha matumizi ya ardhi iitwayo Real Time Kinematic (RTK). Fedha hizi pia zilitumika kuwezesha timu ya wataalamu waliotumia masaa mengi nje ya muda wa kazi kupima maeneo na kuweka alama za kudumu.

**5.0 RASLIMALI**

Manispaa pamoja na jamii ya Kasisiwe ilitumia aina mbalimbaliza raslimali kufikia uboreshaji na urasimishaji wa matumizi ya ardhi. Licha ya watumishi wa Manispaa ambao walitoa huduma za kitaalamu, kamati ya mradi, vioongozi wa kijiji, watu maarufu, timu ya menejimenti ya manispaa, mkurugenzi wa manispaa na wananchi kwa ujumla walitumia nafasi zao vema. Maafisa wa Mipango Miji, wapimaji na maafisa wa maendeleo ya jamii walihudumu katika kujenga uwezo kwa wananchi. Maafisa wa mipango miji na upimaji walishiriki kikamilifu katika zoezi hili kwa kuzalisha ramani za mji na matokeo ya upimaji. Ushiriki wao ulisaidia kupunguza gharama na kujiridhisha kuhusu ubora wa mradi.



***Maafisa wakiwa katika Upimaji***

Jamii ilitumia raslimali fedha; kutokana na ukweli kuwa jitihada ya urasimishaji ilipewa kipaombele na watu wa kasisiwe, ukusanyaji wa fedha haukuwa na changamoto. Kila kaya ilichangia TSZ. 50,000/- kwa

kila kiwanja kilichopimwa kwa ajili ya gharama za mipango miji, upimaji na upitishaji wa ramani katika ngazi ya wizara. Jumla ya TZS 32,000,000/- zilikusanywa kutoka kwa jamii. Raslimali nyingine zilijumuisha ardhi na vifaa vya upimaji wa ardhi kama Real Time Kinematic (RTK), mfumo wa taarifa za kijiografia (GPS) and alama za mipaka.

**6.0 MATOKEO**

Urasimishaji wa makazi yasiyo rasmi huleta usalama katika umiliki wa ardhi kwa wakazi husika na upatikanaji wa huduma za msingi za mijini. Urasimishaji wa makazi una faida nyingi zilizo dhahiri; huhamasisha kaya kuboresha nyumba zao, huwezesha uwekezaji katika shughuli zinazoweza kufanywa nyumbani na ambazo zina mchango mkubwa katika kupunguza umaskini, huboresha utoaji wa huduma mbalimbali za mijijini katika makazi na husaidia kuziunganisha jamii kuchangia usimamizi na uboreshaji wa mazingira ya makazi.



***Ufunguaji wa barabara katika Kijiji cha Kasisiwe***

Maboresho katika ukusanyaji wa taka ngumu na mazigira ya kuvutia; Kijiji cha kasisiwe kimeshuhudia ukusanyaji taka ngumu ulioboreshwa kwani kumekuwa na vituo vya kukusanyia taka ambavyo uchafu huondolewa mara kwa mara. Kijiji hiki kwa sasa kina mazingira bora kwa ujenzi wa nyumba za makazi na biashara na hivyo kuwa mazingira bora ya uwekezaji na uzalishaji wa fursa za ajiara.

Kuongezeka kwa thamani ya ardhi na majengo; thamani ya ardhi imeomgezeka kutoka TZS 1000/$m^2$ mwaka 2015 hadi TZS 3000/$m^2$ - 5000/$m^2$ mwak 2017. Ongezeko hili linatokana na upimaji wa viwanja na urasimishaji wa ardhi na majengo. Licha ya kuwepo kwa miundombinu inayoruhusu upatikanaji wa huduma mbalimbali za jamii, kijiji kimependezeshwa na maeneo ya wazi yenye bustani na udhibiti wa moto na ajali za barabarani umekuwa wa uhakika.

Kijiji cha Kasisiwe kimekuwa kituo cha kujifunzia; kutokana na kufanikiwa kukamilika kwa utekelezaji wa jitihada hii, vijiji na mitaa ya jirani imeanza kujifunza na kutumia uzoefu wa Kasisiwe kuanzisha na kutekeleza miradi kam hii katika maeneo yao. Maeneo haya ni pamoja na vijiji vya Msua, King’ombe na Eden ambavyo vipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji. Manispaa nayo imekuwa mbele katika mipango na matumizi ya ardhi. Ikienda sambamba na jitihada ya Kasisiwe, Manispaa ya Sumbawanga imepima viwanja katika eneo la Nambogo na inagawa viwanja kwa gharama nafuu. Picha iliyopo hapa chini inadhirisha ukweli huu.




***Viwanja vilivyopimwa katika eneo la Nambogo***

**7.0 MIKAKATI YA UENDELEVU**

Ili kuleta uendelevu wa jitihada hii Halmashauri imekuwa ikitoa ramani za upimaji wa ardhi na kusimamia zoezi la kugawa wa viwanja kwa watu binafsi, kuendesha mikutano ya mara kwa mara ili kuelimisha jamii katika kuzingatia michoro ya upimaji na umuhimu wa kujenga majengo kulingana na michoro iliyopitishwa na kuidhiniswa na kuendelea kuhamasisha urasimishaji katika maeneo mengine yenye makazi yasiyo rasmi.

Viongozi wa kijiji wameendelea kuhamasisha jamii kuendelea kutoa michango kwa ajili ya kupima ardhi na viwanja. Mikakati mingine ni pamoja na;

(i) Kuandaa sheria ndogo itakayomlazimu kila mkazi kuhakikisha kuwa ardhi na viwanja vyake vimepimwa.

(ii) Kuitisha mikutano ya mara kwa mara kati ya viongozi na jamii ili kuipatia jamii ya kasisiwe na umma kwa ujumla taarifa za maendeleo ya mradi.

(iii) Kwa kushirikiana na wakala wa barabara za vijijini na mijini, Halmashauri itaziboresha barabara na mitaa katika maeneo yaliyorasimishwa na kuweka alama za barabarani ili kuwepo na matumizi na usimamizi bora wa barabara.

(iv) Kuendelea kuwahimiza viongozi wa jamii kuhusu uwazi, umoja na usimamizi bora wa raslimali.

**8.0 SIRI YA MAFANIKIO**

Urasimishaji wa ardhi na majengo katika kijiji cha Kasisiswe ulifanikiwa kutokana na vigezo mbalimbali ambavyo kwa kifupi vimetajwa hapa chini;

(i) Jitithada hii ilitokana na hitaji la jamii; hivyo wazo lenyewe pamoja na namna ya utekelezaji vilitoka kwa jamii. Kupitia mikutano, umakini na utayari wa kujitoa kukoka kwa jamii uliamshwa na kufanya ukusanyaji wa fedha za jitihada hii kuwa rahisi.

(ii) Uongozi bora katika ngazi za Kijiji na Kata ulifanya kazi nzuri ya kuunganisha na kuhamasisha jamii. Viongozi wa jamii walitumia uwazi wa hali ya juu katika matumizi ya raslimali na kusababisha kuongezeka kwa imani kwa viongozi na ari ya jamii.

(iii) Ushauri wa haraka, wenye hekima na utaalamu uliobobea kutoka Halmashauri ulichangia kwa kiasi kikubwa mafanikio ya mradi wa urasimishaji.

# HALMASHAURI YA MANISPA YA KIGOMA UJIJI


**URASIMISHAJI WA UMILIKI WA ARDHI ILI KUTOKOMEZA MAKAZI HOLELA NA MIGOGORO**



*Uzoefu wa Manispaa ya Kigoma Ujiji*

**1.0 UTANGULIZI**

Manispaa ya Kigoma Ujiji ni moja ya Halsmahuri 8 za Mkoa wa Kigoma iliyoanzishwa kama Mji tangu enzi za Waarabu ukiwa kituo muhimu cha biashara ya watumwa kwenye njia ya biashara hiyo iliyoanza Kongo hadi Bagamoyo. Manispaa hii ipo kwenye fukwe za Kaskazini za ziwa la pili kwa kina duniani (Ziwa Tanganyika) katika Latitudo 4.9115° Kusini na Longitudo 29.6746° Mashariki. Halmashauri ina eneo la 128km$^2$ ambazo 127.85km$^2$ ni nchi kavu na 15km$^2$ ni maji. Kwa mujibu wa sensa ya mwaka 2012, Manispaa ya Kigoma Ujiji ina wakazi 215,458; 104,185 ni wanaume na 111,273 wanawake na wasatani wa kaya wa 5.0. Kiutawala, Manispaaa ina Tarafa 2 (Kigoma Kaskazini na Kigoma Kusini), Kata 19 na Mitaa 68.




Source: Kifaro et al. (2013)
FIGURE 1: Map of Kigoma region showing the three districts where some of the Rift Valley fever virus-positive sheep and goats were identified.

***Ramani ya Manispaa ya Kigoma Ujiji***

Uchumi wa Mnispaa unatemenea kilimo cha kujikimu cha wakulima wadogodogo na ufugaji. Mifugo katika manispaa hii hujumuisha ng'ombe wa kienyeji, mbuzi na kondoo. Shughuli nyingine za kiunchmi ni uvunaji wa misitu, uvuvi na utalii kwenye maeneo ya Ziwa Tanzganyika. Manispaa hii hufanya biashara na nchi za Kongo na Burundi ambazo hazina bahari.

Urasimishaji wa ardhi katika Manispaa ya Kigoma Ujiji ulifanyika katika maeneo ambayo hayajapimwa yaliyokuwa na majengo holela kwenye eneo lenye 7,850ha sawa na 61.3% ya eneo lote la Manispaa. Maeneo ambayo hayana majengo hutumiwa kwa kilimo sawa na 4,949.2ha, yaani 38.7%. Eneo ambalo limepimwa na kupangwa kitaalamu ni 3,473.9ha sawa na 27.14% ya eneo lote la manispaa na makazi ambayo hayajapimwa ni 879.2ha sawa na 6.9% ya eneo lote. Zaidi ya 80% ya eneo ambalo limepangwa halijapimwa kikamilifu; kuna mipaka tu ya viwanja ambayo imewekwa na wamiliki na haiwezi kutumiwa kuomba umiliki kamili bali hati za umiliki wa muda mfupi.

**2.0 TATIZO**

Manispaa ya Kigoma Ujiji ilikuwa na migogoro mingi ya ardhi katika maeneo ya Bangwe, Kamala, Mwasenga, Vamia and Kagera. Mwaka 2016, jumla ya migogoro ya ardhi 419 iliandikishwa. Asili ya migogoro iliyoletwa Manispaa ilisababishwa na ukosefu wa mipango ya upimaji ardhi, kukosekana kwa matumizi ya ardhi yaliyoratibiwa, ukosefu wa miundombinu hasa barabara, umiliki ardhi usio rasmi na uwepo wa madalali wa uuzaji ardhi kinyume na sheria (kwa mfano, kulikuwa hati za muda za umiliki 70 ambazo ni bandia, vyeti vya umiliki na risiti nyingi zilishikiliwa kinyume na sheria). Kulikuwa na utulivu

duni katika jamii za maeneo ya Bangwe, Kamala na Machinjioni na hali hii ilijitokeza dhahiri kwa kuvamiwa maafisa wa manispaa walipojaribu kufika ili kupima na kurasimisha maeneo haya.

Maeneo ya pembezoni mwa mji kama Machinjioni, Buhanda (Mwasenga area), Gungu (maeneo ya Kikungu na Kabingo) na Kibirizi (maeneo ya Kahabwa, Buronge and Butunga) yalikumbwa na shughuli za ujenzi holela wa kasi ilihali palikuwa hapajapangwa wala kupimwa. Hali hii ilisababisha kutokuwepo kwa ardhi kwa ajili miundombinu ya umma, mifumo ya maji na umeme na maeneo ya wazi. Michoro, ramani na mipaka (vya muda) iliyokuwepo haikuweza kusuluhisha migogoro ya ardhi kutokana na kukosekana vipimo vya kisasa (coordinates) vyenye uhakika. Hali hii ilichangiwa na upungufu mkubwa wa watumishi katika sekta ya ardhi na mipango miji; Manispaa ilikuwa na watumishi 6 tu (mkuu wa idara, mpimaji 1, mthamini 1, afisa ardhi 1, maafisa mipango miji 2) badala ya maafisa 26 wanaotakiwa katika Idara. Kulikuwa na upungufu katika bajeti na upungufu wa vifaa vya upimaji kuanzia milingoti hadi darubini.

**3.0 LENGO**

Lengo kuu la jitihada hii lilikuwa kupunguza migogoro ya ardhi na kutokomeza makazi yasiyo rasmi katika Manisapaa. Aidha malengo mahsusi ya Manisapaa ya Kigoma Ujiji yalikuwa;

(i) Kuendesha zoezi la mipango miji na kufanya upimaji wa ardhi katika maeneo yote ya Manispaa ambayo yana majengo lakini hayajapangwa na kupimwa.
(ii) Kuandaa michoro ya mipango miji na kuratibu uwekaji wa mipaka ili kupitisha na kusajili upimaji katika maeneno yate yaliyoainishwa.
(iii) Kuimarisha ushirikiano kati ya serikali, wamiliki wa ardhi, sekta binafsi (mashirika na watu binafsi waliosajiliwa kujihusisha na mipango miji na upimaji wa ardhi).
(iv) Kuendesha shughuli za upangaji na upimaji wa ardhi kwa ushirikiano na uwazi na kujenga uaminifu na Imani kati ya wamiliki ardhi na watumishi wa serikali.
(v) Kuwa na hali ya ushindi kwa pande zote mbili (serikali na wamiliki wa ardhi) kwa kutenga ardhi kwa ajili ya miundombinu ya umma na huduma za jamii bila fidia.
(vi) Kuleta maendeleo kwa mujibu wa matumizi elekezi ya ardhi katika michoro ya mipango miji.
(vii) Kuboresha usalama wa umiliki ardhi kwa wamiliki wa ardhi.

**4.0 MIKAKATI YA UTEKELEZAJI**

Novemba Mwaka 2016, Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi alifanya ziara mkoani Kigoma. Katika ziara hii Waziri aliiagiza ofisi ya Kamishna Msadizi wa Ardhi kuainisha migogoro yote ya ardhi na kutafuta mikakati ya kuimaliza kwa ushirikiano na Manispaa. Wakazi wote waliokuwa na migogoro ya ardhi waliombwa kuandika barua na kuleta malalamiko yao ambapo migogoro 419 ilisajiliwa. Idadi hii kubwa ya migogoro iliilazimu Manisapaa kuingilia kati kwa kuanzisha ushirika na wamiliki ardhi kwenye zoezi la upimaji. Utaratibu huu uliwezesha kulipia gharama za mipango miji na upimaji, upatikanaji wa ardhi kwa ajili ya miundombinu ya umma na huduma za jamii na ushiriki wa sekta binafsi katika zoezi la urasimishaji.

Utumiaji wa programu ya urasimishaji wa ardhi; Manisapaa ya Kigoma Ujiji iliamua kutumia mwongozo wa mwaka 2016 wa urashimishaji ardhi ambao unaanzisha kamati 4 za kiutawala katika zoezi la urasimishaji; kamati hizi ni Kamati ya Uendeshaji (timu ya menejimenti ya manisapaa), Kamati ya Ufundi, Kikosi Kazi na Kamati ya Wananchi. Pamoja na kufuata mwongozo, Manispaa iliboresha muundo katika kuunda kamati ya wananchi, ambapo, badala ya viongozi wa jamii (kama mwongozo unavyoeelekeza), wamiliki wa ardhi walipewa fursa ya kuchagua mwakilishi wao wanayemwamini kuwa mjumbe wa kamati ya wananchi. Nyongeza hii ilikuwa muhimu kupunguza misuguano na itikadi za kisiasa katika urasimishaji wa ardhi. Hatua zilizochukuliwa katika urasimishaji zimeelezwa kwa kina hapa chini.

Uhamasishaji wa jamii; shughuli hii ilifanyika kupitia mikutano ya umma iliyoendeshwa katika maeneo ya mradi. Mikutano hii ilijumuisha viongozi wa jamii (Diwani, afisa mtendaji wa kata, wenyeviti wa mitaa, watendaji wa mitaa na wajumbe wa kamati za mitaa), wamiliki wa ardhi na watumishi wa Manipaa (afisa mipango miji, mpimaji, afisa ardhi, mthamini na afisa maendeleo ya jamii). Lengo mikutano ya uhamasishaji lilikuwa kutoa maelezo ya mradi, kuelezea umuhimu wa kuishi katika maeneo yaliyopangwa na kupimwa na kuainisha hatua zitakazofuatwa kukamilisha mchakato. Aidha, mikutano iliendeshwa ili kuwaptia elimu na uelewa wa kina kuhusu umiliki wa ardhi na usajili, tofauti kati ya kuweka mipaka na upimaji, maana ya hati ya muda ya umiliki na cheti/hati cha umiliki na mchakato wa kupitisha umiliki. Pia mikutano hii ililenga kuwapa mwanga wamiliki wa ardhi kuhusu umuhimu wa ushirikiano kati ya jamii, sekta binafsi na Manispaa. Wamiliki wa ardhi walielewa na kuona umuhimu wa kulipia zoezi la mipango miji na upimaji. Kiasi walicholipa kilianzia TZS 60,000 hadi TZS 120,000 isipokuwa eneo la Kilimahewa ambapo malipo yalikuwa TZS 200,000 kutegemea idadi ya viwanja na aina uendelezaji wa ardhi utakaofanyika.


Uundaji wa Kamati Jamii ya ardhi; baada ya uhamasishaji kukamilika, jamii iliunda kamati ya ardhi ya wajumbe 7 – 9 kwa kufanya uchaguzi katika mkutano wa wamiliki wa ardhi wote. Kamati ina mwenyekiti, katibu, mweka hazina na wajumbe; wote hufanya kazi kwa kujitolea.

Kuandaa katiba ya kamati, kusajiliwa na kufungua akaunti ya benki; baada ya kuunda kamati jamii ya ardhi, katiba iliandaliwa ili kuongoza na kuelekeza utekelezaji. Kamati ilisajiliwa kama kikundi cha kijamii na kupatiwa cheti cha usajili ili kwezesha mchakato wa kufungua akaunti benki. Kamati ilifungua akaunti kati benki za NMB, CRDB, EXIM na TPB ambapo michango yote ya wamiliki wa ardhi ilihifadhiwa.

Ukusanyaji wa taarifa na maandalizi ya michoro ya mipango miji; mazoezi haya yaliendeshwa na Manispaa kwa kushirikiana na kamati ya wananchi na kampuni binafsi iliyopewa kandarasi ya zoesi hili. Majukumu ya kamati ya wananchi yalikuwa kuainisha wamiliki wa ardhi, kuamua migogoro ya mipaka ya ardhi na kuweka timu kwa kila mmiliki wa ardhi wakati wa ukusanyaji wa taarifa (uliohusu kusoma na kuandika vipimo kwa *GPS* na mitambo ya *total station* za mkononi). Baada ya ukusanyaji wa taarifa michoro ya mipango miji iliandaliwa na kuwasilishwa kwenye mkutano wa wamiliki wote kwa ajili ya majadiliano. Baada ya kupitishwa na mkutano wa wamiliki michoro hii iliwasiliswa kwenye kamati ya Manispaa ya Mipango miji, Miundombinu na Mazingira ili kupitishwa. Michoro hii ilipelekwa Sekretarieti ya Mkoa kwa uchambuzi zaidi na kibali cha kupeleka kwa Mkurugenzi wa Mipango (Mijni na Vijijini) katika Wizara ya Ardhi kupata idhinisho (kibali) la mwisho.

Upimaji na kutolewa kwa idhini; baada ya kuapata idhini ya michoro ya mipango miji kutoka wizarani na ushauriano na kamati ya wananchi, Manispaa iliipa kampuni binafsi kandarasi ya kuendesha zoezi la upimaji kwa mujibu wa kanuni na viwango vya serikali.

Utoaji wa vyeti (hati) za umiliki; Manispaa iliendelea na mchakato wa kusajili viwanja vilivyopimwa na ada zitakazolipwa. Wamiliki wa viwanja walitakiwa kulipa ada za maombi (TZS 20,000), mipango miji (TZS 20,000), usajili na cheti cha umiliki (TZS 50,000), malipo ya muhuri na ongezeko la thamani 2.5% ya tahmani ya ardhi.  Wamiliki wa viwanja walipewa fursa ya kuona kiasi kilichotakiwa kulipwa katika ofisi ya kata ili kupata vyeti vya umiliki. Kabla ya malipo mmiliki alitakiwa kupata fomu ya tathmini ya kiasi kianchotakiwa kulipwa kwa kila kiwanja, kuchukua ankara kutoka ofisi ya ardhi na kulipia kupitia mfumo wa malipo wa serikali wa GePG. Mwisho, wamiliki wa viwanja walipatiwa uthibitisho wa kupokelewa kwa malipo. Hatua zauUtekelezaji wa mradi huu zimeelezwa kwa kifupi katika mchoro hapa chini.




***Modeli ya Utekelezaji wa Mradi***

**5.0 RASLIMALI**

Utekelezaji wa jitihada hii ulitumia raslimali za aina mbalimbali. Raslimali fedha zilijumuisha michango toka kwa wamiliki wa ardhi ikiwa jumla ya TZS 332,140,000.00 kwa ajili ya upimaji wa viwanja 4,864 mwaka 2016. Raslimali zilijumuisha watumishi wa manispaa, wakandarasi na wamiliki wa ardhi. Raslimali nyingine ni zilijumuisha ardhi, vyombo vya usafiri na vifaa vya upimaji.

**6.0 MATOKEO**

Manispaa ya Kigoma Ujiji imefanikiwa kupima viwanja 4,864 katika maeneo mbalimbali; Kilimahewa (513), Katubuka (197), Kabingo (430), Kahabwa/Buronge (1,155), Nazareti (330), Masanga (360), Mwasenga (122), Vamia (684), Airport (491), Burega (321) and Mwanga Vamia (31). Wamiliki wa viwanja walilipa gharama za hati za umiliki wa ardhi na kupokea vyeti 650 vya haki ya umiliki; vyeti 208 mwaka 2016 na vyeti 442 mwaka 2017.

Kuongezeka kwa mapato ya Manisapaa; urasimishaji wa ardhi umeongeza idadi ya viwanja na hivyo kuongeza mapato ya Manispaa yatokanato na kodi ya ardhi kutoka TZS 170 millioni mwak 2015/2016 hadi TZS 1.12 billion mwaka 2016/2017. Manispaa imepata ardhi ya kutosha kwa ajili ya huduma za jamii bila julipa fidia. Ardhi ambayo Manispaa imepata inajumuisha maeneo ya wazi, shule, makaburi, vituo vya polisi, masoko na barabara.

Ufanisi wa kazi kwa watumishi wa Manispaa umeongezeka; kuwepo kwa maeneo yaliyopangwa vizuri na kupimwa kumepunguza migogogoro ya ardhi na kuongeza ufanisi katika utoaji wa huduma kwani watumishi wa Manispaa wamepata muda wa kutosha wa kushughulika na masuala ya kitaalamu. Kwa mfano migogoro ya ardhi imepunguzwa kutoka 10 – 5 kwa mwaka katika Kata ya Kahabwa. Kwa sasa migogoro ya ardhi inatatuliwa kwa urahisi kutokana na ardhi kuwa imepimwa na kuna mipaka yenye vipimo.

Thamani ya ardhi imeongezeka; katika maeneo ambapo jitihada hii ilifanyika, thamani ya ardhi imeongezeka kutoka TZS 500,000/= kabla ya urasimishaji hadi TZS 2,000,000 na TZS 3,000,000 kwa kiwanja kimoja. Katika eneo la Kilimahewa thamani ya kiwanja ilikuwa TZS 3,000,000 kbala ya urasimishaji; kwa sasa thamani imeongezeka hadi kufika kati ya TZS 4,000,000 na TZS 6,000,000/= kwa kiwanja kimoja. Aidha, umiliki wa kisheria wa ardhi umewapa uhakika wamiliki wa kuweza kutukia vyeti vyao vya umiliki kuomba mikopo katika taasisi za fedha.

**7.0 MIKAKATI YA UENDELEVU**

Manispaa na jamii kwa ujumla zimejiwekea mhakikisha jitihada hii ni endelevu. Mikakati hii ni pamoja na msisitizo wa kuendeleza viwanja na ardhi ambayo imepimwa kwa kufuata taratibu za vibali vya ujenzi. Aidha, Manispaa inaendelea inawashirikisha Maafisa watendaji wa Kata na Mitaa katika kuhamasisha na kutoa elimu kwa jamii kukubaliana na mchakato wa urasimishaji katika maeneo ambayo bado hayajajapangwa wala kupimwa. Manispaa itaendelea kujenga na kuimarisha uwezo wa kamati ya wanancnhi ili kuhakikisha uendelevu wa urasimishaji ardhi na makazi.

**8.0 SIRI YA MAFANIKIO**

Mafanikio ya jitihada hii yanatokana na sababu mbalimbali; sababu hizi ni pamoja uchangiaji wa pamoja wa gharama za urasimishaji, utayari wa jamii kushiriki kikamilifu, ushirikiano bora na sekta binafsi na mahusiano fanisi kati ya wadau mbalimbali. Ziara ya Waziri na maelekezo yake ya kutokomeza migogoro ya ardhi ilichangia sana kufanikiwa kwa urasimishaji wa ardhi na makazi katika Manispaa ya Kigoma Ujiji.

# HALMASHAURI YA MJI KIBAHA

**UJENZI SHIRIKISHI WA SOKO KWA AJILI YA KUBORESHA HALI YA MAISHA**




***Uzoefu wa H/Mji wa Kibaha***

## 1.0 UTANGULIZI

Halmashauri ya Mji wa Kibaha ni moja kati ya Halmashauri 9 za Mkoa wa Pwani iliyoanzishwa mwaka 2004 na inapatikana umbali wa 40km kutoka Jiji la Dar es Salaam. Inapakana na Manispaa ya Ubungo upande wa Mashariki, H/W ya Bagamoyo upande wa Kaskazini, H/W ya Kisarawe upande wa Kusini na Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mlandizi upande wa Kaskazini. Halmashauri ya Mji wa Kibaha inapatikana kati ya Latitudo 6.8° Kusini na Longitudo 38.2° na 38.5° Mashariki. Kwa mujibu wa Sensa ya mwaka 2012, Halmashauri ilikuwa na idadi ya watu 128,488 kati yao wanawake 65,835 na wanaume 62,653, idadi ya kaya ni 17,788 na wastani wa watu katika kaya ni 4.1. Kufikia mwaka 2017 kadirio la watu ilikuwa 144,241; wanaume 70,334 na wanawake 73,906.

Wenyeji asilia wa Mji wa Kibaha ni Wazaramo, Wamatumbi na Wangindo. Makabila mengine ni Wayao, Wamakonde, Wakwere, Wangoni, Wagogo, Wasukuma, Wanyamwezi, Wandengereko, Wamwera, Wachaga, Wapare na Wagweno. Mchanganyiko wa makabila unatokana na kuongezeka kwa wahamiaji kutoka maeneo mbalimbali ya nchi wakitafuta fursa kwenye viwanda na biashara mbalimbali.

Halmashauri ya Mji ina eneo la 750km$^2$. Kiutawala, Halmashauri ina Tarafa 2 (Kibaha na Kongowe), Kata 14, (Tumbi, Mailimoja, Kibaha, Visiga, Mkunza, Kongowe, Misugusugu, Picha ya Ndege, Msagani, Mbwawa, Pangani, Viziwaziwa, Tangini na Sofu) na Mitaa 73.




***Ramani ya H/M wa Kibaha***

Masoko yapo chini ya kitengo cha biashara ndani ya idara ya fedha na biashara. Majukumu ya kitengo cha biashara ni kusimamia masuala ya biashara ndani ya Halmashauri. Ukuaji wa biashara ndani H/Mji wa Kibaha inakadiriwa kufika 8% kwa mwaka. Kwa mfano, Kitengo cha biashara kwa muda mfupi kimeweza kutoa leseni za biashara 4,015. Halmashauri ilikusanya takwimu za viwanda na biashara na kubaini kwamba kuna viwanda vya kati 13, viwanda vidogovidogo 1,250 na biashara za kawaida 4,015. Kitengo cha Biashara kinachangia kwa kiasi kikubwa ukuaji wa Mji wa Kibaha kwa kujihusisha na ukusanyaji wa mapato yatokanayo na leseni za biashara na vileo, ushuru wa hoteli, kuboresha mazingira ya uwekezaji wa viwanda vikubwa na vidogo, kukusanya taarifa za viwanda na masoko na kutoa elimu ya ujasiriamali kwa wafanyabiashara wadogo.

**2.0 TATIZO**

Katika mazingira ya Mijini na Vijijini miundombinu ya masoko ni muhimu, inatoa fursa kwa watu wa maeneo hayo kununua na kuuza bidhaa mbalimbali hasa vyakula. Masoko yanaongeza fursa za ajira kwa idadi kubwa ya watu. Wazalishaji wa mazao hutegemea soko kuuza mazao na walaji hutegemea soko kupata mahitaji yao. Masoko hujumuisha aina zote za biashara, maduka na uuzaji wa jumla na rejareja wa bidhaa za viwandani. Masoko ni moja ya miundombinu muhimu katika mazingira ya Halmashauri za Wilaya na za Miji.

Mfumo wa soko wa ufanisi unaweza kutoa bei bora kwa wazalishaji na kuboresha upatikanaji wa mazao na bidhaa kwa bei yenye ushindani. Ujenzi wa masoko au uboreshaji wa masoko unaweza kusaidia kutatua changamoto zinazokabili masoko. Hata hivyo, kabla ya kuchuka uamuzi wa kuboresha masoko, ni muhimu kubaini hasa changamoto kabla ya kuamua kuziondoa. Changamoto hizo zinaweza kuwa ukosefu wa barabara katika eneo la soko, ukosefu wa elimu ya biashara kwa wafanyabiashara na wateja na uhaba wa bidhaa za kuvutia wateja.

Halmashauri ya Mji wa Kibaha ambayo ndio makao makuu ya Mkoa wa Pwani ilikua na soko moja katika eneo la Mailimoja ambalo lilijengwa mwanzoni mwa miaka ya 1970. Wakati wa ujenzi wa soko hilo, idadi ya watu ilikuwa ndogo; Kibaha ilikuwa na watu 19,010 tu. Soko lilikuwa dogo na lilikuwa na uwezo wa kuhifadhi wafanyabiashara 400 tu. Aidha, soko la Mailimoja halikuwa na miundombinu ya kisasa ya masoko ya mijini, hapakuwa na vitendea kazi na mfumo thabiti wa kudhibiti taka ngumu. Eneo la soko lilibaki kuwa chafu hivyo kusababisha hatari ya kuzuka kwa magonjwa ya mlipuko na uchafuzi wa hewa. Ongezeko la watu na biashara lilisababisha miundombinu ya soko kushindwa kumudu mahitaji ya wakazi wa Mji wa Kibaha hadi mwaka 2016.



***Gari la Halmashauri likikusanya taka katika soko la Mailimoja***

Mbali na ongezeko la watu na uchakavu wa miundombinu ya soko, upanuzi wa barabara ya Morogoro ulimega eneo la soko ili kupisha ujenzi wa barabara. Kuvunjwa kwa soko kulisababisha Halmashauri kupoteza mapato na wananchi kukosa mahitaji mbalimbali ambayo wangeyapata sokoni. Hali hii ilitoa msukumo kwa Halmashauri kupanga na kutekeleza ujenzi wa soko jipya ili kurahisisha upatikanaji wa huduma na mahitaji ya jamii.

**3.0 LENGO**

Kaulimbiu ya H/Mji wa Kibaha inahusu; “Kutoa huduma bora na kuweka mazingira rafiki kwa uwekezaji kwa kutumia rasilimali zilizopo kwa maendeleo endelevu”. Lengo kuu la utekelezaji wa jitihada ya ujenzi

wa soko jipya la Mnarani ni kuweka miundumbinu ya kutosha ya biashara kwa wafanyabiashara na wateja na kuongeza mapato ya ndani ya Halmashauri. Malengo mahususi ni pamoja na;

(i) Kujenga soko la kisasa lenye huduma zote muhimu
(ii) Kushirikisha jamii katika ujenzi na uendeshaji wa soko
(iii) Kukuza fursa za ajira na kuongeza kipato kwa wafanyabiasahara wadogo
(iv) Kuongeza fursa kwa wafanyabiashara wadogo na kuwahamisha kutoka eneo la Mailimoja
(v) Kuongeza wigo wa kodi kwa Halmashauri na kuimarisha ukusanyaji wa mapato
(vi) Kuboresha mazingira ya utoaji wa huduma kwa wananchi

**4.0 MIKAKATI YA UTEKELEZAJI**

Ujenzi wa soko la Mnarani ulitokana na kuvunjwa kwa soko la Mailimoja kufuatia upanuzi wa barabara na uhitaji wa Halmashauri kuongeza mapato kupitia leseni za biashara. 23/09/2016, wakala wa barabara (TANROADs) waliweka alama za kuashiria kuvunjwa kwa soko lote la Mailimoja ili kupanua barabara. Wamiliki wa vibanda vya biashara walipewa fursa na muda wa kuvunja vibanda vyao wao wenyewe ili kuondoa au kupunguza hasara ambayo wangeweza kuipata na uharibifu wa mali kama uvunjaji ungefanywa na TANROADs. Katika kipindi hiki Halmashauri na wanasiasa waliamua kuhamasisha ujenzi wa soko bora la kisasa. Mkuu wa Mkoa Mh. Evarist Ndikilo alimwomba Meneja wa TANROADS kuwapa muda wa miezi 3 ili kutoa fursa kwa wafanyabiashara na Halmashauri kuhamia eneo jipya la soko; vilevile, Mkuu wa Mkoa alimuomba Waziri wa Ujenzi, Usafirishaji na Mawasiliano Mh. Makame Mbarawa kufanya upanuzi wa 60m kwa kila upande wa barabara badala ya 121m. Ombi hili lililenga kutoa fursa ya kuhama kwa hatua badala ya kuvunja soko kwa wakati mmoja jambo ambalo lingesababisha uharibifu na hasara kubwa kwa wafanyabiashara.

Uamuzi wa TANROADS kuhusu kuvunja soko la Mailimoja ulisababisha taharuki kwa watumiaji wa soko. Hali hii ililazimu kujenga uelewa kwa watumiaji wa soko kuhusu umuhimu wa upanuzi wa miundombinu ya barabara. Kufuatia uamuzi huu, Mkuu wa Wilaya ya Kibaha Mh. Assumpta Mshama alifanya mikutano 3 na jumuiya ya wafanya biashara wadogo ili kuwaomba kuwa watulivu wakati wa kipindi cha mpito. Mikutano hii ilimalizika kwa makubaliano ya kubadilisha uongozi katika kipindi cha mpito kuelekea matumizi ya soko jipya la Mnarani.



***Soko la Mailimoja ambalo lilivunjwa.***

Baada ya hatua zilizochukuliwa na viongozi wa juu wa kisiasa, Halmashauri ya Mji wa Kibaha iliunda mikakati kadhaa kukabiliana na hali ya kubomolewa kwa soko na kuhamia eneo jipya la soko la Mnarani. Halmashauri kwa kushirikana na Umoja wa Wafanyabiashara Wadogo walianza kuwatambua na kuandikisha wafanyabiashara mabao walikuwa wakitumia soko la Mailimoja. Wamiliki 200 wa biashara walitambuliwa. Utambuzi huu ulilenga kuwashirikisha katika kufanya maamuzi na kuwapa fursa ya

kuingia mkataba kujenga vizimba vya biashara na maduka. Katika kujenga uwelewa na hamasa, Halmashauri ilendesha mikutano 10 na wawakilishi wa wafanyabiashara 499.

Ujenzi wa soko jipya ni mradi ambao ulizuka kwa dharura na hivyo Halmashauri ilipaswa kuchukua maamuzi ya haraka. Halmashauri ililazimika kuahirisha baadhi ya vipaumbele vyake katika mwaka wa fedha 2017/2018 ili kutekeleza mradi wa soko. Miradi ambayo iliyoahirishwa ni pamoja na ujenzi wa ofisi unaoendelea, ununuzi wa madawati, uundaji wa ramani za mipango miji, ujenzi wa chumba cha upasuaji katika kituo cha afya cha Mkoani, fidia ya ardhi na maandalizi ya maonesho ya nanenane. Fedha za miradi hii zilielekezwa kwenye ujenzi wa soko la kisasa eneo la Mnarani. Halmashauri iliandaa eneo na kulisafisha kwa ajili ya hatua za awali za ujenzi wa soko na kuandaa michoro ya soko jipya, maduka na majengo ya matumizi mengine.


Halmashauri ilitambua umuhimu wa kuwashirikisha wadau wengine kama TANESCO, SUMATRA, DAWASCO na Polisi. Wadau hawa walikuwa muhimu katika kufanikisha utekelezaji wa mradi na kurahisiha upatikanaji wa miundombinu kama umeme, maji na usafiri wa mabasi ya abiria *(daladala)* katika eneo la soko la Mnarani.



***Eneo jipya la maduka katika soko la Mnarani***

Uhamasishaji na ukusanyaji wa fedha za ujenzi wa soko; kutokana na ufinyu wa rasilimali fedha Halmashauri iliamua kuwashirikisha wamiliki wa biashara kuchangia gharama za ujenzi wa miundombinu ya soko. Baada ya uhamasishaji wa kina wafanyabiashara na wajasiriamali walikubali kuungana na Halmashauri kutekeleza mradi. Utekelezaji wa mradi huu ulifanyika chini ya makubaliano ya ubia wa wafanyabiashara na Serikali wa Jenga-Endesha-Kabidhi (Build-Operate-Transfer agreements).

Ujenzi wa Miundombinu ya soko kwa kutumia misingi ya ubia kati ya serikali na sekta binafsi unahitaji mkataba wa kubainisha aina ya ujenzi, gharama za ujenzi na muda ambao mfanyabiashara atatumia miundombinu hiyo kabla ya kukabidhi umiliki kwa Halmashauri. Jukumu la kuandaa mikataba lilitekelezwa na kitengo cha sheria. Mikataba ilibainisha namna ya utekelezaji wa ujenzi wa miundombinu ya soko na kila mfanyabiashara alipatiwa mkataba. Ujenzi wa soko ulihusisha ujenzi wa vizimba vya biashara ndogo ndogo, eneo la kuuzia nafaka, vizimba vya taka, sehemu ya kutolea huduma za chakula, ujenzi wa mifereji ya maji, ujenzi wa barabara na stendi ya mabasi madogo ya abiria, ujenzi wa vyoo, usimikaji wa mifumo ya umeme wa sola na ujenzi wa fremu za maduka na vioski. Umoja wa Wafanya biashara ulikubali kujenga baadhi ya miundombinu na kuendelea kulipa 50% ya kodi ya pango hadi kukamilisha urejeshaji wa gharama za ujenzi. Ushirikishwaji wa wafanyabiashara ulirahisisha kukamilika kwa mradi mapema.



***Mikataba baina ya Halmashauri na Wafanyabiashara***

Mkakati mwingine muhimu uliotumika ni kubadilisha njia za magari ya abiria (Daladala) na kuzimika kupitia stendi ya mabasi madogo ya soko la Mnarani. Halmashauri kwa usaidizi wa SUMATRA na Polisi walibadilisha njia ya mabasi na kupitia eneo la soko ili kurahisisha usafiri kwa watumiaji wa soko. Hii ndio sababu ya Halmashauri kuamua kujenga stendi ya mabasi katika eneo la soko.




***Eneo la stendi mkabala na soko***

Halmashauri ilifanya maombi rasmi kwa shirika la umeme TANESCO kuunganisha umeme kwenye soko jipya. Ombi hili lilikubaliwa na kutekelezwa kwa wakati. Aidha, Halmashauri ilifanya maombi kwa DAWASCO kusaidia kupatikana kwa maji ya kutosha na ya uhakika. DAWASCO walisimika miundombinu ya maji na kuunganisha maji sehemu zote muhimu za soko. Wafanyabisahra walijenga vyoo vya kisasa kwa makubaliano ya Jenga-Endesha-Kabidhi (Build-Operate-Transfer agreements).

Ili kuhakikisha ubora na uendelevu, Halmashauri kupitia idara ya ujenzi ilitoa usaidizi wa kitaalamu kwa wafanyabiashara, wakandarasi na wadau wengine walioshiriki kwenye ujenzi wa miundombinu ya soko.

**5.0 RASILIMALI**

Jitihada hii kwa kiasi kubwa ni shirikishi; namna ya kufanya maamuzi na ukusanyaji wa wa rasilimali ulihusisha Halmashauri na wamiliki wa biashara. Ujenzi wa soko la Mnarani ulitumia rasilimali za aina mbalimbali. Rasilimali fedha ambazo zimebainishwa katika jedwali Na. 1 hapa chini zilitokana na michango ya wafanyabiashara. Kati ya TZS 3,056, 904, 941 Halmashauri ilichangia TZS 618,904,941 tu kiasi kilichobaki cha TZS 2,438,000,000 zilitokana na michango ya wafanyabiashara.

**Jedwali 1: Rasilimali fedha**

| Na | Kazi | Halmashauri | Wamiliki wa Biashara | Jumla |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Kusafisha eneo la ujenzi | 9,001,040 | | 9,001,040 |
| 2. | Ujenzi wa vizimba vya biashara ndogo ndogo | 189,014,260 | - | 189,014,260 |
| 3. | Vizimba vya kukusanya taka | 14,689,700 | | 14,689,700 |
| 4. | Ujenzi wa ghala za nafaka | 78,000,000 | 38,000,000 | 116,000,000 |
| 5. | Ujenzi wa eneo la migahawa ya vyakula | 88,609,699 | | 88,609,699 |
| 6. | Ujenzi wa mifereji ya maji | 88,641,600 | | 88,641,600 |
| 7. | Ujenzi wa stendi ya mabasi na barabara | 41,926,344 | | 41,926,344 |
| 8. | Ujenzi wa vyoo | 57,000,000 | | 57,000,000 |
| 9. | Ujenzi wa kituo/ nyumba ya kuhifadhi miundombinu ya sola | 7,022,298 | | 7,022,298 |
| 10. | Paneli za Sola | 19,000,000 | | 19,000,000 |
| 11 | Ujenzi wa vyumba vya maduka | - | 2,400,000,000 | |
| 12 | Kazi zingine za ujenzi | 26,000,000 | - | 26,000,000 |
| | Jumla ndogo | 618,904,941 | 2,438,000,000 | 3,056,904,941 |
| | **Jumla Kuu** | | | **3,056,904,941** |

Rasilimali watu inahusisha wadau mbalimbali walioshiriki katika hatua mbalimbali za kukamilisha mradi huu. Wadau hawa ni pamoja na Mkuu wa Mkoa, Mkuu wa Wilaya, Madiwani, Timu ya Menejimenti ya Halmashauri, Idara za Ujenzi, Biashara na maafisa masoko, Afisa Mtendaji wa Kata ya Tangini na Viongozi wa Umoja wa Wafanyabiashara Wadogo. Halmashauri ilitenga eneo la 4.44 ha, Kitalu Na. 158 cha biashara kwa ajili ya ujenzi wa soko na stendi ya magari.

## 6.0 MATOKEO

Jitihada hii imewezesha ujenzi wa soko la kisasa ambalo limekamilika na linafanya kazi. Soko lina sehemu za maduka 101 ya rejareja, Migahawa 10, maduka 23 ya nyama, maduka 18 ya jumla, sehemu 12 za kutolea huduma za shajala, ofisi 5, maduka 51 ya vifaa vya ujenzi, vyumba 5 vya ushonaji, vyumba 6 vya maduka ya vifaa vya umeme, maduka 7 ya dawa za binadamu, maduka 6 ya vyombo vya ndani, grosari 3, salon 5 na maduka 18 ya vifaa vya pikipiki. Eneo jingine ni vizimba vya matunda na mbogamboga ambavyo vinatoa ajira kwa wanawake na vijana.



*Eneo la kuuza bidhaa mchanganyiko na sehemu ya nafaka*



***Sehemu za huduma za chakula***

Ujenzi wa soko umesababisha kuongezeka kwa wafanyabiashara; kumekuwepo kwa ongezeko kubwa la wafanya biashara kutoka 400 mwaka 2016 hadi kufikia 800 mwaka 2017 hivyo kusababisha ongezeko la ajira. Kutokana na kuongezeka kwa wafanyabiashara, mapato ya Halmashauri yameongezeka kutoka TZS 25,000,000 mwaka 2016 kutoka soko la Maili moja hadi kufikia TZS 80,000,000 mwaka 2017 baada ya ujenzi wa soko la Mnarani.

Miundombinu ya soko ni ya kisasa na imeboresha utoaji wa huduma. Mbali na vizimba vilivyozoeleka, miundombinu ya soko inajumuisha maduka ya kisasa ya simu za mkononi, vifaa vya kieletroniki, huduma za fedha kwa njia ya simu na mashine za ATM. Soko limeunganishwa na barabara, mabasi madogo ya abiria (Daladala), stendi ya magari, vyoo vya kisasa, vizimba vya taka vya kisasa, mifumo ya kutiririsha maji wakati wa mvua, na miundombinu ya maji na umeme.




***Eneo la maduka na vizimba vya kukusanya taka***

**7.0 MIKAKATI YA UENDELEVU**

Halmashauri ya Mji wa Kibaha inatarajia kukamilisha soko na kulifanya la kuvutia watu wanaopita eneo hilo ili kuhamasisha umma kuongeza kasi ya kufika sokoni kununua na kuuza bidhaa. Ongezeko la mauzo litasababisha kuongezeka kwa ukusanyaji wa mapato. Mikakati mingine ya uendelevu ni pamoja na;

(i) Utoaji wa elimu kwa umma kuhusu matumizi sahihi ya soko na miundombinu mingine ili kuhakikisha shughuli za biashara zinafanyika kwa usafi unaozingatia misingi ya afya.
(ii) Kuendelea kutenga bajeti kila mwaka kwa ajili ya uendeshaji na ukarabati wa miundombnu ya soko ili kulifanya soko lidumu kwa muda mrefu.
(iii) Kushirikiana na Polisi katika kuanzisha Kituo cha Polisi katika eneo la karibu na soko na stendi ya magari ili kusimamia sheria na usalama wa umma na mali zao.

**8.0 SIRI YA MAFANIKIO**

Halmashauri ya Mji wa Kibaha ilifanikiwa kutekeleza jitihada hii kutokana na siri mbalimbali. Siri hizi ni pamoja na ushirikishwaji wa kina wa wadau mbalimbali kama wanasiasa, Timu ya Menejimenti ya

Halmashauri na wamiliki wa biashara. Ubunifu na utayari wa Mkurugenzi wa Mji na uthubutu wa kuanzisha kikosi kazi na kukipatia mamlaka ya kutosha kusimamia mradi wa soko ni siri nyingine ya mafanikio. Siri nyingine ni uwepo wa ardhi ya kutosha kwa ajili ya ujenzi wa soko ambapo Halmashauri haikuingia gharama za kufidia na vilevile ushirikiano imara baina ya wanasiasa, wataalam wa Halmashauri na wafanyabiashara.

# HALMASHAURI YA WILAYA YA KIBONDO

**USHIRIKI WA JAMII KATIKA USIMAMIZI WA SKIMU YA MAJI**




*Uzoefu wa kijiji cha Kumuhasha*

**1.0 UTANGULIZI**

Halmashauri ya Wilaya ya Kibondo inapatikana Kaskazini mwa Mkoa wa Kigoma kati ya Latitudo $3.9^0$ – $5.0^0$ Kusini na Longitudo $30.2^0$ –$31.50^0$ Mashariki katika mwinuko kati ya 500m - 1,600m juu ya usawa wa bahari. Halmashauri inapakana na H/W za Kakonko upande wa Kaskazini, Urambo (Mkoa wa Tabora) kwa upande wa Mashariki, Kasulu kwa upande wa Kusini na Jamhuri ya Burundi upande wa Magharibi. Kiutawala, Halmashauri imegawanyika katika Tarafa 3 ambazo ni Kibondo, Mabamba na Kifura, Kata 19, Vijiji 50 na Vitongoji 420. Kwa mujibu wa Sensa ya mwaka 2012, H/W ya Kibondo ilikuwa na idadi ya watu 261,331 kati yao wanaume ni 124,518 na wanawake ni 136,81. Wastani wa ongezeko la watu kwa mwaka ni 2.7%.

Kabila kuu ndani ya Halmashauri ni Waha ambao kiasili wanafahamika kama *Buha.* Waha wana asili ya wabantu ambao wanajishughulisha na kilimo kama shughuli kuu ya uzalishaji wa chakula na kipato. Kabila hili pia wanajishughulisha na ufugaji. Mifugo hutumika katika shughuli hasa sherehe za kimila ambazo huunganisha jamii. Historia inabainsha kwamba Waha walijihusisha na shughuli za ufuaji wa zana za chuma. Makabila mengine ndani ya Halmashauri ni Wanyamwezi, Wahaya, Wasukuma, Wajita, Wakurya na Wanyakyusa. Shughuli za kiuchumi ndani ya Halmashauri ni pamoja na Kilimo, Ufugaji, na Kilimo cha mbogamboga. Shughuli nyingine ni biashara, ajira katika sekta za umma viwanda vidogo na utengenezaji wa samani.

Kijiji cha Kumuhasha ambapo jitihada hii imetekelezwa ni moja kati ya vijiji 50 vya H/W ya Kibondo. Kijiji hiki kinapatikana Kata ya Murungu kwa upande wa Kaskazini mwa Halmashauri. Idadi ya watu katika Kijiji hiki ni 6,017 kati yao wanawake ni 3,030 na wanaume ni 2,987. Kijiji kina Vitongoji 10 ambavyo ni Nduta, Katazi, Kumuhasha, Chigazule, Ibohero, Nyamata, Mbugani, Kwisenga, Lukangalizo, na Migombani. Shughuli kuu za kiuchumi ndani ya Kijiji ni kilimo, ufugaji, ufugaji wa nyuki na uhifadhi wa misitu.

**2.0 TATIZO**

Maji safi na salama ni muhimu kwa maisha ya mwanadamu na ni muhimu katika kutatua changamoto za maendeleo ya kijamii na kiuchumi, umasikini na matatizo ya kiafya. Maji ni rasilimali asilia ambapo viumbe vyote hutegemea. Sera ya Maji ya mwaka 2002 inalenga kuhakikisha kwamba wanufaika wa maji wanashiriki kikamilifu katika kuendeleza vyanzo vya maji. Sera inatambua uhusiano wa kimsingi kati ya uwepo wa maji na maendeleo ya kijamii na kiuchumi pamoja na uhifadhi wa mazingira. Sera inasisitiza Kaya ziweze kupata maji safi na salama ndani ya 1km. Halikadhalika, Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 inazitaka Kaya ziweze kupata maji safi na salama ndani ya 400m hivyo kutumia muda mfupi usiozidi dakika 30 wakati wa utafutaji wa maji.

Kabla ya utekelezaji wa jitihada hii, upatikanaji wa maji safi na salama kwa kijiji cha Kumuhasha ulikuwa chini ya 28.7%. Ndani ya kijiji kulikuwa na chemchemu 4 katika bonde la Nyavyumbu na Chigazule. Chemchemu hizi hazikuwa za uhakika kutokana uharibifu wa mazingira katika vyanzo vya maji,na miundombinu ya maji ambayo ilijengwa miaka ya 1990 ilikuwa imeharibika hivyo kushindwa kutoa huduma ya uhakika. Miundombinu ya maji katika kijiji ilihusisha vituo 3 pekee vya kusambazia maji kwa idadi ya watu wapatao 6,017. Kutokana na sababu hii wananchi walilazimika kutembea umbali kati ya 2-4km na kutumia muda wa saa 4 hadi 5 kwa kutafuta maji. Wanawake na watoto walitumia muda mwingi kutafuta maji na kushindwa kujihusisha na shughuli za kimaendeleo kwa wanawake na kuhudhuria

masomo kwa watoto wa shule. Shule za Msingi za Kumuhasha na Nyavyubu walibainisha utoro wa wanafunzi kwa kiwango cha 16% kwa mwezi. Halikadhalika, taarifa za Zahanati ya Kumuhasha zilibainisha uwepo wa magonjwa yatokanayo na uchafuzi wa maji kabla ya utekelezaji wa jitihada hii ambapo magonjwa ya kuhara yalikithiri na wastani wa wagonjwa 26 kwa mwezi walitibiwa katika zahanati hiyo.

Migogoro ndani ya familia ilikithiri kutokana na wanawake kutumia muda mwingi wakati wa kutafuta maji. Kutokana na kutembea umbali mrefu ndani ya misitu ilisababisha uwepo wa hatari ya ubakaji kwa wanawake. Mwaka 2012, taarifa ya ubakaji iliripotiwa kwenye Ofisi ya Serikali ya Kijiji. Wauguzi katika Zahanati ya Kumuhasha mara nyingine walilazimika kusitisha kutoa huduma na kutumia muda huo kutafuta maji kwa ajili ya huduma za zahanati kama kusafisha vifaa tiba na usafi. Wakati mwingine, Wauguzi walilazimika kuwaomba ndugu wa mgonjwa kuchota maji kwa ajili ya kumhudumia mgonjwa wao.

**3.0 LENGO**

Upatikanaji wa maji safi na salama kwa ukaribu unatoa fursa ya kujihusisha na shughuli nyingine ambazo zina mchango katika maendeleo ya kijamii na kiuchumi. Kuimarika kwa huduma na upatikanaji wa maji safi na salama hupunguza kiwango cha magonjwa yatokanayo na maji hivyo kuimarisha afya na kuwafanya wananchi wajishughulishe na shughuli za uzalishaji.

Katika kufikia malengo hapo juu, jitihada hii ililenga kuimarisha upatikaji wa maji safi na salama. Malengo mahsusi ni pamoja na kufufua na kulinda vyanzo vya maji, kukarabati miundombinu ya zamani ya maji, kuihusisha jamii katika kusimamia vyanzo vya maji, kupunguza umbali wa kutafuta maji na kuondoa kabisa magonjwa yatokanayo na maji.

**4.0 MIKAKATI YA UTEKELEZAJI**

Sera ya Maji inahitaji ushiriki kamili wa jamii nufaika katika kupanga, kutekeleza na kusimamia miradi ya maji. Mwaka 2015, Serikali ya Kijiji iliitisha mkutano wa kujadili upungufu wa maji Kijijini na sababu zilizosababisha tatizo hilo. Uharibifu wa vyanzo vya maji na miundombinu chakavu ya maji vilibainishwa kama sababu za upungufu wa maji. Mkutano mkuu wa kijiji uliazimia kuchukua hatua za kuondoa tatizo. Mwaka 2016 mkutano wa pili wa kijiji ulipitisha mikakati ifuatayo katika kutatua tatizo la maji.

Kuandaa na kusimamia pendekezo la kukarabati na kupanua miundombinu ya maji; mwaka 2016, Serikali ya kijiji iliomba msaada kutoka OXFAM kusaidia katika ukarabati miundombinu ya maji. OXFAM ilikubali pendekezo hilo baada ya kuridhishwa na ushiriki wa jamii kikamilifu katika utekelezaji wa mradi. Jamii ilikubali kushiriki kuchimba mitaro ya kulaza bomba, kufukia mitaro na kutengeneza matofali ya ujenzi wa vituo vya kusambazia maji na kukusanya vitendea kazi vya asili kama mawe, kokoto na mchanga. OXFAM ilinunua vifaa vya ukarabati wa miundombinu na wataalamu kutoka Halmashauri walishiriki katika usimamizi wa ujenzi ambao ulianza mwezi Mei, 2017.

Uboreshaji wa miundombinu ya maji; fedha zilizopatikana kutoka OXFAM zilitumika kukarabati na kupanua miundombinu ya maji. Katika kutekeleza mradi huu, utafiti kuhusu sehemu ya kupitisha miundombinu ya maji na ilibainika kwamba baadhi ya nyumba zilipaswa kuondolewa. Nyumba 6 zilibomolewa na wamiliki wenyewe pasipo kudai fidia. Jamii ilishiriki katika kuchimba mitaro na kulaza mabomba chini ya usimamizi wa wataalamu wa Halmashauri.

Kuzuia undeshaji wa shughuli za kibinadamu karibu na vyanzo vya maji; mkutano mkuu wa kijiji uliazimia kuzuia shughuli za kibinadamu kama kutengeneza tofali za kuchoma, kulima, kukata miti na kuchoma mkaa katika maeneo ya kuzunguka vyanzo vya maji. Picha ifuatayo inaonesha shughuli za kibinadamu katika maeneo ya vyanzo vya maji.



***Utengenezaji wa tofali katika maeneo ya chanzo cha maji***

Kuhuisha maeneo ya vyanzo vya maji; jamii iliazimia kwamba vyanzo vyote vya maji vilindwe dhidi ya moto kwa kuanzisha mapalia ya moto na kupanda miti ya kuhifadhi mazingira katika maeneo yaliyoharibiwa. Mwaka 2017, jumla ya miti 930 ambayo ni rafiki kwa mazingira (Mirumba, Migoti na Mikuyu) ilipandwa katika vyanzo viwili vya Chigazule (700) na Katazi (230)na 8km za palia ya kuzuia moto zilianzishwa kuzunguka vyanzo vya maji na misitu.

Kuanzishwa kwa Jumiya ya Watumia maji (COWSO); ili kusimamia na kulinda mradi wa maji, Jumuiya ya watumia maji ilianzishwa Januari 2017, ikiwa na wajumbe 12 (wanaume 6 na wanawake 6) na mafundi wa bomba 2. Halmashauri ya Kijiji ilipeleka maombi kwa H/W ya Kibondo kuwapatia mafunzo wajumbe wa COWSO kuhusu uendeshaji na usimamizi wa skimu za maji. Kufikia Februari 2017, Mhandisi wa Maji na Afisa Maendeleo ya Jamii waliendesha mafunzo hayo. Picha ifuatayo inaonesha wajumbe wa Jumuiya ya watumia maji wa Kijiji cha Kumuhasha.



***Wajumbe wa Jumuiya ya Watumia Maji ya Kumuhasha***

Kuundwa Katiba ya Jumuiya ya watumia maji; mwaka 2017, Jumuiya iliunda katiba inayosimamia maji na kutunza vyanzo vya maji ili mradi uwe endelevu. Katiba inabainisha hatua za kuchukuliwa dhidi ya mtu atakayekiuka taratibu zilizowekwa za kulinda vyanzo vya maji. Sehemu C ya katiba inafafanua adhabu kwa atakayeharibu vyanzo vya maji kama ifuatavyo; kuharibu miundombinu ya maji adhabu yake ni TZS 30,000 na/ au kifungo cha miezi sita jela, kufua nguo katika eneo la kuzunguka chanzo cha maji adhabu yake ni TZS 5,000 na/ au kifungo cha miezi 6 jela na kuendesha shughuli za kibinadamu kama kufyatua tofali na kilimo katika maeneo ya chanzo cha maji adhabu yake ni TZS 30,000 na/ au kifungo cha miezi 6

jela. Katiba vilevile inaanzisha michango kutoka kwa jamii kwa ajili ya kukusanya fedha za kukarabati miundombinu. Kila Kaya inachangia TZS 500 kwa mwezi kama gharama za maji na kwa kaya ambazo wameunganishiwa maji binafsi wanalipia TZS 2,000 kwa mwezi.

**5.0 RASILIMALI**

Utekelezaji wa jitihada hii ya Kijiji cha Kumuhasha ulitumia rasilimali zifuatazo;

(i) Rasilimali fedha; Mradi ulitumia TZS 186,236,610 kununua vifaa vya bomba na ujenzi
(ii) Rasilimali watu; OXFAM na Halmashauri walitoa wataalamu kusimamia utekelezaji wa mradi na kuhakikisha ubora.
(iii) Nguvu Kazi; Jamii ilijitoa kwa kuchangia nguvu kazi katika kuchimba, kulaza mabomba na kufukia mitaro pamoja na kukusanya vifaa vya ujenzi kama mawe, kokoto na mchanga.

**6.0 MATOKEO**

Wakazi wa Kijiji cha Kumuhasha wanapata maji safi na salama ndani ya 400m kama ilivyo matakwa ya Sera ya Taifa ya Maji. Mradi una vituo pacha vya usambazaji wa maji 31 mbali na vituo ambavyo vimewekwa katika maeneo ya shule. Muda mwingi ambao ulitumiwa na wanawake na watoto katika kutafuta maji sasa unatumika katika kutekeleza shughuli za kimaendeleo. Hii ilithibitishwa na Angelista Richard ambaye alisema maneno yafuatayo "*tulikuwa tunaamka mapema alfajiri muda wa saa 12 asubuhi kwa ajili ya kuchota maji… tulitumia muda wa saa 5 hadi 6… tulitumia muda mwingi ambao tungeweza kutumia katika shughuli za shambani… siku hizi tunatumia dakika kumi tu kupata maji na kurejea nyumbani….. na kujishughulisha na shughuli nyingine za kimaendeleo."* Shule za Msingi na Sekondari zimenufaika kutokana na mradi huu wa maji. Katika shule ya msingi Kumuhasha ambayo ina wanafunzi 511 kuna kituo kimoja cha kusambazia maji na katika Shule ya Sekondari ya Murungu (bweni) ina vituo 4 vya kusambazia maji. Hali hii imesaidia kupunguza utoro shuleni kutoka 16% hadi 7% kwa mwezi.



***Mama akifurahia kupata maji jirani na shule***

Upatikanaji wa maji katika kijiji cha Kumuhasha umeongezeka kutoka 29% hadi 100% hivyo kufanya wakazi wanaotumia maji safi na salama kuongezeka. Kutokana na upatikanaji wa maji safi na salama, magonjwa yatokanayo na maji kama kuhara yamepungua kutoka 26 hadi 13 kwa mwezi. Uwepo wa maji umechochea kasi ya ujenzi wa nyumba bora za matofali kutokana na urahisi wa kutengeneza tofali katika eneo la ujenzi.



*Ujenzi wa nyumba ya matofali (kushoto) na nyumba ya matofali iliyokamilika (kulia)*

Usafi katika maeneo ya shule za Msingi za Nyavyumbu na Kumuhasha, Shule ya Sekondari ya Murungu na Zahanati ya Kumuhasha umeboreshwa. Kabla ya utekelezaji wa jitihada hii, usafi katika maeneo ya Shule ulifanyika mara moja kwa wiki lakini kutokana na uwepo wa maji usafi wa jumla hufanyika kila siku. Shule na baadhi ya wakazi wameboresha mazingira kwa kuanzisha bustani za maua na mbogamboga na humwagilia kutokana na maji ya mradi. Maeneo ya shule yanapendeza kwa kupambwa na maua mazuri.



*Bustani za mbogamboga katika kijiji cha Kumuhasha*

Kuanzishwa kwa vitalu vya miti kwa madhumuni mbalimbali; wanakijiji wameanzisha vitalu vya miti kwa lengo la kuboresha misitu na kujiimarisha kiuchumi. Kwa mfano, Kikundi cha Nyamata kinajihusisha na uzalishaji wa miche ya miti kwa lengo la kuuza.



*Kitalu cha Miti katika Kijiji cha Kumuhasha*

Jitihada za jamii katika kuhifadhi mazingira zimeongezeka; ufahamu wa jamii kuhusu uhifadhi wa mazingira umeimarika kutokana na kutekeleza matakwa ya Katiba ya Jumuiya ya Watumia Maji ambayo inakataza kuendesha shughuli za kibinadamu katika vyanzo vya maji.  Urejesho wa mimea ya asili katika vyanzo vya maji umeongezeka.



***Uoto wa asili katika chanzo cha maji***

Kijiji cha Kumuhasha kimehifadhi chemchem 3 za maji na kimejenga tangi la kuhifadhi maji la lita 90,000 ambalo linasambaza maji katika maeneo ya makazi, shule na zahanati.




***Tangi la maji***



***Kituo cha Maji***

Uwepo wa Jumuiya imara ya watumia maji; Jumuiya hii ina kamati imara za kusimamia usambazaji wa maji, kuunganisha na kukarabati miundombinu ya maji, kusimamia sheria za kuhifadhi vyanzo vya maji, miundombinu na kukusanya ada kutoka kwa watumia maji.




***Majina ya Wajumbe wa Kamati za Jumuiya ya Watumia Maji***

**7.0 MIKAKATI YA UENDELEVU**

Ili kuhakikisha jitihada hii inakuwa endelevu, jamii iliamua kukusanya fedha kwa ajili ya matengenezo ya miundombinu ya mara kwa mara. Kila Kaya huchangia TZS 500 kwa mwezi na Kaya ambazo zimeunganishiwa maji moja kwa moja zinalipa TZS 2000 kwa mwezi. Fedha hizo huhifadhiwa kwenye akaunti ya benki. Jumuiya ina katiba ya kusimamia uendeshaji wa mradi wa maji. Wajumbe wa Kamati

ya COWSO wamepatiwa mafunzo kuhusu uhifadhi wa mazingira, matumizi bora ya ardhi na utunzaji wa misitu. Dhana ya umiliki wa mradi kwa jamii imeimarika hivyo kuthibitisha uendelevu.

**8.0 SIRI YA MAFANIKIO**

Mafanikio ya jitihada hii yalitokana na uthubutu wa viongozi wa kijiji katika kuwaunganisha wanakijiji kubaini tatizo na ufumbuzi wa changamoto hizo. Vilevile, jitihada hii ilitokana na hitaji la jamii. Mradi wa maji ulikuwa ni hitaji halisi la jamii hivyo jamii ilikuwa tayari kushiriki katika hatua zote za utekelezaji wa mradi. Sababu nyingine ni utayari wa H/W ya Kibondo na OXFAM kusaidia jitihada za jamii, uwepo wa jumuiya imara ya watumia maji na uwepo wa vyanzo vya uhakika vya maji.

# HALMASHAURI YA WILAYA YA MAFIA


**USHIRIKI WA JAMII KATIKA UJENZI NA USIMAMIZI WA SKIMU YA MAJI**



***Uzoefu wa H/W ya Mafia***

**1.0 UTANGULIZI**

Halmashauri ya Wilaya ya Mafia ni moja kati ya Halmashauri 9 za Mkoa wa Pwani. Kijiografia, H/W ya Mafia ni kisiwa ndani ya bahari ya Hindi kinachoundwa na visiwa vidogo 7 ambavyo ni Jibondo, Chole, Juani, Bwejuu, Mbarakuni, Shungimbili na Nyororo. Hata hivyo visiwa vya Shungimbili na Nyororo hutumika tu kwa shughuli za uvuvi hivyo hakuna makazi ya kudumu. Halmashauri inapatikana upande wa Kusini Mashariki mwa Mkoa wa Pwani na inapakana na H/W ya Mkuranga upande wa Kaskazini Magharibi, H/W za Kibiti na Kilwa upande wa Kusini Magharibi na Bahari ya Hindi upande wa Mashariki na Kusini Mashariki. H/W ya Mafia ina eneo la 972km$^2$ ambapo 407km$^2$ ni ardhi kavu na 565km$^2$ ni sehemu ya bahari ya Hindi. Kwa mujibu wa sensa ya mwaka 2012, Halmashauri ina watu 46,438 kati yao wanawake 23,484 na wanaume 22,954. Wastani wa ongezeko la watu ni 1.5% na wastani wa watu katika kaya ni 4. Kiutawala Halmashauri ina Tarafa 2 (Tarafa ya Kaskazini na Tarafa ya Kusini), Kata 8(Kanga, Kirongwe, Baleni, Kilindoni, Kiegeani, Miburani, Ndagoni na Jibondo), vijiji 23 na Vitongoji 136.




***Ramani ya H/W ya Mafia***

Hali ya hewa ya Kisiwa cha Mafia ni ya kitropiki, wastani wa joto ni 26.7°C na wastani wa mvua ni 1,705mm. Kuna kipindi kimoja cha mvua ambazo hunyesha kati ya mwezi Machi na Mei na kipindi cha kiangazi kati ya mwezi Julai na Oktoba. Shughuli za kiuchumi ni pamoja na uvuvi, kilimo cha kujikimu na biashara ndogo ndogo. Kisiwa pia huvutia utalii hasa katika fukwe na kufanya michezo ya uvuvi.

Japokuwa Mafia imezungukwa na maji chumvi ya bahari, 74.2% ya wakazi wanapata maji safi na salama ndani ya 400m kama ilivyo hitaji la Sera ya Taifa ya Maji. Vyanzo vya maji ni pamoja na chemchem 1, mifumo 40 ya kuvuna maji ya mvua, visima virefu 58 vinavyotumia pampu za umeme, na visima vya kawaida 153 vinavyotumia pamu za mkono. Kiwango hiki cha usambazaji wa maji kimefikiwa baada ya kukamilisha miradi 7 ya maji iliyotekelezwa chini ya Mradi wa Maendeleo ya Sekta ya Maji ndani ya vijiji 9. Jitihada hii ya ushiriki wa jamii katika kujenga na kusimamia miradi ya maji ilitekelezwa katika vijiji vya Juani na Chole.

Vijiji vya Juani na Chole ni moja kati ya vijiji vinavyounda Kata ya Jibondo. Kijiografia vijiji hivi ni visiwa vilivyojitenga. Vijiji vya Juani na Chole vinapakana na Kitongoji cha Utende ambacho kipo kijiji cha Kiegeani katika kisiwa kikuu. Vijiji hivi kwa pamoja vina Vitongoji 7; Vitongoji 4 Juani na 3 Chole. Kwa mujibu wa sensa ya 2012 vijiji hivi vina idadi ya watu 1,920. Shughuli za kiuchumi ni pamoja na uvuvi, kilimo cha mwani, muhogo na minazi.

**2.0 TATIZO**

Maji ni moja ya rasilimali muhimu ambayo inagusa nyanja zote za maisha ya mwanadamu kuanzia matumizi ya nyumbani, kilimo, na maendeleo ya viwanda, mila na tamaduni za jamii. Vijiji vya Juani na Chole havikuwa na maji safi na salama tangu kuanzishwa kwake kutokana na kutokuwepo kwa vyanzo vya maji na miundombinu ya maji katika vijiji hivyo.

Wananchi wa Vijiji vya Juani na Chole walikuwa wakitegemea maji ya mvua katika msimu wa mvua na kipindi cha kiangazi iliwalazimu kufuata maji katika kitongoji cha Utende kilichopo kisiwa kingine. Wananchi walitumia mitumbwi na ngalawa kuvuka eneo la bahari umbali wa 3km kwa wakazi wa Juani na 7km kwa wakazi wa Chole. Wakazi ambao hawakuweza kufuata maji katika umbali huo walilazimika kununua maji kwa bei kubwa ya kati ya TZS 500 na TZS 1000 kwa ujazo wa lita 20. Kutokana na kukosekana kwa maji safi na salama katika vijiji hivyo, iliwalazimu wananchi kutumia muda mwingi kufuata maji hivyo kushindwa kujishughulisha na shughuli nyingine za kiuchumi. Baadhi ya wananchi walitumia maji kutoka kwenye visima vifupi ambavyo maji yake hayana ubora kwa matumizi. Hii ilsababisha wananchi kupata magonjwa yatokanayo na maji machafu kama kuhara na homa ya matumbo. Picha zifuatazo zinaonesha baadhi ya visima vifupi na maji machafu katika Kijiji cha Chole.



*Maji machafu katika visima vifupi kijiji cha Chole*

**3.0 LENGO**

Lengo kuu la jitihada hii lilikuwa kuwezesha jamii kupata maji safi na salama ya kutosha katika vijiji vyao. Malengo mahususi ya jitihada hii ni pamoja na kupunguza umbali na muda wa kutafuta maji kutoka kijiji kingine,kuondoa magonjwa yatokanayo na maji machafu, kupunguza gharama za maji kutoka TZS 500 -

TZS1000 kwa lita 20 hadi TZS 100 kwa Lita 20 na kupunguza hatari ya kusafiri ndani ya bahari kwa mitumbwi na ngalawa wakati wa kufuata maji kijiji cha jirani.

**4.0 MIKAKATI YA UTEKELEZAJI**.
Baada ya kubaini uhitaji wa maji, wananchi kutoka Vijiji vya Juani na Chole walionesha uhitaji wa maji wakati wa mchakato wa kupanga bajeti ya mwaka 2014/2015. Kutokana na uwezeshwaji wa mpango wa Fursa na Vikwazo kwa Maendeleo (O&OD) uhitaji wa maji ulianinishwa kama hitaji la kwanza la vijiji hivyo. Vijiji hivi vilitumia fursa ya Mpango wa Maendeleo ya Sekta ya Maji (WSDP) ambao unafadhiliwa na Benki ya Dunia kutekeleza jitihada hii. H/W ilikubali kushirikiana na wananchi katika utekelezaji wa jitihada hii na walitekeleza mikakati ifuatayo.

Kujenga uelewa; mbinu hii ilitumika kuwaunganisha wananchi na kujenga uelewa wa pamoja juu ya namna ya kushirikiana na Serikali katika kutekeleza mradi huu. Kikosi Kazi kilichoundwa na wajumbe kutoka Benki ya Dunia na Halmashauri walifanya mikutano ya kujenga uelewa wa jamii kwa kufafanua majukumu ya jamii katika kutekeleza mradi, namna ya kuunda kamati za kusimamia mradi na kuhamasisha uchangiaji wa rasilimali za kutekeleza mradi.

Mikutano ya uhamasishaji; Afisa Maendeleo ya Jamii na Mhandisi wa Maji waliendesha mikutano katika vijiji vya Juani na Chole kuhamasisha jamii kushiriki katika kutekeleza mradi kwa kuchangia rasilimali na kushiriki katika kazi za ujenzi wa miundombinu ya maji. Baada ya kufanyika kwa uhamasishaji ilikubalika kwamba jamii ichangie 2.5% ya gharama za mradi. Kila Kaya ilipaswa kuchangia TZS 60,000 ili kufikia kiwango cha TZS 23,757,075 ambayo ndio 2.5% ya gharama za mradi. Ili kurahisisha ukusanyaji wa michango kutoka kwa wananchi, kamati ya muda iliundwa kuratibu shughuli zote za ukusanyaji wa michango hiyo. Halmashauri za Vijiji ziliamua kutoa usaidizi kwa baadhi ya Kaya ambazo hazikuwa na uwezo wa kuchangia kiasi cha TZS 60,000 kwa kuwasaidia kiasi cha TZS 55,000 hivyo Kaya masikini zilichangia kiasi cha TZS 5,000. Fedha za Halmashauri za Vijiji zilitokana na mapato ya ndani ya vijiji husika kutokana na ushuru wa shughuli za uvuvi.

Ununuzi wa ardhi kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya maji; Vijiji hivi vilinunua ardhi yenye eneo la 2,178$m^2$ katika kijiji cha Utende ambapo ndipo miundombinu ya maji (Kisima kirefu,Tangi la maji na Nyumba ya mashine ya kusukuma maji) imejengwa. Gharama ya ununuzi wa eneo hilo ni TZS 4,060,000 ambazo zilichangwa na vijiji vyote viwili kwa uwiano sawa. Sababu za kununua ardhi katika kijiji cha Utende ni kutokana na kutokuwepo kwa chanzo cha maji safi na salama katika vijiji vya Chole na Juani.

Kutafuta fedha kutoka Serikali Kuu; mradi huu umetekelezwa kupitia Mpango wa Maendeleo ya Sekta ya Maji (WSDP). Halmashauri ilifanya ufuatiliaji wa karibu katika Wizara ya Maji kupata fedha za mradi kiasi cha TZS 950,283,000 kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya maji ikiwa ni pamoja na kuchimba kisima, kulaza mabomba na kujenga vituo vya usambazaji wa maji. Jamii ilishiriki kwenye utekelezaji wa shughuli za mradi zilizohitaji nguvu kazi ili kuchochea kasi ya utekelezaji wa mradi pamoja na kujipatia kipato kutokana na malipo ya kazi wanazofanya. Kazi zilizotekelezwa na wananchi ni pamoja na kuchimba mitaro, kufyatua matofali, ujenzi wa tangi la maji, ujenzi wa nyumba ya kuhifadhi pampu ya kusukuma maji, na usimikaji wa mabomba. Wakati wa utekelezaji wa jitihada hii, Halmashauri ilihusika katika usimamizi wa hatua zote za utekelezaji wa mradi ili kuhakikisha ubora wa mradi. Picha zifuatazo zinaonesha wananchi wakishiriki kuchimba mitaro na kulaza mabomba yanayokatisha eneo la bahari.



***Uchimbaji wa mitaro na kulaza mabomba kwa kukatiza eneo la bahari***

Ununuzi wa vifaa vya ujenzi; ununuzi wa vifaa vya ujenzi kama saruji, mabomba na vifaa vya kuunganisha maji vilinunuliwa Dar es Salaam na Kokoto zilinunuliwa Lugoba H/W ya Chalinze. Halmashauri iliamua kununua vifaa hivi nje ya Mafia kutokana na unafuu wa bei kuliko gharama za vifaa husika ndani ya kisiwa cha Mafia.

Kutoa mafunzo kwa wapiga mbizi; Wananchi walioshiriki katika kusimika bomba katika eneo la bahari kutoka Utende hadi vijiji vya Juani na Chole walipatiwa mafunzo ya namna ya kusimika mabomba hayo. Kutokana na kwamba vijiji hivi vimetenganishwa na eneo la bahari ililazimu mabomba kusimikwa katika kina cha bahari. Zoezi la usimikaji wa bomba lilikuwa gumu hivyo lilihitaji watu wenye nguvu na uzoefu wa kupiga mbizi ndani ya kina kirefu cha maji. Jumla ya wapiga mbizi 26 walitambuliwa na kupatiwa mafunzo na mkandarasi juu ya namna ya kusimika na kuunganisha mabomba wakiwa ndani ya maji.

Uundaji wa Jumuiya ya Watumia Maji na Katiba; jumuiya ya watumia maji (COWSO) ambayo inajulikana kama Jumuiya ya watumia maji Juani na Chole iliundwa kusimamia mradi wa maji. Jumuiya hii inawajibika kukusanya ada za maji, na kufanya matengenezo ya miundombinu ya maji. Vilevile, Katiba iliundwa kusimamia uendeshaji wa mradi na kuhakikisha mradi unakuwa endelevu. Mwaka 2014, COWSO ilianzisha kamati ya wajumbe 7 (wajumbe 4 Kijiji cha Juani na wajumbe 3 Kijiji cha Chole). Majukumu ya Kamati hii ni kusimamia, kufanya ufuatiliaji na kukusanya ada za mwezi kutoka kwenye Kaya.

Kufungua akaunti ya benki; Kamati ilianzisha akaunti ya benki yenye namba 21510004865 na jina la *JUMUIYA YA MAJI JUANI NA CHOLE* katika Benki ya NMB tawi la Mafia. Hadi kufikia Januari 6, 2018 akaunti ilikuwa na kiasi cha TZS 22,147,789.6 zilizotokana na makusanyo ya ada za maji. Fedha hizi zinatumika kulipa mishahara za wasimamizi na wauzaji wa maji katika vituo vya usambazaji (DPs) na matengenezo ya miundombinu pale inapohitajika.

## 5.0 RASILIMALI

Ujenzi wa mradi wa maji wa Vijiji vya Juani na Chole ulitumia rasilimali mbalimbali. Rasilimali fedha zipatazo TZS 978,100,075 kama zinavyooneshwa kwenye jedwali Na 1 zilitumika.

**Jedwali 1: Rasilimali Fedha**

| S/n | Chanzo cha fedha | Kiasi (TZS) |
|---|---|---|
| **1.** | Wizara ya Maji | 950,283,000 |
| **2.** | Wananchi wa Juani na Chole | 23,757,075 |
| **3.** | Vijiji vya Chole na Juani kununua ardhi | 4,060,000 |
| | **JUMLA** | **978,100,075** |

Rasilimali watu; Viongozi wa Vijiji waliziunganisha jamii, na jamii ilishiriki katika utekelezaji wa mradi kwa kuchimba mitaro, kufyatua matofali, kujenga tangi la maji, kujenga nyumba ya kuhifadhi mashine ya kusukuma maji na kusimika bomba ndani ya bahari. Wataalamu wa Halmashauri walisimamia mchakato wa utekelezaji. Rasilimali nyingine ni ardhi na vitendea kazi vilivyotumika.

**6.0MATOKEO**

Utekelezaji wa Mradi huu hadi kukamilika umeleta matokeo mbalimbali. Kwanza uwepo wa miundombinu ya maji kama tangi la maji, nyumba ya kuhifadhia mashine ya kusukuma maji bomba za maji na vituo vya kutolea huduma ya maji ni tokeo moja wapo. Vitongoji vyote vya kijiji cha Chole (Mwapepo, Kilimani and Mnyonge) na Vitongoji vyote vya kijiji cha Juani (Manda, Vikomba, Juani mjini na Juani Shule) vimeunganishwa na maji. Uwepo wa maji safi na salama umepunguza kwa kiasi kikubwa magonjwa yatokanayo na maji. Picha zifuatazo ni baadhi ya miundombinu iliyojengwa.



***Tangi la maji, Nyumba ya mashine ya kusukuma maji na kituo cha maji***

Muda uliotumika wakati wa kuteka maji na umbali kuyafikia maji umepungua kwa kiasi kikubwa; Wananchi wanapata maji ndani ya 400m ikilinganishwa na 3km-7km kabla ya utekelezji wa mradi huu. Wananchi wanapata muda wa kujihusisha na shughuli nyingine za uchumi kama kilimo na uvuvi, kuhudhuria mikutano ya vijiji na kushiriki kwenye kazi za jamii kama ujenzi wa miundombinu ya shule na zahanati. Vile vile, kukamilika kwa mradi wa maji wa vijiji vya Juani na Chole kumepunguza gharama za maji kutoka TZS 500 – 1000 kwa lita 20 hadi TZS 100 kwa lita 20. Upatikanaji wa maji umechangia kupunguza ukali wa maisha.

Hoteli za Kitalii za Chole na Juani zimeunganishiwa maji safi na salama hivyo kuchochea kuongezeka kwa idadi ya watalii katika vijiji hivyo ukilinganisha na hali ilivyokuwa kabla ya utekelezaji wa mradi wa maji.Kuongezeka kwa utalii kuna mchango mkubwa kwenye uchumi wa vijiji hivyo kutokana na uhalisia kwamba wananchi wanapata fursa ya kuuza bidhaa zao kama urembo na mapambo yaliyotengenezwa kiasili na mapambo kutoka mabaki ya viumbe wa baharini.

Fursa za ajira zimeongezeka; wakati wa utekelezaji wa mradi wananchi walipata ajira za muda katika kazi za ujenzi wa miundombinu, kuchimba mitaro na kulaza mabomba. Baada ya kukamilika kwa mradi watu 10 kutoka kwenye vijiji husika wamepata ajira. Watu hawa ni Afisa wa matengenezo ya bomba, wasaidizi

wa fundi (2) na wauzaji wa maji (7) wafanyakazi hawa wanalipwa jumla ya TZS 520,000 kwa mwezi, Wananchi pia waliamua kumlipa katibu wa kamati na mhasibu mshahara wa TZS 100,000 kwa mwezi kila mmoja.

Uwepo wa Jumuiya ya watumia maji imara; COWSO ina kamati tendaji, katibu na mhasibu na akaunti ya kutunza fedha. Kamati tendaji imeongeza idadi ya wajumbe wa jumuiya ya watumia maji kwa kuwaunganisha na huduma za maji. Aidha, kamati ina jukumu la kukusanya ada ya mwezi kutoka kwa wateja; Akaunti ina jumla ya TZS 23,757,075 hadi kufikia Januari, 2018. Kamati inafanya ukarabati wa miundombinu panapotokea uharibifu.

**7.0 MIKAKATI YA UENDELEVU**

Jumuiya ya watumia maji na Halmashauri wamejizatiti kuhakikisha matokeo ya jitihada hii yanakuwa endelevu. Ili kuhakikisha uendelevu wa jitihada hii, mikakati ifuatayo imezingatiwa.

(i) Kuendelea kuimarisha na kutekeleza sheria ndogo zilizoanzishwa kusimamia mradi wa maji katika vijiji vya Juani na Chole. Sheria hizi zinabainisha majukumu ya jamii katika kusimamia miundombinu ya mradi na zinataja adhabu dhidi ya wahalifu wa miundombinu ya mradi.

(ii) Uwepo wa Kamati ya Watumia Maji; vijiji viliunda kamati imara ya watumia maji ambayo inashughulika na usimamizi wa skimu ya maji. Kamati hii hufanya ukaguzi wa mara kwa mara wa miundombinu ya maji na inapobaini uharibifu huchukua hatua ya kufanya matengenezo na kuhakikisha huduma ya maji inakuwepo wakati wote na miundombinu ipo katika ubora.

(iii) Kuanzishwa kwa ada ya watumia maji; ili kuhakikisha uendelevu wa huduma ya maji, ilikubaliwa kwamba huduma ya maji itatolewa kwa malipo ya TZS 100 kwa lita 20, fedha ambazo zitatumika katika matengenezo ya miundombinu pale itakapolazimu.

(iv) Kuendelea kupanua wigo wa huduma ya maji; kamati ya maji inaendelea kuongeza huduma ya maji kwa kuendelea kujenga vituo vya usambazaji (DPs). Upanuzi huu umefanyika katika taasisi kama shule, zahanati, wawekezaji na kaya binafsi. Lengo la upanuzi ni kusogeza huduma kwa watumiaji na kuongeza mapato ya COWSO.

**8.0 SIRI YA MAFANIKIO**

Kufanikiwa kwa jitihada hii kumetokana na utayari wa jamii kushiriki katika kupanga, kutekeleza na kusimamia mradi huu. Jamii ilibainisha kwamba, hitaji lao kuu lilikuwa ni maji hivyo kila mwanajamii alikuwa tayari kuhamasisha utekelezwaji wa jitihada hii. Uwepo wa uongozi wa vijiji wenye maono na ushawishi pamoja na wataalamu kutoka Halmashauri uliweza kuunganisha jamii na kuwajengea uelewa kuhusu utekelezaji wa jitihada hii. Sababu nyingine ni matumizi bora ya rasilimali kutoka Serikali Kuu na uwepo wa COWSO na Kamati ya Watumia Maji.

# HALMASHAURI YA WILAYA YA KALIUA

**UHIFADHI WA MAZINGIRA KWA MAENDELEO ENDELEVU**



***Uzoefu wa H/W ya Kaliua***

**1.0 UTANGULIZI**

Halmashauri ya Wilaya ya Kaliua ni moja kati ya Halmashauri 8 za Mkoa wa Tabora na inapatikana umbali wa 125km kutoka makao makuu ya mkoa wa Tabora. Halmashauri inapakana na H/W za Urambo na Tabora upande wa Mashariki, Uvinza na Kibondo (Mkoa wa Kigoma) upande wa Magharibi, Mpanda na Mlele (Mkoa wa Katavi) upande wa Kusini, Ushetu (Mkoa wa Shinyanga) na Bukombe (Mkoa wa Geita) upande wa Kaskazini. Kwa mujibu wa Sensa ya mwaka 2012, Halmashauri ina watu 393,358; wanaume 196,369 na wanawake 196,989.

Kiutawala, H/W ya Kaliua imegawanyika katika Tarafa 2, Kata 28 na Vijiji 101. Halmashauri ina eneo la 14,050km$^2$ ambapo 11% ya ardhi inatumika kwa shughuli za uzalishaji wa mazao na 89% ni hifadhi ya misitu. Shughuli kuu za kiuchumi ni pamoja na kilimo, ufugaji, ufugaji nyuki, uchimbaji wa madini na biashara ndogo na za kati za mazao ya kilimo na maliasili. Mazao makuu yanayolimwa ni tumbaku, mahindi, muhogo, mtama, karanga, pamba, viazi vitamu na alizeti.

**2.0 TATIZO**

H/W ya Kaliua na Mkoa wa Tabora kwa ujumla, kwa kipindi kirefu ilikuwa na misitu mikubwa. Hata hivyo katika miongo ya hivi karibuni hali ya misitu imebadilika kwa kasi kubwa kutokana na shughuli za kibinadamu kama kuchoma mkaa, uchomaji wa misitu, kilimo cha kuhamahama, ukataji wa magogo na miti kwa ajili ya kukaushia tumbaku na ongezeko la mifugo. Pamoja na shughuli zote hizi, takwimu zinaonesha uharibifu wa misitu kwa H/W ya Kaliua kwa 80% umetokana na ukaushaji wa tumbaku ambao unahitaji kuni nyingi. Takwimu zinaonesha kwamba 60% ya wakazi wa H/W ya Kaliua wanajishughulisha na kilimo cha tumbaku kinachohitaji ardhi yenye rutuba na kuni kwa ajili ya kukausha majani ya tumbaku. Mahitaji ya kilimo hiki yamechochea uharibifu wa misitu ndani ya Halmashauri na Mkoa kwa ujumla. Picha ifuatayo inaonesha hali halisi ya ukataji wa miti kwa ajili ya ukaushaji wa tumbaku na kuacha ardhi bila miti.



***Ukataji wa miti na uharibifu wa mazingira***

Matokeo ya ukataji miti katika Halmashauri ni mengi na dhahiri. Athari hizi zimejikitita katika uharibifu wa rasilimali za mazingira (misitu, ardhi, maji na mazao ya kilimo), mabadiliko ya hali ya hewa na athari kwa maisha ya viumbe hai. Kiwango cha mvua kimekuwa kikipungua mara kwa mara. Endapo hatua za kutatua changamoto hii hazitachukuliwa zitasababisha Mkoa wa Tabora kubadilika na kuwa jangwa. Katika miaka ya 1980 kiwango cha mvua kilikuwa ni zaidi ya 1800mm kwa mwaka, hata hivyo takwimu za miaka ya karibuni zinabainisha kupungua kwa kiwango cha mvua chini ya 1000mm kwa mwaka. Athari hizi ni za wazi na wakazi wa Kaliua wanakiri kwamba mabadiliko haya yametokana na shughuli za kibinadamu hivyo kuwafanya kuwa tayari kushiriki pamoja katika kutatua changamoto hizi.

Tatizo la ukataji miti katika H/W ya Kaliua liliendelea hadi mwaka 1997 kipindi ambacho Halmashauri ilianza kuchukua hatua za kutatua tatizo hili kwa kuanzisha mbinu ya "Utunzaji Misitu Shirikishi" (PFM); Mbinu hii ililenga kuiamsha jamii itambue kwamba athari zinazotokana na ukataji miti ovyo zimesababishwa na jamii yenyewe na hivyo utatuzi wa tatizo hilo ni jukumu la pamoja la jamii.

**3.0 LENGO**

Uanzishwaji wa jitihada ya Utunzaji wa Misitu Shirikishi kwa ujumla ulilenga kulinda na kuimarisha rasilimali za misitu ambazo zimekuwa hatarini kutoweka kwa muda mrefu. Mahsusi, jitihada hii ililenga kufanikisha yafuatayo;

(a) Kubadilisha mtazamo wa watu na vitendo vinavyochochea uharibifu wa mazingira na kuwafanya wawe rafiki wa mazingira na kuyatunza.
(b) Kuongeza idadi ya miti katika maeneo ya makazi, mazingira ya taasisi na katika maeneo ya mashamba.
(c) Kuhamasisha mashirika yanayojihusisha na ununuzi wa tumbaku kujihusisha na kampeni za uhifadhi wa mazingira.
(d) Kuanzisha na kusambaza teknolojia rahisi ambazo zinatoa vyanzo mbadala vya nishati kwa matumizi ya nyumbani

**4.0 MIKAKATI YA UTEKELEZAJI**

Mkakati wa uhifadhi mazingira kwa maendeleo endelevu unaendana na Sera ya Taifa ya Mazingira ya mwaka 1997 ambayo ina lengo la kuhakikisha uendelevu, usalama na usawa wa matumizi ya rasilimali kwa ajili ya kukidhi mahitaji ya msingi ya kizazi cha sasa na cha baadaye bila kuharibu mazingira au kuhatarisha afya na usalama, kuinua ufahamu wa umma na uelewa wa umuhimu wa mahusiano kati ya mazingira na maendeleo na kukuza ushiriki binafsi ama jamii kwa ujumla katika kutunza mazingira. Ili kufikia malengo ya jitihada hii na matakwa ya Sera ya Taifa ya Mazingira ya mwaka 1997, mikakati ifuatayo ilitekelezwa.

Kujenga uelewa; uelewa kuhusu athari za kimazingira zitokanazo na shughuli za kibinadamu ulijengwa kwa jamii. Kampeni za kujenga uelewa juu ya athari za shughuli za kibinadamu kwenye mazingira zilianzishwa mwaka 1997 na mwanaharakati wa uhifadhi wa mazingira Bwana Sadick Ismail. Ndugu Sadick amekuwa na mchango mkubwa katika historia ya uhifadhi wa mazingira. Amekuwa na msukumo mkubwa katika shughuli za uhifadhi wa mazingira kwa zaidi ya miongo miwili. Alianza kwa kuhamasisha watu washiriki katika kampeni za upandaji miti baada ya kubaini uharibifu mkubwa wa misitu uliotokana na ukataji wa miti kuliosababishwa na ukaushaji wa majani ya tumbaku. Kutokana na jitihada ya bwana Sadick, Halmashauri ilishawishika na kuamua kutoa usaidizi katika kutekeleza jitihada hii.

Kuanzisha kikundi cha KIKUMUMI; Bw. Sadick alifanikiwa kushawishi watu wawili zaidi ambao ni Johari Idd na Sudi Nobert kujiunga kwenye kikundi kinachojulikana kama KIKUMUMI (Kikundi cha Kutunza Mazingira na Utafiti wa Miti). Kikundi kinajihusisha na uhifadhi wa mazingira na kufanya tafiti kuhusu miti. Kikundi hiki cha wajumbe 3 kiliendelea kujenga ufahamu kwa watu kuhusu mwenendo wa ukataji misitu hovyo unaendelea na matokeo yake kwa mazingira na maisha ya watu. Ingawa ilikuwa vigumu kwao kueleweka, wallijitahidi na kusisitiza jitihada yao ya upandaji miti. Kikundi hiki kilifanya majaribio rahisi ya kutambua aina za miti zinazofaa na kustawi kwenye ya mazingira na hali ya hewa ya Kaliua. Katika siku za mwanzo, kikundi kiliendelea na mbinu ya kujaribu mpaka kupata aina tofauti za miti ambazo zinakua vizuri.

Uanzishwaji wa vitalu vya miti na uzambazaji wa miche; baada ya majaribio kadhaa, kikundi cha KIKUMUMI kilianzisha kitalu cha miti kwa lengo la kuzalisha na kukuza maelfu ya miche ambayo ilisambazwa kwa jamii na kuipanda katika maeneo ya makazi na mashamba. Miche mingine ilitolewa bure kwa taasisi mbalimbali kama makanisa, shule, misikiti, mahakama,vituo vya polisi na hospitali. Usambazaji wa miti bure kwa taasisi hizi ulikuwa ni mkakati wa kukubalika kwa wadau mbalimbali na kuwafanya washiriki katika jitihada za upandaji miti.

Kuitisha mikutano ya jamii; mbinu nyingine iliyotekelezwa ni kuitisha na kuendesha mikutano na wanajamii katika vijiji mbalimbali ambapo katika mikutano hiyo walijadili masuala mbalimbali ikiwemo hali halisi ya ukataji hovyo wa miti na kampeni za upandaji miti katika kukabiliana na hali halisi ya mazingira. Katika mikutano hii, walitoa huduma ya chakula kama mbinu ya kushawishi wananchi kuhudhuria mikutano na kupata fursa ya kupata ujumbe uliokusudiwa.

Uundaji wa Vikundi vya Ushirika (Cooperative Union Groups - CUGs); ushirika huu wa vikundi vidogo ndani ya jamii vinatekeleza majukumu yao kwa hiari kutekeleza malengo ya maendeleo. Mashirika mengi ya maendeleo ya Kitaifa na Kimataifa yanaona vikundi hivi kama kiungo cha kuingia jamii wakati wa kutekeleza jitihada yoyote inayolenga kutatua changamoto za kijamii au kiuchumi zinazokabili jamii. Jitihada hii ya uhifadhi wa mazingira ilianza na kikundi cha KIKUMUMI ambacho kilikuwa na wajumbe 3 wenye ari ya kutunza mazingira. Kupitia kikundi hiki, ndani ya muda mfupi walianza kufundisha vikundi vingine (CUGs) na jamii kwa ujumla kuhusu utunzaji wa mazingira. Hadi kufikia sasa jumla ya vikundi 54 vimeanzishwa na vinafanya kazi mbalimbali za kiuchumi, kitamaduni, na uhifadhi wa mazingira. Makampuni ya tumbaku yamekuwa yakitumia vikundi hivi pia katika uzalishaji wa tumbaku.

Kuzalisha na kusambaza miche ya miti kwa watu binafsi na taasisi pamoja na kufanya ufuatiliaji wa karibu kuhakikisha miche hiyo inapandwa na kutunzwa. Vikundi vilivyoanzishwa vilipatiwa mafunzo juu ya namna ya kusia mbegu, kukuza miche na kusambaza kwa watu binafsi na taasisi pamoja na kuhamasisha upandaji wa miti kuzunguka maeneo makazi. Jumla ya vitalu 54 vilivyoanzishwa vimezalisha miche ya miti zaidi ya million 2.8 iliyosambazwa kwenye shule na wakulima katika msimu wa kilimo wa 2017/2018. Viongozi wa vyama vya ushirika waliwezeshwa ujuzi wa kupanda na kutunza miche iliyogawiwa kwa wajumbe wa vyama vyao vya ushirika na kutoa usaidizi kwa wajumbe wao pale wanapokwama.



***Moja ya kitalu cha miti kilichoanzishwa na kikundi cha ushirika***

Kuanzisha teknolojia ya kutengeneza mkaa mbadala kwa ajili ya matumizi ya nyumbani ili kupunguza kutegemea mkaa utokanao na magogo ya miti; Halmashauri kama mdau mkuu wa uhifadhi wa mazingira, ilianzisha teknolojia ya utengenezaji wa mkaa inayotumia mabaki ya mazao kama magunzi ya mahindi, maganda ya karanga na vumbi la mbao kutengeneza mkaa ambao unafanya kazi sawa na mkaa utokanao na miti. Mchakato wa utengenezaji wa aina hii ya mkaa umeelezewa katika sanduku na 1 lifuatalo;

***Sanduku 1: Maelezo mafupi kuhusu mchakato wa utengenezaji wa mkaa mbadala kutokana na mabaki ya mazao***

*Mchakato wa kutengeneza mkaa mbadala unaanza na ukusanyaji wa mabaki ya mazao kama magunzi ya mahindi, pumba za mpunga au maganda ya karanga. Mabaki haya huchomwa moto katika kiwango kidogo cha hewa na kuzalisha majivu ya rangi nyeusi. Majivu haya huchanganywa na udongo wa mfinyanzi ama saruji. Mchanganyiko huu hutiwa maji na kutengeneza tope zito ambalo husindikwa kwenye mashine (picha hapo chini inaonesha) ambayo hugandamiza mchanganyiko huo na kutengeneza vipande vya mkaa na kukausha tayari kwa matumizi.*

Mkaa uliotengenezwa na majivu ya mabaki ya mazao umefanyiwa majaribio na kubainika unadumu zaidi kuliko mkaa utokanao na miti ambao unawaka kwa muda mchache kabla ya kugeuka majivu. Picha zifuatazo zinaonesha majivu ya mazao, mashine yakutengenezea mkaa, jiko la mkaa na ukaushaji wa mkaa.



***Majivu na mashine ya kutengeneza mkaa***



***Ukaushaji wa mkaa na matumizi ya mkaa***

**5.0 RASILIMALI**

Rasilimali mbalimbali zilitumika katika utekelezaji wa jitihada hii tangu kuanzishwa kwake. Rasilimali fedha zilitumika kununua mbegu za miti, mbolea ya kupandia na usafirishaji wa miche kutoka katika vitalu hadi sehemu ya kuoteshwa. Chanzo kikuu cha fedha kilitokana na mapato ya ndani ya H/W ya Kaliua. Rasilimali nyingine ni pamoja na rasilimali watu wenye ujuzi mbalimbali kuhusu misitu, kilimo na

masuala ya mazingira. Maafisa wa Halmashauri walitoa muongozo wa uchaguzi bora wa aina ya mbegu za miti, ushauri wa kitaalamu wa namna ya kuzalisha miche ya miti na upandaji wa miche ya miti. Aidha, wadau wengine walihusika katika kutunza miti katika vitalu kwa kumwagilia na kutoa taarifa kwa wataalamu juu ya maendeleo ya ukuaji wa miche na kuomba msaada pale ilipobidi.

**6.0MATOKEO**

Utekelezaji wa jitihada hii umeleta matokeo makubwa kama ifuatavyo;

Kuongezeka kwa mabadilio ya kimtazamo wa watu na kuachana na vitendo vya mazoea ya uharibifu wa mazingira na badala yake kuhamasika kutekeleza vitendo rafiki vinavyotunza mazingira. Mabadiliko haya yamewafanya wananchi kuelewa athari za uharibifu wa mazingira na hivyo kuwa na ari ya kurejesha rasilimali za misitu ambazo zilikuwa hatarini kutoweka.

Kuongezeka kwa ufahamu wa watu kuhusu umuhimu wa miti kwa mazingira na maisha ya watu; idadi ya miti katika maeneo ya makazi, maeneo jirani na ya taasisi imeongezeka. Mnamo Desemba 2016 kwa mfano, miche zaidi ya 1,210,000 ilipandwa katika sehemu mbalimbali za Halmashauri, kati ya hizo 81% ya miche imestawi na kuendelea kukua na kuwa miti mikubwa. Desemba 2017, miche ipatayo 2,810,000 ilizalishwa na 30% ya miche hiyo imesambazwa kwa taasisi na wakulima binafsi kwa ajili ya kupandwa. Shule za msingi na sekondari walipatiwa miche ya miti 35,000, wakulima wa tumbaku miche 1,325,000 na watumishi wa Halmashauri miche 10,000. Aidha, kiwango cha ukataji miti kimepungua kuashiria kubadilika kwa mtazamo wa jamii juu ya uhifadhi wa mazingira.

Uanzishwaji wa vitalu binafsi vya uzalishaji wa miche ya miti ni kashiria kingine cha kubadilka kimtazamo kwa watu wa H/W ya Kaliua. Idadi ya vitalu vya miche ya miti vimeongezeka kutoka kitalu kimoja kilichokuwepo wakati wa uanzishaji wa jitihada hii hadi kufikia vitalu 45. Uzalishaji wa miche ya miti umeongezeka kufikia zaidi ya miche 2,800,000. Uzalishaji huu umeshawishi Halmashauri na Serikali Kuu kutoa usaidizi katika kampeni za upandaji miti. Wanachama wa KIKUMUMI walitambuliwa rasmi na Serikali kama wahusika wakuu katika jitihada hii ya upandaji miti. Katika kuunga mkono jitihada za kikundi, Halmashauri na Serikali Kuu walinunua miche ya miti na kuigawa katika shule na miche mingine kupandwa katika maeneo ya wazi. Vile vile, wanachama wa KIKUMUMI walipewa fursa ya kutembelea maeneo mengi ndani ya nchi na kujifunza zaidi juu ya ukuzaji wa miche na kilimo cha misitu. Ziara za mafunzo zilifadhiliwa na Halmashauri.

Kuongezeka kwa mapato ya wanachama wa kikundi; awali jitihada hii ya upandaji miti haikulenga kukuza faida, lakini kutokana na kuongezeka kwa ufahamu wa jamii juu ya uhifadhi wa mazingira, upandaji wa miti uliongezeka. Mahitaji ya miche ya miti yaliongezeka kwa hiyo kikundi kiliamua kuongeza juhudi za uzalishaji wa miche ya ziada ya kuuza kwa bei nafuu kwa watu binafsi. Vile vile, KIKUMUMI kilikuwa kituo cha kujifunzia harakati za uhifadhi wa mazingira ambapo taasisi za Serikali kama Tumbi COTC, shule za jirani na wajumbe wa ALAT Tabora mwaka 2002 walitembelea kikundi kwa lengo la kujifunza masuala yanayohusiana na ukuzaji na upandaji wa miche ya miti.

Ushiriki wa makampuni ya ununuzi wa tumbaku katika kampeni za uhifadhi wa mazingira; makampuni yanayonunua tumbaku kutoka kwa wakulima yamekubali kushiriki katika kampeni za uhifadhi wa mazingira. Majadiliano kati ya Halmashauri na Makampuni hayo yaliweka makubaliano kwamba kila kampuni itatoa mchango wa kifedha kulingana na ukubwa wa mashamba yanayomilikiwa na wanachama wa vikundi kwa mfuko wa hifadhi ya mazingira wa Mkoa na kutoa usaidizi kwa wakulima wa mikopo nafuu ambayo inalipwa baada ya mavuno. Mikopo hii hutumika kununua pembejeo za kilimo

kama mbolea, madawa, mbegu na viuatilifu. Aidha, makampuni haya ya tumbaku yamepewa wajibu wa kuwasaidia wakulima kununua miche ya miti kutoka kwenye vitalu mbalimbali. Makampuni haya ya tumbaku yamenunua na kugawa miche ya miti 1,325, 000 kwa wakulima ambayo ilipandwa katika msimu wa mvua wa mwaka 2017.

Kuanzishwa kwa kilimo cha korosho; kikundi kimeanzisha kitalu maalumu cha kuzalisha miche ya korosho kwa malengo mawili; kwanza ni kwamba korosho hukua haraka ikilinganishwa na aina nyingine ya miti hivyo huchukua muda mfupi kuboresha mazingira ambayo yaliharibiwa na pili, miti ya korosho huzalisha zao la korosho ambalo huuzwa na kuongeza kipato hivyo lingeweza kuvutia watu wengi zaidi kushiriki katika kilimo cha korosho. Uzalishaji wa miche ya korosho ulifanyika baada ya utafiti uliofanywa na Wizara ya Kilimo ambayo ilibaini uwezekano wa kustawisha korosho katika H/W ya Kaliua. Picha hapa chini ni kitalu cha miche ya korosho.



***Kitalu cha miche ya korosho***

Kuanzishwa na kusambazwa kwa teknolojia rahisi ya utengenezaji wa mkaa mbadala wa kuzalisha nishati ya matumizi ya nyumbani. Bw. Idrisa Hamisi Nyachenga na kikundi chake cha *Green power* walisambaza teknolojia ya utengenezaji wa mkaa mbadala kwa jamii ya watu wa Kaliua, lakini bidhaa zao zimekuwa zikiuzwa maeneo tofauti ambapo uhitaji wa nishati ni mkubwa kama vile Dar es Salaam, Dodoma, Mwanza na Arusha.

**7.0 MIKAKATI YA UENDELEVU**

Uendelevu wa jitihada hii unategemea mikakati ifuatayo; Halmashauri inaendelea kuimarisha jitihada za uhifadhi wa mazingira kwa kuunga mkono jitihada za CUGs, CBOs, kusimamia utekelezaji wa sheria za nchi, kanuni na miongozo na kuendeleza ushirikiano baina ya makampuni ya ununuzi wa tumbaku na wakulima.

Kuimarisha na kusambaza teknolojia mbadala ya kutengeneza mkaa; uvumbuzi wa mkaa mbadala una mchango mara mbili katika kuleta uendelevu wa jitihada hii. Kwanza, kwa kuwa mahitaji ya mkaa ni ya juu kabisa kona zote za nchi, wanajamii wanaojihusisha katika biashara hii daima watatengeneza fedha na wataendelea na biashara katika maisha yao bila shinikizo kutoka kwa Serikali. Pia, kutokana na matumizi ya mkaa mbadala, matumizi ya mkaa wa kawaida kutokana na miti yatapungua hivyo kutoa mchango mkubwa katika uhifadhi wa misitu ambayo ni kiashiria cha uendelevu. Aidha, malighafi ya utengenezaji wa mkaa mbadala inapatikana kwa wingi hivyo basi utengenezaji na usambazaji wa mkaa huo utaendelea kwa miaka mingi ijayo.

**8.0 SIRI YA MAFANIKIO**

Siri ya mafanikio ya jitihada hii ni kujitolea kwa viongozi wa jamii na wanajamii katika jitihada hii ya uhifadhi wa mazingira. Watu wote ambao walichagiza jitihada hii, walifanya kazi zote kwa kujitolea bila malipo yoyote. Moyo huu wa kujitolea umekuwa hazina kubwa katika mafanikio yaliyofikiwa. Siri nyingine kujengeka kwa imani kati ya wanachama wenyewe katika utekelezaji wa jitihada hii. Uwazi na ushirikishwaji wa wananchama wote katika kupanga na kufanya maamuzi uliwafanya kujenga uaminifu kwa kila mmoja hivyo kuongezeka kwa kushirikiano na hatimaye kufikia matokeo yaliyoelezwa hapo juu.



***Wanachama wa KIKUMUMI***

# HALMASHAURI YA WILAYA YA UVINZA

**UANZISHAJI WA KARAKANA YA USEREMALA YA HALMASHAURI KATIKA KUBORESHA UTOAJI WA ELIMU**






***Uzoefu wa H/W ya Uvinza***

**1.0 UTANGULIZI**

Halmashauri ya Wilaya ya Uvinza ni moja kati ya Halmashauri 8 za Mkoa wa Kigoma ambayo ilianzishwa mwaka 2013. Halmashauri ina eneo la 10,178km$^2$. Halmashauri hii inapakana na H/W za Kasulu na Kigoma kwa upande wa Kaskazini, Mkoa wa Tabora upande wa Mashariki, Mkoa wa Katavi upande wa Kusini na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo kwa upande wa Magharibi. Halmashauri ina kanda 3 za kiikolojia, ukanda wa chini unaombaa na Ziwa Tanganyika, Ukanda wa juu na ukanda wa miti ya Miombo.

Kiutawala, Halmashauri ina Tarafa 3, Kata 16 na Vijiji 61. Kwa mujibu wa sensa ya watu na makazi ya mwaka 2012, Halmashauri ina watu 351,990; wanaume 173,635 na wanawake 178,355. Shughuli kuu za kiuchumi ni pamoja na kilimo (mazao makuu yanayozalishwa ni mahindi, muhogo, maharage, mpunga, mawese na tumbaku), biashara ndogo ndogo, uchimbaji wa chumvi, uvuvi na ufugaji.




***Ramani ya H/W ya Uvinza***

Ingawa kiutawala Halmashauri ina Kata 16, kwa upande wa sekta ya elimu Kata zipo 17 kwa ajili ya kurahisisha usimamizi wa elimu. Kata ya Sunuka imegawanyika katika sehemu mbili: Sunuka A na Sunuka B kutokana na mtawanyiko wa vijiji 8. Halmashauri ina shule za msingi 118, walimu 1,179 (wanaume 874 na wanawake 305), wanafunzi 76,532 ( wavulana 38,861 na wasichana 37,671) na uwiano wa walimu kwa wanafunzi ni 1:65.

**2.0 TATIZO**

Kabla ya mwaka 2015, H/W ya Uvinza ilikabiliwa na changamoto ya uhaba wa madawati kwa wanafunzi wa shule za msingi. Uwiano wa dawati kwa wanafunzi ulikuwa 1:6 badala ya 1:3 kulingana na Sera ya Taifa ya Elimu. Tatizo liliongezeka zaidi baada ya kutekeleza sera ya Serikali ya elimu bure kuanzia 2016. Katika kipindi hiki uandikishaji wa watoto shuleni uliongezeka maradufu na kusababisha kuongezeka kwa upungufu wa madawati. Idadi ya wanafunzi iliongezeka kutoka 69,499 mwaka 2015/2016 hadi kufikia 76,532 mwaka 2016/2017. Idadi ya madawati iliyokuwepo ni 11,639 wakati uhitaji wa madawati ulikuwa 23,166 hivyo upungufu wa madwati ulikuwa 11,558. Hali hii ilisababisha mazingira magumu ya kujifunzia (Baadhi ya wanafunzi walilazimika kuketi sakafuni, utoro uliongezeka, na msongamano wa wanafunzi darasani uliongezeka) na kusababisha matokeo hafifu katika mitihani. Picha zifuatazo zinaonesha hali halisi kabla ya utekelezaji wa jitihada hii na jedwali na 1 linaonesha hali ya ufaulu wa wanafunzi kabla na baada ya kutekeleza jitihada hii.



***Wanafunzi wakiwa wameketi sakafuni na msongamano ndani ya darasa***

**Jedwali 1: Matokeo ya shule za msingi katika mtihani wa kumaliza elimu ya msingi**

| S/n | Mwaka | Ufaulu wa wanafunzi | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | Wavulana | Wasichana | Jumla | % ya ufaulu |
| 1 | 2014 | 1,255 | 626 | 1,881 | 35 |
| 2 | 2015 | 1480 | 848 | 2,328 | 52 |
| 3 | 2016 | 1,879 | 1083 | 2,962 | 59 |
| 4 | 2017 | 2,357 | 1758 | 4,115 | 68 |

## 3.0 LENGO

Lengo kuu la uanzishwaji wa karakana ya Halmashauri ilikuwa kuboresha mazingira ya kufundisha na kujifunza kwa kuhakikisha upatikanaji wa samani bora (madawati, viti na meza) kwa ajili ya shule za msingi na sekondari. Malengo mahususi ni pamoja na; kuanzisha karakana ya Halmashauri itakayopunguza gharama za utengenezaji wa madawati ikilinganishwa na kutumia karakana za watu binafsi, kuondoa tatizo la ukosefu wa madawati, kupunguza utoro na kuongeza ufaulu.

## 4.0 MIKAKATI YA UTEKELEZAJI

Timu ya Menejimenti ya Halmashauri (CMT), wazazi na wanafunzi hawakufurahishwa na kitendo cha wanafunzi kuketi sakafuni kutokana na uhaba wa madawati. Timu ya Menejimenti ya Halmashauri ilifanya uchambuzi wa gharama za utengenezaji wa madawati kwa kutumia karakana za watu binafsi ikilinganishwa na kuanzisha karakana ya Halmashauri ambayo ingeweza kutumika kutengeneza madawati kwa kipindi chote cha uhitaji. Mwanzoni mwa mwaka 2016, wazo liliwasilishwa kwenye Timu ya Menejimenti ya Halmashauri na kujadiliwa ambapo ilipendekezwa kuwasilishwa kwenye vikao vya Baraza la Halmashauri. Madiwani walipokea na kukubali wazo hili na kuwa mstari wa mbele katika kuhamasisha jamii katika Kata zao kushiriki katika utekelezaji wa jitihada hii. Katika utekelezaji mikakati ifuatayo ilitumika;

Uteuzi wa kikosi kazi cha kuratibu zoezi; CMT iliteua maafisa 6 kutoka idara za Elimu, Maendeleo ya Jamii na idara ya Maliasili ili kusimamia, kuratibu na kuandaa taarifa ya masuala yote yanayohusu uanzishwaji wa karakana. Maafisa hawa walipunguziwa majukumu yao ili kupata muda wa kutosha kuratibu zoezi la kuanzisha karakana ikiwa ni pamoja na mchakato wa kununua mashine za karakana. Kikosi kazi kiliwasilisha taarifa ya uchambuzi ikibainisha faida ambazo Halmashauri ingepata kwa kuanzisha karakana yake binafsi ikilinganisha na gharama ambazo Halmashauri ingelipa kwa kununua samani zilzotengenezwa na karakana za watu binafsi. Faida hizo ni pamoja na kupunguza gharama za utengenezaji wa madawati, uwezekano wa kutengeneza samani za ofisi na kuongeza fursa za ajira kwa vijana watakaoshiriki kufanya kazi kwenye karakana ya Halmashauri.

Uhamasishaji wa jamii; kampeni za uhamasishaji ziliratibiwa katika ngazi za Vitongoji, Halmashauri ya Kijiji, Mikutano Mikuu ya Vijiji na Mkutano wa KMK ambapo wazo hili liliwasilishwa na kujadiliwa. Jamii ilikubali na kupokea wazo hili na kuamua kushiriki kikamilifu katika utekelezaji wake. Jamii ilishiriki katika kuchana mbao, kukusanya na kuzilinda. Mafundi kutoka kwenye jamii walijitolea kufanya shughuli zote za karakana kwa malipo ya posho ya chakula cha mchana na sabuni yaliyowezeshwa na Halmashauri. Usafirishaji wa mbao kutoka kwenye misitu hadi eneo la karakana ulifanywa na Halmashauri.

Ununuzi wa vifaa vya karakana; CMT ilihakikisha kwamba karakana inakuwa na vifaa vya kutosha vyenye ubora hivyo ilinunua vitendea kazi, kufunga mashine na kuunganisha umeme. Kabla ya ununuzi, Menejimenti ilipitia maduka mbalimbali kubaini mashine bora za bei nafuu. Mashine zilizonunuliwa ni Chain saw 2, (aina ya *HUSQSARNA270), Circular saw 2, grander 3, disks*, mashine ya kukata kutoka SIDO 1, Mashine za kutoboa 2, misumari, gundi ya mbao na futi kamba.

Uteuzi wa walezi wa Kata; kila mkuu wa idara na kitengo alipewa ulezi wa Kata. Walezi wa Kata walipewa jukumu la kusimamia na kutoa taarifa ya wiki kuhusu changamoto jamii inayokumbana nazo wakati wa kuchana, kususanya na kusafirisha mbao. Changamoto zote ziliwasilishwa kwenye menejementi na kutatuliwa kwa wakati ili zoezi liende kwa wakati. Kwa masuala ambayo yalikuwa nje ya uwezo wa Halmashauri na yalihitaji utatuzi wa haraka, Menejimenti iliwasilisha kwa Mkuu wa Wilaya kupata ushauri na utatuzi.

Ushirikishwaji wa wadau katika utekelezaji; Halmashauri ilifanya mawasiliano na wadau mabalimbali kuomba usaidizi na ushiriki wa wadau katika kutengeneza madawati. Mkurugenzi wa Halmashauri alifanya majadiliano ya ana kwa ana na wakuu wa taasisi za JKT Bulombora, SARATOGA, TFS na TANAPA kwa lengo la kupata msaada. JKT Bulombora walitoa mafundi seremala kusaidia katika zoezi la kutengeneza madawati kwa malipo ya Tsh 10,000 tu kwa kila dawati. JKT pia walitoa gari la kusafirisha mbao na kusambaza madawati katika shule mbalimbali. Halmashauri iligharamia mafuta, matengenezo ya gari na posho ya dereva.

Usimamizi; Mhandisi wa Halmashauri alipewa jukumu la kuwasimamia mafundi kuhakikisha madawati yanayotengenezwa ni bora na imara. Mhandisi wa Halmashauri alitekeleza jukumu hili kwa kushirikiana na wataalamu walipo chini yake, Maafisa Elimu na wajumbe wa kikosi kazi kukagua ubora wa mbao zilizotumika, namna madawati yalivyotengenezwa na upakaji wa polishi.

Ugawaji wa madwati; kikosi kazi kwa kushirikiana na Waratibu Elimu waliratibu zoezi la ugawaji wa madawati kutokana na uhitaji. Picha zifuatazo zinaonesha mafundi wakitengeneza madawati.



*Utengenezaji wa madawati*



*Madawati yakiwa tayari kwa matumizi*

**5.0 RASILIMALI**

Rasilimali fedha, watu na vitendea kazi, zilitumika katika kufanikisha jitihada hii. Rasilimali watu ni pamoja na Madiwani, Timu ya Menejimenti ya Halmashauri, Kikosi kazi, Mafundi wa jamii, na jamii yenyewe. Vitendea kazi ni pamoja na gari la usafirishaji wa mbao na madawati, vifaa vya karakana, miti na mbao. Rasilimali fedha ni pamoja na fedha za ununuzi wa vifaa vya karakana (TZS 21,300,000), utengenezaji wa madawati 13,923 (TZS 930,510,000). Wadau (TANAPA, TFS, SARATOGA, DTO na JKT Bulombora) Walichangia TZS 18,000,000. Jedwali lifuatalo linaonesha matumizi ya rasilimali fedha.

**Jedwali 2: Rasilimali Fedha**

| Shughuli | Kiasi (TZS) | Chanzo cha fedha |
|---|---|---|
| Ununuzi wa mashine | | |
| Chain saw 2 | 3,000,000 | Vyanzo vya ndani vya Halmashauri |
| Circular saw 2 | 700,000 | Vyanzo vya ndani vya Halmashauri |
| Grenda 3 | 600,000 | Vyanzo vya ndani vya Halmashauri |
| Mashine ya kukata mbao kutoka SIDO KIGOMA | 5,000,000 | Vyanzo vya ndani vya Halmashauri |
| Mashine 2 za kukata mbao kutoka DAR | 7,000,000 | Vyanzo vya ndani vya Halmashauri |
| Misumari, gundi ya mbao, futi kamba na disk | 5,000,000 | Vyanzo vya ndani vya Halmashauri |
| **Jumla ndogo** | **21,300,000** | |
| Utengenezaji wa madawati | | |
| Madawati 9,623 | 673,610,000 | Jamii (72.39%) |
| Madawati 3,307 | 231,490,000 | Halmashauri (24.88%) |
| Madawati 363 | 25,410,000 | Wadau (2.73%) |
| **Jumla ndogo** | **930,510,000** | |
| **Jumla kuu** | **951,810,000** | |

**6.0 MATOKEO**

Karakana ya Useremala ya Halmashauri imeanzishwa na inafanya kazi; Karakana hii imeanzishwa na mashine za kisasa ambazo zimesimikwa na Halmashauri. Kupitia karakana hii idadi kubwa ya madawati yametengenezwa. Mbali na kutengeneza madawati, karakana hii pia inatengeneza samani za ofisi, makabati, mashelfu, mabenchi ya zahanati na vituo vya afya pamoja na mizinga ya kisasa ya nyuki. Utengenezaji wa madawati umekuwa zoezi endelevu la Halmashauri kutokana na kuongezeka kwa idadi ya wanafunzi. Picha zifuatazo zinaonesha samani mbalimbali zilizotengenezwa na Karakana ya Useremala ya Halmashauri.





***Mashine*** ***Madawati*** ***Mizinga ya nyuki***

Watoto wanafurahia kukaa kwenye madawati; mwaka 2016/2017 jumla ya madawati 11,015 yalitengenezwa na madawati 1,911 yalifanyiwa ukarabati hivyo kufanya ongezeko la madawati kufikia 24,565 na kubadilisha uwiano wa dawati kwa wanafunzi kutoka 1:6 (2016/2017) hadi kufikia 1:3 (Disemba, 2017). Mafanikio haya ya wanafunzi kukaa kwenye madawati wakati wa vipindi vya darasani yametoa hamasa kwa waalimu kufundisha na wanafunzi kujifunza. Hamasa hii imepunguza utoro wa wanafunzi ambao ulisababishwa na mazingira magumu ya kusomea. Picha ifuatayo inaonesha wanafunzi 3 wakitumia dawati 1.





***Wanafunzi 3 wakitumia dawati moja***

Fursa za ajira kwa mafundi wenyeji; tangu mwaka 2016, zaidi ya mafundi 50 wanajishughulisha na utengenezaji wa madawati na samani za Halmashauri. Halmashauri inatoa posho kuhamasisha mafundi na kuwafanya wabaki na kuendelea kufanya kazi ndani ya karakana.



***Samani na mizinga ya kisasa vilivyotengenezwa katika karakana ya Halmashauri***

Kuongezeka kwa ufaulu wa wanafunzi; ufaulu wa watoto kwenye mtihani wa darasa la saba umeongezeka kutoka 35% mwaka 2014 hadi 68% mwaka 2017 baada ya kutekeleza jitihada hii.

Gharama za kupata madawati zilipungua kwa kiasi kikubwa; kuanzishwa kwa karakana ya Halmashauri kulisaidia kupunguza gharama ya fedha na muda ambao ungetumika kupata idadi hiyo ya madawati kupitia mzabuni. Gharama ya dawati moja kupitia mzabuni ni TSZ 100,000, kwa idadi ya madawati 13,293 ingegharimu Halmashauri TZS 1,329, 300,000 lakini kupitia karakana ya Halmashauri idadi hiyo ya madawati iligharimu TZS 930,510,000 hivyo kuokoa TZS 298,790,000. Kiasi hiki kinaweza kutumika kwenye shughuli nyingine za maendeleo.

Kuhamasika kwa jamii katika kutekeleza miradi ya maendeleo; uhamasishaji uliofanywa kwenye ngazi zote umeifanya jamii kushiriki kikamilifu katika miradi mingine ya maendeleo inayotekelezwa na Halmashauri kama miradi ya maji, ujenzi wa madarasa na zahanati. Jamii imewezeshwa na inajiamini kwamba "*wanaweza kama wakitaka*" . Jitihada hii imeifanya jamii kuelewa kwamba wanauwezo wa kutatua changamoto zao wenyewe kama wakiamua kufanya hivyo kwa kuunganisha juhudi na rasilimali walizonazo.

**7.0 MIKAKATI YA UENDELEVU**

Ili kufikia malengo ya kuanzishwa kwa karakana hii, Halmashauri imeunda mikakati ya uendelevu ifuatayo.

(i) Halmashauri inaendelea kutenga bajeti kila mwaka kwa ajili ya madawati. Kwa mfano mwaka wa fedha 2018/2019 Halmashauri imetenga TZS 45m kwa ajili ya kutengeneza madawati.
(ii) Kuendelea kuhamasisha jamii kupitia mikutano ya Halmashauri ya Kijiji na Mkutano Mkuu kuhusu utengenezji wa madawati ili kuondoa upungufu.
(iii) Mashine na vitendea kazi vya karakana hufanyiwa ukarabati mara kwa mara ili karakana ifanye kazi wakati wote.
(iv) Halmashauri ina mpango wa kununua mashine nyingi zaidi kukuza karakana
(v) Halmashauri imeteua afisa wa kusimamia karakana wakati wote na kutoa taarifa za karakana.
(vi) Halmashauri inalenga kutafuta vijana ambao wataendesha karakana kibiashara na hivyo kuifanya chanzo cha mapato cha Halmashauri.

**8.0 SIRI YA MAFANIKIO**

Kufanikiwa kwa jitihada hii kunatokana na sababu mbalimbali ikiwa ni pamoja na utayari wa jamii kujihusisha na utengenezaji wa madawati, uongozi thabiti wa CMT wenye maono na ubunifu na uwepo wa wadau (TANAPA, TFS, SARATOGA na DTO) ambao walikuwa tayari kutoa usaidizi katika utekelezaji wa jitihada hii. Utayari na umoja wa watumishi wa Halmashauri pamoja na uwepo wa misitu inayomilikiwa na jamiii (Masanza, Uvinza, Masito na Ugala) na Serikali (Sunuka na Kachambi-Lukunda) ambayo ina miti ya kutosha ya mbao ni siri nyingine ya mafanikio.

# Sura ya Nne

## Maendeleo ya Jamii Kiuchumi

Sura ya Nne ina mbinu bora tatu zinazohusu jitihada za wananchi kujiletea maendeleo ya kiuchumi kupitia dhana mpya ya *"Kijiji Kimoja Zao Moja"*. Dhana hii husisitiza maendeleo yanayotokana na jamii yenyewe kwa kuibua miradi yenye upekee na vijiji vingine. *"Kijiji kimoja zao moja"* (One Village One Product-OVOP movement) ni harakati zilizoanza miaka ya 1970 katika eneo la Oita nchini Japani malengo yakiwa kuinua uchumi vijijini. Lengo mahususi la dhana hii lilikuwa ni kuhamasisha kila kijiji cha Oita kuchagua mradi wa uzalishaji ambao una utofauti wa aina fulani katika mkoa na kuzalisha kwa viwango vinavyokubalika kitaifa na kimataifa.

Dhana ya *"Kijiji Kimoja Zao Moja"* inalenga kuinua maendeleo ya jamii na uchumi katika mkoa kupitia kujitolea kuinua uwezo wa wananchi wa ngazi ya chini. Kabla ya kuanzisha harakati hizi katika eneo la Oita, waanzilishi walipata ushirikiano mkubwa wa jamii kupitia mashindano ya mpira na walikuwa na ushirikiano na miji rafiki ya nchi za nje. Mbinu hizi ziliwaweka watu pamoja, ziliwajengea uwezo wa kimaendeleo, na walishirikishana ujuzi waliopata. Mikakati mingine iliyofuata ilikuwa ni kuanzisha sera za jamii kuongeza zaidi thamani ya bidhaa, kuboresha mifumo, kuanzisha zao jipya au la pekee, ufundi wa kuchakata mazao ya kilimo, utalii, na mtazamo juu ya hali ya jamii.

Dhana ya *"Kijiji Kimoja Zao Moja"* inaonekana kuwa ni njia ya kuimarisha ujasiriamali wa watu wa vijijini kwa kutumia rasilimali, elimu na uzoefu, kufanya kazi zinazoongeza thamani kwa kuvipa utofauti bidhaa zao na kujenga uwezo wa rasilimali watu katika shughuli za uchumi kijijini. Kutumia ujuzi na rasilimali zilizopo bila kuathiri mazingira ni jambo linalotiliwa mkazo sana katika shughuli za dhana hii. Hii ina uhusiano na dhana ya maendeleo yanayotokana na jamii yenyewe. Katika harakati za *Kijiji Kimoja Zao Moja*, kuna msemo maarufu usemao "Fikiri kimataifa lakini tenda kulingana na Mazingira" (*Think globally but act locally*").

Sura hii ya Nne inaelezea mbinu bora tatu kutoka Halmashauri za Kibondo & Kakonko, Sumbawanga na Nkasi. Mbinu bora za Halmashauri za Kibondo na Kakonko zinahusu Ufugaji Nyuki wa Kisasa na Uongezaji Thamani Mazao ya Nyuki. Kabla ya Utekelezaji wa jitihada hii, shughuli za ufugaji wa nyuki zilifanyika kwa njia za duni za jadi. Uzalishaji wa asali ulikuwa mdogo kutokana na mbinu duni zilizotumika katika uzalishaji na soko la asali halikuwa la uhakika. Hakukua na ushirikiano baina ya wazalishaji wa asali, Halmashauri ilishindwa kupata taarifa za kiwango cha uzalishaji na soko la asali ndani ya maeneo yake ya kiutawala. Vilevile, uharibifu wa mazingira ulikithiri kutokana na utengenezaji wa mizinga ya nyuki kwa kutumia magome ya miti na magogo. Halmashauri zote mbili zilibaini changamoto hizi na kuamua kuingilia kati katika kuzitatua kwa kutoa usaidizi kwa wafugaji wa nyuki kutumia mbinu za kisasa za ufugaji, usindikaji, uongezaji thamani wa mazao ya nyuki na uanzishaji wa ushirika wa wafugaji nyuki. Jitihada hizi zilisaidia kuongeza kiwango cha uzalishaji wa asali na bidhaa nyingine zitokanazo na mazao ya nyuki ambazo zimefungashwa vyema na kupewa utambulisho, kupatikana kwa soko la uhakika la mazao ya nyuki na hatimaye kuongeza kipato cha wafugaji wa nyuki na kuboresha maisha yao.

Mbinu bora ya H/W ya Sumbawanga ilijikita katika Usimamizi Shirikishi wa Skimu ya Umwagiliaji uliotekelezwa katika Kijiji cha Sakalilo. Halmashauri iliamua kutekeleza jitihada hii ili kuondoa tatizo la uzalishaji duni uliotokana na matumizi ya miundombinu duni ya umwagiliaji. Wakulima waliathirika na uzalishaji mdogo, kipato kidogo, ugumu wa maisha na hatimaye kushindwa kukidhi gharama za huduma kama elimu na afya. Changamoto hizi ziliilazimu Halmashauri kuingilia kati kwa lengo la kuboresha maisha ya wakulima. H/W ya Sumbawanga kwa kushirikiana na wakulima, ilitafuta raslimali na kujenga miundombinu ya kisasa ya umwagiliaji hivyo kuongeza uzalishaji na kuboresha vipato na maisha ya jamii kwa ujumla.

Mbinu bora ya H/W ya Nkasi inahusu Uanzishaji wa Jumuiya ya Wafugaji Kuhimiza Ufugaji wa Koo Bora za Ng'ombe. Kabla ya mwaka 1995 Halmashauri ilikuwa ikipokea wahamiaji kutoka mikoa mingine wakiwa na makundi makubwa ya mifugo hasa ng'ombe. Hali hii ilisababisha migogoro ya mara kwa mara kati ya wakulima na wafugaji, uharibifu wa mazingira na hatimaye uhaba wa mvua. H/W ya Nkasi iliamua kutatua matatizo haya kwa kuwaunganisha wafugaji kutoka Kata zote na kufanya mikutano ya uhamasishaji kuhusu mbinu za ufugaji bora, kuboresha mifugo, kuanzisha jumuiya ya wafugaji na kutambua washirika wa biashara ili kuanzisha soko la mazao ya mifugo. Matokeo ya jitihada hii ni pamoja na kuanzishwa kwa ufugaji wa kisasa wa aina bora ya ng'ombe, kuongezeka kwa uzalishaji na kuimarika kwa kipato, kuanzishwa kwa matumizi bora ya ardhi na kuondoa migogoro ya ardhi.

# HALMASHAURI ZA WILAYA ZA KIBONDO NA KAKONKO

KIBONDO DISTRICT COUNCIL

HALMASHAURI YA WILAYA YA KAKONKO
KAKONKO DISTRICT COUNCIL

**UFUGAJI NYUKI WA KISASA NA UONGEZAJI THAMANI MAZAO YA NYUKI**



***Uzoefu wa H/W za Kibondo na Kakonko***

**1.0 UTANGULIZI**

Halmashauri za Kibondo na Kakonko zinapatikana upande wa Kaskazini mwa Mkoa wa Kigoma kwenye wastani wa mwiniko kati ya 500m na 1,600m kutoka usawa wa bahari. Awali, Kibondo na Kakonko zilikuwa ni Halmashauri moja ya Kibondo. Tarehe 8 Machi, 2013 H/W ya Kibondo iligawanywa na kuunda Halmashauri mpya ya Kakonko. Halmashauri zote mbili zinapakana na Jamhuri ya Burundi upande wa Mashariki. Kabila kuu katika Halmashauri hizi ni Waha ambao kiasili wanafahamika kama *Buha*.

Hali ya hewa katika H/W za Kibondo na Kakonko zina kipindi kifupi cha kiangazi kati ya mwezi Juni hadi Septemba, mvua za masika hunyesha kati ya Oktoba na Mei. Wastani wa mvua kwa mwaka ni 1,000mm, hali ya joto ni kati ya 15˚C na 27˚C na hufikia kiwango cha juu mwezi Septemba. Kipindi cha baridi ni kati ya mwezi Juni na Agosti ambapo hali ya joto ni kati ya 15˚C na 22˚C. Shughuli kuu za kiuchumi ni kilimo, ufugaji wa nyuki, ufugaji na kilimo cha mboga mboga. Shughuli nyigine ni biashara, ajira katika sekta za umma, viwanda vidogo vidogo vya samani na kilimo.

**2.0 TATIZO**

Ufugaji nyuki ni moja kati ya shughuli muhimu za kiuchumi zinazofanyika maeneo mengi Tanzania. Kwa miaka mingi wakazi wa H/W za Kibondo na Kakonko wamejihusisha na ufugaji nyuki kwa kutumia mizinga ya asili ambayo imetengenezwa kwa magome ya miti na magogo. Ufugaji nyuki wa asili ulifanywa na wazee. Wafugaji nyuki walitengeneza mizinga na kuwaomba vijana kuwasaidia kuitundika kwenye miti ili nyuki waweze kuingia. Ufugaji nyuki ulionekana kama shughuli zinazofanywa na watu maskini. Vilevile kulikuwa na imani kwamba ufugaji wa nyuki uliambatana na imani za kushirikina ambapo wafugaji wa nyuki walitumia ushirikina kuwavuta nyuki kuingia kwenye mizinga. Aidha, kulikuwa na imani kwamba mwanamke akisogelea mzinga wa nyuki huzuia nyuki kuingia kwenye mzinga. Imani hizi ziliwafanya vijana wengi na wanawake kutoshiriki kwenye ufugaji wa nyuki kutokana na kutokuwa tayari kujihusisha na ushirikina.

Kiwango cha uzalishaji wa asali kilikuwa kidogo kutokana na mbinu duni za uzalishaji na soko la asali halikuwa la uhakika. Asali iliyozalishwa mara nyingi iliuzwa kwa watengenezaji wa pombe za asili kwa bei ya chini kati ya TZS 20,000 na TZS 35,000 kwa ndoo ya lita 20. Asali iliyovunwa iliuzwa bila kuchakatwa; wavunaji wa asali hawakuwa na ujuzi wa kutenganisha asali na masega na ufahamu kwamba masega hayo yangeweza kutumika kutengeneza bidhaa nyingine kama mishumaa, rangi za viatu, mvinyo na vipodozi. Wafugaji wa nyuki hawakuwa na ufahamu kwamba ufugaji wa nyuki ungeweza kufanyika kibiashara na kuwapatia fedha nyingi ambazo zingebadilisha maisha yao. Hakukuwa na umoja wa wazalishaji wa asali katika H/W ya Kakonko; kila mzalishaji alifanya shughuli za uzalishaji kwa upekee na kutafuta soko la asali yeye mwenyewe. Kwa upande wa H/W ya Kibondo kulikuwa na ushirika wa wafugaji nyuki lakini hawakuwa na uwezo wa kusimamia soko. Kadhalika, Halmashauri ilishindwa kupata taarifa za uzalishaji na mauzo ya asali ndani ya maeneo ya mipaka yao.

Uharibifu wa mazingira; mizinga ya nyuki ilitengenezwa kwa kutumia magome ya miti na magogo. Hali hii ilisababisha ukataji miti holela. Vile vile, uvunaji wa asali ulifanyika kwa njia za asili kwa kutumia moto kulikosababisha uchomaji wa misitu. Eneo la ufugaji wa nyuki lilikuwa dogo hivyo kusababisha idadi ndogo ya watu kujihusisha na shughuli hii. Jamii zinazozunguka Pori Tengefu la Kigosi na Moyowosi hazikuruhusiwa kufanya shughuli zozote katika eneo hilo.

**3.0 LENGO**

Lengo kuu la jitihada hii ni kuboresha ufugaji nyuki na kuongeza thamani ya mazao ya nyuki ili kuboresha kipato na maisha ya watu. Mahususi; jitihada hii ililenga kuboresha ufugaji wa nyuki kwa kutumia mizinga ya kisasa, kuongeza uzalishaji wa asali, kuchakata na kuongeza thamani ya mazao ya nyuki, kuunganisha wafugaji wa nyuki kuzalisha na kuuza pamoja, kutafuta na kupanua soko kutoka uuzaji wa asali pekee hadi kuuza mazao ya upili ya nyuki na kutunza mazingira kwa kuanzisha ufugaji nyuki wa kisasa.

Mikakati ya utekelezaji wa jitihada hii kwa Halmasahuri hizi mbili imetofautiana. Hii ni kutokana na kutofautiana kwa msukumo wa kuchukua hatua, mazingira na ushirikiano baina ya wafuga nyuki. Kwa H/W ya Kibondo jitihada ilianzishwa na wafugaji nyuki wenyewe ambapo walijipanga na kuomba usaidizi kutoka Halmashauri. Kwa upande wa H/W ya Kakonko jitihada hii ilianzishwa na Halmashauri baada ya kubaini uharibifu wa mazingira ambao ulifanywa na wafugaji nyuki. Mikakati kama kujenga uelewa, kujenga uwezo kwa wafugaji nyuki na mbinu za kuongeza thamani kwa mazao ya nyuki zinafanana kwa Halmashauri zote mbili. Mikakati ya utekelezaji wa jitihada hizi imefafanuliwa kwa kila Halmashauri hapa chini.

**4.1 MIKAKATI YA UTEKELEZAJI (H/W YA KIBONDO)**

Jitihada ya H/W ya Kibondo ilianzishwa na wafugaji nyuki; mwaka 1992 wafugaji nyuki walianzisha ushirika ulioitwa Ushirika wa Wafuga Nyuki Kibondo (UKI) na kusajiliwa mwaka 1998 ukiwa na wanachama 185 (Wanawake 22 na Wanaume 163). Lengo la ushirika lilikuwa kujihusisha na shughuli za ufugaji nyuki, kutafuta na kuomba kibali cha kutumia Pori Tengefu la Moyowosi kutoka mamlaka ya usimamizi wa Pori Tengefu la Moyowosi. Ushirika pia ulijihusisha na ununuzi na uuzaji wa asali ghafi kutoka kwa wazalishaji wa jadi, kuuza na kununua kahawa na kusambaza pembejeo za kilimo. Baadaye, UKI ilifanyiwa maboresho na kujikita katika shughuli moja tu ya ufugaji nyuki na uongezaji thamani wa mazao ya nyuki. UKI mpya iliyoanzishwa ilisajiliwa mwaka 2015 ikiwa na wanachama 469 (Wanawake 63 na wanaume 406).



***Baadhi ya wanachama wa UKI***

Kushiriki Maonesho ya Asali; mwaka 2009, Wizara ya Maliasili na Utalii iliandaa maonesho ya asali mjini Dodoma na baadhi ya wanachama wa UKI walishiriki. Maonesho haya yaliwahamasisha wanachama wa UKI baada ya kujifunza na kupata uzoefu juu ya namna mbalimbali na mbinu za kuongeza thamani kwenye mazao ya nyuki na kuongeza soko na kipato. Baada ya kurejea, wanachama walianza kuchakata mazao ya nyuki na kueneza ujuzi kwa wanachama wengine kuhusu uongezaji wa thamani kwa mazao ya

nyuki. Mrejesho wa Afisa Nyuki wa Halmashauri kwa Timu ya Menejimenti ya Halmashauri ulichochea ari ya kutoa usaidizi katika shughuli za ufugaji nyuki.

Mafunzo juu ya uchakataji wa mazao ya nyuki; kuanzia mwaka 2010 hadi 2014 mafunzo yalitolewa na Afisa Nyuki wa Halmashauri kuhusu uvunaji bora wa asali, utunzaji bora wa asali, usafi wa asali, upimaji wa ubora wa asali kwa kutumia njia za asili na za kisasa na uhifadhi wa asali. Vilevile, wafugaji nyuki walifundishwa namna ya kufungasha asali katika vipimo mbalimbali (1 Kg, 1.4Kg, na 7Kg); kuweka nembo za utambulisho, kuchuja asali na nta kutoka kwenye masega; kanuni za uhifadhi na ufungashaji; utengenezaji wa bidhaa zitokanazo na asali na nta kama vile mishumaa, vipodozi, dawa na vinywaji.



***Mafunzo kuhusu uongezaji thamani wa mazao ya nyuki***

Kuomba kibali kutoka Mamlaka ya Uhifadhi wa Pori Tengefu la Moyowosi; Mwaka 2011, Halmashauri ilitoa usaidizi wa kuomba kibali cha kutumia Pori Tengefu la Moyowosi kwa ajili ya shughuli za ufugaji nyuki. Kibali kilitolewa baada ya Halmashauri kuwasilisha maombi Wizara ya Maliasili na Utalii. Kwa sasa, wafugaji wa nyuki wanatundika mizinga yao kwenye Pori Tengefu la Moyowosi.

Kuanzisha kituo cha kukusanya, kuchakata na kuuza mazao ya nyuki; kituo kinatumika kama sehemu ya wanachama kukutana na kujumuika na wadau mbalimbali. Ghala ambalo awali lilitumika kuhifadhi mazao ya kilimo lilibadilishwa na kuwa kituo cha kukusanya, kuchakata na kuuza mazao ya nyuki. Ghala hili lilibadilishwa ili kupata jengo ambalo linakidhi kiwango cha kutunza mazao ya nyuki na uchakataji. Mwaka 2011, Halmashauri ilifanya ukarabati wa jengo hili na kutenga vyumba mbalimbali kama viwango vya TFDA vinavyoelekeza.



*Jengo lililokarabatiwa kwa lengo la ukusanyaji, uchakataji na uuzaji wa mazao ya nyuki*

Kuunganisha na kujenga mtandao baina ya wafugaji nyuki na wanunuzi kutoka nje; ili kupata soko la uhakika, wafugaji nyuki waliunganishwa na wanunuzi kama Jasmine Bee Company kutoka Moshi na Upendo Honey kutoka Kigoma na kuingia katika makubaliano na UKI. Mwaka 2015, Jasmine Bee Company walinunua tani 12 za asali na tani 1.6 ya nta na baadae mwaka 2016 walinunua tani 30 za asali na mwaka 2017 tani 40 za asali. Kampuni hii inasafirisha asali kutoka Kibondo na kuuza katika soko la Ulaya.

Kuimarisha Ushirika wa wafuga nyuki; Afisa Ushirika wa Halmashauri alitoa mafunzo kwa wanachama wa UKI kuhusu usimamizi, uongozi na utunzaji wa kumbukumbu kwa lengo la kuendesha ushirika kwa ufanisi. Aidha, Afisa Ushirika alisaidia katika kuanzisha Katiba na sheria ndogo za usimamizi wa ushirika. Sheria ndogo zinabainisha wazi mfumo wa uendeshaji masuala ya ushirika na kulinda masilahi ya Jumuiya na ya mwanachama, muundo wa UKI na kuanzisha haki na wajibu wa kila mwanachama, uongozi na wadau.

Kuunganisha UKI na Shirika la Viwango Tanzania (TBS) na Mamlaka ya Chakula na Dawa Tanzania (TFDA); mwaka 2015, Halmashauri iliwaunganisha UKI na TBS na TFDA ili kusimamia ubora na viwango vya bidhaa zinazozalishwa. Baada ya ukaguzi wa bidhaa zinazozalishwa UKI ilipatiwa cheti cha ubora na usalama kwa mlaji kutoka TBS na TFDA. Baada ya kuthibitika kiwango cha ubora bidhaa za UKI zilipata soko zaidi. UKI pia waliunganishwa na Washirika wa Maendeleo kama Shirika la Maendeleo la Ubeligiji (BTC) ambao walitoa msaada wa mafunzo na vifaa vya uchakataji.

### 4.2 MIKAKATI YA UTEKELEZAJI (H/W YA KAKONKO)

Jitihada ya H/W ya Kakonko ilianza mwaka 2004 baada ya Serekali kubaini uharibifu mkubwa wa mazingira katika Vijiji vya Muganza, Kasanda, Kanyonza, Kazilamihunda, Rumashi, Kabare, Muhange, Bukirilo, Nyakayenzi, Kasuga na Kasongati. Uchunguzi uliofanyika ulibaini sababu za uharibifu wa mazingira na ukataji mkubwa wa miti kwa ajili ya kutengeneza mizinga. Mwaka 2005 Halmashauri iliamua kuondoa tatizo na mwaka 2006 wataalamu wa mazingira walikutana H/W ya Kibondo na kukubaliana kwamba wafugaji nyuki wafundishwe mbinu za kisasa za ufugaji nyuki.



*Mzinga wa Kisasa*



*Mzinga wa jadi*

.

Kujenga uelewa; mwaka 2007, wataalamu kutoka Halmashauri waliendesha mafunzo ya ufugaji nyuki wa kisasa kwa washiriki kutoka Kata za Gwanumpu, Mugunzu, Kasanda, Kakonko, Mugange, Nyamtukuza, Kasuga na Kiga. Washiriki 4 kutoka kila Kata walialikwa kwa kigezo kwamba lazima mshiriki kutoka kundi la wanawake ashiriki. Mafunzo yalihusu ufugaji wa nyuki kwa kutumia mizinga ya kisasa.

Kuunganisha na kujenga uwezo wa wafugaji nyuki; katika kukuza ufugaji wa nyuki, Halmashauri iliamua kuunganisha jamii ya watu wa Kakonko kujihusisha na ufugaji nyuki wa kisasa. Jamii zilifundishwa ufugaji nyuki wa kisasa, uvunaji, usindikaji, uongezaji wa thamani na utafutaji wa masoko kwa bidhaa za nyuki na uhifadhi wa mazingira endelevu. Mafunzo ya kujenga uwezo yalifadhiliwa na mradi wa Belgium Technical Cooperation (BTC).

Kupanua/kuongeza eneo la ufugaji nyuki; Halmashauri kwa kushirikana na vikundi vya jamii ilielekeza Vijiji kuanzisha hifadhi za misitu. Vijiji 13 vilikubali pendekezo hili na kuanzisha Hifadhi za Misitu ya Vijiji ya eneo la 5000ha zinazotumiwa kwa shughuli za ufugaji nyuki. Aidha, H/W ya Kakonko iliomba kibali kutoka Wizara ya Maliasili na Utalii cha kutumia sehemu ya Pori Tengefu la Moyowosi na Kigosi ambalo linapakana na H/W ya Kakonko kwa ajili ya ufugaji nyuki; ombi hili lilikubaliwa.

Kuanzisha kituo cha uchakataji; Halmashauri kupitia mradi wa BTC ilijenga jengo la uchakataji pamoja na kununua vifaa vya uchakataji wa mazao ya nyuki vya Ushirika wa Wafuga Nyuki wa Buyungu. Kuanzishwa kwa kituo kulichochea watu wengi kujishughulisha na uzalishaji na uchakataji wa asali.



*Kituo cha kuchakata asali cha Ushirika wa Wafugaji Nyuki Buyungu*

Kutafuta masoko ya asali na mazao mengine ya nyuki; kila mwaka wafugaji wa nyuki wanafadhiliwa na Halmashauri kuhudhuria maonesho kama Nanenane, matamasha ya kitaifa, mbio za mwenge wa uhuru, Maonesho ya Sabasaba na Maonesho ya SIDO kwa lengo la kutafuta masoko.

Kusimamia ubora; Halmashauri ilisaidia wafugaji wa nyuki kukidhi viwango vya kimataifa na kupata nembo ya utambuzi ya kimataifa (international barcode), cheti cha TBS na TFDA ambavyo ni muhimu katika kukuza soko la bidhaa za nyuki.




***Asali yenye utambulisho wa Kakonko***

**5.0 RASILIMALI**

Katika utekelezaji wa jitihada hizi, H/W za Kakonko na Kibondo pamoja na wazalishaji wa mazao ya nyuki walitumia rasilimali mbalimbali. H/W ya Kibondo ilitumia TZS 6m kwa ajili ya ukarabati wa jengo la kuchakata asali na mazao ya nyuki. Jamii ilichangia nguvukazi kama kukusanya tofali, mchanga, mawe ya kujengea, kokoto na maji wakati wa ujenzi na kulipa mafundi wa jamii. Mchango wa jamii unathaminishwa kufikia TZS 35m. BTC ilichangia TZS 15m. H/W ya Kakonko ilitumia rasilimali fedha kununua mizinga ya kisasa, vifaa vya uchakataji wa asali, ujenzi wa kituo cha uchakataji na mafunzo kwa wafugaji wa nyuki. Rasilimali watu katika jitihada hizi ni pamoja na wataalamu kutoka Halmashauri na BTC. Rasilimali nyingine ni pamoja na misitu, majengo, vyombo vya usafiri, na vitendea kazi vya ufugaji nyuki.

**6.0 MATOKEO**

Utekelezaji wa jitihada hizi umesababishwa kuanzishwa kwa vituo vya uchakataji wa mazao ya nyuki. Vituo hivi hutumika kukusanya, kuchakata na kuuza mazao ya nyuki. Kituo cha uchakataji wa mazao ya nyuki cha Busunzu (H/W Kibondo) kina uwezo wa kuchakata tani 56 za asali kwa msimu (Juni – Julai na Agosti - Disemba) na kituo cha Buyungu (H/W Kakonko) kina uwezo wa kuchakata tani 40 za asali kwa msimu. Picha zifuatazo zinaonesha vituo vya Buyungu na Basunzu.



***Kituo cha Buyungu*** ***Kituo cha Busunzu***

Idadi ya watu wanaojishughulisha na ufugaji wa nyuki imeongezeka; kwa H/W ya Kibondo wanachama wa UKI wameongezeka kutoka 185 mwaka 1998 hadi 469 mwaka 2016 kutoka vikundi 16 kutoka vijiji 10. Vyama vya ushirika vya vijiji vya Kifura, Malagarasi na Mlange vimeanzishwa. Vyama hivi vya ushirika vimejenga vituo vya kukusanya, kuchakata na kuuza asali. Katika H/W ya Kakonko, idadi ya wafuga nyuki imeongezeka kutoka 722 mwaka 2005 hadi 790 mwaka 2016.


***Kituo cha uchakataji cha Busunzu***


***Kituo cha uchakataji cha Kifura***

Kuongezeka kwa mazao ya nyuki; wanachama wa ushirika wa Buyungu na UKI wamepata ujuzi wa kuchakata mazao makuu ya nyuki (nta na asali) na kutengeneza bidhaa mbalimbali kama vile vinywaji, mafuta ya kupaka, rangi za viatu na mishumaa. Bidhaa hizi hufungashwa vyema na kuwekewa nembo zenye kuvutia soko. Picha zifuatazo ni baadhi ya bidhaa zinazozalishwa kutokana na mazao ya nyuki katika H/W za Kibondo na Kakonko.



***Asali***


***Nta***


***Mishumaa***


***Rangi za viatu***



***Mafuta ya kupaka***


***Vinywaji vya jadi***

Kuongezeka kwa kipato; uzalishaji na usindikaji wa mazao ya nyuki umeongeza kipato cha mfuga nyuki. Awali, uzalishaji ulikuwa mdogo chini ya 5kg kwa mzinga wa nyuki lakini kuanzishwa kwa ufugaji wa nyuki wa kisasa kumeongeza uzalishaji wa asali kufikia 13kg kwa mzinga mmoja wa nyuki. Bei ya asali imeongezeka kutoka TZS 20,000 kwa ndoo ya asali ghafi hadi kufikia TZS 150,000 kwa ndoo ya asali iliyochakatwa. Hali hii imechangia kuongezeka kwa kipato cha mfuga nyuki na jamii kwa ujumla hivyo kuboresha maisha yao. Sawia Damasi mwanamke mfugaji wa nyuki alithibitisha ukweli huu kwa kusema…. " *Shughuli za ufugaji wa nyuki zimesaidia sana famila yangu…nimeweza kulipa ada za watoto wangu wadogo na mwanangu mkubwa anayesoma Chuo Kikuu shahada ya kwanza…. Kabla ya mradi huu ilikuwa vigumu hata kupata mlo wa siku….. familia yangu ni kubwa, ni ya watu 9….. sasa naweza kukidhi mahitaji ya chakula….. nimeweza kujenga nyumba kutokana na fedha nilizozipata kutokana na shughuli za ufugaji wa nyuki…. Napata zaidi ya TZS 8m kwa mwaka…."*



***Sawia Damasi; nyumba yake imefungwa umeme wa sola***

Kuongezeka kwa soko la uhakika la bidhaa za nyuki; maboresho katika usindikaji yamesababisha kuongezeka kwa soko la uhakika la bidhaa za nyuki. Kampuni za Upendo Honey ya Kigoma na Jasmine Honey ya Moshi ni wanunuzi wakubwa wa asali iliyochakatwa kutoka Kakonko na Kibondo. Vilevile kuboreshwa kwa vifungashio kumevutia wateja wengi. Kwenye maonesho ya Nanenane wanachama wa ushirika huonesha na kuuza bidhaa kwa wateja mbalimbali wa ndani na nje ya mkoa. Kuanzishwa kwa vituo vya usindikaji wa asali kumetatua changamoto ya kupanga bei kwa mtu mmoja mmoja; kwa sasa bei huamuliwa na ushirika na ni moja. Tokeo jingine ni kuboreshwa kwa bidha za nyuki; bidhaa hizo zimeboreshwa hadi kufikia kupata vyeti vya uthibitisho wa ubora kutoka TFDA na TBS. Hali hii imeongeza imani kwa mazao ya nyuki yanayozalishwa Kibondo na Kakonko kwa walaji na hivyo kuongezeka kwa mahitaji, wateja na bei.



***Maonesho ya Nanenane***




***Bei elekezi***

Uongozi wa ushirika umeimarika; pamoja na kuimarika kwa utunzaji wa taarifa, ushirika unaendeshwa na Bodi imara ya Usimamizi wa Ushirika na wajumbe wenye ari na motisha. Bodi inaendesha shughuli zake kwa mikutano katika misingi ya uwazi na uongozi bora.

H/W za Kibondo na Kakonko zimekuwa vituo vya kujifunzia kuhusu ufugaji nyuki; mwaka 2012 wafugaji nyuki kutoka H/W ya Simanjiro walitembelea UKI kujifunza usindikaji wa mazao ya nyuki na uongezaji wa thamani. Kutokana na mafunzo haya baadhi ya wanachama wa UKI walitembelea H/W ya Simanjiro kufundisha wafugaji wa nyuki. Mwaka 2014, wafugaji wa nyuki kutoka H/W ya Kibondo walialikwa kutoa mafunzo ya ufugaji nyuki kwa kikudi cha Kabanga Nickel na kikundi cha wanawake wajasiriamali wa H/W ya Ngara. Vilivile, wafugaji wa nyuki kutoka Burundi na Rwanda walitembelea Kakonko na Kibondo kujifunza ufugaji wa nyuki na uongezaji thamani mazao ya nyuki.



***Wafugaji wa nyuki kutoka Simanjiro walipotembelea Kibondo***

Kuongezeka kwa idadi ya wanawake wanaojihusisha na ufugaji wa nyuki; mila za zamani ambazo zilizuia wanawake kujishughulisha na ufugaji wa nyuki zimepungua. Wanawake wamehamasika na kujiunga na vikundi mbalimbali vya ufugaji nyuki. Kwa mfano, kati ya wafugaji nyuki 790 wa Kakonko, 370 ni wanawake.



***Wanawake wakishiriki katika ufugaji wa nyuki na usindikaji wa asaliH/W ya Kakonko***

**7.0 MIKAKATI YA UENDELEVU**

Katika kusimamia uendelevu wa matokeo ya jitihada hizi, Halmashauri zimeunda mikakati ya uendelevu. Mikakati hii ni pamoja na;

(i) Kuanzisha sheria ndogo ya mazingira ya uhifadhi wa misitu na ufugaji wa nyuki.
(ii) Kuunganisha shughuli za ufugaji nyuki na uhifadhi wa mazingira.
(iii) Kuendelea kutoa usaidizi katika kutafuta masoko ya bidhaa za nyuki na kuhakikisha ushiriki katika maonesho mbalimbali ya kitaifa.
(iv) Kutoa elimu ya misitu kwa maafisa wa vijiji kuhusu wajibu wa jamii wa kuhifadhi misitu.




***Bango la kuhimiza uhifadhi wa mazingira.***

**8.0 SIRI YA MAFANIKIO**

Mafanikio ya jitihada hizi yanatokana na sababu nyingi; jitihada hizi zilitokana na jamii yenyewe, uhitaji wa jamii juu ya jitihada hizi ulisababisha jamii kushiriki kikamilifu katika utekelezaji wake. Uwepo wa rasilimali za asili kuruhusu ufugaji wa nyuki, utayari wa Wizara ya Maliasili na Utalii kusaidia shughuli za ufugaji nyuki katika Pori Tengefu la Moyowosi na Kigosi, kuunganishwa kwa wafugaji nyuki na soko la ndani na nje, utayari na nia ya Halmashauri kusaidia ufugaji nyuki na uwepo wa washirika wa maendeleo kama BTC ni sababu za mafanikio ya jitihada hizi.

# HALMASHAURI YA WILAYA YA SUMBAWANGA


**USIMAMIZI SHIRIKISHI WA SKIMU YA UMWAGILIAJI**



*Uzoefu wa Kijiji cha Sakalilo*

**1.0 UTANGULIZI**

Halmashauri ya Wilaya ya Sumbawanga ni moja kati ya Halmashauri 4 za Mkoa wa Rukwa; Halmashauri nyingine ni Manisapaa ya Sumbawanga, H/W za Kalambo na Nkasi. Halmashauri inapatikana kati ya Latitudo $7^0$8’ na $9^0$ Kusini na Longitudo $31^0$ na $32^0$1’ Mashariki. H/W ya Sumbawanga inapakana na H/W ya Kalambo upande wa Kusini, Mkoa wa Mbeya upande wa Mashariki, Ziwa Rukwa upande wa Kaskazini, H/W ya Nkasi na Manispaa ya Sumbawanga upande wa Magharibi na Mkoa wa Katavi upande wa Kaskazini Magharibi. Kiutawala, Halmashauri ina Tarafa 4, Kata 27 na Vijiji 114. Kwa mujibu wa sensa ya mwaka 2012, Halmashauri ina watu 305,846 kati yao wanawake ni 156,784 na wanaume ni 149,062. Idadi ya Kaya inakadiriwa kufikia 53,841 zenye wastani wa watu 5 kwa kila Kaya.




***Ramani ya H/W ya Sumbawanga***

H/W ya Sumbawanga ina hali ya hewa nzuri yenye wastani wa mvua kati ya 800mm na 1200mm na mwinuko wa 1700m kutoka usawa wa bahari. Wastani wa joto ni kati ya $24^0$C na $27^0$C na kiwango cha chini cha joto ni kati ya $13^0$C na $16^0$C kikiambatana na mvua katika miezi ya Oktoba hadi Aprili. Shughuli kuu za kiuchumi ni kilimo, uvuvi na biashara ndogo ndogo. Udongo una rutuba nzuri kwa uzalishaji wa mazao mbalimbali; 90% ya wakazi wanajishughulisha na kilimo na shughuli nyingine zinazoambatana na kilimo. Mazao yanayolimwa ni mahindi, mpunga, maharage, mtama, karanga, muhogo na alizeti. 9% ya wakazi waliobaki wanajishughulisha na uvuvi kwenye Ziwa Rukwa. Inakadiriwa kwamba wastani wa pato la wananchi wa H/W ya Sumbawanga ni TZS 1,080,000 kwa mwaka ambalo linatokana na kilimo (90%), uvuvi (9%) ufugaji nyuki na shughuli nyingine (1%).

Halmashauri ina skimu 13 za umwagiliaji. Eneo linalofaa kwa umwagiliaji ni 19,826ha, hata hivyo, eneo linalotumika kwenye skimu ya umwagiliaji wa asili ni 1,018ha (11%) tu. Jitihada ya kuimarisha skimu ya umwagiliaji ilitekelezwa katika Kijiji cha Sakalilo Kata ya Ilemba, Tarafa ya Kipeta. Idadi ya watu katika kijiji hiki ni 5, 940 (Wanaume 2,979 na wanawake 2,961).

Skimu ya umwagiliaji ya Sakalilo ina uwezo wa kuhudumia eneo la 4,000ha. Hata hivyo, eneo lilopimwa kwa ajili ya umwagiliaji ni 650ha. Kwa sasa, ni 220ha pekee ambayo ipo chini ya skimu ya umwagiliaji.

Awali, wakulima wa Kijiji cha Sakalilo walitumia miundombinu ya asili ya umwagiliaji kumwagilia mashamba yao kwa kutumia maji ya Mto Mumba. Skimu ya umwagiliaji ya Sakalilo ilianza mwaka 1990 ikiwa na wanachama 136 wa Chama cha Wakulima wa Umwagiliaji Sakaliko (CHAWASA)

**2.0 TATIZO**

Uchumi wa H/W ya Sumbawanga unategemea kilimo. Kabla ya mwaka 2004 Halmashauri ilikumbwa na upungufu katika uzalishaji wa mazao kutokana na uhaba wa mvua. Halmashauri ilikuwa ikipata mvua za wastani wa 700mm kwa mwaka zilizoleta changamoto kwa wakulima waliokuwa wamezoea kuzalisha kipindi chote cha mwaka. Tatizo la upungufu wa mvua katika Bonde la Ziwa Rukwa lilichochea wakulima wa Kijiji cha Sakalilo kuanzisha skimu ya asili ya umwagiliaji. Skimu hii ilijengwa kwa udongo na mawe hivyo kusababisha upotevu mkubwa wa maji na uharibifu wa mashamba.

Tatizo jingine lilikuwa uzalishaji mdogo wa mazao kwa eneo lililopo chini ya umwagiliaji. Kabla ya kuanzisha skimu bora ya umwagiliaji, uzalishaji ulikuwa mdogo wa wastani wa gunia 10 za mpunga kwa ekari. Hali hii iliathiri kipato cha mkulima ikilinganishwa na gharama kubwa za uzalishaji. Uzalishaji mdogo ulisababisha kipato duni, maisha magumu kwa jamii ya Sakaliko, nyumba duni, na uwezo mdogo wa kumudu gharama za huduma za elimu na afya.

**3.0 LENGO**

Lengo kuu la kuimarisha Skimu ya Umwagiliaji ya Sakalilo ni kuongeza uzalishaji na kuboresha maisha. Jitihada ilitegemea kupanua eneo na kuboresha umwagiliaji, wakulima kuongeza uzalishaji, kuongeza kipato na kuongeza uwezo wa kumudu mahitaji ya msingi. Malengo mahususi ya jitihada hii ni pamoja na;

(i) Kupima na kujenga skimu ya kisasa ya umwagiliaji.
(ii) Kusaidia wakulima kulima mazao katika misimu miwili kwa mwaka.
(iii) Kuanzisha matumizi ya mbegu bora.
(iv) Kuongeza uzalishaji kutoka magunia 10 kwa ekari hadi kufikia magunia 35 ya mpunga kwa ekari.
(v) Kuimarisha utoaji wa huduma za ugani katika eneo la skimu.

**4.0 MIKAKATI YA UTEKELEZAJI**

Kabla ya mwaka 2004 wakulima walianzisha skimu ya asili ya umwagiliaji kwa kutumia maji ya Mto Mumba. Wananchi walijenga mtego wa maji (*intake*) na mifereji ya umwagiliaji hadi kwenye mashamba. Mwanzoni mwa mwaka 2004, Halmashauri iliamua kusaidia jitihada ya wakulima kwa kutumia fedha za Mpango wa Maendeleo ya Kilimo (DADPs) na Mfuko wa Wilaya wa Maendeleo ya Umwagiliaji (DIDF). Mradi ulianzishwa kuimarisha eneo muhimu la skimu ya asili ya Sakalilo kwa kuiboresha na kuwa skimu ya kisasa. Kipindi cha utekelezaji wa jitihada hii, Halmashauri ilishirikiana na wadau mbalimbali kama Mamlaka ya Bonde la Ziwa Rukwa, Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika, wahisani kama JICA na jamii. Utekelezaji wa jitihada hii ulihusisha mikakati mbalimbali kama inavyofafanuliwa hapa chini.

Uhamasishaji wa jamii; Halmashauri ilianzisha timu ya uhamasishaji ikijumuisha wajumbe kutoka idara za Maendeleo ya Jamii, Kilimo na Mifugo. Jamii ya watu wa Sakalilo ilihamasishwa kupitia mikutano kuhusu umuhimu wa kushiriki katika utekelezaji kwa kuchangia nguvu kazi na kutoa maeneo yao kuruhusu ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji.

Kufanya upembuzi yakinifu; kwa kushirikiana na wanakijiji, wataalamu kutoka Halmashauri walifanya upembuzi yakinifu kutathmini faida za kuwekeza kwenye skimu ya asili ya umwagiliaji, gharama za

kupanga upya mashamba, mgawanyo wa mashamba kwa wamiliki, kutatua migogoro na faida zitakazopatikana kwa jamii. Mwaka 2004 timu ya wataalamu ilithibitisha kwamba mradi una faida na utanufaisha watu wa Kijiji cha Sakalilo. Halmashauri ilipima maeneo kubaini eneo la mashamba, sehemu ya kujenga tangi la kukusanya maji na miundombinu mingine kama mifereji. Wananchi wa Kijiji cha Sakalilo walishiriki katika upimaji kwa kuchangia nguvu kazi katika kusafisha maeneo, kuchimba barabara na mifereji na kushiriki shughuli za ujenzi. Picha ifuatayo inaonesha ushiriki wa wakulima katika upimaji.



***Wakulima wakishiriki katika upimaji***

Ujenzi wa bwawa la kuhifadhi maji, barabara za kuhudumia skimu na mifereji ya umwagiliaji; kupitia mikutano ilikubalika kwamba mashamba ambayo yataguswa na ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji hayatafidiwa. Iliaminika kwamba jamii yote itafaidika na miundombinu ya umwagiliaji hivyo jamii ilikubali kutoa mashamba yao bila fidia kuruhusu ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji ikiwemo mifereji. Baada ya makubaliano haya, kamati ya ujenzi iliundwa ikihusisha wajumbe kutoka ngazi ya jamii. Picha hapa chini inaonesha wajumbe wa kamati ya ujenzi.




***Wajumbe wa Kamati ya Ujenzi (2004-2006)***

Uandaaji wa vifaa na rasilimali; awali matumizi ya utaratibu maalum wa manunuzi (*force account)* ulitumika kabla ya kumtafuta mkandarasi wa ujenzi wa mradi. Wananchi na wakulima walitakiwa kukusanya mawe kwa ajili ya ujenzi wa mfereji mkuu kutoka kwenye chanzo/mtego. Wakulima walijipanga katika ngazi ya vitongoji na kushiriki katika hatua zote; kukata miti, kuchimba mitaro, kushindilia barabara, kukusanya mawe na mchanga na kusaidia shughuli za ujenzi. Mifereji ya usambazaji wa maji ina urefu wa 2,460m kutoka kwenye chanzo/mtego hadi eneo la mashamba.



***Baadhi ya miundombinu ya skimu ya umwagiliaji ya Sakalilo***

Kuomba kibali cha matumizi ya maji; kwa Tanzania, matumizi ya maji kwa ajili ya umwagiliaji yanahitaji kupata kibali kutoka mamlaka husika ya bonde ambalo lina rasilimali ya maji. Wakulima wa Skimu ya Umwagiliaji ya Sakalilo waliomba kibali cha kutumia maji kutoka Mamlaka ya Bonde la Ziwa Rukwa. Kibali kilitolewa kikionesha masharti ya kutumia maji ya Mto Mumba na kiasi cha fedha cha kulipia matumizi ya maji. Picha ifuatayo inaonesha kibali kilichotolewa na Mamlaka ya Bonde la Ziwa Rukwa.



***Kibali cha Matumizi ya Maji***

Uanzishaji wa ushirika wa umwagiliaji; Halmashauri iliwaunganisha wakulima na kuanzisha ushirika. Ushirika huu ulianzishwa ili kuweka mfumo wa kusimamia skimu ya umwagiliaji, matengenezo na usawa katika ugawaji wa maji ya umwagiliaji kwa wanachama wote. Aidha, ushirika uliunda ya katiba ya uendeshaji wa shughuli za skimu na kuanzisha mchango wa mwaka wa 5% ya mazao yaliyozalishwa ili kupata fedha za upanuzi, ukarabati na usimamizi wa skimu.

Kutoa mafunzo; ili kuhakikisha uendeshaji bora wa skimu na uzalishaji, Maafisa Ugani 2 na wakulima 5 walipatiwa mafunzo kuhusu mfumo wa uzalishaji mpunga (System of Rice Intensification: SRI). Mafunzo haya yalifadhiliwa na kutolewa na Mradi wa kuendeleza kilimo cha mpunga (TANRICE) na Shirika la Maendeleo la Uholanzi (SNV).

**5.0 RASILIMALI**

Utekelezaji wa jitihada hii ulitumia raslimali kutoka kwa jamii, Halmashauri na wadau wengine. Wakati wa upimaji wa mashamba, wakulima walijitolea nguvu kazi katika kusafisha maeneo, kukata miti na kushiriki katika ujenzi. Mchango wa jamii ni sawa na 20% ya gharama za mradi ambapo wananchi walisafisha eneo la mradi, kutengeneza barabara, kung'oa visiki na kuchimba mifereji.

Halmashauri ilitoa utaalamu katika utekelezaji wa mradi. Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika ilisaidia kuunganisha wakulima na washirika wa maendeleo. Wizara pia itoa msaada wa kitaalamu kwa kutoa sera na kanuni zinazohusu skimu za umwagiliaji. Kitengo cha Kanda cha Umwagiliaji kilisaidia kusimamia utekelezaji wa sera ya umwagiliaji na kutoa utaalamu pale ulipohitajika. Utekelezaji wa mradi pia

ulishirikisha Washirika wa Maendeleo kama JICA ambao walitoa fedha kusaidia utekelezaji wa mradi na utaalamu kwa Timu ya Uwezeshaji (DIDFT) na Kamati ya Mradi wa Umwagiliaji ya Sakalilo.
Kiasi kikubwa cha fedha kiliwekezwa katika mradi huu. Rasilimali fedha zimeoneshwa katika majedwali yafuatayo.

**Jedwali 1: Michango ya Jamii**

| S/N | Ufafanuzi | Kiwango | Idadi(m) | Kasi (TShs) | Juma ya fedha (Tshs) |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Kusafisha eneo (200m &13500m) | m2 | 14640 | 1000.00 | 14,640,000.00 |
| 2 | Kusafisha eneo la barabara (2km) | m2 | 12,000 | 1,000.00 | 12,000,000.00 |
| 3 | kuchimba mfereji mkuu (200m) | m3 | 520 | 3,000.00 | 1,560,000.00 |
| 4 | Kuchimba mifereji ya mashambani (13500m) | m3 | 1760 | 1000.00 | 1,760,000.00 |
| 5 | Usimamizi | - | - | 6,800,000.00 | 6,800,000.00 |
| | **Jumla** | | | | **36,760,000.00** |

**Jedwali 2: Rasilimali fedha kutoka Halmashauri**

| S/n | Chanzo cha fedha | Mwaka | Kiasi |
|---|---|---|---|
| **1** | DADPS | 2012/2013 | 28,000,000.00 |
| **2** | DIDF | 2013/2014 | 600,000,000.00 |
| **Jumla** | | | **628,000,000.00** |
| **Jumla kuu (Jamii + Halmashauri)** | | | **664,760,000.00** |

**6.0 MATOKEO**

Skimu ya Umwagiliaji ya Sakalilo ni moja ya miradi iliyofanikiwa zaidi katika H/W ya Sumbawanga. Skimu ina mundombinu ya umwagiliaji ya kudumu; hifadhi ya maji (Tangi), mifereji yenye urefu wa 1,250m na mabanio. Picha zifuatazo zinaonesha tangi la kuhifadhi ya maji na mabanio yaliyojengwa.



***Tangi la kuhifadhi maji na banio katika skimu ya umwagiliaji ya Sakalilo***


Skimu imeongeza kiwango cha uzalishaji; kwa sasa uzalishaji wa mpunga umeongezeka kutoka 0.8t kwa ekari hadi kufikia 2.0t kwa ekari. Ongezeko la uzalishaji limeboresha maisha ya jamii na Kaya za Kijiji cha Sakalilo. Uwezo wa kumudu gharama za huduma mbalimbali umeongezeka na kiwango cha maisha kimeimarika. Hii imethibitika kutokana na kuendelea kwa ujenzi wa nyumba bora na kuongezeka kwa uwezo wa kukidhi gharama za huduma kama elimu na afya. Watu wa Kijiji cha Sakalilo wameshuhudia kuongezeka kwa mwingiliano wa watu kutoka nje wanaofika kijijini kununua mpunga na mchele kutoka mikoa mbalimbali na hata nje ya nchi. Picha zifuatazo zinaonesha nyumba zinazomilikiwa na baadhi ya wakulima.



***Nyumba bora***

Uwepo wa Umoja wa Umwagiliaji; wakulima wa Sakalilo wameanzisha umoja wa umwagiliaji uliosajiliwa mwaka 2011. Lengo la umoja huu ni kuendeleza ustawi wa wananchama kwa uongozi bora na usimamizi wa skimu. Wanachama wameongezeka kutoka 25 mwaka 2004 hadi 117 mwaka 2017; kati yao wanaume ni 103 na wanawake ni 14.

Jumuia imeanzisha taasisi ya kifedha ya mfumo wa SACCOS kutoa huduma ya akiba na mikopo ya fedha na pembejeo yenye riba nafuu kwa wakulima. Uwepo wa huduma hizi umewezesha wakulima kujishughulisha na kilimo zaidi pasipo kupata usumbufu kutoka kwa wakala wa usambazaji wa pembejeo kwani wana uhakika wa kupata pembejeo. Mabadiliko yaliyodhihirika kwenye skimu hii ya umwagiliaji yamechochea vijiji vingine kuiga na kuanzisha skimu za umwagiliaji; vijiji hivyo ni Ilemba, Nankanga na Liwelyamvula. Kwa upande mwingine, mapato ya Halmashauri na Kijiji yameongezeka kutokana na kuimarika kwa uzalishaji.



***Cheti cha usajili***

**7.0 MIKAKATI YA UENDELEVU**

Ili jitihadi hii iwe endelevu, Halmashauri, jamii, Mamlaka ya Bonde la Ziwa Rukwa, Kitengo cha Umwagiliaji cha Kanda na Washirika wa Maendeleo wanaendea kufanya kazi kwa pamoja na ushirikiano. Jamii imeanzisha *"Umoja wa Umwagiliaji Maji Tujikomboe Sakalilo"* (UWAMTUSA) uliosajiliwa tarehe 15 Agosti, 2011 na kupewa namba ya usajili SA 17698. Umoja umepewa kibali cha muda cha matumizi ya maji kutoka Mamlaka ya Bonde la Ziwa Rukwa chenye namba LRB.0191 kilichotolewa tarehe 27 Septemba, 2011. Kibali kinatoa matumizi ya lita 750,000 kwa sekunde. Mikakati hii inaweka uendelevu wa skimu.

Halmashauri imesaidia wakulima kuanzisha kamati ya mradi ambayo inajukumu la kuunganisha na kushawishi wakulima wengine kujiunga na chama cha umwagilaji ili kupunguza migogoro ya rasilimali ya maji. Lengo ni kuwafanya wananchi wote wa kijiji kujiunga katika skimu na kupanua eneo la umwagilaji.

Kuzingatia miongozo ya DIDFT kuhusu matumizi ya maji na usimamizi wa skimu kuhakikisha uendelevu. DIDFT ina wajibu wa kusimamia na kufanya ufuatiliaji, utekelezaji, uendelevu na ukarabati wa mradi. Vilvile DIDFT inatoa utaalamu wa kiufundi kwa jumuia ya umwagiliaji. Mbinu nyingine ni kuendelea kutoa mafunzo kwa Maafisa Ugani kuhusu mifumo ya uzalishaji wa mpunga na kulinda Skimu ya Umwagiliaji ya Sakalilo.

**8.0 SIRI YA MAFANIKIO**

Skimu ya Umwagiliaji ya Sakalilo ilifanikiwa kutokana na uwepo wa Mto Mumba ambao unatoa fursa kwa jamii kuzalisha aina mbalimbali za mazao, uwepo wa ardhi yenye rutuba katika Bonde la Ziwa Rukwa inayowezesha uzalishaji wa mazao ya aina mbalimbali na ubunifu wa jamii toka enzi za skimu ya asili kwa kutumia maji ya Mto Mumba kwa ajili ya umwagiliaji. Siri nyingine ni utaratibu wa mchango wa gunia moja la mpunga kutoka kwa kila mkulima kwa mwaka kwa ajili ya ukarabati. Aidha, mafanikio ya jitihada hii yametokana na utayari na ushiriki kamilifu wa jamii katika utekelezaji.

Siri nyingine ni ushirikiano wa wadau mbalimbali katika kutoa rasilimali na utekelezaji wa mradi pamoja na ushiriki wa sekta mbalimbali kama Kilimo, Maendeleo ya Jamii, Mamlaka ya Bonde la Ziwa Rukwa, Idara ya Ujenzi, Hifadhi ya Mazingira na sekta binafsi . Ushirikiano huu uliwezeshwa na uongozi thabiti na utashi wa kisiasa katika ngazi mbalimbali za Kijiji, Kata ya Ilemba na H/W ya Sumbawanga. Mwisho, mafunzo yaliyotolewa mara kwa mara kwa viongozi wa kamati ya umwagiliaji kuhusu usimamizi na uendeshaji wa umoja wa umwagiliaji yalijenga ari na hamasa kwa viongozi na jamii ya Sakalilo.

# HALMASHAURI YA WILAYA YA NKASI

## UANZISHAJI WA JUMUIYA YA WAFUGAJI KUHIMIZA UFUGAJI WA KOO BORA ZA NG'OMBE



RASIMU YA MPANGO WA KUENDELEZA KONGANO BUNIFU


ANDIKO LA MAOMBI YA FEDHA ZA KUENDELEZA KONGANO LA WAFUGAJI WA NG'OMBE WA NYAMA WILAYA YA NKASI – MKOA WA RUKWA

MAOMBI YAMEWASILISHWA: - COSTECH
SEHEMU YA KONGANO ITAKUWA:- WILAYA YA NKASI

IMEANDALIWA NA:- KONGANO LA NG'OMBE WA NYAMA – MKOA WA RUKWA

| TAREHE | 05 | AGOSTI | 2013 |
|---|---|---|---|


WAKIONGOZWA NA:-
1. Idd Hassan Kimanta: Mkuu wa Wilaya ya Nkasi (Mwezeshaji)
2. Respich Maengo: RS Rukwa (Mwezeshaji)
3. Reuben Yohana Kapongo: Livestock Officer - Nkasi (Mwezeshaji)
4. Fulgence Salangi: SIDO Mkoa wa Rukwa (Mwezeshaji)



*Uzoefu wa H/W ya Nkasi*

**1.0 UTANGULIZI**

Halmashauri ya Wilaya ya Nkasi ni moja kati ya Halmashauri 4 za Mkoa wa Rukwa iliyoanzishwa mwaka 1983. Eneo la Halmashauri ni 13,124km$^2$; 3,749km$^2$ ni sehemu ya maji na 9,375km$^2$ ni nchi kavu. Halmashauri inapatikana Kusini Magharibi mwa Tanzania kwenye mwambao wa Ziwa Tanganyika na Ziwa Rukwa katika Longitudo 30$^o$ 20'- 31$^o$ 30' Mashariki na Latitudo 6$^o$ 58'- 8$^o$ 17" Kusini. Moja ya sifa ya H/W ya Nkasi ni kuwa na pwani ya Ziwa Tanganyika yenye urefu wa 186km kutoka Kijiji cha Kalila hadi H/W ya Kalambo. H/W ya Nkasi inapakana na H/W za Mpanda (Mkoa wa Katavi) upande wa Kaskazini, Sumbawanga upande wa Kusini, Mlele (Mkoa wa Katavi) upande wa Mashariki, Kalambo upande wa Kusini Magharibi na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo katika Ziwa Tanganyika. Halmashauri ina Tarafa 5 (Namanyere, Wampembe, Kirando, Chala na Kate), Kata 28, Vijiji 90 na Vitongoji 721. Kwa mujibu wa sense ya mwaka 2012, H/W ya Nkasi ina watu 281,200; wanaume 137,041 na wanawake 144,159, ikiwa na wastani wa ongezeko la watu ni 4.5% na wastani wa watu 5 katika Kaya.




***Ramani ya H/W ya Nkasi***

Uchumi wa H/W ya Nkasi unategemea kilimo cha kujikimu. 80% ya wananchi wa Nkasi hutegemea kilimo na ufugaji. Shughuli nyingine ni viwanda vidigovidogo, maduka, ufugaji nyuki, uchimbaji mdogo wa madini na biashara ndogondogo. Zaidi ya 40% ya pato la Halmashauri hutegemea kilimo. Mazao ya chakula ni mahindi, muhogo, mpunga, viazi vitamu, jamii za mikunde na migomba. Mazao ya biashara ni pamoja na mananasi, mbogamboga na matunda mengine, maua, miwa, viungo na uyoga. Mazao haya huchangia takriban 17% ya kiwango cha chakula kinachohitajika katika Halmashauri.

**2.0 TATIZO**

Tangu mwaka 1995, H/W ya Nkasi imekuwa ikipokea wahamiaji kutoka mikoa mingine wakiwa na makundi makubwa ya mifugo hasa ng'ombe. Uhamiaji huu wa wafugaji kutoka Mikoa ya Tabora, Mwanza, Simiyu, Mbeya na Shinyanga umesababishwa na kutafuta malisho na maji. Hali hii ilisababisha kuongezeka kwa idadi ya mifugo ndani ya H/W ya Nkasi ikilinganishwa na uwezo wa eneo kuhimili idadi hiyo ya mifugo. Kutokana na sensa ya taifa ya mifugo ilyofanyika Julai hadi Agosti 2017, H/W ya Nkasi ilikuwa na wafugaji 1977 wenye idadi ya mifugo 176,565; hata hivyo baada ya Halmashauri kuendesha zoezi la upigaji chapa mifugo, ilibainika kuwa idadi kamili ya mifugo ilikuwa 201,677. Kutokana na ongezeko hili la mifugo Halmashauri ilikumbwa na matatizo yafuatayo;

(i) Migogoro ya mara kwa mara ya matumizi ya ardhi kati ya wakulima na wafugaji. Migogoro hii ilisababisha vifo vya watu 10 (wakulima 4 na wafugaji 6) katika Kata za Mkwamba, Sintali na Mtenga kati ya mwaka 2000 na 2010.
(ii) Migogoro ya matumizi ya ardhi kati ya wafugaji na Pori la Akiba la Lwafi. Kutokana na uhitaji mkubwa wa malisho, wafugaji walivamia pori hili na kusababisha migogoro ya mara kwa mara.
(iii) Uharibifu wa mazingira; kutokana na ongezeko kubwa la mifugo, vyanzo vya maji na mazingira viliharibiwa kwa kiasi kikubwa.
(iv) Kuongezeka kwa hali ya ukame katika baadhi ya maeneo ikilinganishwa na hali iliyokuwepo kabla ya 1994 idadi ya mifugo ikiwa ya wastani.
(v) Migogoro ya ardhi ilileta kero kubwa kwa idara za ardhi na mifugo katika kutoa huduma na uratibu kutokana na misuguano ya wakulima na wafugaji.
(vi) Uzalishaji duni wa mazao ya mifugo kutokana na kukosekana kwa mbinu bora za ufugaji. Uzalishaji wa mazao ulikuwa duni kutokana na uharibifu wa mazingira uliosababishwa na idadi kubwa ya mifugo.

**3.0 LENGO**

Mwaka 2010, H/W ya Nkasi iliweka mpango wa kuboresha huduma za ufugaji kwa kuhamasisha na kuunganisha wafugaji. Halmashauri iliandaa mafunzo na uhamasishaji wa ufugaji wa koo bora ng'ombe ikiwa ni pamoja na utoaji wa chanjo katika vijiji vyote. Aidha, Idara ya Mifugo na Uvuvi ilithibitisha changamoto ya utekelezaji wa mikakati hii kutokana mtawanyiko wa wafugaji. Baadaye, jitihada hii iliweka wazi lengo mahsusi la kuunganisha wafugaji kwa kuunda Jumuiya ili kupunguza migogoro ya matumizi ya ardhi, uharibifu wa mazingira, ukame na mauaji. Lengo la pili lilikuwa kuboresha mbinu za ufugaji kwa wafugaji wa kuhama hama na wa kudumu ili kuboresha uzalishaji wa mazao ya mifugo na kuongeza kipato.

**4.0 MIKAKATI YA UTEKELEZAJI**

H/W ya Nkasi iliandaa mkakati na mpango wa kufikia malengo ya kuhamasisha na kuunganisha wafugaji katika Kata zote 28. Tarehe 28 Agosti, 2012, Mkuu wa Wilaya, Mh Idd H. Kimanta alizindua utekelezaji wa mpango kwa kufanya mkutano wa uhamasishaji kwa wafugaji 27 wenye ushawishi mkubwa na idadi kubwa ya mifugo. Wakati wa mikutano ya uhamasishaji, wafugaji walielimishwa juu ya umuhimu wa kupunguza idadi ya mifugo na kuwa na idadi ndogo ya mifugo iliyoboreshwa. Mwezeshaji (Bw. Reuben Y. Kapongo – Afisa Mifugo) alitumia mifano ya mafanikio ya wafugaji waliopunguza idadi ya mifugo kwa kufuga idadi ndogo ya koo bora za ng'ombe kutoka Tanzania, Afrika Kusini, Botswana na Kenya. Wafugaji wengi walivutiwa na matokeo makubwa ya wafugaji hao. Baada ya mkutano wa kwanza ambao ulifanikiwa kwa kiasi kikubwa, mkutano wa pili wa uhamasishaji ulifanyika 11 Oktoba 2012 katika kituo cha Namanyere. Kutokana na maamuzi ya mkutano huu, wafugaji 167 waliunda Jumuiya baada ya kuelewa faida za kiuchumi na za kijamii za ufugaji wa koo bora za ng'ombe.


Kuandaa mkakati, malengo na mpango wa kibiashara wa Jumuiya; Mkakati ulitambua wadau muhimu katika jitihada hii kama Mkuu wa Mkoa, Mkuu wa Wilaya, Mkurugenzi wa Halmashauri, Taasisi ya Utafiti ya Uyole (Mbeya) na Taasisi ya Kilimo ya Laela. Mbali na kutambua wadau muhimu, watu muhimu wa kutoa usaidizi wa kitaalamu walitambuliwa; hawa ni pamoja na Bw. Fulgence Salangi- Ofisi ya SIDO Mkoa, Dkt. Mwambene - Taasisi ya Utafiti Uyole na Bw. Mahenge – Taasisi ya Kilimo ya Laela.

Kubaini washirika wa ufugaji wa kibiashara; Jumuiya ilichagua wafugaji ambao wangejihusisha kikamilifu katika kuchochea mabadiliko ili kuboresha ufugaji. Baadhi ya wafugaji hao ni Bw. Msemakweli Msalaba, Bw. Mashishanga Salum, Bw. Heka Mbatilo na Ranchi ya Kalambo. Wafanyabiashara wa nyama

waliochaguliwa ni SAAFI Co. Ltd (kinachomilikiwa na Christopher Mzindakaya) na Bw. Samwel Kisabwiti. Wafanyabiashara wengine wasio rasmi ni Bw. Deogratius Chipawa, Bw. Vidian Lubavya and Bw. Apolinary Tepeli. Ili kufanya mabadiliko haya kuwa endelevu, wauzaji wa pembejeo waliunganishwa kwenye mkakati huu; Bw. Wilbroad Peter na Bw. Malila. Wanunuzi wakubwa wa nyama waliotambuliwa ni pamoja na wananchi kutoka mikoa ya Rukwa, Katavi na Shinyanga, Nchi jirani ya Kongo na Nchi za Kiarabu (United Emirates).

Kuanzishwa kwa uongozi imara wa kuratibu hatua za utekelezaji; Jumuiya iliwachagua Bw. Msemakweli Msalaba (Mwenyekiti), Bw. Mashishanga Salum (Makamu Mwenyekiti), Bw. Jisena Biliya (Katibu), Bw. Dominick Manyama (Katibu Msaidizi), Bw. George Jibunge (Mweka hazina) na wawakilishi wa wafugaji kutoka kila Kata. Hatua za utekelezaji katika kukamilisha shughuli za Jumuiya ni pamoja na kutafuta masoko kwa ajili ya bidhaa za Jumuiya, kubaini chanzo cha fedha za kununua koo bora za ng'ombe, kusimamia na kufanya tathimi ya utekelezaji, kuanzisha mfumo wa usimamizi wa utendaji na ufuatiliaji wa malengo, kufuata kanuni za usimamizi wa mazingira na kutoa elimu ya VVU/UKIMWI kwa wajumbe wa Jumuiya katika ngazi ya Kaya.

Utafutaji wa rasilimali fedha; wafugaji waliamua kutafuta fedha kutoka kwa Washirika wa Maendeleo ili kuweza kutekeleza shughuli zao. Kutokana na jitihada hii mwaka 2013 Jumuiya ilipokea TZS 8,000,000 kutoka Tume ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH). Fedha nyingine zilitokana na michango ya wafugaji kwa mujibu wa katika ya Jumuiya ambapo kila mwanachama anapaswa kulipa ada ya mwezi na michango mingine.




| Na | JINA KAMILI | MAHALI UTOKAKO (KIJIJI) | CHEO / SHUGHULI | SAINI |
|---|---|---|---|---|
| 16 | MIHAYO BUGAKETA | ISALE | MJUMBE - MFUGAJI | |
| 17 | MAHONA SENI | ISALE | MJUMBE - MFUGAJI | |
| 18 | BUYOLE MAGEMBE | ISALE | MJUMBE - MFUGAJI | |
| 19 | MACHIYA NKOLA | ISALE | MJUMBE - MFUGAJI | |
| 20 | RAMADHANI MTAALAMU | ITEKESHA | MJUMBE - MFUGAJI | |
| 21 | CHARLES MALYA | ITEKESHA | MJUMBE - MFUGAJI | |
| 22 | MADIRISHA MTAALAMU | ITEKESHA | MJUMBE - MFUGAJI | |
| 23 | BUNZALI NTAMBI | KACHECHE | MJUMBE - MFUGAJI | |
| 24 | TOGOLO SISI | KAKOMA | MJUMBE - MFUGAJI | |
| 25 | NUHI CHANANJA | KAKOMA | MJUMBE - MFUGAJI | |
| 26 | CHARLES MASALADI | KAKOMA | MJUMBE - MFUGAJI | |
| 27 | NDAMO NGWEKWE | KAKOMA | MJUMBE - MFUGAJI | |
| 28 | BENWEL BENEZETA | KALAMBO | MJUMBE - MFUGAJI | |
| 29 | MALENYE NZALI | KALAMBO | MJUMBE - MFUGAJI | |
| 30 | HAMIDU MAGESHA | KALAMBO 55/13 | MJUMBE - MFUGAJI | |
| 31 | MARTINE LADISLAUS | KALAMBO NARCO | MJUMBE - RANCH MANAGER | |
| 32 | JOAS W. MUYUNGA | KALUNDI | MJUMBE - AFISA UGANI | |
| 33 | SOLO JIKOLO | KANAZI | MJUMBE - MFUGAJI | |
| 34 | HEKA MBATILO | KANAZI | MJUMBE - MFUGAJI | |
| 35 | JUAKALI MASANJA | KANAZI | MJUMBE - MFUGAJI | |
| 36 | SALAWA KADELE | KANAZI | MJUMBE - MFUGAJI | |
| 37 | BULUBA HANGANGA | KANAZI | MJUMBE - MFUGAJI | |
| 38 | MADUKA KONGWA | KANAZI | MJUMBE - MFUGAJI | |
| 39 | KABHISU KANDELE | KANAZI | MJUMBE - MFUGAJI | |
| 40 | SENGEREMA DOFU | KANAZI | MJUMBE - MFUGAJI | |
| 41 | SAID KAUSHI | KANAZI | MJUMBE - MFUGAJI | |
| 42 | SENKENYA KULWA | KANAZI | MJUMBE - MFUGAJI | |
| 43 | OSCAR KALOLO | KASU | MJUMBE - MFUGAJI | |
| 44 | ELISHA LUFUNGA | KATANI | MJUMBE - MFUGAJI | |
| 45 | MASUNGA NKWABI | KATANI | MJUMBE - MFUGAJI | |
| 46 | DAUDI NONGA | KATANI | MJUMBE - MFUGAJI | |
| 47 | MGULU LUTEMA GULUJANGWELU | KATE | MJUMBE - MFUGAJI | |
| 48 | HASSAN MAGEMBE | KATE | MJUMBE - MFUGAJI | |
| 49 | DUNIA NGULU | KATE | MJUMBE - MFUGAJI | |
| 50 | MBASOJA LUSHU | KATE | MJUMBE - MFUGAJI | |
| 51 | GILAGI LUTELEMLA | KIPANDE | MJUMBE - MFUGAJI | |
| 52 | CHONO NZALA | KIPANDE | MJUMBE - MFUGAJI | |
| 53 | MPUYA KOMESHA | KIPILI | MJUMBE - MFUGAJI | |
| 54 | JOHN SHAGEMBE | KIPILI | MJUMBE - MFUGAJI | |
| 55 | KISINZA TAMAAMBAYA | KIPUNDUKALA | MJUMBE - MFUGAJI | |

***Sehemu ya andiko la mkakati wa Jumuiya na orodha ya wanachama***

Utafutaji na ununuzi wa koo bora za ng'ombe; baada ya kuanzisha na kurasimisha mchakato, Jumuiya ya wafugaji ilianza kutafuta madume ya koo bora za ng'ombe kama *Santa getruids, Simmental na Boran.* Afisa Mifugo na Uvuvi Bw. Reuben Kapongo alifanya ziara kwenye mashamba ya ufugaji katika mikoa ya kusini na kubaini uwepo wa koo bora za madume ya ng'ombe katika Mkoa wa Iringa kwenye shamba linalomilikiwa na Bw. Maktela raia wa Afrika Kusini. Taarifa ya kupatikana kwa madume ya koo bora za ng'ombe ilitolewa kwa Jumuiya ya wafugaji na wafugaji 2 Bw. Nyanda Kisinza na Bw. Mashishanga walisafiri kwenda Iringa na kununua madume 4 na majike 3 ya koo bora za ng'ombe aina za *Santa getruids, Simmental na Boran*.




***Koo ya Santa*** ***Koo ya Boran***

Kuimarisha miundombinu ya ufugaji na kutoa elimu; baada ya kuunda Jumuiya na jitihada hii kukubalika kwa wafugaji, Halmashauri ilianzisha mradi wa kusaidia Jumuiya ya wafugaji. Mradi huu ulihusu ujenzi wa majosho 27, machinjio 20 na mabwawa 2 ya kunyweshea mifugo. Miradi hii ilitekelezwa kwa pamoja na utoaji wa mafunzo ya kujenga uwezo kwa Maafisa Ugani kuhusu utoaji wa huduma za ugani kwa wafugaji katika Vijiji na Kata.

Kuboresha mbinu za ufugaji; Halmashauri, kwa kutumia mkakati wa Jumuiya na malengo ya wafugaji, iliongeza wigo wa utoaji huduma za chanjo na uhamilishaji wa ng'ombe kwa wafugaji 167. Mchakato huu ulilenga kupunguza aina ya ng'ombe wa asili ambao uzalishaji ni mdogo ukilinganishwa na koo bora za ng'ombe na kupunguza idadi ya mifugo na uhitaji mkubwa wa ardhi ambao unasababisha migogoro. Kwa kipindi cha miaka 10 H/W ya Nkasi imeshuhudia mabadiliko ya mtazamo wa wafugaji kutoka kuamini kwenye wingi wa ng'ombe hadi kuamini ubora wa ng'ombe.

Kutoa usaidizi kwa wafugaji kuhudhuria maonesho mbalimbali; kila mwaka Halmashauri imekuwa ikidhamini mfugaji mmoja ambaye amefanya vizuri katika ufugaji wa ng'ombe bora kuhudhuria maonesho ya mashindano ya kibiashara ndani ya mkoa, kanda na taifa.

**5.0 RASILIMALI**

Kuanzisha Jumuiya ya wafugaji sio shughuli rahisi. Halmashauri nyingi zimejaribu kuunganisha wafugaji na kubadilisha aina ya ufugaji wa mazoea bila mafanikio kutokana na uhaba wa rasilimali. Katika utekelezaji wa jitihada hii ya kuanzisha Jumuiya ya wafugaji, H/W ya Nkasi ilitumia muda mwingi pamoja rasilimali watu, vitendea kazi na fedha kama ifuatavyo.

(i) Mikutano ya uhamasishaji iliigharimu Halmashauri TZS 25,450,000 katika mwaka wa fedha 2010/2011 hadi 2014/2015.
(ii) Mwaka wa fedha 2010/2011 Halmashauri ilitumia TZS 128,700,000 kujenga miundombinu ya mifugo.
(iii) Mwaka wa fedha 2012/2013 Halmashauri ilitumia TZS 6,750,000 kugharamia ziara ya mafunzo kwa vitendo ya Maafisa Ugani.
(iv) Mwaka wa fedha 2013/2014, 2014/2015 na 2015/2016 huduma ya chanjo iligharimu Halmashauri TZS 45,290,760.
(v) Kila mwaka Halmashauri inagharamia mfugaji mmoja kuhudhuria maonesho mbalimbali. Kati ya mwaka 2011 na 2015 Halmashauri imetumia TZS 26,340,290 kugharamia ushiriki wa maonesho hayo.

**6.0 MATOKEO**

Mafanikio mengi yamepatikana tangu kunganisha wafugaji kwenye Jumuiya. Baadhi ya mafanikio hayo yameelezwa kwa kina hapa chini.

Kuanzishwa kwa Jumuiya ya wafugaji wa koo bora za ng'ombe kumeleta mtazamo chanya kwa wafugaji. Halmashauri ilianza na mjumbe 1 sasa wamefikia wafugaji 7 katika Kata za Isale Asilia, Kate, Nkomolo, Mtenga, Sintali na Ntuchi ambao wameanza kufuga ng'ombe wa koo bora. Aidha, H/W ya Kalambo imeanza kuiga kuanzisha mkakati wa ufugaji ulioboreshwa ili kufikia ubora wa uzalishaji wa ng'ombe wenye tija.

Kutokana na uanzishaji wa ufugaji wa kimkakati, wafugaji wameboresha aina ya ng'ombe hivyo kuongeza uzalishaji na kipato. Hali ya maisha ya baadhi ya wafugaji imekuwa bora na uwezo wa kukidhi mahitaji umeongezeka. Baadhi ya wafugaji wameweza kumudu gharama za ada za wanafunzi, ujenzi wa nyumba bora, kupata mikopo, kukidhi huduma za afya na kufanya uwekezaji. Mafanikio haya yamesaidia kupunguza migogoro ya ardhi kati ya wakulima na wafugaji; kwa mfano migogoro impepungua kutoka 50 mwaka 2010 hadi 2 tu 2017.

Wafugaji 7 walihudhuria mkutano wa wafugaji ulionadaliwa na COSTECH mwaka 2013 na kupokea vyeti vya utambulisho kama wawezeshaji wa Jumuiya. Wafugaji 7 waliohudhuria mkutano huu walijumuika na wafugaji wengine kutoka Jumuiya nyingine Tanzania; mkutano huu ulifanyikia Bagamoyo mwaka 2014. Vile vile wafugaji kutoka Nkasi walialikwa kuhudhuria kongamano la ushindani la Afrika (*Pan African Competitiveness Forum – PACF)* ambalo lilifanyika Afrika Kusini mwaka 2015 na Senegal mwaka 2016. Tokeo jingine ni kuongezeka kwa koo bora za ng'ombe kutoka aina 3 mwaka 2009 hadi aina 5 mwaka 2017. Koo hizi bora ng'ombe ni *Ufipa, Tarime zebu*, *Boran, Santa gertruids* na *Simmental.*



***Ongezeko la koo bora za ng'ombe na chotara***

Kumekuwa na ongezeko kubwa la madume bora ya mbegu kutoka 109 mwaka 2009 hadi 771 mwaka 2016. Madume bora haya ni ya koo za Boran, Santa gertruids na Simmental. Madume haya yanatumiwa na wanachama kupandisha ng'ombe wa asili ili kutokomeza koo za asili. Wafugaji wanafurahia kuanzishwa kwa mradi wa uboreshaji wa ng'ombe. Zaidi ya ng'ombe chotara 4,710 wamezalishwa na kunenepeshwa.

Wafugaji wamekuwa wakishiriki katika mashindano mbalimbali ya wafugaji katika ngazi ya Mkoa, Kanda na Kitaifa. Jumuiya ya wafugaji H/W ya Nkasi imekuwa ikishinda katika mashindano ya kitaifa mfululizo kuanzia mwaka 2011 hadi 2015 kama mshindi wa kwanza katika kanda mwaka 2011-2015 na 2017 na mshindi wa kwanza katika ngazi ya Mkoa kwa kipindi cha 2011-2015 na 2017. Aidha, Jumuiya inatambuliwa na Mradi wa Ukuaji wa Kilimo Nyanda za Kusini (Southern Agricultural Growth Corridor of

Tanzania -SACGOT); H/W ya Nkasi imetambuliwa kama eneo ambalo halina magonjwa ya mifugo. Hii imekuwa fursa kwa Halmashauri kuzalisha ng'ombe bora wa nyama ambao huuzwa katika kiwanda cha nyama cha SAAFI CO L.T.D kilichopo Sumbawanga pamoja na nchi nyingine.

Katikati ya mwaka wa fedha 2017/2018, Halmashauri ilikusanya kiasi cha TZS 50,000,000 kama mtaji uliotokana na ada ya mwezi na michango mingine itokanayo na shughuli za Jumuiya. Halmashauri imekuwa kituo cha kujifunza.Viongozi wa Kitaifa na Mkoa wamekuwa wakitembelea H/W ya Nkasi kujifunza uendeshaji wa Jumuiya na mafanikio ya Halmashauri. Mwaka 2014 Waziri wa Kilimo na Uvuvi Dkt. Titus Kamani alitembelea Jumuiya ya wafugaji na kuziagiza Halimashauri nyingine kuanzisha Jumuiya za wafugaji wa koo bora za ng'ombe.



***Madume ya koo bora yanayomilikiwa na Bw. Nyanda Kisinza***

**7.0 MIKAKATI YA UENDELEVU**

Katika kufanya jitihada hii kuwa endelevu, H/W ya Nkasi imeweka mikakati ya uendelevu ikiwa ni pamoja na; kuhamasisha wafugaji kila robo mwaka kushiriki katika ufugaji wa koo bora za ng'ombe na kutoa usaidizi wa kitaalamu kuhusu ufugaji bora na wa kisasa kupitia Maafisa Ugani wanaotembelea wafugaji katika maeneo yao. Halmashauri inalenga kuendelea kutoa motisha kwa Maafisa Ugani kwa kuwalipa posho, mikopo ya riba nafuu na kununua pikipiki ambayo baadae itakuwa mali ya afisa. Halmashauri pia inalenga kujenga mtandao ambao utaruhusu wafugaji waliofanikiwa kupitia Jumuiya kuwa chachu ya mabadiliko kwa kuonesha mafanikio yao kwa wafugaji wengine jinsi ambayo wameweza kufuga koo bora za ng'ombe.

Mikakati mingine ni pamoja na; Kusaidia wafugaji kushiriki katika makongamano mbalimbali ya ufugaji kwa lengo kujifunza, kubadili mtazamo, kuendeleza uhamilishaji wa ng'ombe ili kuongeza kasi ya kuenea kwa koo bora za ng'ombe na kuwagawa kwa wanachama wa Jumuiya. Aidha, wataalamu wa Halmashauri wanaendelea kuhamasisha kudhibiti ng'ombe kuzaliana wenyewe kwa wenyewe na badala yake watumie madume ya koo bora za ng'ombe.

**8.0 SIRI YA MAFANIKIO**

Siri ya mafanikio ya kuanzisha Jumuiya ya wafugaji inatokana na kufanya kazi kwa pamoja kati ya Mkuu wa Wilaya, Mkurugenzi wa Halmashauri, Ofisi ya Mifugo na Uvuvi, wafugaji na wadau. Ubunifu wa Mkuu wa idara ya Mifugo na Uvuvi Bw. Reuben Kapongo na watumishi wengine wa idara kuhusu matumizi ya koo bora za ng'ombe umechangia mafanikio ya jitihada hii. Mafanikio pia yametokana na utayari wa Halmashauri kuwatambua na kusajili wafugaji kwa lengo la kurahisisha utoaji wa huduma za ufugaji. Aidha, madiwani walisaidia katika kuhakikisha Jumuiya ya wafugaji inaanzishwa na inafanya kazi kwa ufanisi.

# Rejea

*Abiona, A. I. and Bello, W. N. (2013). Grassroots Participation in Decision-Making Process and Development Programmes as Correlate of Sustainability of Community Development Programmes in Nigeria, Journal of Sustainable Development; Vol. 6 (3):47-57. Canadian Centre of Science and Education, [www.ccsenet.org/jsd] site visited on 19 /03/ 2013.*

Apolo, Kansiime (2013). The Impact of Public Procurement Reforms on Service Delivery in Uganda; Bishop Stuart University.

Chibehe, M.M. (2004). Factors Affecting Sustainability of Farmer Groups: the case of Twikinde Malimbichi Cooperative Society. MA Dissertation, SUA, Unpublished, 90pp.

Helene Bie Lielleor and Ulrik Lund-Sorensen (2013). FARMERS' CHOICE evaluating an approach to agricultural technology and adoption in Tanzania, Rockwool Foundation research Unit, PRACTICAL ACTION Publishing, pp. 154.

Helmsing, A. H. J. (1995). *Local Government Central Finance.*An Introduction: NewYork USA

Howlett. D and J. Nagu. (1997). *Agricultural Project Planning in Tanzania, A handbook on cycles and sequences, participation, identification, planning and design, economic and financial analysis, and environmental assessment of agricultural projects.* ISBN 1898828261. pp 89.

Kusago, Takayoshi. (2008). *Sustainable Livelihood and Happy Generation in Minamata-City Japan*: A Model for Endogenous Community Development.

Makonda, K.S.C. (2003). Partnership and sustainability of water supply systems in Bukombe District, Tanzania. *MA Dissertation*, Sokoine University of Agriculture, Morogoro, Tanzania. Unpublished. pp.154

Mwanga, J.N. (2011). Empowerment of Local Society in Tanzania –the Nucleus for Development- With Experience from Indonesia and Japan, *Rare Series Policy Paper*, Local Government Training Institute, Dodoma Tanzania. 100 pp.

Ohama, Y. (2002). Basic Framework and viewpoints of Participatory Local Social Development (PLSD) and construction of its evaluation framework.

Porter, Michael E. (1998). *Competitive Advantage: Creating and Sustaining Superior Performance*, 397 pp, Amazon.

Pretty, J.N. (1995). Participatory learning for sustainable agriculture. *World Development* 23(8): 1247-1263.

Scoones, I. and John Thompson (1994). *BEYOND FARMER FIRST: Rural people's knowledge, agricultural research and extension practice*. Intermediate Technology Publications LTD, London, UK, pp.301.

Sharma, P.N. and Ohama, Y. (2007*). Participatory Local Social Development-An Emerging Discipline*, Bharat Book Centre Publishers & Distributors, Lucknow India. pp. 467.

Shikuku, O.M. (2012). Community related Variables influencing sustainability of water projects in Nyando District a case. *MA Dissertation*, University of Nairobi, Digital Repository

URT (1998). Local Government Reform Agenda

URT, (2010). Public private partnership (PPP) *Act*, no 18 of 2010, pp 21

URT (2011). Millennium Development Goals, Tanzania country report. Ministry of Finance and Economic Affairs, Dar es Salaam – Tanzania.

Zadeh, B.S. and Nobaya, A. (2010). Participation and Community Development. *Current Research Journal of Social Sciences* 2(1): 13-14, 2010. [http://maxwellsci.com/print/crjss/v2-13-14.pdf] site visited on 22/07/2014.